

**UFUMBAJI WA ITIKADI KIJAZANDA KWENYE NYIMBO ZA KIASILI ZA
KIKAMBA**

NA

MUE ELIZABETH KASAU

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SANAA NA
SAYANSI ZA JAMII, IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA
KIAFRIKA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA
YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI**

CHUO KIKUU CHA MOI

2025

IKIRARI**MTAHINIWA**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya utafiti katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa nia ya kutunukiwa shahada yoyote.

Sahihi: _____ Tarehe: _____

Mue Elizabeth Kasau

SASS/DPHIL/KIS/06/2017

WASIMAMIZI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini na ridhaa yetu kama washauri na wasimamizi wa mzamifu walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi: _____ Tarehe: _____

Prof. Robert Oduori

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Kijamii

Chuo Kikuu cha Moi,

ELDORET.

Sahihi: _____ Tarehe: _____

Dkt. Magdaline Nakhumicha Wafula

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Kijamii

Chuo Kikuu cha Moi,

ELDORET.

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia ndugu yangu mpendwa marehemu Geoffrey Kasamba Mue aliyegharamia elimu yangu ya kiwango cha shule ya upili. Vilevile, naitabaruku tasnifu hii kwa babangu mpendwa marehemu Daniel Mue Kasamba aliyeahidi kila mara kuwa angefanya lolote kuhakikisha kuwa wanawe wote wanapata elimu ya kutosha. Laiti wangelikuwa hai kuyashuhudia mafanikio haya!

SHUKRANI

Nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kukamilisha safari hii. Nakiri kwamba safari yenyewe haikuwa rahisi kwa maana ilijawa na changamoto nyingi. Hata hivyo, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema na fadhili zake ambazo zimeniwezesha kuhitimisha utafiti wangu salama. Ahimidiwe milele. Shukrani za dharti pia ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Robert Oduori na Dkt. Magdaline Wafula wa Chuo kikuu cha Moi. Wamekuwa walezi bora kiakademia. Ushauri na uongozi wao umeniwezesha kuikamilisha kazi hii. Nawaombea baraka na maisha marefu ili waendeele kuwafaa wanafunzi wengine.

Ninawashukuru wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Moi kwa mawaidha yao. Hao ni pamoja na Prof. Kandagor, Prof. Obuchi, Dkt. Ibala na marehemu Dkt. Opijah miongoni mwa wengine. Siwezi kuwasahau wazamifu wenzangu Omutimba Washiali, Jonathan Rotich na Samson Nzyoka. Asanteni kwa ushirika wenu na ninawaombea nanyi mkamilishe masomo yenu.

Ningependa kumshukuru kwa dharti mume wangu mpendwa Samson Kivuti kwa kunifaa kwa hali na mali katika kuifanikisha kazi hii. Nawashukuru pia watoto wangu Gift Muuo, Patience Mutheu na Wisdom Ukilyo kwa kuniombea na kunihimiza nilipokuwa naishughulikia tasnifu hii. Shukrani za pekee zimwendee mama yangu mpendwa kwa kuniombea, kunilea na kunisomesha. Siwezi kuwasahau ndugu zangu, jamaa na marafiki waliosimama nami kwa njia moja au nyingine. Nawatakia mafanikio maishani mwenu.

IKISIRI

Nyimbo za kiasili ni maarufu sana miongoni mwa jamii ya Wakamba. Nyimbo hizi huimbwa katika kila hafla ya kijamii na husheheni itikadi ya Wakamba kuhusiana na masuala mbalimbali. Hata hivyo, itikadi katika nyimbo hizi za kiasili hufumbatwa kijazanda. Azma ya utafiti huu ni kuchunguza iwapo kuna uhusiano baina ya jazanda zinazotumika katika nyimbo za kiasili za Kikamba na itikadi ya jamii ya Wakamba. Malengo maalum ya utafiti ni matatu. Kwanza, ni kupambanua jazanda mahsusi katika nyimbo za kiasili za Kikamba zinazowasilishwa kwenye hafla maalum. Pili, kuhakiki itikadi za Wakamba zinazofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo hizo za kiasili. Tatu, kutathmini uamilifu wa jazanda mahsusi kifani na kimaudhui kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Utafiti huu umechukua muundo wa kithamano ambapo nyimbo za kiasili za Kikamba zimehakikiwa na kufasiriwa kwa kuzingatia muktadha wa kijamii ambamo nyimbo hizo zinaimbwa na kupokelewa. Data ya kimsingi ilitokana na nyimbo za kiasili za Kikamba zilizokusanywa kutoka Kamisheni ya kudumu ya Muziki ya Rais (PPMC) nchini Kenya. Nyimbo zilizosheheni jazanda zilisampuliwa kimakusudi, zikatafsiriwa kutoka Kikamba hadi Kiswahili na kuchanganuliwa. Uchanganuzi wa data uliegemezwa kwenye malengo ya utafiti na mihimili ya kinadharia. Nadharia ya Jazanda Dhanifu kwa mujibu wa Lakoff na Johnson na Nadharia ya Itikadi ilivyofafanuliwa na Van Dijk ndizo msingi wa utafiti huu. Nadharia ya Jazanda Dhanifu ilielekeza uhakiki wa itikadi zilizofumbatwa kijazanda na uamilifu wa jazanda hizo kifani na kimaudhui katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Nadharia ya Itikadi nayo ilitumika kupambanua maumbo ya kimsingi ya utambuzi wa kijamii yalivyodhihirika katika hafla za kijamii ambamo nyimbo za kiasili za Kikamba hutokea. Matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba huambatana na hafla mahsusi za kijamii. Nyimbo hizi za kiasili husheheni jazanda ambazo hufumbata mwonoulimwengu, mielekeo na maadili ya jamii ya Wakamba kuhusiana na masuala kama vile; siasa na uongozi, ndoa na malezi, uchumi na uwajibikaji. Tunaweza kuhitimisha kuwa jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba ni nyenzo muhimu ya kuwasilisha itikadi ya Wakamba kwa hadhira lengwa. Jazanda hizi zinajidhihirisha kama nguzo kuu ya kuwasilisha imani, maadili na mienendo ya Wakamba. Kwa hivyo, kimaudhui, jazanda zinazotumika katika nyimbo hizi za kiasili zinakuza na kuthabitisha akilini mwa hadhira ujumbe unaowasilishwa kitaswira. Kifani, jazanda zinasafidi lugha inayotumiwa kimaumbo katika nyimbo za kiasili na kwa njia hii kupunguza makali kihisia miongoni mwa hadhira. Aidha, utafiti umeonyesha kuwa matumizi ya jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba huibua picha ya dhana zinazorejelewa akilini mwa hadhira na hivyo kuimarisha kumbukumbu ya virejelewa na burudani. Kitaaluma, matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa vile yatakuza maarifa kuhusiana na uamilifu wa nyimbo za kiasili za Kikamba na fasihi simulizi ya jamii za Kiafrika kwa ujumla. Kijamii, utafiti ni hatua mojawapo ya kuhifadhi utamaduni na utambulisho wa jamii ya Wakamba. Kiuchumi, ni kichocheo kwa wasanii wa nyimbo za kiasili kutumia vipawa vyao kujipatia riziki. Kwa hivyo, utafiti huu unapendekeza kutekelezwa kwa Mwongozo wa Sera ya Kitaifa ya Muziki unaopendekeza wanamuziki na wasanii kwa ujumla wanufaike kikamilifu kutokana na kazi zao za kisanaa.

ABSTRACT

Folksongs are particularly significant in the Kamba community. Virtually every social ceremony is accompanied by a relevant folksong. These folksongs are a powerful means through which the Kamba people are able to communicate to their audience the community's ideology on pertinent issues. However, the ideology in the folksongs is usually presented metaphorically. The purpose of this study was to examine the ideological representations encapsulated in the metaphors deployed in the Kamba folksongs. The study's specific objectives were firstly, to establish the metaphors captured in the Kamba folksongs sung in specific social occasions. Secondly, to critically examine ideologies metaphorically depicted in the Kamba folksongs and thirdly, to evaluate the thematic and aesthetic functions of the metaphors in Kamba folksongs. This study employed a qualitative research design from a constructivist philosophical perspective particularly in analyzing metaphors and ideology in the Kamba folksongs as social constructs. This involved a critical analysis of the selected Kamba folksongs based on the Conceptual Metaphor Theory expounded by Lakoff & Johnson and the Ideology Theory as propagated by Van Dijk. The Conceptual Metaphor Theory was useful in deciphering the ideological relationship between the metaphors captured in the Kamba folksongs including their thematic and aesthetic function. On the other hand, Ideology Theory guided the explication of ideologies as basic frameworks of social cognition constituting socio-cultural values, worldviews and attitudes expressed through folksongs in social functions. The data for the study was derived from the Kamba folksongs purposefully sampled from *The Permanent Presidential Music Commission*. The data was critically analyzed as guided by the Conceptual Metaphor Theory where the Kamba folksongs are deciphered to relay ideological perspectives of the community while at the same time serving as a literally device that enhance the aesthetics of the songs to elicit humor in the audience. The findings reveal that Kamba folksongs are laden with metaphors that convey the community's ideology regarding pertinent socio-cultural and political issues. The metaphors convey values such as integrity among leaders, courage, hard work and fidelity in marriage as captured in the circumcision and marriage folksongs. Therefore, thematically, metaphors are used in the folksongs to cement the community's ideologies, values and virtues in the minds of the audience through analogies that elicit familiar images. Aesthetically, the study reveals that metaphors deployed in Kamba folksongs serve as euphemisms that elicit humor and laughter that not only entertain the audience but also provoke critical thinking regarding the veiled ideologies. From a sociological perspective, the study findings attest to the fact that African literature is laden with thematic and aesthetic functions and should be nurtured and preserved for posterity. The study is a motivation to folklore artists to harness their talents for economic empowerment. This study recommends full implementation of the National Music Policy Guidelines that recommend music producers and artists in general benefit from their creative works.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI	v
ABSTRACT.....	vi
YALIYOMO.....	vii
ORODHA YA VIELELEZO	xi
TAFSIRI YA ISTILAHU MUHIMU	xiii
VIFUPISHO.....	xiv
SURA YA KWANZA	1
MSINGI WA UTAFITI.....	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti	1
1.2 Suala la Utafiti	4
1.4 Maswali ya Utafiti.....	5
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....	6
1.6 Umuhimu wa Utafiti	7
1.7 Upeo wa Utafiti.....	8
SURA YA PILI.....	11
TAHAKIKI YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA.....	11
2.0 Utangulizi.....	11
2.1 Msingi wa Nadharia.....	11
2.1.1 Nadharia ya Jazanda Dhanifu.....	11
2.1.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Jazanda Dhanifu	14
2.1.1.2 Matumizi ya Nadharia ya Jazanda Dhanifu katika Utafiti	16
2.1.2 Nadharia ya Itikadi	19
2.1.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Itikadi	20
2.1.2.2 Matumizi ya Mihimili ya Nadharia ya Itikadi katika Utafiti.....	21
2.2 Tahakiki ya Maandishi Kuhusu Mada ya Utafiti.....	28
2.2.1 Mapitio ya Maandishi kuhusu Nyimbo za Kiasili.....	28
2.2.2 Mapitio ya Maandishi kuhusu Nyimbo za Kiasili za Kikamba	30
2.2.3 Mapitio ya Maandishi kuhusu Itikadi katika Fasihi	33

2.2.4 Mapitio ya Maandishi kuhusu Jazanda	36
2.2.5 Mapitio ya Maandishi kuhusu Jamii ya Wakamba	37
2.3 Hitimisho.....	40
SURA YA TATU.....	41
MBINU ZA UTAFITI.....	41
3.0 Utangulizi.....	41
3.1 Mkabala wa Utafiti	41
3.2 Eneo la Utafiti	41
3.2.1 Maktabani.....	41
3.3 Sampuli na Usampulishaji	42
3.4 Vifaa vya Kukusanya na Kuhifadhi Data	42
3.5 Uchanganuzi na Ufasiri wa Data	43
3.6 Upangaji na Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti.....	43
SURA YA NNE	45
JAZANDA KATIKA NYIMBO ZA KIASILI ZA KIKAMBA KWENYE	
HAFLA MBALIMBALI	45
4.0 Utangulizi.....	45
4.1 Upambanuzi wa Hafla Zinamoimbwa Nyimbo za Kiasili za Kikamba.....	45
4.1.1 Hafla Rasmi.....	46
4.1.1.1 <i>Syathi sya nzaiko</i> (Hafla za tohara)	47
4.1.1.2 <i>Syathi sya siasa</i> (Hafla za kisiasa).....	53
4.1.1.3 <i>Syathi sya kithaitho</i> (Hafla za kidini)	68
4.1.1.4 <i>Syathi sya mathiko</i> (Hafla za mazishi)	71
4.1.1.5 <i>Syathi sya mutwaano</i> (Hafla za ndoa)	75
4.1.1.6 <i>Syathi sya kusyawa kwa syana</i> (Hafla za kuzaliwa kwa watoto)	92
4.1.1.7 <i>Syathi sya wia wa ikundi</i> (Hafla za kazi za makundi ya watu).....	96
4.1.2 Hafla Zisizo Rasmi.....	101
4.1.2.1 <i>Syathi sya wia wa mundu umwe</i> (Hafla za kazi ya mtu mmoja)	102
4.1.2.2 <i>Syathi sya kuongola syana</i> (Hafla za kuwaongoa watoto).....	102
4.1.2.3 <i>Syathi sya unywi wa nzovi</i> (Hafla za ulevi)	104
4.1.2.4 <i>Syathi sya ithau ya syana</i> (Hafla za michezo ya watoto)	105
4.1.2.5 <i>Syathi sya uvithukii/kau</i> (Hafla ya mashambulizi/vita)	109
4.2 Uchanganuzi wa Jazanda katika Nyimbo za Kiasili za Kikamba.....	113
4.2.1 Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Tohara.....	114

4.2.2 Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Kazi	128
4.2.3 Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Kidini.....	135
4.2.4 Jazanda zinazojitokeza kwenye NKK zinazowasilishwa katika Hafla za Ndoa na Arusi	136
4.2.5. Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Kuzaliwa kwa Watoto	144
4.2.6 Jazanda zinazojitokeza kwenye NKK zinazowasilishwa katika Hafla za kisiasa	147
4.2.7 Jazanda zinazojitokeza kwenye NKK zinazowasilishwa katika Hafla za Mazishi	154
4.2.8 Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Michezo ya Watoto	158
4.2.9 Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Vita	159
4.3 Hitimisho.....	160
SURA YA TANO	162
UHAKIKI WA ITIKADI ZILIZOFUMBATWA KIJAZANDA KWENYE	
NYIMBO ZA KIASILI ZA KIKAMBA	162
5.0 Utangulizi.....	162
5.1 Itikadi Zilizofumbatwa Kijazanda katika Nyimbo za Kiasili za Kikamba	162
5.1.1 Itikadi kuhusu Tohara.....	163
5.1.2 Itikadi kuhusu Kazi	169
5.1.3 Itikadi kuhusu Dini.....	174
5.1.4 Itikadi kuhusu Ndoa na Mapenzi	177
5.1.5 Itikadi kuhusu Ubikira.....	182
5.1.6 Itikadi kuhusu Utamaduni	184
5.1.7 Itikadi kuhusu Malezi.....	189
5.1.8 Itikadi kuhusu Siasa na Uongozi	192
5.1.9 Itikadi kuhusu Utambulisho	197
5.1.10 Itikadi kuhusu Mauti	198
5.1.11 Itikadi kuhusu Ufisadi	201
5.2 Hitimisho.....	204
SURA YA SITA.....	205
UAMILIFU WA JAZANDA KIFANI NA KIMAUDHUI KWENYE NYIMBO	
ZA KIASILI ZA KIKAMBA	205
6.0 Utangulizi.....	205

6.1 Uamilifu wa Jazanda Mahsusi Kifani na Kimaudhui kwenye Nyimbo za Kiasili za Kikamba	205
6.1.1 Jazanda Hukuza Maana Inayowasilishwa	206
6.1.2 Jazanda Huimarisha kumbukumbu na Kuthabitisha Ujumbe	207
6.1.3 Jazanda Huimarisha Ujumi wa Lugha	208
6.1.4 Jazanda Hukuza Hisia	209
6.1.5 Jazanda Husitiri Ujumbe	209
6.1.6 Jazanda Hukuza Fikra za Kiuhakiki	211
6.1.7 Jazanda Hupanua maana ya Dhana	212
6.1.8 Jazanda na Uashiraji	212
6.1.9 Jazanda hutumika kama Tasfida	213
6.2 Hitimisho	214
SURA YA SABA	216
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	216
7.0 Utangulizi	216
7.1 Mutasari wa Matokeo ya Utafiti	216
7.2 Hitimisho	221
7.3 Mapendekezo ya Utafiti	222
MAREJELEO	223
VIAMBATISHO	229
Kiambatisho 1: Nakala za Nyimbo za Kiasili za Kikamba	229
Kiambatisho 2: Idhini ya Utafiti – PPMC	254
Kiambatisho 3: Cheti cha Kutozingatia Wizi (Anti-plagiarism)	255

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 2.1: Uhamishaji wa sifa za Uwanja Asilia A hadi Uwanja Lengwa B	14
Kielelezo 4.1: Fasiri ya Jazanda ya <i>Muti Mumu</i> (Mti uliokomaa).....	115
Kielelezo 4.2: Fasiri ya Jazanda ya Mbilano (Kazi)	116
Kielelezo 4.3: Fasiri ya Jazanda ya <i>Matila ma Kiimani</i> (Wajinga wa Milimani).....	117
Kielelezo 4.4: Fasiri ya Jazanda ya <i>Munyambu</i> (Simba).....	119
Kielelezo 4.5: Fasiri ya Jazanda ya <i>Ndiani</i> (Kidimbwini).....	120
Kielelezo 4.6: Fasiri ya Jazanda ya <i>Kaindo</i> (Kakitu)	122
Kielelezo 4.7: Fasiri ya Jazanda ya <i>Mwatu</i> (Mzinga).....	123
Kielelezo 4.8: Fasiri ya Jazanda ya <i>Nzuki Mbingi</i> (Nyuki Wengi).....	125
Kielelezo 4.9: Fasiri ya Jazanda ya <i>Uki</i> (Asali).....	126
Kielelezo 4.10: Fasiri ya Jazanda ya Ngaku (Aina ya mnyama anayewala Nyuki) ..	128
Kielelezo 4.11: Fasiri ya Jazanda ya <i>Tumikeve Twili</i> (Mikebe Miwili)	129
Kielelezo 4.12: Fasiri ya Jazanda za Kathungi (Kiondo), Kamulo (Jembe) na Kavelu (Mbegu)	131
Kielelezo 4.13: Fasiri ya Jazanda ya <i>Muundani</i> (Shambani).....	132
Kielelezo 4.14: Fasiri ya Jazanda ya <i>Ndeke</i> (Ndege).....	133
Kielelezo 4.15: Fasiri ya Jazanda ya Kavuli (Anayetwanga)	134
Kielelezo 4.16: Fasiri ya Jazanda ya <i>Ngima</i> (Ugali).....	135
Kielelezo 4.17: Fasiri ya Jazanda za <i>malenge</i> (Maboga), <i>Nzuu</i> (Mbaazi) na <i>Mboso</i> (Maharagwe)	136
Kielelezo 4.18: Fasiri ya Jazanda ya <i>Katanda</i> (Kitanda).....	138
Kielelezo 4.19: Fasiri ya Jazanda ya <i>Ngali</i> (Gari)	139
Kielelezo 4.20: Fasiri ya Jazanda ya <i>Sikala</i> (Sigara).....	140
Kielelezo 4.21: Fasiri ya Jazanda ya <i>Ngate</i> (Mikate)	142
Kielelezo 4.22: Fasiri ya Jazanda ya <i>Uki wa Ngilu</i> (Asali Mwitu).....	143
Kielelezo 4.23: Fasiri ya Jazanda ya <i>Mutunda</i> (Mtunda)	144
Kielelezo 4.24: Fasiri ya Jazanda ya <i>Kaindo</i> (Kijitu).....	145
Kielelezo 4.25: Fasiri ya Jazanda za <i>Mukwa</i> (Kamba Pana) na <i>Ikanda</i> (Kamba)	147
Kielelezo 4.26: Fasiri ya Jazanda ya <i>Kuthambya Nzele</i> (Uoshwaji wa Kata)	148
Kielelezo 4.27: Fasiri ya Jazanda ya <i>Nzele yi Kiko</i> (Kata Chafu)	149
Kielelezo 4.28: Fasiri ya Jazanda ya <i>Simba ii syi Ngunyuu</i> (Simba wenye Makucha)	151
Kielelezo 4.29: Fasiri ya Jazanda ya <i>Nzou</i> (Ndovu).....	152

Kielelezo 4.30: Fasiri ya Jazanda ya <i>Ng'ombe sya Mutavo</i> (Ng'ombe wa Wizi)	153
Kielelezo 4.31: Fasiri ya Jazanda ya <i>Kaletio</i> (Redio).....	154
Kielelezo 4.32:Fasiri ya Jazanda ya <i>Kivila</i> (Kiti)	155
Kielelezo 4.33: Fasiri ya Jazanda ya <i>Musyimi ute tei</i> (Mwindaji asiye na huruma)..	157
Kielelezo 4.34: Fasiri ya Jazanda ya <i>Muvutani ute tei</i> (mnyang'anyi asiyye na huruma)	158
Kielelezo 4.36: Fasiri ya Jazanda ya <i>Ng'ombe sya utuku</i> (Ng'ombe wa usiku).....	159
Kielelezo 4.37: Fasiri ya Jazanda ya Malenge matemangiwe (Maboga yaliyokatwakatwa).....	160

TAFSIRI YA ISTILAHU MUHIMU

- Aimu:*** Roho za mababu waliokwisha aga dunia.
- Akavi:*** Wavamizi Wamaasai walioshambuliana na jamii ya Wakamba mara kwa mara na kuibiana mifugo.
- Ilute:*** Fahali aliyehasiwa aliyechinjwa katika sherehe ya ndoa (*ntheo*).
- Kikonde:*** Sehemu ya nyama iliyoliwa na wanandoa watarajiwa katika sherehe ya *Ntheo* kama ishara ya kuidhinisha kwa uhusiano wao.
- Kilumi:*** Ni aina ya ngoma inayochezwa katika shughuli ya ibada kwenye jamii ya Wakamba hasa wanapoomba Mungu awape mvua au kuwaondolea majanga kama vile njaa, ukame na uvamizi miongoni mwa mengine.
- Kuuswa:*** Ni tambiko la utakaso katika jamii ya Wakamba.
- Mutaa:*** Aina ya mmea uliotumika katika tambiko la utakaso (*kuuswa*)
- Mwethya/Mwilaso:*** Kundi la wanajamii lililoundwa kwa nia ya kusaidiana kazi hasa za shambani kama vile kulima, kuvuna, miongoni mwa nyingine.
- Ngaku:*** Aina ya mnyama anayewaangamiza nyuki
- Nthele:*** Ni mwanaume ambaye amepitia sherehe ya tohara na kutiwa jandoni, ameo na ana watoto.
- Ntheo:*** Sherehe ya mwanzo ya ndoa katika jamii ya Wakamba
- Permanent Presidential Music Commission:*** Kamisheni ya kudumu ya Muziki ya Rais (PPMC) nchini Kenya. Inajihusisha na ukusanyaji na uhifadhi wa nyimbo kwenye hafla mbalimbali nchini Kenya.

VIFUPISHO

- NJD:** Nadharia ya Jazanda Dhanifu
- NKK:** Nyimbo za Kiasili za Kikamba
- PPMC:** Permanent Presidential Music Commission

SURA YA KWANZA

MSINGI WA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Utafiti huu unachunguza ufumbaji wa itikadi kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba zinazoimbwa kwenye hafla maalum. Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa njia ya tasnifu. Tasnifu yenyewe imegawika katika sura saba. Sura hii ya kwanza imepambanua msingi wa utafiti. Vipengee vinavyojadiliwa katika sura hii ni vifuatavyo: usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti.

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Kwa mujibu wa King'ei na Kisovi (2005) wimbo ni utungo ambao una mpangilio maalumu wa maneno na una mahadhi. Wimbo unaweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi cha watu na kuhusiana na suala maalum katika maisha ya jamii. Kimsingi, wimbo hujengwa kwa maneno na sauti ambayo hudhihirisha mahadhi au mapigo yanayoufanya uimbike.

Nyimbo zinaweza kuainishwa katika makundi mbalimbali kutegemea kipengee cha msingi kinachohimili muainisho huo. Mathalani tukizingatia dhima na ujumbe wa nyimbo tunaweza kugawa nyimbo katika makundi yafuatayo: bembembezi, nyiso, nyimbo za kazi, nyimbo za arusi, nyimbo za siasa, nyimbo za kidini, nyimbo za matanga au mbolezi, nyimbo za usasi na nyimbo za vita. Kwa upande mwingine, tukizingatia utendaji na uwasilishaji wa nyimbo tunapata nyimbo za kisasa na nyimbo za kiasili.

Akipambanua dhana ya wimbo wa kiasili, Wamitila (2008) anadai kwamba wimbo wa kiasili au jadiya ni aina ya wimbo unaopatikana katika fasihi simulizi za jamii

nyingi na hupokezanwa kwa njia ya mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Anasitiza kuwa nyimbo za kiasili huzungumzia masuala mbalimbali. Matei (2011) anakubaliana na Wamitila anaposema kwamba wimbo wa kiasili ni wimbo wa kitamaduni ambao unaimbwa na kupokezwa kwa mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Anaongezea kuwa nyimbo za kiasili kimsingi husimulia historia na utamaduni wa jamii husika.

Titon, akinukuliwa na Bauman (1992) anashikilia kuwa ujumbe wa wimbo wa kiasili hufasiriwa kutokana na muktadha ambamo wimbo huo unawasilishwa. Hii ni kwa sababu watu hujifunza nyimbo za kiasili kupitia uigaji na mifano badala ya maagizo rasmi au makala yaliyoandikwa. Titon anasisitiza kwamba nyimbo za kiasili husheheni tajriba za wanajamii ambazo huwasilishwa kwa hadhira kiusimulizi na kiutendaji. Ni kwa msingi huu ndipo nyimbo za kiasili zinahusishwa na hafla mahsusi za kijamii kwa kuwa huwasilishwa kwa wanajamii wakati wamekusanyika kwenye hafla au sherehe za kijamii. Titon anaongezea kuwa japo nyimbo za kiasili huwasilishwa kwa njia ya mdomo huku zikihifadhiwa akilini, zinaweza pia kuhifadhiwa kwenye kanda za sauti.

Cuddon (1991) anaeleza kuwa nyimbo za kiasili ni sehemu ya fasihi simulizi na utamaduni wa jamii inayohusika. Nyimbo hizi hutungwa na kuimbwa miongoni mwa wanajamii wanaoshiriki na kujitambulisha na imani na utamaduni maalum. Aidha, watunzi wa nyimbo hizi huchochewa na imani na lugha walizorithi kutoka kwa mababu zao na pia matukio yanayotendeka katika maisha yao halisi. Kwa kuwa nyimbo za kiasili huwasilishwa kwa njia ya mdomo, nyimbo hizi hubadilika kadri wakati unavyopita. Mabadiliko hudhihirika katika maumbo ya nyimbo, muktadha wa uwasilisho wazo na hata maudhui yanayowasilishwa kwenye nyimbo husika. Nyimbo

za kiasili huhusishwa na miktadha maalum ya kijamii kwa kuwa kiasili hukusudiwa mawasiliano ya ana kwa ana ambapo m(wa)imbaji hutagusana na hadhira lengwa.

Nyimbo za kiasili za Kikamba zikiwa mojawapo ya vipera vya fasihi simulizi ya jamii ya Wakamba ni hazina kubwa kifani na kimaudhui. Matumizi ya lugha, mbinu za kisanaa zinazotumika na maudhui katika nyimbo hizi ni vipengele vinavyozifanya kuwa chemichemi ya burudani na maarifa kwa wanajamii. Wasanii hutumia NKK kuiburudisha na kueleleisha jamii kuhusu masuala mbalimbali kuhusiana na jamii ya Wakamba yakiwemo: maadili na tabia njema, historia, itikadi na utambulisho wa utamaduni wa jamii ya Wakamba kwa ujumla.

Nyimbo za kiasili za kikamba huambatana na hafla mahsusi za kijamii. Nyimbo hizi zina ukwasi wa kipekee kifani na kimaudhui. Takriban kila shughuli miongoni mwa Wakamba huambatana na nyimbo maalum za kiasili. Mathalan kuna NKK zinazoimbwa katika sherehe za kuzaliwa kwa mtoto na kupewa jina, mikutano ya kisiasa kama kutawazwa kwa kiongozi, shughuli za kidini, sherehe za mazishi, sherehe za jando na hata sherehe za harusi.

Jamii ya Wakamba kama zilivyo jamii zingine zozote hai imo katika mpito na inabadilika kila uchao. Hata hivyo, nyimbo za kiasili ni kipera cha fasihi simulizi katika jamii ya Wakamba ambacho kimeendelea kutamalaki katika maisha ya kila siku tangu jadi. Kushamiri kwa nyimbo hizi za kiasili kunaashiria thamani ambayo inawekwa kwenye kipera hiki cha fasihi simulizi miongoni mwa Wakamaba. NKK hutekeleza dhima mbalimbali miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, nyimbo hizi ni nyenzo kuu ya kutoa burudani, kuelimisha jamii kuhusu masuala anuai na kuwasilisha historia na itikadi ya jamii ya Wakamba.

Kikiwa mojawapo ya vipengele vya maudhui katika fasihi, itikadi ni dhana ambayo hufumbatwa kifani katika tungo za kifasihi. Mojawapo ya vipengele vya fani ambavyo vinaelekea kufumbata itikadi katika nyimbo za kiasili za Kikamba ni jazanda. Nyimbo za kiasili za Kikamba zinatumia lugha ambayo imejaa jazanda ambazo zinatumiwa maksudi kuwasilisha ujumbe maalum zikiwemo itikadi mahsusi katika jamii ya Wakamba.

Dhima kuu ya lugha ni kufanikisha mawasiliano baina ya mzungumzaji na hadhira lengwa. Kwa hivyo, watunzi na waimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba hulenga kufikisha ujumbe mahsusi kwa hadhira lengwa wanapotumia lugha ya kijazanda. Utafiti huu ulikusudia kuchanganua jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba ili kudhihirisha itikadi zilizofumbatwa.

Utafiti wenyewe unachukulia itikadi kuwa kipengee muhimu na cha msingi ambacho kinaathiri namna nyimbo za kiasili za Kikamba zinatungwa na kuwasilishwa katika miktadha mbalimbali. Aghalabu itikadi katika NKK ni dhana ambayo imefumbatwa kijazanda. Kwa hivyo, ufumbuzi wa itikadi katika nyimbo za kiasili za Kikamba huhitaji mtu mwenye umilisi wa lugha na utamaduni wa jamii ya Wakamba. Mtafiti ni mzaliwa wa jamii ya Wakamba na kwa hivyo ana umilisi wa lugha na utamaduni wa Wakamba unaomwezesha kubaini jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba na kutathmini itikadi zinazofumbatwa katika jazanda hizo.

1.2 Suala la Utafiti

Japo itikadi ni kipengee ambacho huongoza shughuli mbalimbali za jamii yoyote ile, tafiti chache sana zimechunguza namna itikadi inawasilishwa katika tanzu mahsusi za fasihi simulizi na hasa katika nyimbo za kiasili. Mtunzi wa NKK hutawaliwa na itikadi maalum ambayo hufumbata mwonoulimwengu wake kutokana na lugha na

mbinu za kisanaa anazotumia kutunga nyimbo maalum. Hili ni pengo la kiutafiti ambalo utafiti ulikusudia kuliziba kwa kuchunguza matumizi ya jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba na namna jazanda hizo zinasitiri itikadi zinazoambatana na hafla mbalimbali za kijamii. Kwa hivyo utafiti huu unadhihirisha uamilifu wa jazanda kifani na kimaudhui katika nyimbo za kiasili za Kikamba.

1.3 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza ufumbaji wa itikadi kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Kulifikia lengo hili, mtafiti aliongozwa na malengo maalum yafuatayo:

- i) Kupambanua jazanda zinazotumika katika nyimbo za kiasili za Kikamba zinazoimbwa kwenye hafla maalum.
- ii) Kuhakiki itikadi za Wakamba zinazofumbatwa katika jazanda zinazotumika kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba.
- iii) Kutathmini uamilifu wa jazanda mahsusi kifani na kimaudhui kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

- i) Ni jazanda gani zinatumika katika nyimbo za kiasili za Kikamba zinazoimbwa katika hafla za kijamii?
- ii) Ni itikadi zipi za Wakamba zinafumbatwa katika jazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba?
- iii) Jazanda zinazotumika kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba zinatekeleza dhima gani kifani na kimaudhui?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Uchaguzi wa mada hii ya utafiti umetokana na sababu mbalimbali. Kwanza, kipera cha wimbo na hasa nyimbo za kiasili kinapewa umuhimu mkubwa na jamii ya Wakamba. Hata hivyo, nyimbo hizi husheheni jazanda nyingi ambazo mtafiti alifikiria huenda zinafumbata ujumbe maalum ikiwemo itikadi za jamii ya Wakamba. Kwa hivyo, mada hii ilichochea na imani kuwa lugha hutumiwa ili kufanikisha mawasiliano kati ya mwimbaji na msikilizaji. Mawasiliano nayo hutokea iwapo msikilizaji ataelewa alichowasilisha mwimbaji. Ujumbe wa mwimbaji sharti umfikie msikilizaji bila utata wowote. Waimbaji wa NKK huwasilisha yaliyomo kwa njia ya ufumbaji wa kijazanda. Uchunguzi huu unabainisha jinsi waimbaji wa NKK wanavyotumia fani ya ufumbaji wa kijazanda katika kuwasilisha itikadi mbalimbali za Wakamba. Ufumbaji kijazanda kama mbinu ya kuwasilisha itikadi za jamii ya Wakamba katika NKK ni suala ambalo halikuwa limechunguzwa na watafiti watangulizi. Watafiti wengi walioshughulikia NKK wameegemea zaidi mabadiliko kimaudhui kama inavyojitokeza katika tafiti za Musembi (2016) na Wathome (2009). Kwa hivyo, utafiti huu umeliziba pengo hili la maarifa.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ya utafiti ni kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba ni maarufu sana miongoni mwa Wakamba. Hata hivyo, NKK kwa kawaida husheheni jazanda nyingi ambazo huenda zimefumbata ujumbe ambao huenda ukapotea iwapo fasiri muafaka ya jazanda husika haitatolewa. Mtafiti ni mmilisi mzaliwa wa Kikamba na kwa hivyo aliweza kutoa fasiri faafu ya jazanda kwenye NKK. Kwa vile nyimbo hizi ni nyenzo ya kuwasiliana na hadhira mbali na kuiburudisha, utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo kuna itikadi maalum ambazo zimefumbatwa kijazanda. Kwa hivyo, mtafiti aliamua kuzitafitia nyimbo za kiasili za Kikamba ili kwanza kupambanua jazanda zinazotumika kwenye nyimbo hizo. Pili,

kubainisha itikadi inayofumbatwa katika jazanda hizo na tatu kutathmini misingi ya kutumia jazanda hizo katika nyimbo za kiasili za Kikamba kwenye hafla mbalimbali za Wakamba.

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umejishughulisha na ufumbaji wa itikadi kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Utafiti wenyewe umegundua kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba huwasilishwa kijazanda ambapo jazanda zenyewe hufumbata itikadi mbalimbali za jamii ya Wakamba. Baadhi ya itikadi zinazowasilishwa kijazanda kupitia nyimbo teule zinahusiana na masuala ya ndoa na ubikira, tohara, dini, uhai na mauti, kazi na uchumi wa mali na utamaduni wa jamii ya Wakamba kwa ujumla. Baadhi ya jazanda zilizofumbata itikadi ya Wakamba kwenye nyimbo teule ni pamoja na *Mukwa* (Kamba pana), *Ndeke* (ndege), *Nzele* (kata), *Kivila* (kiti), *Ng'ombe sya Mutavo* (ng'ombe wa wizi), *Sikala* (sigara), *Ngima* (ugali), *Mwatu* (mzinga) na *Nzou* (Ndovu) kati ya nyingine.

Matokeo ya utafiti huu ni ya manufaa kwa watunzi na waimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba kwa kuwa itikadi iliyofumbatwa katika jazanda zinazotumika katika nyimbo maalum zimefumbuliwa. Vilevile, kupitia utafiti huu baadhi ya watunzi wa nyimbo hizi wataweza kubaini uhusiano uliopo kati ya hafla maalum na itikadi za nyimbo za kiasili za Kikamba. Hili litawasaidia watunzi hawa kufahamu kwamba utunzi wa nyimbo za kiasili za Kikamba hauhusishi tu upazaji wa sauti bali pia huhusisha uteuzi wa jazanda mwafaka katika ujengaji wa itikadi mbalimbali kwenye jamii inayohusika.

Zaidi ya hayo, utafiti huu unachangia pakubwa katika mitaala ya elimu nchini Kenya. Nyimbo za kiasili ni miongoni mwa maarifa ya kiasili yanayopaswa kufundishwa

kupitia mtalaa mpya wa C.B.C. Kwa hivyo, maarifa yanayotokana na utafiti huu yatakuwa na mchango mkubwa katika kubainisha baadhi ya vipengee vya kuzingatiwa katika utunzi na uwasilishaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba. Miongoni mwa vipengee hivi ni uteuzi wa jazanda mwafaka katika kuwasilisha itikadi kwenye nyimbo za kiasili. Hivyo, vipengee hivi vinaweza kuzingatiwa na wadau wa wizara ya elimu kama vigezo vya kutathmini uwasilishaji wa nyimbo hizi kwenye tamasha na shughuli mbalimbali za kimtaala.

Matokeo ya utafiti huu ni hazina kubwa katika taaluma za lugha na fasihi ya Kiswahili. Wataalam wa fasihi simulizi, fasihi linganishi na tafsiri wanaweza kurejelea tasnifu hii kuendeleza tafiti katika maeneo yao mahsusi. Uchunguzi huu umefanywa na kuwasilishwa kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo, matokeo yake ni nyongeza katika fasihi ya Kiswahili. Tafsiri ya nyimbo hizi katika Kiswahili ni njia mojawapo ya kuikuza fasihi simulizi ya Kiswahili. Vilevile, maarifa haya ni chemichemi ya fasihi linganishi ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika. Pamoja na hayo, fasihi ya Kikamba imenufaika kwa maana uchunguzi wenyewe unahusu kipera mojawapo cha fasihi ya Kikamba.

Tasnifu hii ni rejeleo muhimu kwa wasomi na wataalam mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili na ya Kikamba. Hivyo, utafiti huu utakuwa na umuhimu wa kutumika kama rejeleo muhimu katika tafiti za baadaye kuhusiana na nyimbo za kiasili.

1.7 Upeo wa Utafiti

Utanzu wa fasihi simulizi unahusisha vipera vingi vikiwemo ngano, nyimbo, hadithi, methali, maigizo, majigambo na ushairi miongoni mwa vingine. Hivyo, fasihi simulizi ni uwanja mpana. Kwa mujibu wa utafiti huu, tanzu nyinginezo za fasihi simulizi hazikuzingatiwa ila kipengee cha nyimbo pekee. Utanzu wa nyimbo nao unahusisha

aina na vipera mbalimbali kutegemea kipengee kinachoangaziwa. Kwa mfano, kwa kuzingatia kipengee cha jamii lugha inayohusika, tunapata nyimbo za Kiswahili, nyimbo za Kidholuo, nyimbo za Kitaita, Nyimbo za Kidigo na nyimbo za Kikamba miongoni mwa nyingine. Vilevile, kutegemea kipengee cha namna ya utendaji na uwasilishaji, tunapata nyimbo za kiasili na nyimbo za kisasa. Kwa mujibu wa utafiti huu, nyimbo za kiasili za Kikamba tu ndizo ziliangaziwa. Mtafiti aliangazia Nyimbo za Kiasili za Kikamba kwa sababu zinawasilishwa kwa lugha ya Kikamba ambayo anailewa na hivyo ana nafasi nzuri ya kufasiri itikadi na masuala yanayowasilishwa katika nyimbo husika.

Pamoja na hayo, uchunguzi wa kifasihi ukiwemo wa nyimbo za kiasili za Kikamba unaweza kuhusisha vipengee mbalimbali vya kimaudhui na kifani. Vipengee vyenyewe ni kama vile utendaji, uhalisia, mazingaombwe, usimulizi, itikadi, methali, na ufumbaji miongoni mwa vipengee vingine. Kifani, utafiti huu ulijihusisha tu na ufumbaji kupitia kwa jazanda na kimaudhui uliangazia suala la itikadi kwa mujibu wa NKK.

Kuhusu msingi wa data, utafiti ulijikita kwenye data ya pili yaani iliyohifadhiwa kwenye makavazi. Hii ni kwa sababu lengo kuu lilikuwa kuhakiki dhima ya jazanda kikiwa kipengele cha fani kwenye NKK na uwasilishaji wa zinavyowasilisha itikadi kikiwa kipengele cha maudhui katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Kwa hivyo, uhakiki wa jazanda kwenye NKK katika utafiti huu ni wa kimsamiati na kiumbuji zaidi. Suala utendaji wa NKK katika utafiti huu ulizingatiwa tu pale ambapo ufasiri wa itikadi katika jazanda mahsusi ulihusishwa na muktadha wa kijamii ambamo NKK zilitokea. Hivyo, utafiti huu umeshughulikia ufumbaji wa itikadi kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba zinazowasilishwa kwenye hafla maalum.

Kupitia uchunguzi wenyewe, itikadi mbalimbali zilizofumbatwa kijazanda zimechunguzwa na kuwekwa wazi.

SURA YA PILI

TAHAKIKI YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.0 Utangulizi

Sura hii inahusu tahakiki ya maandishi na ufafanuzi wa nadharia zilizoongoza utafiti huu. Tahakiki ya maandishi yanayohusiana na jamii ya Wakamba, nyimbo za kiasili za Kikamba pamoja na tafiti na maandishi kuhusu itikadi katika fasihi yamezingatiwa.

2.1 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili. Hizi ni pamoja na Nadharia ya Itikadi kwa mujibu wa Van Dijk (1998) pamoja na ile ya Jazanda Dhanifu kulingana na Kovecses (2002). Nadharia mbili zimetumika kwa sababu hakuna nadharia moja inayojitosheleza katika kuyafikia malengo yote ya utafiti huu kivyake. Kwa hivyo, nadharia zote mbili zimechangia katika kuyafikia malengo ya utafiti.

2.1.1 Nadharia ya Jazanda Dhanifu

Nadharia ya Jazanda Dhanifu ilielekeza uhakiki wa itikadi zilizofumbatwa kijazanda na uamilifu wa jazanda hizo kifani na kimaudhui katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Nadharia hii huegemezwa kwenye mawazo ya George Lakoff na Mark Johnson (1980). Nadharia hii inachukulia jazanda kuwa mchakato wa kiakili ambapo uwanja mmoja wa ufahamu (B) unaeleweka kwa misingi ya uwanja mwingine (A). Kovecses (2002), anaeleza kuwa jazanda huwa na uwanja asilia (A) na uwanja lengwa (B). Uwanja asilia unahusisha vitu vinavyoweza kuonekana na kushikika huku uwanja lengwa ukihusisha vitu dhahania kwa kiasi fulani. Kwa hivyo, jazanda ni mfumo wa lugha ya kiishara ambapo uhusiano wa moja kwa moja hufanyika kati ya vitu viwili tofauti vilivyo na mfanano fulani. Katika jazanda, kitengo fulani hueleweka kwa misingi ya kitengo kingine. Uchunguzi na uchanganuzi wa jazanda huhusishwa na mwanafalsafa wa Kigiriki Aristotle (383-K.K-322 K.K). Aristotle,

akirejelewa na Lan Chun (2003), anaeleza kuwa jazanda ni ‘kule kupatia kitu jina la kitu kingine, ambapo uhamishaji huo huhusisha sifa zenye mahusiano’. Richard I.A. (1936) anaeleza kwamba maelezo ya kijazanda katika lugha huwa ni dhana mbili katika moja. Hivyo, jazanda sio kitu cha kiisimu tu bali pia ni namna ya kufikiria. Kulingana na Lakoff na Johnson (1980), jazanda ni kitu dhanifu kinachohusishwa na mienendo na fikra za watu. Kulingana nao, jazanda sio lugha tu, bali pia ni mchakato wa kufikiria. Kwa kuzingatia mtazamo wa Isimu Tambuzi, jazanda inaelezwa kama ufafanuzi wa uwanja dhanifu mmoja kwa kurejelea uwanja dhanifu mwingine. Naye Kovecses (2002), anaeleza kwamba ufasiri wa jazanda unahusisha kufafanua uwanja dhanifu lengwa (B) kwa kurejelea uwanja dhanifu asilia (A). Mtaalamu huyu anairejelea hii kama jazanda dhanifu. Kovecses (keshatajwa), anaziainisha jazanda dhanifu katika makundi matatu yafuatayo:

i) Jazanda za Kimaumbo

Jazanda za kimaumbo ni aina za jazanda ambazo katika ufafanuzi wake, uwanja asilia (A) hutoa ufahamu mkubwa wa kimsingi kwa uwanja lengwa (B). Ni mfumo wa kijazanda ambao kwake, dhana moja changamani au dhahania huwasilishwa kupitia dhana nyingine inayoeleweka zaidi. Kwa mfano ‘Biashara ni mapigano’. Kutokana na mfano huu, dhana *mapigano* inachukuliwa kuwa uwanja asilia (A) unaotoa sifa mbalimbali zinazohamishwa katika uwanja lengwa (B), *Biashara*. Hapa, biashara inalinganishwa na mapigano. Kutokana na dhana ya mapigano, mahusiano kati ya vipengee mbalimbali vya kiuchumi yanadhihirika. Kwa mfano, biashara inalinganishwa na mapigano, uchumi unahusishwa na uwanja wa mapigano, wafanyi biashara nao wanahusishwa na wapiganaji vita, huku mapigano yakihusishwa na dhana za *mashambulizi* na *kinga/ulinzi*. Hivyo, ulinzi/mashambulizi yanayofaulu husababisha *ushindi* na kinyume chake.

ii) Jazanda za Kiontolojia

Jazanda za kiontolojia nazo ni zile zinazosaidia katika kupanga ufahamu wa dhana zisizoweza kugusika, zisizoonekana wala kuzoeleka pamoja na matukio na matendo mbalimbali. Ufahamu wa dhana hizo hupatikana kwa kulinganisha dhana husika na uzoefu wetu halisi pamoja na vitu vinavyopatikana katika mazingira tuliyomo. Ni namna inayotuwezesha kuona matukio, matendo, hisia, mawazo, n.k. kama vitu halisi. Kwa mfano, ‘Maisha yamemdaganya’, ‘Kifo kimemkondolea macho’. Maisha na kifo sio vitu vilivyo na uhai. Hata hivyo, vitu hivi vimehuishwa kwa kupewa uwezo wa kibinadamu kama vile wa kudaganya na kukodoleana macho mtawalia. Tunapovipa vitu visivyokuwa na uhai uwezo huo wa kuwa hai, ni njia moja ya kusaidia kuvielewa vyema vitu hivyo

iii) Jazanda Elekezi

Jazanda Elekezi ni aina za jazanda ambazo huwezesha kundi la dhana lengwa kufafanulika kwa ufasaha kwenye mfumo wa kiakili wa mhusika. Ni mbinu ya kisanaa inayopanga mfumo wote wa dhana kwa mujibu wa namna zinavyohusiana. Jazanda hizi huhusiana na maelekezo ya anga kama vile juu-chini, ndani-nje, mbele-nyuma. Kwa mfano, dhana zifuatazo zimepangwa kwa mahusiano ya juu-chini:


Afya bora ni juu, ugonjwa ni chini
Wingi ni juu, uchache ni chini
Ufahamu ni juu, ukosefu wa ufahamu ni chini
Furaha ni juu, huzuni ni chini
Utajiri ni juu, ufukara ni chini

Hapa, maelekezo ya juu yanalandana na tathmini chanya huku yale ya chini yakihusiana na tathmini hasi. Kovecses (2002) anaeleza kwamba dhima ya jazanda hizi ni kurahisisha uelewa wa uwanja lengwa (B) kwa kuzingatia umbo la uwanja asilia (A). Kovecses anaendelea kueleza kwamba upo uhamishaji kati ya nyanja hizo mbili; Asilia na Lengwa. Hivyo, jazanda sio tu mfanano kati ya maana wazi na maana

fiche bali pia huhusisha jinsi ya kuunda maana kwa kuhamisha ujumbe kutoka kwa kitengo kimoja cha kiakili hadi kwenye kitengo kingine cha kiakili. Kwa hivyo, uundaji wa maana ya jazanda huhusisha kuhamisha sifa fulani za uwanja asilia hadi kwenye uwanja lengwa. Tazama mchoro ufuatao:

Uwanja Lengwa B

Uwanja Asilia A



Kielelezo 2.1: Uhamishaji wa sifa za Uwanja Asilia A hadi Uwanja Lengwa B

Kwa hivyo, kutokana na mchoro na maelezo yaliyopo hapo juu, jazanda ni mbinu ya kisanaa inayohusisha hali ya kulinganisha vitu viwili moja kwa moja bila kutumia viunganishi. Hapa, jina linalotumika hurejelea kitu kingine kilicho na sifa fulani sawa na hicho. Nyimbo za kiasili za Kikamba husheheni jazanda mbalimbali. Jazanda hizi hubeba ujumbe fiche. Hivyo, msikilizaji wa nyimbo hizi huhitaji ufahamu wa hali ya juu ili kuweza kufumbua itikadi zinazofumbika kwenye nyimbo teule kijazanda. Hivi ni sawa na kusema kwamba inawezekana mtu akazisikiliza nyimbo husika zikiwasilishwa bila ya kuuelewa ujumbe uliomo. Hii ni kwa sababu mara nyingi lugha inayotumika huwa ya kimapumbo mno. Utafiti huu umejikusisha na ufumbaji wa itikadi kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Uchunguzi wenyewe umefumbua jazanda zilizomo kwenye nyimbo husika ili kudhihirisha itikadi mbalimbali zinazopitishwa mle.

2.1.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Jazanda Dhanifu

Nadharia ya Jazanda Dhanifu hufafanua jazanda kama kipengee cha lugha ambacho kwake uwanja mmoja wa kiakili huonekana kupitia kwa uwanja mwingine kutokana

na athari za kitamathali. Hata hivyo, nadharia ya Jazanda dhanifu ina mikabala mbalimbali iliyotoholewa kutokana na mtazamo huu. Nadharia hii hufafanua maana za jazanda kwa kutumia misingi mitatu ifuatayo:

i). Ukawaida wa Jazanda

Mhimili huu unashikilia kwamba daima matumizi ya jazanda hujikita kwenye aina mbalimbali za matumizi ya lugha. Aina hizi ni pamoja na matumizi ya lugha kifasihi na lugha ya mazungumzo ya kawaida ya kila siku. Hivyo, matumizi ya lugha ya kijazanda huzoeleka na watumiaji wa lugha inayohusika. Kwa hivyo, uzoefu wa maelezo ya kijazanda huimarisha maana za kimsingi katika akili za wazungumzaji wa lugha yoyote inayohusika.

ii). Umbo Dhanifu la Jazanda

Mhimili huu unashikilia kwamba jazanda ni tukio la lugha linalotumia maneno ili kuwasilisha maana. Vilevile, mhimili huu unadai kwamba jazanda hushirikisha hatua za kiakili au kiutambuzi zinazohusisha mfumo dhanifu kwenye ubongo wa mzungumzaji wa lugha. Hivyo, jazanda si kifaa cha lugha kinachohusisha maana iliyo wazi tu, bali pia ni kifaa cha utambuzi kinachohusisha maana fiche. Hivyo, utambuzi ni muhimu sana katika kuelewa maana ya kitu fulani kupitia kwa kukielewa kingine. Hivi ni sawa na kusema kwamba, katika kuzifasiri jazanda, mfasiri anahamisha sifa za Uwanja asilia (A) anaoufahamu, hadi katika Uwanja lengwa (B) asioufahamu, ili kuelewa maana iliyokusudiwa. Basi, hili linadhihirisha kwamba mfumo dhanifu wa binadamu ni wa kijazanda.

iii). Uhusiano wa Jazanda na Tajriba halisi za Wazungumzaji wa Lugha

Mhimili huu unaeleza kwamba ufasiri wa jazanda unahusisha kuelewa uzoefu halisi pamoja na mifumo ya kimwili na mielekeo ya mtumiaji wa lugha anayehusika. Hivyo,

hoja zinazolengwa hazigusiki, hazijazoeleka na wala hazionekani moja kwa moja. Kwa upande mwingine, hoja asilia huweza kugusika, kuonekana au hata zimezoeleka na mtumiaji wa lugha anayehusika. Haya ni kwa mujibu wa Lakoff & Johnson, (1987). Hivyo, ikifahamika kwamba maumbo dhanifu katika ubongo wa binadamu ni ya kijazanda, basi ufahamu dhanifu hutegemea hali ya maumbile yetu. Anderson (2003) aliirejelea hali hii kama ‘uzoefu wa kimwili’. Kwa hivyo, uundaji, ufasiri na uelewaji wa jazanda huhusisha mchakato huohuo wa kiutambuzi pamoja na uhamishaji wa maana kwa mujibu wa maarifa ya kimsingi ya kila siku kuhusiana na mazingira yanayohusika.

2.1.1.2 Matumizi ya Nadharia ya Jazanda Dhanifu katika Utafiti

Nadharia hii ya Jazanda Dhanifu inajihusisha na namna ya kufasiri jazanda mbalimbali ili kupata maana iliyokusudiwa. Hivyo, nadharia yenyewe imeuongoza utafiti huu katika kufumbua itikadi zilizofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Kwa mujibu wa utafiti huu, mihimili ya nadharia ya jazanda dhanifu imetumika kama ifuatavyo:

i). Ukawaida wa Jazanda

Mhimili huu unashikilia kwamba matumizi ya jazanda hujikita kwenye aina mbalimbali za matumizi ya lugha ambapo matumizi ya lugha kijazanda huzoeleka na watumiaji wa lugha inayohusika. Hali hii inadhihirika katika wimbo wa kiasili wa Kikamba *Usumbi ni Nzou* (Urais ni Ndovu). Wimbo wenyewe unasheheni muktadha wa uwindaji wa ndovu katika jamii ya Wakamba. Katika jamii ya Wakamba, imezoeleka kwamba wawindaji wa ndovu hawafai kwenda na mbwa mawindoni. Hii ni kwa sababu **kelele za mbwa** huenda zikawazuia kulipata window lao. Hata hivyo, wawindaji wenyewe hutarajiwa kumnyemelea mnyama husika kwa uangalifu na umakinifu mkubwa ili wampate. Kelele za mbwa hapa zimetumika kama ishara ya

vita vya wenyewe kwa wenyewe. Aidha, matumizi ya jazanda hii yanawasilisha ujumbe kwamba kelele za vyura havimzuii ng'ombe kunywa maji. Hivyo, mwimbaji wa wimbo *Usumbi ni nzou* (Urais ni **ndovu**) ameutumia uzoefu wake wa maarifa ya uwindaji kuteua jazanda zinazoulinganisha urais na ndovu. *Usumbi ni nzou* (urais ni **ndovu**) ni jazanda inayokilinganisha cheo cha urais na tembo. Jazanda hii imefumbata itikadi ya siasa na uongozi kwamba wangombeaji wa nyadhifa mbalimbali hawana budi kuwa makini na waangalifu katika shughuli zao. Pia, jazanda ya *Nzou* (ndovu) inaendeleza itikadi ya uongozi kwamba uongozi si rahisi. Yaani, uongozi unamhitaji kiongozi mkakamavu, mstahimilivu na mwenye subira asiyevejika moyo kwa haraka. Hii ni kwa sababu uongozi hasa wa kisiasa huandamana na changamoto anuwai ambazo zinamhitaji mhusika atakayekabiliana nazo pasipo kujuta wala kushindwa.

ii). Umbo Dhanifu la Jazanda

Mhimili huu unashikilia kwamba jazanda ni tukio la lugha linalotumia maneno ili kuwasilisha maana. Vilevile, mhimili huu unadai kwamba jazanda hushirikisha hatua za kiakili au kiutambuzi zinazohusisha mfumo dhanifu kwenye ubongo wa mzungumzaji wa lugha. Hivyo, jazanda si kifaa cha lugha kinachohusisha maana iliyo wazi tu, bali pia ni kifaa cha utambuzi kinachohusisha maana fiche. Hivyo, utambuzi ni muhimu sana katika kuelewa maana ya kitu fulani kupitia kwa kukielewa kingine. Hivi ni sawa na kusema kwamba, katika kuzifasiri jazanda, mfasiri anahamisha sifa za Uwanja asilia (A) anaoufahamu, hadi katika Uwanja lengwa (B) asioufahamu, ili kuelewa maana iliyokusudiwa. Basi, hili linadhihirisha kwamba mfumo dhanifu wa binadamu ni wa kijazanda. Kwa mfano, *mbande mutunda* (nipande **mtunda**) ni jazanda inayohusisha nyanja mbili ambazo ni **mutunda** (**mtunda**) kama Uwanja dhanifu asilia (A) na **mavatano** (**mapatano**) kama uwanja dhanifu lengwa (B).

Mtunda ni mti unaozaa matunda. Hivyo, unapoupanda huwa ni ishara ya mazao na matumaini mapya. Kwa hivyo, neno mtunda limetumika kijazanda kurejelea matumaini ya kufanikiwa kindoa. Hapa, itikadi ya ndoa inapitishwa kwamba ni muhimu kuwa na makubaliano na matumaini ya kuendelea kindoa hata baada ya kukumbwa na changamoto za kindoa. Kwa hivyo, changamoto zinazozikumba ndoa nyingi si mwisho wake, bali zinafaa kuwa mwanzo wa kufanikiwa kwake. Aidha, kukatika kwa mwiko si mwisho wa kupika ugali. Hivyo, uwanja dhanifu lengwa unafafanuliwa kupitia kwa kuuelewa uwanja dhanifu asilia. Iwapo uwanja dhanifu asilia haufahamiki na mfasiri wa jazanda hii, basi itakuwa vigumu kuielewa jazanda hiyo. Hivi ni kumaanisha kwamba iwapo mhusika anaelewa maana ya mtunda, basi itakuwa rahisi kwake kuelewa namna mtunda (mti unaozaa matunda) unavyolinganishwa na mapatano kati ya wanandoa na hatimaye kuifahamu itikadi iliyofumbatwa kijazanda kwenye wimbo teule.

iii). Uhusishaji wa Jazanda na Tajriba za Wazungumzaji wa Lugha

Mhimili huu unaeleza kwamba ufasiri wa jazanda unahusisha kuelewa uzoefu halisi pamoja na mifumo ya kimwili na mielekeo ya mtumiaji wa lugha anayehusika. Hivyo, uundaji, ufasiri na uelewekaji wa jazanda huhusisha mchakato wa kiutambuzi pamoja na uhamishaji wa maana kwa mujibu wa maarifa ya kimsingi ya kila siku kuhusiana na mazingira yanayohusika. Kwa mfano, kutokana na maarifa ya kimsingi pamoja na tajriba za Wakamba, ni mazoea kwamba *nzele* (kata) hutumika katika kazi mbalimbali jikoni. Kwa mfano, kata hutumiwa katika kupakulia chakula, kunywa uji na kuchotea maji kwenye mtungi miongoni mwa matumizi mengine. Baada ya matumizi, kata hiyo hiyo huchafuka na kuhitaji kusafishwa ili iwe tayari kwa matumizi mengine. Ni katika hali hii ya kuoshwa ambapo neno **nzele (kata)** limetumika kijazanda katika wimbo *Nzambi akithambya Nzele* (Nzambi akiosha kata). Hapa, jina **Nzambi**

limetumika kama ishara ya kiongozi mpya aliyeteuliwa na wanajamii. Vilevile, neno **kata** limetumika kwa kulinganishwa na wadhifa unaomilikiwa na kiongozi mpya mteule. Hivyo, **uchafu** ulio kwenye kata unalinganishwa na **ufisadi**. Ujumbe unaopitishwa hapa ni kwamba kiongozi huyu mpya yumo katika hali ya kuuondoa **ufisadi** uliotekelezwa na viongozi tangulizi. Hivyo, wanajamii wanaombwa wawe na subira kwa maana bila shaka kazi yake itaanza kuonekana. Kutokana na maelezo hayo, mwimbaji anapitisha itikadi ya siasa na uongozi kwamba ni muhimu viongozi wajiepushe na matendo na matukio ya ufasidi.

Kwa mujibu wa utafiti huu, mihimili yote mitatu imetumika katika kuchunguza namna jazanda zinafumbata itikadi ya Wakamba katika NKK. Hivyo, mihimili ya nadharia ya Jazanda Dhanifu imetumika katika kulifikia lengo la pili na lengo la tatu katika utafiti huu.

2.1.2 Nadharia ya Itikadi

Nadharia ya Itikadi imeuongoza utafiti huu katika kupambanua maumbo ya kimsingi ya utambuzi wa kijamii yalivyodhihirika katika hafla za kijamii ambamo nyimbo za kiasili za Kikamba hutokea. Dhana ya itikadi imefafanuliwa na wataalam mbalimbali akiwemo Vincent (1992), anayeeleza kuwa dhana ya itikadi imepokea fasili mbalimbali na inaendelea kupata maana mpya kila uchao. Vincent (keshatajwa) anasisitiza kuwa dhana ya itikadi ni changamano kwa vile inaweza kufasiliwa kwa namna tofautitofauti. Hata hivyo kihistoria, matumizi ya dhana hii yalianzia katika kipindi cha Mapinduzi ya kiviwanda kule Ufaransa, mnamo miaka ya 1790. Kutokana na uchangamani wake, dhana ya itikadi imezua mijadala mingi miongoni mwa wahakiki na wasomi mbalimbali. Dhana yenyewe inahusishwa na taaluma kama vile falsafa, sayansi ya kisiasa na sayansi za kijamii. Wataalam mbalimbali (Thompson, 1990; Eagleton, 1991; Hawkes, 2003 na Decker, 2004) wanakubaliana kwamba

hakuna fasili moja maalumu ya dhana ya itikadi. Dhana hii inaweza kufasiriwa kwa namna tofautitofauti kutegemea madhumuni na dhamira ya mtumiaji. Hivyo, kila taaluma huifafanua dhana ya itikadi kwa namna tofauti.

Van Djik (1998), anaifafanua itikadi kama misingi ya imani za kijamii zinazoshirikishwa na kundi la kijamii. Mtazamo huu unashikilia kwamba itikadi huumbwa kwenye akili za washiriki wa makundi husika. Anaendelea kusema kuwa itikadi ni imani za kijamii ambazo hupanga, huchangia na kudhibiti maoni ya makundi ya wanajamii. Imani hizi huangazia yanayoaminika kuwa ukweli au uongo, mazuri au mabaya, na pia sahihi au yasiyo sahihi katika jamii. Van Djik (1998) anasisitiza kwamba imani za kijamii zinaweza kujengwa, kuhifadhiwa, kuchochewa na kupangwa katika maumbo makubwa makubwa. Hivyo, michakato ya aina hii hufanyika katika hali ya kuyatimiza majukumu ya kiutambuzi. Vipengee vya maisha kama vile hofu, fantasia au woga vinaweza kuwa imani tu. Utafiti huu umezingatia dhana ya itikadi kama imani kwa maana waimbaji wa nyimbo za kiasili huwasilisha imani zao kuhusiana na masuala mbalimbali kupitia nyimbo za kiasili za Kikamba.

2.1.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Itikadi

Ifuatayo ndiyo mihimili ya nadharia ya Itikadi kama ilivyopendekezwa na Van Dijk (1998):

- i. Maadili: Mhimili huu unashikilia kwamba itikadi ni mifumo ya utambuzi wa kijamii ambayo inaweza kutathminiwa. Yaani, itikadi haina budi kuweka msingi wa maamuzi kuhusu kilicho kizuri au kibaya.
- ii. Miundo ya itikadi. Mhimili wa miundo ya itikadi unadai kwamba itikadi huweza kuainishwa katika makundi mbalimbali kutegemea sifa mahsusi za itikadi.

- iii. Mielekeo: Mhimili wa mielekeo unadai kwamba dhima moja kuu ya kiutambuzi-kijamii ya itikadi ni kupanga makundi maalum ya maoni yanayohusiana na masuala ya kijamii.
- iv. Maumbo ya kijamii: Mhimili huu unadai kwamba itikadi za wanajamii hazina budi kuwakilisha tajriba zao. Maumbo ya kijamii yanarejelea uwakilishaji wa kiakili wa tajriba za kibinafsi kuhusu shughuli, matukio au hali maalum.
- v. Maumbo ya Muktadha: Mhimili huu unashikilia kwamba umbo la muktadha hutekeleza wajibu muhimu katika matini na mawasiliano.
- vi. Tambuzi nyinginezo za kibinafsi: Mhimili huu unasisitiza ujumlishaji wa maumbo ya muktadha pamoja na matukio.
- vii. Maumbo ya kiitikadi: Mhimili huu unadai kwamba maoni na mielekeo ya wanajamii inaweza kuwa ya kiitikadi.
- viii. Uchunguzi wa matini za kiitikadi: Mhimili huu unaeleza kwamba uchunguzi wa matini za kiitikadi unaweza kufanywa kwa njia mbali mbali.

2.1.2.2 Matumizi ya Mhimili ya Nadharia ya Itikadi katika Utafiti

i)Maadili

Mhimili huu unadai kuwa itikadi haina budi kuweka msingi wa maamuzi kuhusu kilicho kizuri au kibaya. Maadili hutoa mwongozo wa kimsingi wa mtazamo na maingiliano ya kijamii. Mfano wa maadili ni ukweli, haki au usawa miongoni mwa mengine. Maadili yenyewe hayawekewi mipaka ya kuhusishwa na makundi fulani bali huwa na umuhimu mpana wa kitamaduni. Hata hivyo, baadhi ya maadili yanaweza kupatikana kwa upana kama vile kitaifa na kimataifa. Kila kikundi huwa na namna yake ya kuteua na kuyapa maadili husika umuhimu kiviwango. Mhimili huu

ulitumika katika kuhakiki masuala mbalimbali yanayohusiana na itikadi zinazofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo husika.

Kwa mfano, kupitia kwenye wimbo *Kaveti kaanu* (Kamwanamke kazembe), mwimbaji anapitisha maadili ya bidii kazini. Anaelezea namna ambavyo mwanamke anafaa kujitahidi kazini hasa ya shambani katika msimu wa mvua. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anawakejeli wanawake wazembe huku akikashifu tabia ya uzembe na kusisitiza utiaji wa bidii kazini. Hivyo, maadili ya bidii yametumika katika kukuza itikadi ya kazi miongoni mwa wanajamii Wakamba. Vilevile, maadili ya kuwa na kiasi yanapitishwa kwenye wimbo *Mwatu* (mzinga). Wimbo wenyewe umewalenga vijana hasa watahiriwa. Kupitia kwenye wimbo huu, mwimbaji anawashauri vijana wawe na kiasi katika maisha yao. Anawaeleza kwamba ukosefu wa kiasi unaweza kuwaongoza katika matendo mabaya kama yale ya unajisi. Hivyo, mwimbaji anawaeleza kwamba wajiepushe na matendo hayo huku akisisitiza maadili ya kiasi. Maadili haya yametumika katika kukuza itikadi ya tohara, ubikira pamoja na ndoa na mapenzi.

ii) Miundo ya Itikadi

Mhimili wa miundo ya itikadi umeuongoza utafiti huu katika kulifikia lengo la pili. Uhakiki wa itikadi za Wakamba zilizofumbatwa kijazanda kwenye NKK umezingatia miundo ya itikadi. Uhakiki husika umedhihirisha itikadi zinazohusiana na mapenzi na ndoa, zile zinazohusiana na siasa na uongozi, miongoni mwa nyingine.

Itikadi nyingi hufafanuliwa kwa namna ya makundi. Hali hii ni dhahiri katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Kwa mfano, itikadi kuhusu dini katika jamii ya Wakamba inajipanga katika makundi kama vile waumini na wasiomwamini Mungu, masharti ya kidini na athari za kutoyazingatia masharti hayo, miongoni mwa mengine. Kwa

mfano, kama inavyobainika katika nyimbo za kiasili za Kikamba, imani ya wanajamii Wakamba ni kwamba zipo hatari zinazoambatana na kutomtii Mungu na mababu walioaga dunia. Kwa mfano, kupitia kwa wimbo *Tuthii Kithembeoni* (Twendeni Madhabahuni), mwimbaji anawashauri wasikilizaji waende mathabahuni ili wamwabudu Mungu. Kulingana naye, ibada yao kwa Mungu wao inasababisha yeye kuwanyeshea mvua na hatimaye wanapata mazao chungu nzima mashambani. Hata hivyo, athari za kumkosea Mungu na kutomwabudu zinadhihirika katika wimbo *Undu Ukwona Ngisilila uu* (Vile Ninavyoshangilia). Hapa, mwimbaji anaeleza kwamba hajalala usiku kucha kwa maana alikuwa amehudhuria shughuli ya *kilumi* ambako walikuwa wakiiombea mvua. Hivyo, madhara yanayodhihirika hapa ni ya kiangazi na njaa. Yaani, wanajamii wanapokosa kuzingatia masharti ya kidini huenda wakakumbwa na majanga kama vile njaa, kiangazi, vita na maradhi.

iii) Mielekeo ya kijamii

Mhimili huu umezingatiwa katika kuhakiki itikadi mbalimbali zilizofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo teule. Uhakiki husika umefanywa kwa kuzingatia mielekeo inayopitishwa kijazanda kwenye NKK. Mielekeo hiyo ni sehemu ya itikadi maalum zinazowasilishwa. Kwa mfano, chini ya uthibiti wa itikadi ya ndoa, tunatarajia mielekeo maalum inayohusiana na itikadi hiyo. Hivyo, mielekeo inayozungumziwa hapa ni ile inayoshikiliwa na washirika wa kundi fulani la kijamii.

Kupitia kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba, tunapata itikadi za aina mbalimbali. Itikadi hizo zimejengwa na mielekeo ya aina mbalimbali. Kwa mfano, kutokana na wimbo *Uka usuvie Utwae* (Njoo uitunze ndoa), mwimbaji anaiwasilisha itikadi kuhusu ndoa na mapenzi. Itikadi yenyewe imegemezwa kwenye mielekeo mbalimbali ya kijamii na kitamaduni. Kwa mfano, mielekeo kuhusu wajibu wa mwanamke katika ndoa inadhihirika kupitia wimbo teule. Kwanza, inadhihirika

kwamba ni wajibu wa mwanamke kuitunza ndoa yake. Pili, upo mwelekeo kwamba mwanamke anapaswa kuwa mvumilivu katika ndoa. Hivyo, ndoa inaposambaratika mwanamke ndiye hulaumiwa kwa kiwango kikubwa. Hii ni kutokana na imani kwamba mwanamke mwenye hekima ndiye huijenga nyumba yake, huku mwanamke mjinga akiibomoa nyumba hiyo hiyo kwa mikono yake miwili. Hata hivyo, maoni yangu ni kwamba kufaulu au kutofaulu kwa ndoa huwategemea wanandoa wote wawili wanaohusika. Hii ni kwa sababu mwanamke anaweza kujitahidi kabisa kuidumisha ndoa yake huku mwenzake wa kiume akiwa hayupo tayari kwa ndoa hiyo. Inapotokea hivyo, basi ndoa hiyo haina budi kusambaratika na kinyume chake. Hivyo, katika hali kama hii mwanamke hafai kulaumiwa kwa hilo.

iv) Maumbo ya kijamii

Mhimili wa maumbo ya kijamii umeuongoza utafiti huu katika kuhakiki itikadi zilizofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo teule. Uhakiki wenyewe umezingatia shughuli, matukio na hali maalum zinazodhihirisha itikadi mbalimbali. Mhimili huu unashikilia kwamba itikadi za kijamii husheheni tajriba za wanajamii. Maumbo ya kijamii huhusisha shughuli, matukio au hali maalum. Maumbo haya pia hurejelewa kama ‘maumbo ya hali’, ‘maumbo ya matukio’ au ‘maumbo ya kibinafsi’. Hivyo, iwapo kikundi cha watu kinashiriki mielekeo ya kijamii kuhusu mazingira yao kwa ujumla, washirika binafsi wa kikundi hicho huwa na uwakilishaji fulani, yaani, maumbo yanayohusiana na mazingira hayo. Maumbo hayo huunda msingi wa kiakili wa mazungumzo na matini inayohusika: ni kile watu huzungumzia au kurejelea. Husheheni maumbo ya matukio yaliyopita, yaliyopo na yajayo; husheheni tajriba za kibinafsi pamoja na mipango ya shughuli husika. Maumbo huwakilisha ufahamu wetu wa shughuli na matukio mengine pamoja na wahusika wa matukio hayo. Vilevile, maumbo huwakilisha maoni yetu maalum ya kibinafsi. Kila mtu huwa na umbo

maalum (ufasiri) la kila matini kwenye kila hali inayohusika. Kwa hivyo, usomaji au usikilizaji wa baadaye wa matini hiyo hiyo unaweza kusababisha umbo tofauti, aidha lililobadilishwa au lililosasishwa.

Maumbo ya kijamii yanadhihirika katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Maumbo yenyewe ndiyo husababisha uwepo wa maarifa ya kimsingi. Maarifa haya huzingatiwa katika ufasiri wa itikadi zinazowasilishwa kwenye nyimbo teule. Kwa mfano, wimbo wa *Tingilingili* (Tingilingili) unadhihirisha haya. Ufasiri wa wimbo huu umechangiwa na maumbo ya matukio yaliyopita. Yaani, hapo zamani kwenye jamii ya Wakamba kulikuwepo vita vya kuviziana na kuibiana mifugo kati ya wanajamii Wakamba na wanajamii Wamaasai na Wasomali hasa kwenye maeneo ya mipakani. Wimbo wenyewe umesawiri mazingira ya aina hii. Wimbo wa *Tingilingili* (Tingilingili) huimbwa na watoto wakati wanapocheza. Hata hivyo, wimbo wenyewe umebeba ujumbe muhimu kwa wanajamii Wakamba. Hapa, mwimbaji anaelezea namna ng'ombe wa babake wanavyoibwa wakati wa usiku. Hata hivyo, mwimbaji anaelezea kwamba ng'ombe wanaopatikana usiku, hupotea usiku pia. Yaani, mali ya wizi hupotea kwa njia ya wizi pia. Kupitia kwenye wimbo teule, mwimbaji anawasilisha itikadi kuhusu vita na ufisadi. Anapitisha ujumbe kwamba vita na ufisadi havifai kamwe yaani, havina faida yoyote.

v) Maumbo ya Mukdadha

Mhimili huu umeuongoza utafiti katika kupambanua NKK zinazoimbwa katika hafla maalum. Mhimili wenyewe unasisitiza umuhimu wa umbo la mukdadha katika matini na mawasiliano. Umbo la mukdadha ni uwakilishaji wa matukio, hali na watendaji. Ni uwakilishaji wa mukdadha na tukio wasilishi linaloendelea. Ili kubaini itikadi zilizofumbatwa kijazanda kwenye NKK, mtafiti hana budi kuuzingatia mukdadha wa uimbaji wa wimbo husika.

Maumbo ya muktadha ni vipengee muhimu katika ufasiri na uelewekaji wa NKK. Umbo la muktadha linarejelea mazingira. Muktadha wa nyimbo za kiasili za Kikamba ni mazingira ambamo nyimbo hizo hutungiwa au kuwasilishwa. Kwa mfano, wimbo *Kaveti Kaanu* (Kamwanamke Kazembe) huwasilishwa kwenye mazingira ya kazi hasa katika msimu wa mvua. Hivyo, wimbo huu huwasilishwa kwa wanajamii Wakamba wanapoendelea na kazi hasa ya shambani. Wimbo wenyewe huimbwa ili kuwatia motisha wafanyakazi huku wakizikashifu tabia za uzembe. Wimbo huu unaiendeleza itikadi kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii.

Pamoja na hayo, wimbo wa *Nzambi Akithambya Nzele* (Nzambi akiosha Kata) huwasilishwa katika mazingira ya kisiasa. Wimbo wenyewe unarejelea viongozi tangulizi na viongozi wa sasa katika jamii ya Wakamba. Kupitia kwake, mwimbaji anawashauri wanajamii wampee nafasi kiongozi wa sasa ili aitekeleze kazi yake. Anaieleza kwamba kiongozi huyu yumo katika mchakato wa kuuondoa uchafu na uovu ulioendelezwa na viongozi tangulizi. Hivyo, wakimpa nafasi kwa uvumilivu hawana budi kuiona au kushuhudia kazi yake. Wimbo wenyewe unaendeleza itikadi inayohusiana na siasa na uongozi kwamba ufasidi haufai kamwe.

vi) Tambuzi Nyinginezo za Kibinafsi

Mhimili huu umezingatiwa kwenye utafiti katika kutilia maanani mawazo, maoni na tajriba za mtafiti kama mwanajamii Mkamba aliyezaliwa na kukulia kwenye mazingira ya Ukambani. Mhimili wenyewe unasisitiza kuwa maumbo ya muktadha na matukio yanaweza kujumlishwa kama vile ambavyo tajriba zetu binafsi zinaweza kutokana na wakati, mahali au vipengee vinginevyo vinavyohusika. Kwa kawaida, ufahamu wetu binafsi huwa wa aina hii ya kijumla. Hali hiyo pia inaweza kudhihirika kwenye maoni yetu ya kibinafsi.

vii) Maumbo ya Kiitikadi (Miundo yenye Upendeleo)

Mhimili huu umeuongoza utafiti huu katika kuchanganua itikadi mbalimbali zinazowasilishwa kupitia kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Mhimili wenyewe unadai kwamba maoni na mielekeo ya wanajamii inaweza kuwa ya kiitikadi. Kwa hivyo, tunapozungumzia ufasiri wenye upendeleo wa matini ni kumaanisha kwamba watumiaji wa lugha wametumia upendeleo wa kiitikadi katika uundaji wa maumbo yao ya matukio na muktadha wa mawasiliano. Ni kupitia kwa maumbo ya kiitikadi ambapo matini zenyewe zinaweza kuwa za kiitikadi au zinatafsiriwa kiitikadi.

Kwa mfano, maumbo ya kiitikadi katika nyimbo za *Undu Ukwona Ngisilila uu* (Ninaposhangilia hivi) na *Tuthii Kithembeoni* (Twendeni Madhabahuni) yanadhihirisha itikadi kuhusu dini. Vilevile, maumbo ya kiitikadi katika nyimbo za *Sikala* (Sigara), *Mundu Mwiu* e Kiliko (Mwafrika ni mwenye Akili) na *Wongweta na Kyeni* (Ukinitaja kwa *kyeni*) zinawasilisha itikadi kuhusu utamaduni. Pamoja na hayo, nyimbo za *Ngulu wa Ngao* (Ngulu wa Ngao) na *Ndumane Ngethi* (Nitumane Salamu) na *Ngune Kithuki* (Nipige Mbiu) zinawasilisha maumbo yanayopitisha itikadi kuhusu vita.

viii) Uchunguzi wa Matini za Kiitikadi

Mhimili huu unaeleza kwamba uchunguzi wa matini za kiitikadi unaweza kufanywa kwa njia mbali mbali. Mhimili huu uliuongoza utafiti katika kuhakiki itikadi zilizofumbatwa kijazanda kwenye NKK. Itikadi mbalimbali zilihakikiwa na kudhihirishwa kwa kuzingatia zilivyofumbatwa kijazanda kwenye NKK. Kwa mfano, haya yamefanywa kwa kupambanua maumbo ya kimsingi ya utambuzi wa kijamii yalivyodhihirika katika hafla za kijamii ambamo nyimbo za kiasili za Kikamba hutokea.

Kwa kuhitimisha, mihimili ya Nadharia ya Jazanda Dhanifu na ile ya Itikadi imetumika katika kuuongoza utafiti huu. Nadharia ya Jazanda Dhanifu ilielekeza uhakiki wa itikadi zilizofumbatwa kijazanda na uamilifu wa jazanda hizo kifani na kimaudhui katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Nadharia ya Itikadi nayo ilitumika kupambanua maumbo ya kimsingi ya utambuzi wa kijamii yalivyodhihirika katika hafla za kijamii ambamo nyimbo za kiasili za Kikamba hutokea. Hivyo, nadharia hizi mbili zilikidhi mahitaji ya utafiti huu.

2.2 Tahakiki ya Maandishi Kuhusu Mada ya Utafiti

Kama zilivyo jamii nyingine za Kiafrika, Wakamba wana utamaduni na itikadi ambazo hujitokeza katika lugha na fasihi simulizi yao. Kipera cha nyimbo za kiasili za Kikamba ni maarufu sana miongoni mwa Wakamba. Kupitia kwa nyimbo hizi, falsafa, mawazo, maadili, imani za kidini, matamano pamoja na tajriba za jamii ya Wakamba huwasilishwa kwa hadhira lengwa. Hata hivyo, mapitio ya maandishi yamethibitisha kwamba hakuna utafiti uliofanywa ulioangazia ufumbaji wa itikadi kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Hili ndilo pengo la kimaarifa ambalo utafiti huu unajaribu kuliziba. Maandishi yaliyohakikiwa yanahusu nyimbo za kiasili kwa ujumla, nyimbo za kiasili za kikamba, dhana ya itikadi kwa ujumla, itikadi katika fasihi, jazanda na jamii ya Wakamba.

2.2.1 Mapitio ya Maandishi kuhusu Nyimbo za Kiasili

Katika utafiti huu, dhana ya wimbo wa kiasili inarejelea aina ya wimbo unaoangazia mila na utamaduni wa jamii maalum katika muktadha mahsusi na ambao unawasilishwa kwa sauti yenye mahadhi, maneno na matendo kwa hadhira hai. Kwa kuwa nyimbo za kiasili huwasilishwa kwa njia ya mdomo, nyimbo hizi hubadilika kadri wakati unavyopita. Mabadiliko hudhihirika katika maumbo ya nyimbo, muktadha wa uwasilisho, wazo na hata maudhui yanayowasilishwa kwenye nyimbo

husika. Nyimbo za kiasili huhusishwa na miktadha maalum ya kijamii kwa kuwa nyimbo zenyewe hukusudiwa mawasiliano ya ana kwa ana ambapo m(wa)imbaji hutagusana na hadhira lengwa.

Mutwiri (2005), amefanya utafiti wa nyimbo za tohara za jamii ya Watigania kwa kuzingatia mtazamo wa utendakazi wa nyimbo za kiasili. Mtafiti huyu ameeleza sababu zinazopelekea kutokufa kwa tamaduni licha ya upinzani mkubwa uliopo kutokana na maingiliano ya tamaduni za Kiafrika pamoja na zile za Kimagharibi. Utafiti wa Mutwiri na huu unalingana kwa vile tafiti hizi zote zimejikusisha na nyimbo za kiasili. Hata hivyo, ipo tofauti kubwa kati ya kazi yetu na ile ya Mutwiri. Hii ni kwa sababu nyimbo alizoziangazia Mutwiri zinahusisha utamaduni tofauti na ule wa zetu. Vilevile, vipengee alivyoviangazia mtafiti huyu ni tofauti na vyetu ambapo tumejikusisha na ufumbaji wa itikadi kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba, tofauti naye aliyeangazia utendakazi wa nyimbo husika. Hivyo, utafiti wetu umejikusisha na dhima ya kiitikadi kwenye nyimbo teule.

Naye Wanjala (2007), amechunguza maudhui na matumizi ya lugha katika nyiso za Wabukusu. Wanjala (keshatajwa) amejikusisha na jinsi fanani hubadilisha lugha na maudhui katika nyiso za Wabukusu ili kutekeleza madhumuni yake. Utafiti wake ulijikita katika vipindi viwili vya kihistoria. Utafiti huu ulitambua kuwa watunzi wa nyiso za Wabukusu huzingatia vipengee mbalimbali wakati wa kutunga na kuimba nyimbo husika. Vipengee hivyo ni pamoja na muktadha, jukwaa la tukio, hadhira lengwa, washiriki, namna ya uwasilishaji, sifa za fanani na sajili husika. Utafiti huu umetufaidi kwa upande wa umuhimu wa muktadha katika utunzi na uwasilishaji wa nyimbo za kiasili. Lengo la kwanza la utafiti wetu ni kupambanua jazanda zinazojitokeza katika NKK zinazowasilishwa kwenye hafla maalum. Upambanuzi wetu umezingatia hafla mbalimbali ambazo NKK huimbwa. Hata hivyo, utafiti wa

Wanjala ni tofauti na wetu. Hii ni kwa sababu amejikita katika nyimbo za Wabukusu walio na utamaduni tofauti na ule wa Wakamba. Vilevile, nadharia alizozitumia Wanjala ni tofauti na tulizozitumia katika utafiti huu. Jambo hili limefanya tuwe na matokeo tofauti kati ya tafiti hizi mbili.

Kobia (2008), amejihusisha na taswira za kiuana za wanaume miongoni mwa Waigembe. Utafiti wake ulihakiki majukumu, itikadi na mahusiano ya kiuana katika jamii ya Waigembe kupitia nyimbo zao za tohara. Utafiti wa Kobia (keshatajwa) umetufaa kwa upande wa kiuhakiki. Hata hivyo, utafiti wetu ni tofauti na ule wa Kobia kwa sababu wetu umejikita katika ufumbaji wa itikadi kijazanda katika NKK. Uchunguzi wetu umejikita katika kipengee cha kijazanda huku Kobia (keshatajwa) akijihusisha na kipengee cha taswira.

2.2.2 Mapitio ya Maandishi kuhusu Nyimbo za Kiasili za Kikamba

Katika utafiti huu, inachukuliwa kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba ni aina za nyimbo zinazowasilishwa kwa lugha ya Kikamba na ambazo zinahusiana na historia, utamaduni, jamii, mazingira na tajriba za jamii ya Wakamba. Awali nyimbo za kiasili za Kikamba ziliwasilishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo na kuhifadhiwa akilini mwa wanajamii. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia, nyimbo za kiasili za Kikamba zimehifadhiwa mitandaoni, kwenye kanda za sauti, video na video tepetevu.

Katika tasnifu yake ya uzamili, Wathome (2009), amechunguza mitindo katika nyiso za jamii ya Wakamba wa Masaku, Tarafa ya Kati. Utafiti wake umejikita kwenye mabadiliko ya kimitindo kwenye nyiso husika. Wathome (keshatajwa), anaeleza kuwa nyiso za kisasa za Wakamba zinatumia mitindo ambayo inaleta mawazo tofauti kabisa na yale ya nyiso za kimapokeo. Pia, imebainika kwamba muundo pamoja na fani za

nyiso za kisasa ni tofauti kabisa na zile za kimapokeo. Hali hii imesababishwa na mabadiliko ya kielimu pamoja na mbinu mpya ya tohara ambapo kisasa, tohara nyingi hutekelezwa hospitalini. Utafiti huu umetufaa kwa upande wa historia ya jamii ya Wakamba. Wathome amethibitisha kuwa NKK zinasheheni fani mahsusi. Utafiti wetu unaangazia kipengee cha jazanda ambacho hujitokeza katika nyimbo za kiasili za Kikamba.

Utafiti mwingine unaohusiana na nyimbo za kiasili za Kikamba ni ule wa Musyoka (2012) aliyechunguza mtindo wa nyimbo za mazishi miongoni mwa Wakamba. Anaeleza kwamba, nyimbo za mazishi katika jamii ya Wakamba hutumia kauli na maneno teule yanayowasilishwa kwa mahadhi maalumu, ili ziweze kutekeleza jukumu lake muhimu la kuliwaza waathiriwa. Mtafiti huyu amelenga kubainisha kuwa, kauli za lugha zinazotumiwa katika nyimbo za mazishi za Wakamba husaidia kuibua taswira ya kimawazo kuhusu kifo. Utafiti wa Musyoka (2012), umeunufaisha wetu kwa upande wa uchanganuzi wa kimaudhui. Tofauti iliyopo baina ya tafiti hizi mbili ni kwamba, tumejihusisha na vipengee tofauti na vile vilivyoshughulikiwa na Musyoka. Hivyo, huku Musyoka akiangazia kipengee cha mtindo katika nyimbo za mazishi, utafiti wetu umeangazia ufumbaji wa itikadi kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba.

Musembi (2016), ameangazia mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando na hasa nyiso katika jamii ya Wakamba. Uchunguzi wake umejikita katika vipindi vya kabla na baada ya ukoloni. Musembi (keshatajwa) amebainisha kwamba maudhui ya nyimbo za jando za jamii ya Wakamba yamebadilika kulingana na mpito wa wakati katika. Kuhusiana na hoja hii, mtafiti huyu amebainisha kwamba nyiso za kabla ya wakoloni zilikuwa na maudhui ya kitamaduni. Maudhui hayo yalilenga masuala mahsusi yaliyoibuka kutokana na hali ya jamii na wakati wake. Hii ni kutokana na

sababu kwamba asasi za kitamaduni katika jamii hii zilikuwa imara na mwelekeo wa kitamaduni ulitawala shughuli zote za kijamii. Hata hivyo, Musembi (keshatajwa) anaeleza kwamba baada ya ukoloni, utamaduni wa Wakamba uliathiriwa na dini ya Kikristo pamoja na elimu ya kimagharibi. Hivyo, utangamano baina ya Wakamba na wakoloni uliathiri maisha ya Wakamba. Utafiti wa Musembi (2016) unatofautiana na wetu. Hii ni kwa sababu utafiti wake umejihusisha na mabadiliko ya kimaudhui kwenye nyiso za Wakamba ilhali utafiti wetu umeangazia kipengee cha itikadi na hasa kilivyofumbatwa kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba, nyiso zikiwemo.

Naye Kimondiu (2019) ameangazia usawiri wa mwanamke katika sifo za jamii ya Wakamba. Mtafiti huyu alikusudia kuchunguza iwapo mwanamke anadunishwa katika nyimbo hizi, anadunishwa vipi na iwapo anayetewa katika jamii dhidi ya imani dunishi ya mfumo-dume. Utafiti wa Kimondiu umedhihirisha kuwa mwanamke amesawiriwa kwa njia chanya pamoja na njia hasi katika nyimbo za sifo za Wakamba. Hata hivyo, utafiti wetu ni tofauti na wake kwa maana tumejihusisha na ufumbaji wa itikadi kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba.

Mtafiti mwingine aliyeshughulikia nyimbo za kiasili za Kikamba ni Muema (2019) ambaye amechunguza tasfida katika nyimbo za Kikamba. Uchunguzi wake umebainisha matumizi ya tasfida mbalimbali katika nyimbo teule. Utafiti wa Muema (2019) umetufaa kwa upande wa uchanganuzi wa lugha. Hata hivyo, utafiti huo umetofautiana na wetu kwa sababu tumejihusisha na ufumbaji wa itikadi kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba, tofauti naye aliyejikita katika tasfida.

2.2.3 Mapitio ya Maandishi kuhusu Itikadi katika Fasihi

Takriban shughuli zote za maisha ya wanajamii huongozwa na itikadi. Katika utafiti huu, itikadi ni dhana inayorejelea mkusanyiko wa mawazo, imani, maadili, mitazamo na tabia ambazo kwazo, wanajamii hujenga maana ya ulimwengu wao na shughuli zao zote. Itikadi huchangia katika namna wanajamii wanafikiria na kuyafasiri mambo mbalimbali. Itikadi basi ni msingi wa kaida na kanuni za jamii ambazo huongoza maamuzi kuhusiana na masuala mahsusi. Katika jamii ya Wakamba, itikadi zao hudhihirika kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, itikadi hizi hubainika kupitia kwa mavazi, matendo, mazungumzo yao ya kila siku au hata kwenye kazi zao za kisanaa. Hivyo, itikadi hudhibiti uzoefu wa kijamii wa kikundi kinachohusika pamoja na matini, mazungumzo na fasihi ya wanajamii wanaohusika.

Watunzi wa nyimbo za kiasili za Kikamba hutunga nyimbo zao huku wakiongozwa na itikadi fulani kwenye mazingira wanamojipata. Itikadi hizo zinaweza kuhusiana na masuala ya siasa, dini, ndoa, uhai na mauti, kazi na uchumi na maadili ya kijamii kwa ujumla. Itikadi zenyewe huonyesha mwelekeo na imani za watunzi na wanajamii kuhusu masuala wanayoyashughulikia.

Licha ya kuwa itikadi ni kipengee muhimu cha kimaudhui katika fasihi, hakijamakinikiwa na watafiti wa nyimbo za kiasili za Kikamba. Kadiri ninavyojua, hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusu itikadi kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Chuachua (2011) anaeleza kwamba itikadi katika kazi za fasihi ni kipengee ambacho hakijatafitiwa kwa kiasi kikubwa na wataalam wa fasihi ikilinganishwa na vipengee vingine vya maudhui na fani. Baadhi ya watafiti waliochunguza nyimbo za kiasili za Kikamba wameangazia vipengee vingine vya fasihi tofauti na kipengee cha itikadi. Hawa ni kama vile Musembi (2016), Musyoka (2012), Wathome (2009) na Kieti (1999).

Mwaifuge (2001), katika tasnifu yake ya Uzamili amechunguza masuala ya imani na itikadi katika tamthilia zote za Ebrahim Hussein. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa katika tamthilia za Ebrahim Hussein kunasawiriwa imani ya dini ya Kiislamu, dini za Kiafrika na itikadi za uganga na ushirikiana, Ujamaa na kujitegemea, mapinduzi ya kitabaka na umoja na mshikamano. Kwa mfano, katika tamthilia ya Kinjekitile kunatokeza itikadi ya uganga na ushirikina ambapo mtama na maji vinatazamwa kuwa ni silaha madhubuti ya kupambana na adui vitani kuliko bunduki na mabomu ya kisasa. Hii ni itikadi ambayo ilisaidia Watanganyika kupambana na Wajerumani katika vita vya Majimaji (1905-1907). Tofauti na utafiti wa Mwaifuge (2001), utafiti huu umechunguza ufumbaji wa itikadi kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba.

Naye Chuachua (2011), ameangazia itikadi katika riwaya ya Kiswahili kwa kurejelea riwaya za Shaaban Robert. Katika utafiti wake amebaini kuwa Shaaban Robert anasawiri itikadi mbalimbali kama vile, ujamaa na kujitegemea, ubepari, utandawazi, umoja na mshikamano na kufanya kazi kwa bidii. Kazi hii imetusaidia kwa kutoa mwongozo wa uchanganuzi wa kiitikadi. Kutokana na utafiti wa Chuachua (keshatajwa) ni bayana kwamba kazi ya kifasihi inaweza kufumbata itikadi mbalimbali. Utafiti wetu unapiga hatua zaidi kwa kuangazia namna itikadi inafumbatwa kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba.

Shemweta (2015) ameangazia itikadi katika tamthilia za Emmanuel Mbogo ambapo amefanya utafiti linganishi wa *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Lengo kuu la utafiti wake lilikuwa ni kuchunguza itikadi katika tamthilia mbili husika. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa itikadi kama vile, ushirikina wa kichawi na kiganga, mapinduzi, ujamaa, ubepari, utamaduni, mapenzi na ndoa na dini zimejitokeza katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Kwa upande wa *Fumo*

Liongo, itikadi za masuala ya sihiri, utawala wa milele, mapenzi ya dhati kwa jamii na malezi na uzazi zimejitokeza. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa itikadi ya uganga wa kichawi inafanana sana katika tamthilia zote mbili ikilinganishwa na itikadi nyingine. Itikadi hii imetawala katika tamthilia hizi, jambo linaloashiria kuwa hata katika jamii itikadi hii imetawala katika maisha ya watu walio wengi. Itikadi juu ya kuamini katika dini imejitokeza katika tamthilia zote mbili. Hali hii inadhihirisha kuwa kwa asili mwanadamu ni mtu ambaye anazaliwa akiwa na itikadi juu ya uwepo wa Mungu.

Kazi ya Shemweta (2015) imechangia pakubwa utafiti wetu kwa kubainisha kuwa itikadi katika tamthilia teule zinajengwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa. Mbinu hizi zinajumuisha tamathali za usemi kama vie: tashibiha, sitiari, kejeli, takriri na misemo. Utafiti wetu unapiga hatua zaidi kwa kuchunguza jazanda kama mbinu ya kisanaa inayowasilisha itikadi za Wakamba katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Vilevile, nadharia alizozitumia kwenye utafiti wake ni tofauti na zile tulizozitumia. Pamoja na hayo, Shemweta (2015) ameangazia utanzu wa riwaya huku utafiti wetu ukijikita kwenye utanzu wa nyimbo hasa za kiasili za Kikamba.

Mtafiti mwingine aliyejijhusisha na suala la itikadi ni Makhulo (2015). Mtafiti huyu ameangazia mamlaka na itikadi katika nyimbo teule za taarab za *Zilipendwa* ulioimbwa na Khadija Yusuf na *Utalijua Jiji* ulioimbwa na Afua Suleimani. Makhulo (keshatajwa) amehitimisha kuwa itikadi ya ubabedume ndiyo inayotawala katika nyimbo teule na kwamba mahusiano ya mamlaka hujidhihirisha vilevile katika nyimbo hizi. Utafiti huu umetufaa kwa upande wa uchanganuzi wa itikadi. Hata hivyo, utafiti wetu umejikita katika namna itikadi zilivyofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba ilhali Makhulo (keshatajwa) anajihusisha na mikakati

ya kipragmatiki na mchango wake katika ujenzi wa mamlaka na itikadi katika nyimbo teule.

Abdulla (2016) amejihusisha na uchunguzi wa athari za itikadi katika nyimbo za harusi za Kizanzibar. Utafiti wake umefanyika katika visiwa vya Unguja na Pemba. Abdulla (2016) amedai kuwa nyimbo za harusi za Kizanzibari huimbwa katika miktadha tafauti kama vile wakati wa kuwekwa ndani mwari harusi kwa ajili ya mafunzo na matayarisho ya harusi, wakati wa kwenda kuoja, wakati wa kurudi na bibi harusi, na kadhalika. Aidha, utafiti wa Abdulla umegundua kuwa nyimbo za harusi za Kizanzibari zimebeba itikadi mbalimbali kama vile itikadi juu ya umuhimu wa utii, usafi, kuheshimu ndoa, ushirikiano pamoja na itikadi ya uvumilivu katika ndoa. Utafiti huu umeunufaisha wetu kwa upande wa umuhimu wa jazanda katika ufumbaji wa itikadi kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Hata hivyo, tafiti hizi mbili ni tofauti kwa maana malengo yaliyokusudiwa ni tofauti.

2.2.4 Mapitio ya Maandishi kuhusu Jazanda

Jazanda ni dhana ambayo imejadiliwa na wataalam mbalimbali. Kwa mujibu wa Kovecses (2002), jazanda ni mchakato wa kiakili ambapo uwanja mmoja wa ufahamu (B) unaeleweka kwa misingi ya uwanja mwingine (A). Hivyo, jazanda huwa na uwanja asilia (A) na uwanja lengwa (B) kwa namna ambavyo uwanja asilia unahusisha vitu vinavyoweza kuonekana na kushikika huku uwanja lengwa ukihusisha vitu dhahania. Kwa hivyo, jazanda ni mfumo wa lugha ya kiishara ambapo uhusiano wa moja kwa moja hujitokeza baina ya vitu viwili au hali mbili tofauti. Katika jazanda, kitengo fulani hueleweka kwa misingi ya kitengo kingine. King'ei (2002) anaunga mkono wazo hili anaposema kuwa jazanda ni fumbo ambamo ndani mwake maana ya kitu imefichama. Ni ulinganishaji wa vitu viwili moja kwa moja.

Mbatia (2000) anaeleza kwamba jazanda ni kunga ya utunzi ambapo lugha inatumiwa kusawiri picha fulani kutokana na maelezo yanayotumia maneno teule au tamathali za usemi. Katika jazanda, maneno teule hutumiwa kisanaa ambapo vitu viwili hulinganishwa moja kwa moja bila kutumia viunganishi. Hapa, jina linalotumika hurejelea kitu kingine kilicho na sifa fulani sawa na hicho. Lugha inayotumiwa katika kazi yoyote ya fasihi zikiwemo nyimbo za kiasili za Kikamba inaweza kutinga au kurahisisha uelewekaji wa ujumbe unaopitishwa. Kwa mfano, mara nyingi nyimbo za kiasili za Kikamba husheheni lugha ya kijazanda. Jazanda mbalimbali hubeba ujumbe uliofichika. Hivyo, jazanda zenyewe huhitaji ufumbuzi unaofaa ili kupata ung'amuzi wa dhamira na ujumbe wa mtunzi. Kwa hivyo, msikilizaji huhitaji ufahamu wa hali ya juu ili kufumbua itikadi zinazofumbika kijazanda kwenye nyimbo mahsusii. Hivi ni sawa na kusema kwamba inawezekana mtu akazisikiliza nyimbo husika zikiwasilishwa bila ya kuuelewa ujumbe uliomo. Utafiti huu umechunguza namna itikadi zimefumbatwa kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba zinazoimbwa katika hafla mbalimbali za kijamii.

2.2.5 Mapitio ya Maandishi kuhusu Jamii ya Wakamba

Japo Wakamba wanaweza kupatikana katika maeneo mbalimbali nchini, wengi wao wana asili katika kaunti za Kitui, Machakos na Makueni nchini Kenya. Hivyo, eneo hili lote hujulikana kama Ukambani. Hata hivyo, Kieti na Coughlin (1990) wanaeleza kwamba kuna Wakamba ambao wanapatikana katika sehemu nyingine kama vile Mwea katika Kaunti ya Embu, sehemu za pwani hasa Shimba hills, katika wilaya ya Kwale, sehemu za Taita Taveta pamoja na kisiwani Mombasa. Baadhi ya maeneo wanamoishi Wakamba huwa ni makavu na hupata mvua ya kiwango cha mililita 700 kwa mwaka na wakati mwingine mvua ikipungua hadi kiwango cha mililita 400 kwa mwaka. Maelezo haya ni kwa mujibu wa Kavyu (1980).

Baadhi ya watafiti wa fasihi simulizi ya Wakamba wameizungumzia jamii hii katika kipindi cha kabla ya ukoloni. Miongoni mwa wataalam hawa ni pamoja na Kimilu (1962), Mbiti (1969), Ndeti (1972), Kavyu (1980), Nzioki (1982), King'ei (1982) na Kieti (1999). Watafiti hawa wanaafikiana kuwa kipindi kilichotangulia wakoloni kilikuwa kabla ya mwaka wa 1906. Katika kipindi hiki, tamaduni za Wakamba zilikuwa zimekita mizizi katika nyanja zote. Hii ni kwa sababu, hapakuwa na mwingiliano wala kuathiriana na tamaduni zingine.

Kwa mujibu wa Mbiti (1969), hiki kilikuwa kipindi cha ujamaa katika jamii ya Wakamba. Hivyo, watu waliishi kwa ushirika na walitekeleza shughuli zao za kitamaduni kwa mshikamano. Pia, mila na desturi zilizingatiwa na kila mwanajamii. Akizugumzia hoja hii, Nzioki (1982) anaeleza kuwa kila shughuli ilikuwa na nyimbo zake. Nyimbo hizi zilikuwa na maudhui na mitindo iliyodhihirika. Mitindo yenyewe ilichangia katika kuwasilisha maudhui yaliyokusudiwa. Maudhui ya nyimbo hizi yalisawiri maisha katika uhalisia wa jamii hii. Kwa hivyo, nyimbo zilitekeleza majukumu muhimu katika utamaduni wa Wakamba. Waliabudu Mungu kupitia kafara na matambiko mbalimbali. Aidha, walikuwa na vita vya kuviziana vya mara kwa mara kati yao na jirani zao kama vile Wamasai na Wagikuyu.

Akizungumzia mifumo ya kisiasa miongoni mwa Wakamba, Kimilu (1962) anaeleza kwamba ukoo ulikuwa asasi muhimu katika jamii hii. Wanajamii waliokuwa katika *mbai* (koo) mbalimbali walitegemeana kwa hali zote za maisha. Hivyo, ukoo ulihusu watu ambao walikuwa wa nasaba moja kutoka kwa mzazi mmoja wa jadi. Pia, wanaukoo walikuwa na uhusiano wa karibu kiasi kwamba, waliitana kaka na dada. Kulingana na Nzioki (1982), King'ei (1982), Kieti na Coughlin (1990) koo kumi na mbili zilikuwa zimebainika vyema katika jamii hii. Hizi ni pamoja na: Atangwa,

Aanziu, Auani, Atwii, Aombe, Ambua, Amuunda, Akitutu, Aiini, Akitondo, Amuui na Amwitu.

Uongozi katika jamii ya Wakamba ulilenga misingi ya ukoo. Wazee (*atumia*) ndio waliotwikwa jukumu la kuiongoza jamii na kushughulikia mambo ya kidini kama vile matambiko ya kijamii na kafara miongoni mwa mengine mengi. Haya ni kulingana na Nzioki (1982). Naye King'ei (1982), anaeleza kwamba umri, ndoa na uadilifu ndivyo vigezo vilivyozingatiwa katika uteuzi wa viongozi. Katika jamii hii, wanaume walianza kutwikwa majukumu kadhaa baada ya kupashwa tohara. Mbiti (1969) anadai kuwa pindi tu vijana walipofuzu sherehe za jando, waliitwa *anake* kwani sasa walitwikwa jukumu la kuilinda jamii dhidi ya maadui. Mbele yao palikuwa na kundi lingine la *nthele* ambao walitwikwa majukumu ya uongozi. *Nthele* ni mwanaume ambaye amepitia sherehe ya tohara na kutiwa jandoni, ameo na ana watoto. Kimilu (1962), anasema kuwa *Nthele*, alihitajika kupitia sherehe ya mpito ijulikanayo kama *kukula* ili awe *nthele* anayetambulika na wanajamii. Jamii ya Wakamba ilitegemea *atumia* na *nthele* katika uongozi na maamuzi ya kesi zozote zile za kijamii. Chifu naye aliteuliwa na baraza la *atumia ma kivalo*. Uteuzi wake ulizingatia sifa za *nthele* kwa mfano uwezo wa kuikimu familia yake vizuri bila misukosuko, ulimbikizaji wa mali hususan mifugo na mashamba, uaminifu, ushujaa pamoja na busara. Akizungumzia kauli hii, King'ei (1982) anaongezea kwamba baraza la juu kabisa la uongozi lilikuwa kundi la *atumia ma kisuka*. Hawa ni wazee waliokuwa na umri wa kuanzia miaka 60. Kwa mujibu wa Kimilu (1962), Nzioki (1982) na Andrew & Salvadori (1980), jamii ya Wakamba imekuwa ikijihusisha na inajihusisha na shughuli mbalimbali zinazochangia katika utekaji wa uchumi wao. Hizi ni pamoja na ukulima, biashara, uchongaji, uhunzi, ufinyanzi miongoni mwa nyingine.

Hivyo, mfumo wa jamii ya Wakamba unaongozwa na itikadi maalum ambazo hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Itikadi zenyewe hudhihirika katika maisha yao ya kila siku. Maisha yenyewe yanahusisha shughuli na kazi mbalimbali wanazozifanya. Kazi na shughuli mbalimbali za Wakamba huambatana na nyimbo zikiwemo za kiasili. Hivyo, inaaminika kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba ni mojawapo wa mbinu za upitishaji wa itikadi kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hata hivyo, itikadi zenyewe haziwasilishwi tu waziwazi bali hufumbatwa kijazanda kwenye nyimbo teule. Hali hii imepelekea uchunguzi wa ufumbaji wa itikadi kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Utafiti wenyewe umefumbua itikadi mbalimbali zinazowasilishwa kijazanda katika nyimbo teule.

2.3 Hitimisho

Sura hii imejikita katika msingi wa nadharia na tahakiki ya maandishi kuhusu mada ya utafiti. Imebainika kwamba nadharia mbili zimetumika katika kuuongoza uchunguzi huu. Hizi ni pamoja na nadharia ya Jazanda Dhanifu na ile ya Itikadi. Mihimili mahsusi ya nadharia hizi imejadiliwa mintarafu ya malengo ya utafiti wetu. Vilevile, tahakiki ya maandishi yanayohusiana na mada ta utafiti yamebainisha pengo la kiutafiti kuhusiana na ufumbaji wa itikadi kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Sura ya tatu inayofuata inajadili mbinu za utafiti zilizotumiwa ili kuyafikia malengo matatu ya utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura ya tatu inaangazia mbinu zilizozingatiwa katika kuutekeleza utafiti huu. Miongoni mwa vipengele vinavyojadiliwa ni muundo au mkabala wa utafiti, sampuli na usampulishaji wake, eneo la utafiti na vifaa vya kukusanya na kuhifadhi data ya utafiti. Uchanganuzi na ufasiri wa data umeelezwa hali kadhalika upangaji na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti umefafanuliwa kikamilifu.

3.1 Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu ulizingatia mkabala au muundo wa kithamano ambapo maelezo ya mahusiano ya vipengele muhimu vilivyochunguzwa yanatolewa. Maelezo yametolewa kudhihirisha uhusiano uliopo kati ya jazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba na itikadi inayowasilishwa na jazanda hizo. Mihimili ya nadharia zilizoongoza utafiti huu imetumika katika kufafanua matokeo ya utafiti hali kadhalika mifano muafaka kutokana na data iliyokusanywa imetolewa kushereshea matokeo na mahitimisho ya utafiti.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umejikita kwenye fasihi simulizi na hasa utanzu wa ushairi simulizi. Katika ushairi simulizi kipera cha wimbo na hasa wimbo wa kiasili wa Kikamba ndio umechunguzwa.

3.2.1 Maktabani

Asili ya data ya utafiti huu ni maktabani kumaanisha kuwa mtafiti hakuenda nyanjani kukusanya data kutokana na utendaji hai wa NKK. Data kuhusiana na malengo ya utafiti ilitokana na Tume ya *Permanent Presidential Music Commission*. Mtafiti

alipata udhuru wa kuzuru makavazi ya tume hiyo ambako nyimbo za kiasili za jamii mbalimbali za Kiafrika hukusanywa wakati zinawasilishwa katika mazingira asilia na kuhifadhiwa. Nyimbo hizi baada ya kukusanywa huhifadhiwa kwenye mitandao, diski, video tepetevu na hata kanda za sauti.

Data ya ziada kuhusiana na suala la utafiti ilipatikana kutokana na Chuo Kikuu cha Moi na Chuo Kikuu cha Kenyatta, miongoni mwa maktaba nyingine. Pale maktabani, vitabu, majarida, tasnifu na makala ya mtandaoni yanayohusiana na mada ya utafiti yamesomwa. Vilevile, makala na vitabu kuhusiana na nadharia za utafiti vimesomwa na kuhusishwa katika utafiti huu. Pamoja na hayo, usomi umefanyiwa maktabani ili kupata ufahamu wa yale yaliyofanywa na wasomi wengine kuhusu mada tuliyoishughulikia. Hapa, nimezinakili hoja muhimu zinazohusiana na mada husika.

3.3 Sampuli na Usampulishaji

Kwenye tume ya *Permanent Presidential Music Commission* nilizipakua nyimbo za kiasili za Kikamba 68 na kuzihifadhi kwenye diski. Kisha, nilizisikiliza, nikaziteua, nikazinakili, nikazipanga na kuzichanganua nyimbo za kiasili za Kikamba arobaini na moja tu. Uteuzi wa nyimbo hizo umefanywa kimakusudi ambapo sampuli iliteuliwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Hivyo, nyimbo zinazowasilisha itikadi kijazanda ndizo ziliteuliwa. Sampuli lengwa hapa imekuwa ni nyimbo za kiasili za Kikamba zinazowasilisha itikadi kijazanda. Aidha, nyimbo arobaini na moja zimeteuliwa kimakusudi kwa mujibu wa malengo na nadharia za utafiti.

3.4 Vifaa vya Kukusanya na Kuhifadhi Data

Vifaa vilivyotumika katika utafiti huu ni pamoja na kalamu, karatasi, kipakatalishi, diski, daftari na shajara. Kwenye tume ya *Permanent Presidential Music Commission*, nyimbo sitini na nane za kiasili za Kikamba zilipakuliwa na kuhifadhiwa kwenye

diski. Nyimbo hizo zilisikilizwa, kupangwa na kunakiliwa kwenye daftari. Hivyo, nyimbo hizo zimerejelewa mara kwa mara ambapo data za utafiti zimechaguliwa na hatimaye kunakiliwa. Data ya utafiti huu imetokana na nyimbo arobaini na moja za kiasili za Kikamba zinazoimbwa katika hafla maalum. Nyimbo zilizolengwa hapa ni zile zinazosheheni jazanda na ambazo zinawasilisha itikadi mbalimbali.

3.5 Uchanganuzi na Ufasiri wa Data

Data iliyokusanywa ilipangwa na kuchanganuliwa kwa kuiainisha kulingana na malengo ya utafiti. Uchanganuzi na ufasiri wa data umeongozwa na malengo, maswali pamoja na mihimili ya nadharia za utafiti. Mtafiti amezipambanua nyimbo za kiasili za Kikamba kwa mujibu wa hafla zinamowasilishwa. Hapa, nyimbo 41 zimeainishwa kwa mujibu wa ni wapi, lini na kwa nini zinawasilishwa. Pia, mtafiti amezichanganua jazanda zinazojitokeza katika nyimbo mahsusi kwenye hafla mbalimbali. Baada ya kuzitambua jazanda katika nyimbo teule, mtafiti amezibainisha kwa kuzifafanua. Baadaye, mtafiti alizichanganua itikadi zilizowasilishwa kijazanda katika nyimbo mahsusi za Kikamba. Mtafiti amezifasiri jazanda hizo kwa kuonyesha itikadi mbalimbali zilizofumbatwa mle. Hapa, uchanganuzi wenyewe umezingatia maoni na tajriba ya mtafiti kama mwanajamii Mkamba, pamoja na mihimili ya nadharia za utafiti. Hatimaye, uamilifu wa jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba ulihakikiwa.

3.6 Upangaji na Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Upangaji na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu umefanywa kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Utafiti wenyewe umedhihirisha matokeo kupitia vielelezo kutokana na nyimbo teule. Pia, vielelezo vya michoro vimetumika kwenye uchanganuzi wa jazanda mahsusi zinazojitokeza kwenye NKK. Baada ya uchanganuzi na ufasiri wa data, upangaji na uwasilishaji wa matokeo umefanywa kwa njia ya

kimaelezo. Maelezo ya matokeo ya utafiti yamewasilishwa katika sura mahsusi za tasnifu hii.

SURA YA NNE

JAZANDA KATIKA NYIMBO ZA KIASILI ZA KIKAMBA KWENYE

HAFLA MBALIMBALI

4.0 Utangulizi

Sura hii imeegemezwa kwenye lengo la kwanza la utafiti huu. Lengo lenyewe ni upambanuzi wa jazanda mahsusi zinazojitokeza katika nyimbo za kiasili za Kikamba zinazowasilishwa kwenye hafla maalum za kijamii. Uchunguzi wa hafla umeongozwa na mhimili wa tano wa nadharia ya Itikadi ambao unaangazia maumbo ya muktadha. Kwa upande mwingine, upambanuzi wa jazanda zinazojitokeza katika nyimbo teule umeongozwa na nadharia ya Jazanda Dhanifu.

4.1 Upambanuzi wa Hafla Zinamoimbwa Nyimbo za Kiasili za Kikamba

Uchunguzi wa hafla zinamoimbwa NKK umeongozwa na mhimili wa maumbo ya muktadha. Mhimili wa maumbo ya muktadha unashikilia kuwa muktadha ndilo umbo la kipekee linalotekeleza wajibu muhimu katika matini na mawasiliano. Muktadha unachangia pakubwa katika ufasiri wa ujumbe unaopitishwa katika kazi yoyote ya kifasihi zikiwemo nyimbo za kiasili za Kikamba. Hii ni kwa sababu uteuzi wa lugha inayotumika katika kutunga na kuwasilisha wimbo maalum hutegemea muktadha. Kwa msingi huu, uteuzi wa matumizi ya jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba hutegemea mazingira ambamo nyimbo teule zimetungiwa na kupokelewa. Hali kadhalika, ufasiri wa ujumbe unaopitishwa kijazanda katika NKK hutegemea muktadha wa utunzi na upokezi wa nyimbo hizi. Maumbo ya muktadha yanaweza kuwa ya kisiasa, kindoa, kidini, kikazi na hata kitohara kutegemea sherehe muktadha inayohusika. Kwa hivyo, maumbo haya ya kimuktadha ndiyo hafla ambamo NKK hujikita au huimbwa. Upambanuzi wa hafla zinamoimbwa nyimbo za kiasili za Kikamba unachangia katika uelewekaji wa jazanda na ufasiri wake. Hii ni kwa sababu

umuhimu wa jazanda katika kazi yoyote ya fasihi hudhihirika katika uamilifu wake kwenye muktadha unaohusika. Hivyo, mtafiti wa kazi ya fasihi hana budi kuangazia hafla mbalimbali ambamo utanzu unaohusika huwasilishwa. Dhana ya hafla imetumika kurejelea shughuli, hali na maeneo mbalimbali ambamo nyimbo za kiasili za Kikamba huimbwa. Hafla ya kijamii hapa inajibu maswali: *Je, wimbo maalum wa kiasili unaimbiwa wapi, unaimbwa lini na katika mazingira gani?*

Utafiti huu umebaini kuwa nyimbo za kiasili za Kikamba hutungwa na kuimbwa kwa makusudi maalum na katika hafla mahsusi ya kijamii. Aidha, imedhihirika kuwa uainishaji wa hafla za uimbaji wa nyimbo za kiasili huzingatia vipengele mbalimbali. Vipengee hivi ni kama vile idadi ya waimbaji, jinsia yao, hadhi yao kijamii na hara umri wao.

Zaidi ya hayo, utafiti huu utafiti huu umetambua kwamba urasmi wa tukio la uimbaji ndicho kipengee muhimu zaidi katika kupambanua hafla husika. Kwa hivyo katika utafiti huu, uainishaji wa hafla za uimbaji wa NKK umeegemezwa kwenye kigezo cha matukio rasmi na matukio yasiyo rasmi.

4.1.1 Hafla Rasmi

Hafla za uimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba huchukuliwa kuwa rasmi iwapo zimepangwa, zimeagizwa na wakati mwingine kuratibiwa. Katika hali kama hii, shughuli maalum ya kijamii haikamiliki bila kuwepo kwa nyimbo maalum za kiasili za Kikamba. Miongoni mwa hafla rasmi ni sherehe za kuzaliwa kwa watoto, arusi, mazishi, tohara, uongozi na ibaada za kidini. Kwa mfano, *Mbathi sya Mathiko/Iio* (Mbolezi) huimbwa katika hafla ya mazishi huku *Mbathi sya Nzaiko* (Nyiso) zikiwasilishwa katika hafla za tohara. Vilevile, *Mbathi sya Mutwaano* (Nyimbo za ndoa) ni nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za arusi au ndoa.

4.1.1.1 *Syathi sya nzaiko* (Hafla za tohara)

Syathi sya Nzaiko (Hafla za Tohara) huhusiana na tohara. Katika jamii ya Wakamba, tohara ni hatua muhimu katika maisha ya wanajamii. Mojawapo wa wimbo wa kiasili wa Kikamba unaowasilishwa katika hafla ya tohara ni *Kwa Sisy Wone* (Angalia Uone) kama unavyodhihirika katika mfano **NA.1**.

NA. 1. Kwa Sisy Wone

Aikwa: *Twauma kuasa. Twauma kuasa ii. Tukite nzaikoni kwa Mutinda. Kwa sisy wone Kwa sisy wone*

Mwaiki: **Muti** uu ni mumu. Muti uu ni mumu. Umite nza na nthini nomwiu. Ninguutila! Watahiriwa: Tila

Mwaiki: *Ninguutila*

Aikwa: *Tila*

Mwaikwa: *Ekai ukia ta **matila ma kiimani** Matesi **mbilano***

Tafsiri

Angalia Uone

Watahiriwa: *Tumetoka mbali. Tumetoka mbali. Tumekuja jandoni kwa Mutinda. Angalia uone Angalia uone.*

Ngariba: *Mti huu umekauka. **Mti huu umekauka.** Umekauka nje lakini ndani ni mbichi Nitaukata*

Watahiriwa: *Ukate*

Ngariba: *Nitaukata*

Watahiriwa: *Ukate*

Ngariba: *Wacheni kuogopa Kama **wajinga wa milimani** wasiojua **kazi.***

Wimbo huu huimbwa na watahiriwa wakieleza kwamba kwamba wametoka mbali kuja kushiriki katika tohara iliyoandaliwa katika boma la mmoja wao, Mutinda.

Tazama mshororo huu:

*Twauma kuasa. Twauma kuasa ii. Tukite nzaikoni kwa Mutinda.
Kwa sisy wone Kwa sisy wone*

Tafsiri: *Tumetoka mbali. Tumetoka mbali. Tumekuja jandoni kwa Mutinda.*

Maelezo haya yanaashiria umuhimu wa hatua hii ya tohara katika maisha ya watahiriwa. Kupitia kwa hatua hii, mhusika alifuzu kutoka utotoni hadi utu uzima. Naye ngariba anauendeleza wimbo kwa kusema kuwa mti huu umekauka nje lakini

ndani ni mbichi. Anawauliza watahiriwa iwapo watamrufusu aukate nao wanajibu kuwa aukate. Tazama kifungu hiki:

Ngariba: Muti uu ni mumu. Muti uu ni mumu. Umite nza na nthini nomwuu. Ninguuutila! (Mti huu umekauka. Umekauka nje lakini ndani ni mbichi Nitaukata)

Watahiriwa: *Tila* (ukate)

Mti unaorejelewa hapa ni mboo za watahiriwa. Mboo zenyewe ndizo hukatwa wakati wa tohara. Ukataji wa sehemu hii ya mwili ni ishara ya kutoka utotoni hadi utu uzima. Baada ya tohara, watahiriwa hutwikwa majukumu mbalimbali ya utu uzima. Kwa mfano baada ya tohara, watahiriwa huwa amehitimu kuo na kutekeleza tendo la ndoa. Kupitia wimbo huu, watahiriwa wanahimizwa wasiwe waoga kama wajinga wa mlimani. Hapa wajinga wa mlimani ni kirai nomino kinachorejelea jamii ya Wakikuyu ambao ni majirani wa Wakamba. Wakamba huwabeza Wakikuyu kuwa ni wazembe hasa katika masuala ya ngono. Wanahimizwa watekeleze majukumu yote ipasavyo.

Wimbo huu ulikusudiwa kuwaandaa kihisia watahiriwa kwa kuwapa ari ya kustahimili wembe wa ngariba. Maneno *muti mumu (mti uliokomaa)*, *mbilano (kazi)* na *matila ma kiimani (wajinga wa milimani)* yametumika kijazanda ili kuwasilisha itikadi maalum kuhusiana na tohara. Wakati wa tohara, watahiriwa walipokezwa mafunzo na stadi mbalimbali kuhusu maisha. Kwa mfano, ni wakati huu ambapo wahusika walipewa mafunzo kuhusu tendo la ndoa. Kupitia kwenye wimbo huu, watahiriwa wanashauriwa wasiwe waoga kama wajinga wa milimani wasiojua kazi. Woga unaorejelewa hapa ni wa kiwembe cha ngariba pamoja na majukumu yanayoambatana na ndoa. Kwenye jamii ya Wakamba, inaaminika kwamba ndoa na tendo la ndoa ndiyo njia ya pekee ya kuviendeleza vizazi vyao.

Mfano mwingine wa wimbo wa kiasili wa Kikamba uliowasilishwa kwenye hafla ya tohara ni *Munyambu nuukiva* (Simba ananguruma). Wimbo huu unadhihirika katika mfano NA.2.

NA. 2. *Munyambu Nuukiva*

*Munyambu nuukiva. Munyambu nuukiva wi ukavi. Ni nau uwitie
Munyambu nuukiva. Ni nau uwitie. Sisy ndukalilie. Ni nau uwitie*

Tafsiri

Simba Ananguruma

Simba ananguruma. Simba ananguruma akiwa Umasaini. Ni baba aliyemwita. Simba ananguruma. Ni baba aliyemwita. Chunga usitetemeke. Ni baba aliyemwita.

Wimbo NA. 2 unasimulia kuhusu simba ambaye ananguruma na aliyemitwa na baba mzazi wa mtahiriwa. Wimbo huu uliimbwa ili kumsifu ngariba. Jukumu la kuchagua ngariba atakayetahiri vijana lilitwikwa baba wa mtahiriwa au mjomba wake. Ngariba alichaguliwa kwa kuzingatia hulka zake, tajriba na ustadi wake wa kutahiri vijana vizuri na ambaye alitumia dawa nzuri ya kuponya kidonda haraka. Kwa kumsifu ngariba, watahiriwa waliweza kuwa na imani naye na pia ngariba alihisi amethaminiwa na jamii. Katika muktadha huu wa tohara, neno *munyambu* (simba) limetumika kijazanda kurejelea ngariba maarufu na shupavu.

Mfano mwingine wa wimbo wa kiasili wa Kikamba uliowasilishwa kwenye hafla ya tohara ni *Mwaikwa Niwalika Ndiani* (Mtahiriwa Umeingia Kidimbwini) kama unavyodhihirika katika NA. 3.

NA. 3. *Mwaikwa Niwalika Ndiani*

Onthe: *Mwaikwa ii*

Mwaikwa: *Mwaikwa ii*

Onthe: *Yu niwalika ndiani*

Mwaikwa: *Yu niwalika ndiani*

Onthe: *Ndiani ya kulungilwa.*

Mwaikwa: *Mwaikwa niwalika ndiani*

Onthe: *Neewua maikulanya Kavila
eya kyau?*

Mwaikwa: *Neewua maikulanya Kavila
eya kyau?*

Tafsiri

Mtahiriwa Umeingia Kidimbwini

Wote: Mtahiriwa ii

Mtahiriwa: Mtahiriwa ii

Wote: Sasa ameingia **kidimbwini**.

Mtahiriwa: Sasa ameingia kidimbwini

Wote: Kidimbwi cha kujitegemea.

Mtahiriwa: Mtahiriwa umeingia
kidimbwini.

Wote: Nimesikia wakiulizana Kavila
atakula nini?

Mtahiriwa: Nimesikia wakiulizana Kavila
atakula nini?

Mwimbaji katika wimbo huu anaeleza kwamba mtahiriwa ameingia katika kidimbwi.

Neno **ndiani** (**kidimbwini**) limetumika kijazanda kurejelea hali ya kujitegemea.

Wimbo huu ulikusudiwa kumpa mtahiriwa mawaidha ya maisha ya utu uzima na majukumu yanayomsubiri pasipo kuwategemea wazazi wake. Watahiriwa wanajuzwa kuhusu majukumu yao mapya na kile jamii inatarjia kutoka kwao. Kupitia kwa wimbo huu, watahiriwa wanaandaliwa kisaikolojia kuwa kuachana na tabia za kitoto na kuwa tayari kutekeleza majukumu ya watu wazima. Kwa hivyo wimbo **NA.3** unawashajiisha watahiriwa kuwa na hamu ya kutoka katika hatua ya utoto na kuingia katika hatua ya utu uzima.

Wimbo mwingine wa kiasili unaowasilishwa kwenye hafla ya tohara miongoni mwa

Wakamba ni **Kaindo** unaodhihirika katika mfano **NA.4**

NA.4. Kaindo

*Ve **kaindo** kala ngumanza kana niwe uvithite na ndandavasya ngumanza. Ve kaindo kala ngumanza Kana niwe uvithite, Na ndandavasya ngumanza. **Kanyaa** niwe uvithite, Na ndandavasya ngumanza. Ve **kaindo** kala ngumanza kana niwe uvithite na ndandavasya ngumanza. **Kanyaa** niwe uvithite, Na ndandavasya ngumanza. Ve **kaindo** kala ngumanza kana niwe uvithite na ndandavasya ngumanza **Vaati** niwe uvithite, na ndandavasya ngumanza. Ngutavye niwe uvithitei, na ndandavasya ngumanza.*

Ngutavye niwe uvithitei, na ndandavasya ngumanza. Mulekye niwe uvithite, na ndandavasya ngumanza.

Tafsiri

Kijitu

Kuna **kijitu** ninachokitafuta, sijui kama ndiye amekificha, na haniambii nikikitafuta. Kuna kijitu ninachokitafuta, Sijui kama ndiye amekificha na haniambii nikikitafuta. **Kanyaa** ndiye amekificha na haniambii nikikitafuta. Kuna **kijitu** ninachokitafuta, sijui kama ndiye amekificha, na haniambii nikikitafuta. **Kanyaa** ndiye amekificha, na haniambii nikikitafuta. Kuna **kijitu** ninachokitafuta, sijui kama ndiye amekificha, na haniambii nikikitafuta. **Vaati** ndiye amekificha, na haniambii nikikitafuta. **Mulekye** ndiye amekificha na haniambii nikikitafuta.

Wimbo huu uliwalenga watahiriwa wa kiume. Mwimbaji anaeleza kwamba kuna kijitu anachokitafuta na hana hakika na aliyekificha. Hapa, mwimbaji anataja baadhi ya majina ya jinsia ya kike kama vile **Kanyaa, Vaati** na **Mulekye** miongoni mwa Wakamba. Anadai wao ndio waliokificha kijitu anachokitafuta. Katika muktadha wa tohara, watahiriwa wa kiume walitarajiwa kuoa. Hivyo, majina ya wahusika wa kike **Kanyaa, Vaati** na **Mulekye** yametumika kijazanda kurejelea utayari wa watahiriwa kupata jiko. Wimbo wenyewe umebeba itikadi ya tohara kwamba watahiriwa wamehitimu kuoa au kupata jiko. Hivyo, wimbo wenyewe unawaandaa wahusika kwa jukumu la ndoa baada ya kupashwa tohara. Hivyo, maneno **Kanyaa, Vaati, Mulekye** na **Kaindo** yametumika kijazanda ili kufumbata itikadi ya ndoa na tohara katika wimbo huu.

Mfano wa tano wa wimbo wa tohara ni kama ufuatao:

NA.5. Mwatu

Ila wiw'aa ngiweta, ila wiw'aa ngiweta ndeto sya usenyo mwinawa ala usemba wone watungwa na ikwani. Ila wiw'aa ngiweta, ila wiw'aa ngiweta ndeto sya usenyo mwinawa ala usemba wone watungwa na ikwani. Ala usemba wone, watungwa na ikwani. Ala usemba wone, watungwa na ikwani.

Nyamu ni ndevelovumendi niyo king'ong'o wona kana ka mundu tata na vinya usembe ndukatumbwe ni ikwani. Ala usemba wone,

watumbwa ni ikwani. Wona kana ka mundu tata na vinya wivithe ndukatumbwe ni ikwani. Ala usemba wone, watumbwa ni ikwani.

*Ukwa **mwatu** uno nukutha na ndwina **uki** mwinawa mwatu uno nukutha **nzuki** na ndwina nzuki mwinawa kai syiminwa ni **ngaku** mwatu usu nduuisiasya. Ukwa mwatu uno nukutha na ndwina nzuki mwinawa mwatu uno nukutha na ndwina nzuki mwinawa kai syiminwa ni ngaku mwatu usu nduuisiasya.*

Tafsiri

Mzinga

Unaposikia nikisema, unaposikia nikisema maneno ya kushangaza ndugu yangu mdogo, hebu kimbia uone ukirudishwa na kesi. Unaposikia nikisema, unaposikia nikisema maneno ya kushangaza ndugu yangu mdogo, hebu kimbia uone ukirudishwa na kesi. Hebu kimbia uone ukirudishwa na kesi. Hebu kimbia uone ukirudishwa na kesi.

Tendo hili linaitwa kunaswa na mtego ukimwona mtoto wa mwenyewe jaribu ujepushe naye usiangukiwe na kesi. Hebu kimbia uone, utaangukiwa na kesi. Ukimwona mtoto wa mwenyewe jaribu ujifiche usiangukiwe na kesi.

Unajua huu **mzinga** unaonekana kama una **nyuki** wengi na kumbe hamna **asali** kaka yangu, kumbe nyuki wanaangamizwa na **ngaku**, hujachunguza mzinga vizuri. Unajua huu mzinga unaonekana kama una nyuki wengi na kumbe hamna kaka yangu, kumbe nyuki wanaangamizwa na ngaku hujachunguza mzinga vizuri.

Katika wimbo huu, mwimbaji anaanza kwa kutusawiria hali ambapo kijana husika amejipata pabaya kutokana na uhusiano wa kimapenzi na msichana mndogo. Anamweleza kwamba kwa sasa yumo mashakani kwa maana ameshtakiwa na ana kesi, inayomfanya kuwa na mashtaka ya kujibu kortini. Wimbo huu unabainisha kuwa katika sherehe ya jando, mwanajamii mwenye tabia hasi alitajwa na kosa lake likakejeliwa hadharani kupitia nyimbo. Kwa sababu hii, kila mwanajamii alijaribu kukwepa kutenda jambo lolote lililoenda kinyume na maadili ya jamii asije akaaibishwa wakati wa sherehe za jando.

Ni katika hali hii ambapo mwimbaji anawaonya vijana watahiriwa kuwa wasijihusishe na mahusiano yasiyokuwa halali. Ujumbe unaopitishwa hapa ni

kwamba uhusiano wa kimapenzi baina ya watoto si halali. Yaani, inawezekana ukamwona kijana ambaye ni mkubwa kimwili, ila kiumri hajafikisha kiwango cha utu uzima. Hivyo, mahusiano ya aina hiyo yamepigwa marufuku miongoni mwa Wakamba. Mahusiano kama hayo ni kinyume cha sheria na huenda yakamtumbukiza mtu katika matatizo.

Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anawaonya vijana wajiepushe na tabia za unajisi. Anawaeleza kwamba wasipokuwa waangalifu huenda wakajipata kwenye kesi za ubakaji. Mwimbaji anawaonya vijana wasijihusishe kingono na watoto wadogo. Mwimbaji anaposema “Mzinga hauna asali japo nyuki wanaonekana wakiuzingira” anafumbata ujumbe kijazanda kumaanisha kwamba japo watoto wanaweza kuvutia, hawajakomaa kushiriki tendo la ngono. Maneno **nzuki (nyuki)**, **ngaku (mnyama anayewala nyuki)** na **mwatu (mzinga)** yametumika kijazanda ili kuwasilisha itikadi ya jamii ya Wakamba kuhusiana na suala la ngono.

Ni bayana kuwa nyimbo za kiasili za Kikamba zilizoimbwa katika hafla ya tohara zilitumia jazanda mbalimbali. Jazanda hizi zilifumbata itikadi kuhusiana na hulka na tabia za washiriki katika tohara na pia majukumu hasa ya watahiriwa katika Maisha yao ya utu uzima.

4.1.1.2 Syathi sya siasa (Hafla za kisiasa)

Syathi sya siasa (Hafla za kisiasa) zinahusisha sherehe na mikutano katika miktadha ya kisiasa. *Mbathi sya siasa* ni aina ya nyimbo zinazoimbwa katika hafla za kisiasa miongoni mwa Wakamba. Mara nyingi nyimbo hizi huwasilisha masuala mapana kama vile mapambano, propaganda, kuzindua, kuhamasisha, kukejeli, kuhimiza au kutia ari. Katika vipindi vya uchaguzi wa viongozi nchini, baadhi ya wanasiasa wa jamii ya Wakamba huwalipa watunzi na waimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba

ili wawasaidie katika kampeni zao. Kupitia kwa nyimbo hizi, wanasiasa huuza sera, ajenda na manifesto zao na hatimaye kupata nyadhifa za uongozi. Nyimbo za kiasili za Kikamba za kisiasa huimbwa na wasanii wenyewe, wanasiasa, wafuasi wa wanasiasa hao pamoja na hadhira katika mikutano ya kisiasa.

Mara kwa mara, baadhi ya waimbaji mashuhuri wa nyimbo husika huzawadiwa na wanasiasa au hadhira ya watazamaji na wasikilizaji wakati wanapoziwasilisha nyimbo hizo. Wakati mwingine, baadhi ya waimbaji hutunga nyimbo zinazoendeleza sera za serikali iliyomo uongozini. Kwa mujibu wa utafiti huu, imebainika kwamba baadhi ya nyimbo za kisiasa huwasifu viongozi wanaohusika. Wakati mwingine, nyimbo hizi hutumika kuwakejeli na kuwakashifu viongozi wasiokuwa waadilifu. Hivyo, wimbo wa siasa unachukuliwa kuwa ule unaohusisha siasa, matukio, ajenda, vyama na mawazo ya kisiasa. Ufuatao ni mfano wa wimbo wa kiasili wa Kikamba unaoimbwa katika hafla za kisiasa:

NA.6. Maendeleo ma Wia

Iyuu, Uhulu na nowe silikali tutanie silikali na utanu mwingi, silikali ina muuo ngitunga muvea. Miongo thanthatu na itatu nowo twosie usumbi. Ii wambiiwe ii ni Kinyatta ukaatiswa laisi ii mwikilye nimutavye Uulu nukuthukuma athukume na kithito. Iyuu, Uulu na nowe silikali tutanie silikali na utanu mwingi, silikali ina muuo ngitunga muvea. Miongo thanthatu na itatu nowo twosie usumbi. Ii wambiiwe ii ni Kinyatta ukaatiswa laisi ii mwikilye nimutavye Uulu nukuthukuma athukume na kithito.

Ii miongo thanthatu na itatu now'o twosie usumbi. Ii wambiiwe ii ni Kinyatta ukaatiswa laisi ii mwikilye nimutavye Uulu nukuthukuma athukume na kithito. Ii miongo thanthatu na itatu now'o twosie usumbi. Ii wambiiwe ii ni Kinyatta ukaatiswa laisi ii mwikilye nimutavye Uulu nukuthukuma athukume na kithito.

*Iyaaii, Savali nongwenda kuulukya **kikungu** ngome ngiivindua, nonguthingithangya valasa ndia nawina. Niwina nesa Velezi niwina nikue, ngenuka nenda mwa Uhulu ndwose ngethi. Maendeleo kwitu nguluvu twenda ngwatano, maendeleo ma wia. Maendeleo kwitu nguluvu twenda ngwatano, maendeleo ma wia. Ithyonze twenda kwiw'ana, maendeleo ma wia. Uulu twenda kwiw'ana, maendeleo ma wia.*

Tafsiri

Maendeleo ya Kazi

Iyaa! Uhuru na ndiye serikali tufurahie serikali kwa furaha kubwa. Serikali ina amani natoa shukrani. Sitini na tatu ndio tuliupata uhuru. Ee aliyeanzisha ni Kenyatta kisha akafuatia rais ee, wacha niwaambie, Uhuru atafanya kazi aifanye kwa bidii. Iyaa! Uhuru na ndiye serikali tufurahie serikali kwa furaha kubwa. Serikali ina Amani natoa shukrani. Sitini na tatu ndio tuliupata uhuru. Ee aliyeanzisha ni Kenyatta kisha akafuatia rais ee, wacha niwaambie, Uhuru atafanya kazi aifanye kwa bidii.

Sitini na tatu ndio tuliupata uhuru. Ee aliyeanzisha ni Kenyatta kisha akafuatia rais ee, wacha niwaambie, Uhuru atafanya kazi aifanye kwa bidii. Sitini na tatu ndio tuliupata uhuru. Ee aliyeanzisha ni Kenyatta kisha akafuatia rais ee, wacha niwaambie, Uhuru atafanya kazi aifanye kwa bidii

Iyaaii, Savali nataka kusababisha **vumbi**, nilale nikijigeuza, nitawaguza wanabaraza, nitaimba vilivyo. Nitauimba vizuri Velesi nitauimba (wimbo) hadi nitosheke. Nitaenda nyumbani nitakapohitaji kufanya hivyo, Uhuru pokea salamu. Maendeleo kwetu wanavikundi tunahitaji umoja, maendeleo ya kazi. Sote twahitaji umoja, maendeleo ya kazi. Uhuru twahitaji masikilizano, maendeleo ya kazi.

Katika wimbo *Maendeleo ma wia (Maendeleo ya Kazi)*, mwimbaji anaanza kwa kutoa shukrani zake kwa rais kwa sababu ya amani inayoshuhudiwa kote nchini. Anaendelea kumsifu kiongozi huyo huku akieleza kwamba hana shaka kwamba rais anayehusika atafanya kazi kwa bidii na kwamba juhudi zake zitaleta maendeleo nchini. Vilevile mwimbaji anaeleza kwamba nchi hii ilijipatia uhuru mnamo mwaka wa 1963, huku rais wa kwanza wa Jamhuri ya Kenya akiwa Mzee Jomo Kenyatta. Katika ubeti wa mwisho wa wimbo huu, mwimbaji anaeleza kwamba ataimba na kucheza hadi **vumbi** isambae kote.

Wimbo huu umetumika kama rekodi ya tukio la kihistoria la upiganiaji na upataji wa uhuru nchini. Wimbo huu pia unawasilisha ujumbe unaohusiana na itikadi ya kisiasa kwa jamii ya Wakamba. Kwa hivyo, ujumbe huu wa kisiasa ndio unaorejelewa kijazanda kama vumbi. Katika muktadha wa kisiasa ambamo wimbo huu umeimbwa, neno **vumbi** limetumika kijazanda kuashiria ujumbe unaokusudiwa kuwafikia

hadhira. Mwimbaji anatarajia kwamba ujumbe wake utaenea kote kama ambavyo **vumbi** huenea inapoeperushwa na upepo. Ujumbe wenyewe ni kwamba wanajamii wasiwe na shaka kwani kiongozi aliye mamlakani ana uwezo wa kuwafanyia kazi itakayozaa matunda ya maendeleo nchini.

Mfano mwingine wa wimbo katika hafla ya kisiasa ni ufuatao:

NA.7. Nzambi akithambya Nzele

Nzambi akithambya nzele ii ya kuthamba ii we wimwia ii undu uu ni waki? Nzambi akithambya nzele. Nzambi akithambya nzele ii ya kuthamba ii we wimwia ii undu uu ni waki? Nzambi akithambya nzele. Ekai umwia ii wa Katuta ii, Nzambi akithambya nzele. Ndanaumyai mundu uu Katuta? Nzambi akithambya nzele. Ekai ukulya ii ai kuyi na mbua ii niki? Nzambi akithambya nzele. Mukulasya ii mundu uu watata ii Nzambi akithambya nzele.

Tafsiri

Nzambi Akiosha Kata

Nzambi akiosha **kata** ya kuogea ee wewe unamwambia eti hivi ni kwa nini? Nzambi akiosha kata. Nzambi akiosha kata ya kuoga ee wewe unamwambia eti hivi ni kwa nini? Nzambi akiosha kata. Wacheni kumwambia ee eti wa Katuta, Nzambi akiosha kata. Hajaitoa ewe mtu wa Katuta, Nzambi akiosha nzele. Wacheni kuuliza eti na hakuna mvua kwa nini? Nzambi akiosha kata. Mnauliza mtu huyu mtoto wa babangu, Nzambi akiosha kata.

Katika wimbo *Nzambi akithambya nzele* (Nzambi akiosha kata), mwimbaji anatusawiria hali ambapo mhusika Nzambi anaosha vyombo aina ya kata. Tunaelezewa hali ambapo Nzambi anapoosha kata, kuna wale walio na maswali na malalamishi mbalimbali. Hivyo, mwimbaji anawarai walalamishi husika wampe muda Nzambi afanye kazi anayoishughulikia. Wimbo huu ni wa kisiasa ambao umewasilishwa kimapumbo. Katika muktadha wa kisiasa, maneno **Nzambi (huoga/msafi)** na **nzele (kata)** yametumika kijazanda kurejelea kiongozi mpya aliyepewa uongozi. **Kata** ni vyombo ambavyo vinahitaji kuoshwa baada ya kutumiwa. Katika muktadha huu mwimbaji anahimiza hadhira impe kiongozi wao nafasi ya kuondoa ufisadi na maovu yaliyofanywa na kiongozi wa awali.

Wimbo wa tatu katika hafla ya kisiasa ni NA. 8. kwa jina *Munuve* kama ifuatavyo:

NA. 8. Munuve

*Munuve tata ii manya ukia kindu **simba ii syi ngunyu** nitwasyelile.
Munuve tata ii manya ukia kindu **simba ii syi ngunyu** nitwasyelile.
Munuve tata ii manya ukia kindu **simba ii syi ngunyu** nitwasyelile.
Munuve tata ii manya ukia kindu **simba ii syi ngunyu** nitwasyelile.*

*Mundu ungi ndasyoka mbunge, Mundu ungi ndasyoka mbunge
matuku kenda twitunga Munuve. Matuku aa ii twitunga Munuve.
Asevuye kisomo, twitunga Munuve. Mwana waitu ii, ndukile
utwokoe. Mwana wa Mati ii, ndukile utwokoe.*

*Twina thina mwingi, twina thina mwingi na ukilitye misyi, ndukile
tata ii ndukile utwokoe. Twina thina mwingi, twina thina mwingi na
ukilitye misyi, ndukile tata ii ndukile utwokoe. Andu ma Tseikuru
tuikwenda mundu masiwa lala twenda ngumbau mundu ta **Munuve***

Tafsiri

Munuve

Munuve baba, ee usiogope chochote **simba wenye makucha** tushayakata. Munuve baba, ee usiogope chochote **simba wenye makucha** tushayakata. Munuve baba, ee usiogope chochote **simba wenye makucha** tushayakata.

Mtu mwingine hawezi kurudi bungeni, Mtu mwingine hawezi kurudi mbungeni tarehe tisa tutamrudisha Munuve. Tarehe hii ee, tutamrudisha Munuve. Aunde elimu, tutamrudisha Munuve. Mtoto wetu ee, amka utuokoe. Mwana wa Mati ee, amka utuokoe.

Tuna shida nyingi, tuna shida nyingi zimejaajaa humu nyumbani, amka baba amka utuokoe. Tuna shida nyingi, tuna shida nyingi zimejaajaa humu nyumbani, amka baba amka utuokoe. Watu wa Tseikuru hatutaki mtu **maziwa lala** tunataka jasiri mtu kama **Munuve**.

Wimbo wa *Munuve* ni wa kisiasa pia. Katika kifungu cha kwanza, waimbaji wanamhimiza mwanasiasa Munuve kwamba asiwe na hofu. Wanamrai ajitose katika kinyang'anyiro cha kung'ang'ania cheo cha ubunge. Katika kifungu cha pili, wanaahidi kuwa watamuunga mkono katika shughuli hiyo. Wanaeleza kwamba tarehe tisa, tarehe ya uchaguzi, watampigia (Munuve) kura. Kwenye vifungu vya mwisho, waimbaji hawa wanaonekana wakiwa na matumaini makubwa na mwanao huyu

ambaye wangetaka awe mbunge ili kuwatatulia matatizo na shida nyingi wanazozishuhudia. Katika wimbo Na.8 tunapata jazanda ya **Munuve (anayewanyima)** inayorejelea kiongozi wa upinzani. Jina lenyewe linaashiria hali ya kutowapa nafasi viongozi wafisadi. **Simba wenye makucha** nao wanarejelea viongozi fisadi. Kwa hivyo, mwimbaji anamhimiza mpinzani wa kiongozi aliyepo asiogope kujitokeza nyanjani kumpinga kiongozi ambaye ametumia mamlaka vibaya.

Wimbo NA. 9. ni mfano mwingine wa wimbo wa hafla ya siasa:

NA. 9. Usumbi ni Nzou

*Ni mukwatania wa tene wakutungiania mbai Kuma enzi ya Moi kuvika o vaa Kibaki unaminile utawala tutanambiia **mirugo** kurugania ta mang'oi. Myaka isu twimina na uruga uruga.*

Ngumangano ila mwinasyo ikwiwa ni sya kumanza usumbi usumbi ndwaamanzwa ii nandu kwaandikawa mathi maumange angi. Nasu namo mokile na mithato makeyumie vau mwinatetheka mwiteethya mavisi

*Andu ala mwi ngaliko ino Na ala mwi ngaliko iya mukwona muyonania muyonania winzi mukanyungia unyungia. Ngiti syathi na mukwato nzyima ndyendeeaa mwithi mukove ii **ngiti** Ii **nyamu** syonze ti sya ngiti **Nzou** ikungiawa ukungiwa.*

*Usumbi aume ni **nzou** na nzou **ngiti** ikwamba uu ndithengeeleka isu kila mundu ndove syake na mukuthi Mwambasa Muthama mukevingie. Muvisi ava ndikwona vandu mutathi nzi ino mwina Nduya Muthama kwaambiia a ve Musila, Kiema nginya Charity. Andu onthe matungianiwe ndokta Malombe twambe kumbania mbai Kivutha evo Kivwana Musimba e vau vau na unyuvani wavika ungamya ula ukwenda na ndukaume asu angi. Mundu umwe atwike ngavana **kitanda** ndukilisya **aume** eli me vamwe.*

*Ninisi ninaananga **ngima** neekia ve **mboka** nauluania vandu vamwe mwiiya vau inywonthe. Ii aa Masika Mutambu Mwendwa wa Mwova wikilye **kiw'u** umathambye. Mathambye meiiya vau monze. Ii mbaa lili ta Akamba ukilai mwaangumangei wathi unokie uilye uu.*

*Andu ala mwi ngaliko ino na ala mwi ngaliko iya mukwona muyonania muyonania winzi (**mwiv'a**) mukanyenya **mithumo**. Ngiti syathi na mukwato **nzyima** ndyendeeaa mwithi mukove ii **ngiti** nyamu syonze ti sya ngiti **nzou** ikungiawa ukungiwa.*

Tafsiri

Urais ni Ndovu

Mimi ni mpatanishi wa mbari wa tangu jadi, tangu nyakati za Moi hadi hivi majuzi ambapo Kibaki alikamilishia utawala wake kabla ya kuanza **urukaji** kurukaruka kama punda miaka hiyo tutaimaliza kwa kurukaruka?

Matusi mliyonayo yanasemekana ni ya kutafuta urais urais haujawahi tafutwa eti kwa kuwatuma watu waende kuwatusi wengine. Hao nao wainuke kwa hasira kuwatusi wenzao pia. Hapo hamjasaidika mmewasaidia vijana.

Watu mlio upande huu na wale mlio upande ule, vile hamwezi kuonyeshana (mwiba) ulio chini ni kunusa mtanusia urais. Mbwa wakienda mawindoni na hisia za kimapenzi uwindaji haufanyiki Nendeni mkawafunge hawa **mbwa wanyama** wote si wa mbwa **Ndovu** hunyemelewa kunyemelewa

Jamani urais ni **ndovu** na huwezi kumkaribia ndovu **mbwa** wakibweka hivyo. Hao, kila mtu afunge wake. Halafu Muthama mwende Mombasa mjifungie. Muvisi sioni popote hamwezi kwenda nchini mkiwa na Nduuya Muthama. Kuanzia alipo Musila, Kiema hata Charity watu wote waunganishwe Daktari Malombe. Tuanze kwa kuikusanya jamii ya Mkamba Kivutha akiwepo Kivwana. Musimba akiwa hapo hapo na uchaguzi ukifika simamisha yule unataka na usiwatusi wale wengine. Mtu mmoja awe gavana haupandishi **wanaume** wawili kwenye **kitanda** kimoja.

Najua nimeharibu **ugali** nikachanganya na **mboga** nikachanganya pamoja mtakulia hapo nyote. Ee akina Masika Mutambu Mwendwa wa Mwova weka **maji** uwanawishe wanawishe watalia hapo wote. Ee akina fulani kama Wakamba amkeni mkanitusi wimbo ulikuja ukiwa hivyo.

Watu mlio upande huu na wale mlio upande ule vile hamwezi kuonyeshana ulio chini (**mwiba**) mtaramba **visigino**. Mbwa wakienda **mawindoni** na hisia za kimapenzi uwindaji haufanyiki. Nendeni mkawafunge hawa **mbwa** wanyama wote si wa mbwa **ndovu** hunyemelewa kunyemelewa.

Wimbo *Usumbi ni Nzou (Urais ni Ndovu)* unatumia jazanda ya ndovu ambapo mwimbaji anaifananisha hali ya kutafuta cheo cha urais na uwindaji wa ndovu. Hapa, anaeleza kwamba wawindaji wa ndovu hawafai kwenda kwenye mawindo na mbwa.

Kifungu **kelele za mbwa** kimetumika kurejelea manunguniko, malalamishi na kutoelewana kwa wanasiasa katika jamii ya Wakamba. Tunaelezwa namna wanasiasa

wa jamii hii walivyogawanyika katika makundi mawili. Mwimbaji anawahimiza wawe na umoja. Muungano na utangamano ni muhimu iwapo wanahitaji kufanikiwa kisiasa. Katika wimbo huu, jazanda **ngiti (mbwa)**, **miambile ya ngiti (kelele za mbwa)**, **nyamu (Wanyama)**, **nzou (ndovu)**, **aume (wanaume)** na **kitanda (kitanda)** zimefumbata ujumbe wa kisiasa.

Ufuatao ni wimbo mwingine uliowasilishwa kwenye hafla ya kisiasa:

NA. 11. Kithio kya Mukamba

*Kithio twatiie kyonze vyu kithio kitu Syokimau letiu, letiu Kaundi, Athiani, Musyi, Kyeni, Mbaitu Mwenge mukilye kililimbi twai na mwathani mwathani wa ukamba **Syokimau** kithio tukituungiie Mukamba akuthuka ambiaa kwasya ni musomu ni mutangiie ndyendaa siasa ndyendaa kithio ni mutangiie na usu mundu ukathi umwithie akumiswa mayini malikile ku e mutangiie? Wamwithia Mombasa niwe **Bakari** niwe **Juma** Juma mukamba mwenda ndini syonze Mukamba ndusyoke syoka kithioni umanyiswe undu*

*Yila mwewaa mwana kuna **ngua** ti ngua ilinda kanywa nukunawa nzoni syi kanywani niw'o umanaa mwana wa Mukamba syoka kithioni umanyiswe undu. Ona usumbi uu mukumanza muimanye ni wa nzi ti wa matuni na mwiumanza mwi nzi na I nzi nayo I syithio Apokomo I kithio kyoo na kya Masaai nakyo Akamba kyoo kyaendie ku?*

Tafsiri

Utamaduni wa Mkamba

Utamaduni tuliuaacha wote kabisa utamaduni wetu Syokimau redio, redio Kaundi Athiani, Musyi, Kyeni, Mbaitu Mwenge muinue kiwango. Tulikuwa na nabii nabii wa Ukambani **Syokimau** tuurejeshe utamaduni. Mkamba akianza kupotoka huanza kwa kusema kwamba nimesoma, nimeokoka sipendi siasa sipendi utamaduni nimeokoka na huyo mtu utampata akitolewa mapepo yaliingilia wapi akiwa ameokoka? Ukimpata Mombasa ndiye **Bakari**, ndiye **Juma**, Juma Mkamba mpenda dini zote Mkamba si urudi rudi kwenye utamaduni ufundishwe jambo.

Mliposikia mwana piga **nguo** Si nguo rinda, mdomo hupigwa pia soni zimo mdomoni, ndio unaotukanana mwana wa Mkamba rudi kwenye utamaduni ufundishwe jambo. Hata urais huu mnaoutafuta mjue ni wa hapa duniani si wa mbinguni na mnautafuta mkiwa duniani na dunia nayo ina tamaduni Wapokomo wana utamaduni wao na waMaasai Nao Wakamba wao ulienda wapi?

Kupitia kwenye wimbo huu, mwimbaji anaelezea umuhimu wa utamaduni katika maisha ya kila siku ya Wakamba. Hivyo, mwimbaji anawarai Wakamba wazingatie utamaduni wao. Anaukejeli ukengeushi unaotokana na athari za dini za kigeni. Anasisitiza umuhimu wa kutilia utamaduni maanani katika vipengee vya maisha hata kwenye sekta ya kisiasa. Mwimbaji anatumia maneno *Syokimau*, *Bakari* na *Juma* kijazanda ili kuifumbata itikadi ya utamaduni kwamba ni kitu muhimu kwa wanajamii.

Angalia Wimbo NA. 12. ambao ni mfano wa wimbo wa hafla ya kisiasa:

NA. 12. Ngai wa Nzou Nowe wa Nduti

*Ii Ngai ndamamaa Mulungu ndakomaa Ngai ula wa **nzou** nowe wa **nduti** Ngai nowe usu Ngai ula wa athwii nowe ukusuviaa asuviaa ngya isu Ngai ndamamaa Ngai ula wa matu nowe ukusuviaa twindo tula twi nzi twi nzi ta nduti Ngai niwe usuviaa nzungu*

*Wathi ninia Katutu Mulango ndavye andu Kwa-Siku Ona ala me Ndovoini Ngai ula wa **nguku** nowe wa **nzou** Mulungu ndakomaa Ngilu nunaetiwe atendesye nzi kula kwi **maliko maima** maneekitwe utwike mutendea withie Asumali na Akala menyithya kiw'u kwa Kimanzi yiya ni Ngengi aa Kambua Kitaka Metinda mailye vamwe Nzangi na aa Katembu Mbula withie Kitundu nanga nimwaya kyaliti tondu nimwakata Mbiti wa Mulonzya kalima kangi kulisa kayulisa Ngura ningwate Munenii ii nduku ya Mutwii Mavulya mwalimu ii nguutambua ndwose ngethi nothi ungethesya Malu Mivukoni **Musungu** yu nunaendie Kitui kaundi twina Mukamba.*

Tafsiri

Mungu wa Ndovu ndiye wa Siafu

Ee Mungu halali Mungu hasinzii Mungu yule wa **ndovu** ndiye wa **siafu** Mungu ndiye huyo, Mungu yule wa matajiri ndiye anayekulinda yeye hulinda maskini hao Mungu halali Mungu wa mbinguni ndiye akulindaye viumbe wadogowadogo walio hapa duniani Mungu ndiye hulinda **siafu**

Wimbo nauimbia Katutu Mulango niwaambie watu Kwa-Siku hata wale wako Ndovoini Mungu wa **kuku** ndiye wa **ndovu** Mungu halali Ngilu aliletwa anyoroshe nchi palipo na **mashimo** na **mabonde** yaliyowekwa yanyoroke kabisa iwe Wasomali na Wagalla Wananyunyuzia maji kwa Kimanzi jameni. Akina Kambua Kitaka wanashinda pamoja Nzangi na akina Katembu Mbula iwe kwamba mmebahatika kwa maana mmetafuta Mbiti wa Mulonzya hakuna

kupanda mlima mwingine, Ngura imeshikwa vilivyo Muneeni ee ndugu ya Mutwii Mavulya mwalimu nakutambua poka salamu na umsalimu Malu Mivukoni **mzungu** alienda Jimbo la Kitui tuna Mkamba sasa.

Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anaeleza kwamba Mungu ni mwenye haki kwa sababu Mungu yuyo huyo wa ndovu ndiye Mungu wa siafu. Mwimbaji anaendelea kueleza kwamba Mungu amesikia maombi ya maskini kwa kuwapatia kiongozi mpya ambaye hana kiburi. Hivyo, mwimbaji anasimulia namna kiongozi tangulizi alivyowanyanyasa maskini na watu wa viwango vya chini. Maneno **musungu** (**mzungu**), **nduti** (**siafu**) na **nzou** (**ndovu**) yametumika kijazanda kupitisha itikadi ya kisiasa.

Tazama wimbo mwingine uliowasilishwa katika hafla ya kisiasa:

NA. 13. Kikamba ni Kyakwa

*Kikamba kyoomie kyoomie ona tene ona ila kwai nguano teka syathelile aka nimo meesi ndia syikwo mwita. Mundu tyuu mwanake niwauka na ndesi auka utee wa muunda kumanza ki? Ukethia kula ii syiitwa kiitene ii undu ungi syetaw'a kuu ni aa Manandu na Mwangu wa Ivuti **nguano** Kikamba ala maivita metitye kwitya mutino utevo ni andu anini kila ninaa ki mwalyuli walyula kii nake e muthinzio wa ngili ili*

*Ula undu Makau Vulovesa mwisi wisene na Kithungu, Kikamba nikyakwa niika umuunyulila kunyula kunyula. Nimwisi mutaa ula wa kuathima kasele natulya kathaku vandu kau keyaa vau no keumuathima kioko tene nina muikiio. Ngilasya naweta ngwatano ngwiwa ningwitanga **liu** nzi ninaeka kwananga liu wenyu. Nainie ngwatano vandu va mwaka umwe myei ikumi na ili nimanzite ngwatano ya Musila na Kaluki inywonze mwi ngusi na mwaema nethia nethia kilya nine nimainganisye*

*Mbikilye nzame niyo luka twisi Mukamba athukaa na kwenda nzamithyo. **Maanga** nzamithye **makwasi** nzamithye Mukamba nukwenda usama **manyanya** na ethia ndwimuvata nukusama vyu. Ndumbikilye nzame niyo luka twisi Mukamba athukiaa kwenda usamithwa **Maanga** nzamithye **makwasi** nzamithye Mukamba nukwisa usamithwa utongosya na ethiwa ndwimuvata nukweendee*

*Ndinengawe kindu ai mukambia Wathi uu ni kindu ai kindu ngwenda ndinengawe kindu ona kava inywi mwina musaala na maluvuluvu Mulyungi anoonie kundu kutoneka **nguunguu** yonaa vandu vaasa tyo vaa ve kimba ithyi twona vau*

Tafsiri

Kikamba ni Lugha Yangu

Kikamba kimekuwa kigumu hata kitambo kulipokuwa na uchumba ni vile uliisha tu, wanawake ndio walijua kuwa wapo wajinga wengi. Mtu ni huyu mtanashati amekuja na hajui amekuja kando ya shamba kufanya nini? Ingekuwa kwamba kura hizi zinaitishwa kama kitambo ee kama zilivyoitishwa huku na akina Manandu na akina Mwangu wa Ivuti **uchumba** Kikamba wanaoweza kuzipita wakiwa wameziomba pasi bahati mbaya ni watu wachache. Ninachoimba kina mfasiri awezaye kufasiri hiki ana zawadi ya elfu mbili

Kama vile mnajua Makau Profesa anajuana na Kiingereza Kikamba ni changu nawagawia kidogo tu kugawa kidogo kidogo tu. Mnajua **mutaa** (aina ya mmea) ule wa kubariki Nimewekelea **Kata** juu pahali hako katalala hapo katawabariki asubuhi na mapema, nina imani. Huwa nikitaja muungano ninaambiwa namwagamwaga **chakula**. Nimeacha kuharibu chakula chenu, niliimba muungano kwa mwaka mmoja miezi kumi na miwili nikitafuta muungano wa Musila na Kaluki nyote ni mashahidi na ikashindikana nikaamua niimbe niwachochee

Niwekee nionje ndiyo lugha tunayoifahamu Mkamba huharibika kwa kutaka kuonjeshwa. **Mihogo** nionjeshe Mkamba anataka kuonja **nyanya** na kama hutamkataza ataonja kabisa Niwekee nionje ndiyo lugha tunayojua Mkamba huzidi kwa kutaka kuonjeshwa **Mihogo** nionjeshe **viazi vitamu** nionjeshe Mkamba ataonjeshwa uongozi na kama hutamkataza ataendeleaaa

Sipewi kitu eti mtaniambia Wimbo huu ni kitu eti kitu ninataka sipewi kitu hata heri nyinyi Mna mishahara na marupurupu Mulyungi aliona kusikoonekana **kunguru** huona mbali si hapa tu penye mzoga sisi tunaona hapo.

Mwimbaji wa wimbo huu anasisitiza umuhimu wa wanasiasa kuungana. Bila muungano na mshikamano miongoni mwa wanasiasa Wakamba, hawawezi kukipata kiti cha urais. Mwimbaji anakiri kwamba lugha yake ya Kikamba ina utajiri wa mafumbo na kwa hivyo kupata ujumbe uliomo kunahitaji mfasiri atakayeufasiri ujumbe wake kwa namna inayofaa. Tunaelezwa kwamba Mkamba hupenda kuonjeshwa mihogo, viazi tamu, chakula, nyanya na hata asipokuwa mwangalifu atadai aonjeshwe uongozi. Itikadi ya kisiasa imefumbatwa kijazanda kwenye wimbo teule. Hivyo, maneno **maanga (mihogo)**, **makwasi (viazi vitamu)**, **liu (chakula)**, **manyanya(nyanya)** na **nguano (harakati za uchumba)** yametumika kijazanda

kurejelea uongozi. Mwimbaji anawasilisha ujumbe kwamba kuupata uongozi si kazi rahisi na hivyo kunahitaji umoja na utangamano wa wanasiasa Wakamba.

Wimbo NA. 14. ***Kativa Muuo wa Ndee (Katiba Amani ya Maeneo ya Mipakani)*** ni

wa hafla ya kisiasa:

NA. 14. Kativa Muuo wa Ndee

*Andu ma ndee twalei kusyoka tusyoke utee o kula myaka miongo itatu na ili a mutai asyae nooka umusomethya kila kitawa sumali shifita ni mundu wa utee mbaitu tea matu nimusomethye. Nzia twatiile o kuula kwa Mweu ivinda ya Manandu andu aa mweewie Mutua wa Kioko aviviswe musyi na andu make. Ukasi mooawa ivinda ya Manandu nzia twoisye ku twatyiile nzia o kula kwa Mweu ivinda ya Manandu ala mweewie Mutua wa Kioko aviviswe musyi na andu make moonze mooawa ivinda ya Manandu nzia twoisye kuu yu **nzia** isu mukuna kaa kii nditethya niyo tutindiiiaa? Asumali siasa twenda tumonie ingi.*

Me vaati vyu masamu aa twonaa kau wa ndongoi uimatethesya. Mainatumina makatumina mainatuuaa makatuuaa mumye andu ala anyuve mumye monze vyu musakue angi ona asu muusakua onamo mukaumya Asomali nonaa makatuthinia mainatuthinia makatuthinia mainatuuaa makatutemanga

Manandu akumanzithya undu ula ukwikana na mashifita a mamuvingaa matwitasyya i kula ona Asomali asu vayi utamaweta ndukakengwe a maendie mbunge monze ni shifita maendaa na Asomali aa ninyee ndawa yamo ninguthi umamina na maemee vau Nyayo twai nake ndeke ii Ngomeni okite umamina na amatiie vau ninoonie nzia ukukuluswa andu ala makwithisye.

*Mwanaa Mweu Mwikya niwe wi thayu andu ala ma tene vyu maendie mbunge Vuti ndamanya undu wa mashifita Kisini ndukile twalyulanie **uta** uu kula kwi ii mbee **uta** tuvindue Mwikya niwisi undu wa mashifita Kisini ndukile wa wa Mwatha nenda withiwe wa kamitii kau kativa ikusenzwa kundu kula muuo utaakwatikana itheka sya ndee kundu kuu miao isenzwe undu ungi na ti kuu kwitu ni Kenya yonze itheka ii syi ndee ii syenda miao isenzwe undu ungi isu ya ukoloni nditutethasya twaitye mathayu ma andu maitu maingi teka na kuu kuasa o vaa Muniyithya wa Mwinzi woowailwe*

Kuma vau ni andu miongo itatu na kenda moae kuma Kaningo kuvika Endau na Mutha ndwi vau ala uwongela no kwongela kungi nuumanya undu ngwasya ndukambuthisye na mwewa ngwina uu mwikasye no ngui ikwamba ta ila ingi. Thii muumbane mawokili na andu ma ndee mwithi muumbane na ngavana na anyuvwa ma ndee musuvie ndee nayo no miao ivandiliswe undu ungi ino ya ukoloni kuvika vau ii nditutethasya.

Tafsiri

Katiba Amani ya Maeneo ya Mipakani

Watu wa mipakani hebu turudini kule kando kule miaka thelathini na miwili iliyopita wale hamkuwa mmezaliwa nimekuja kuwafundisha kinachoitwa Wasomali Shifta mimi ni mtu wa mpakani jameni tega masikio niwafundishe. Njia tuliachia kule kwa kina Mweu wakati wa Manandu kwa wale mliosikia Mutua wa Kioko alichomewa nyumba pamoja na watu wake Ukasi wakauawa wakati wa Manandu tuliachia njia huko. Tuliachia njia kule kwa Mweu wakati wa Manandu kwa wale mliosikia Mutua wa Kioko alichomewa nyumba pamoja na watu wake wote waliuawa wakati wa Manandu tuliachia njia huko. Sasa hiyo **njia** mnapitia Kwa kweli haiwezi kutusaidia ndiyo tutairudia?

Manandu akitafuta namna ya kuwafanyia waliompinga walituitisha hizo kura kwa kisingizio cha kuwamaliza mashifta hakuna mwenye hakuwataja, usidaganywe. Walioenda mbunge wote ni shifta wao huenda kwa madai kuwa Mashifta hawa mimi ndiye dawa yao nitaenda kuwamaliza lakini wameenea hapo. Tulikuwa na Nyayo aliacha ndege yake Ngomeni ila aliwaacha hapo Alikuwa amekuja kuwamaliza ila aliwaacha hapo niliona namna waliofiwa walivyoteseka

Watu wa zamani sana walioenda mbungeni mwana wa Mweu Mwikya ni wewe uko hai Vuti hawezi kujua kuhusu mashifta Kisini amka uende kwa gavana tugeuze huu **uta** kulikokuwa mbele, tugeuze **uta** Mwikya unajua kuhusu mashifta Kisini amka wa Mwatha nataka uwe mwanakamati hiyo Katiba ikibadilishwa maeneo ambamo amani haikupatikana maeneo ya mipakani maeneo haya sheria zibadilishwe kwa namna nyingine na si huku kwetu tu, ni Kenya nzima. Maeneo haya yaliyo mipakani yanahitaji sheria zibadilishwe kwa namna nyingine sheria hizi za nyakati za ukoloni hazitusaidii. Tumepoteza nafsi za watu wengi kando na huko nyuma sana kipindi hiki tu ambapo Muniyithya wa Mwinzi aliuliwa.

Kuanzia hapo ni watu thelathini na tisa wameuliwa kutoka Kaningo hadi Endau na Mutha iko hapo wale mnaongeza mnaweza kuongeza unajua vile ninasema usinidharau. Na mkisikia nikiimba hivyo, msiseme ni mwimbaji anasema kama wengine nendeni mkusanyike mawokili na watu wa maeneo ya mipakani. Nendeni mkusanyike na magavana na wanajamii wa mipakani mtunze mipakani pia ni sharti sheria zibadilishwe kwa njia nyingine hizi za ukoloni kufikia hapo hizi hazitusaidii.

Wimbo huu unasimulia umuhimu wa mabadiliko ya katiba. Mwimbaji anazungumzia ukosefu wa amani kwenye maeneo ya mipakani ambapo anapendekeza kwamba kubadilishwa kwa katiba kutawasuluhishia matatizo ya aina hii. Hivyo, mwimbaji anaeleza maafa yanayotokana na mashambulizi ya mara kwa mara hasa katika

maeneo ya mipakani. Hivyo, anapendekeza kwamba ubadilishaji wa katiba unafaa kuzingatia namna matatizo yao yatashughulikiwa kikatiba kwa maana sheria za tangu ukoloni hazivasaidii. Kwa hivyo, mwimbaji anatumia jazanda kama vile *nzia* (*njia*) na *uta* (*uta*) ili kupitisha itikadi ya siasa na uongozi kwamba katiba haina budi kuzingatia haki kwa wanajamii wote.

Tazama mfano mwingine wa wimbo uliowasilishwa katika hafla ya kisiasa pia:

NA.15. Muviisi Ungi

Ng'ombe ii sya mutavo syendaa nongi wavena mundu kivetu na mbesa umanye ukakivenwa uu Sya mutavo syendaa nongi **Ng'ombe** sya mutavo syendaa nongi Ng'ombe syataviwe usumali ikaetwe ukamba isu ng'ombe sikesiwa nangi sya mutavo syendaa nongi **kithika** wosie utuvite chifu na ngusi ukaiva kikaung'endye kithitu kikaingwa uminiwa andu vya kivila wosie uivite andu kuiva kuiva makaivwa nangi nokwikwa o ta Mwau sya mutavo syendaa nongi

*Nisoma ivuku ndyusoma mundu ekai kwisoma ni wathi ngwina nye na nye niwina ula undu ukie utuku uilye na ndiweengeesya ve undu wi vaa ukuthinya andu na mayuuweta Maiyu nuuwete. Undu tyuu vaa uuthinya andu na Akamba muyuuweta nuuwete ninye **kaletiu** ka Syokimau nuke ndumusye Akamba*

*Kamwana ti kaa kanini vya kailite usakuwa kailye nzi ona katanaungama ni kavitie **kilaa** kyumaa nzi na miw'a yakyo kaa kenda utwilwa mata Kalonzo ala utwila wone muvisi ungi tyuu. Mauta ma ng'ombe ulovotye mbokani muuke museo **muti** wa uvosya ndwikiawa mwingi Kivutha Kibwana vena undu ninaw'o uka Nguni wisie muthinzio ndila ngunenge na nundu wi ngavana ninisi nduka nika uminenge Ileli wetewe Makueni. we minista munini Kivwana niwokie ukethania Kyethani uka Nguni wisie muthinzio ndila ngunenge na nundu wi ngavana ninisi nduka nika uminengane Kivutha wetewe Makueni.*

Tafsiri

Kijana Mwingine

Ng'ombe hawa wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia ukimnyang'anya mtu mkewe kwa pesa ujue nawe utanyang'anywa vivyo hivyo wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia. **Ng'ombe** wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia Ng'ombe walioibiwa Somalia wakaletwe Ukambani hao ng'ombe watakujiwa na wengine wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia. **Ardhi** uliyomiliki kwa kuwahonga chifu na mashahidi utailipia usiionee fahari mila ya 'Kuinga Kithitu' ikifanywa wanafamilia wako wataangamia wote cheo ulichokipata kwa kuwalipa watu

vilivyo watalipwa na wengine na ufanyiwe kama Mwau wa wizi hutorosha kwa wizi pia

Nasoma kitabu sisomi mtu wacheni kujisoma ni wimbo ninaimba mimi nami nitauimba vile ulivyokuja usiku na siwezi kuupotosha kuna jambo hapa linawatatiza watu na hawalitaji Maiyu nitalitaja. Jambo ni hili hapa linawatatiza watu na Wakamba hawalitaji nitalitaja mimi ndiye **karedio** ka Syokimau nije niwaongeleshe Wakamba

Kijana ni huyu mdogo sana anafaa kuchaguliwa akiwa ameketi hata akiwa hajasimama tayari amepita **kilaa** (aina ya mmea wenye miiba) hutoa miiba yake tangu uchangani huyu anahitaji kutemewa mate Kalonzo hebu tema uone. Kijana mwingine ndiye huyu **mafuta** ya ng'ombe umwage kwenye mboga harufu mwafaka **dawa** hainyewi nyingi Kivutha Kibwana niko na jambo njoo Nguni ukujie zawadi Beberu nikupatie na kwa maana wewe ni gavana najua huwezi kuja nitatumana Ileli uletewe Makueni wewe naibu minister ulikuja kutembelea Kyethani njoo Nguni ukujie zawadi beberu nikupatie na kwa maana wewe ni gavana najua huwezi kuja nitatumana Kivutha uletewe Makueni.

Wimbo huu unazungumzia mwanasiasa ambaye amejitokeza katika jamii ya Wakamba. Mwimbaji anaeleza kwamba mwanasiasa mwenyewe ana kibali cha uongozi na hivyo anawaomba viongozi wengine wamkubali na kumbariki kama mmoja wao. Mwimbaji anamsifia kutokana na weledi wake katika masuala ya kisiasa. Hata hivyo, mwimbaji anatangulia kwa kueleza namna ambavyo ufisadi haunufaishi. Anaeleza kwamba mali ya wizi hupotea kwa njia hiyo hiyo ya wizi. Hapa, mwimbaji anatumia maneno kama vile **kitheka** (ardhi), **kiveti** (mke) na **ng'ombe** (ng'ombe) kijazanda ili kuwasilisha itikadi ya ufisadi. Hivyo, itikadi hii imefumbatwa kijazanda kwenye wimbo unaohusika.

Katika hafla ya kisiasa, Wakamba huwa na nyimbo za kiasili ambamo hufumbatwa masuala yanayohusiana na uongozi kijazanda. Kwa hivyo, jumbe za kisiasa zinazowasilishwa kupitia jazanda huwa ni kama fumbo linalohitaji kufumbuliwa. Msikilizaji hana budi kuzifasiri jazanda husika kwa njia mwafaka ili itikadi zinazowasilishwa zifahamike.

4.1.1.3 *Syathi sya kithaitho* (Hafla za kidini)

Syathi sya kithaitho (Sherehe za kidini) ni hafla zinazohusiana na ibada za kidini. Nyimbo zinazowasilishwa katika hafla za aina hii hurejelewa kama nyimbo za kidini. Hivyo, uimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba za kidini huzingatia imani juu ya uwepo wa Mungu. Nyimbo zenyewe hujihusisha na sifa zinazohusiana na matendo yake mazuri, ukuu wake au ufanisi wake. Hivyo, nyimbo hizo huimbwa kama njia ya kumtolea Mungu ibada ya sifa. Pamoja na hayo, nyimbo za kiasili za kidini zinaweza kujihusisha na kuwarai watu watubu makosa yao na kufanya mapenzi ya Mungu. Kwa mujibu wa utafiti huu, Wakamba waliamini na wanaamini uwepo wa Mungu mkuu mmoja waliyemwomba na kumtolea sadaka. Jamii hii ilimpa Mungu majina mbalimbali kama vile *Ngai Asa* (Bwana mwenye nguvu), *Ngai Mumbi* (Mungu muumbaji), *Ngai mwatuangi* (Mungu anayepasuapasua), miongoni mwa mengine. Kwa hivyo, nyimbo za kiasili za Kikamba za kidini huimbwa katika muktadha wa ibada kwa Mungu. Tazama mfano ufuatao wa wimbo wa kiasili wa Kikamba unaoimbwa katika hafla ya kidini:

NA.16. Undu Ukwona Ngisilila Uu

Undu ukwona ngisilila uu, Undu ukwona ngisilila uu Ndinakoma musyi. Undu ukwona ngisilila uu, Undu ukwona ngisilila uu Ndinakoma musyi. Niwee kilumini ngivoyea misyi, Niwee kilumini ngivoyea misyi. Niwee kilumini ngivoyea muuo, Niwee kilumini ngivoyea muuo. Niwee kilumini ngivoyea mbua, Niwee kilumini ngivoyea mbua. Niwee kilumini kwa Mutava musyi, Niwee kilumini kwa Mutava musyi. Kula kwi miti minene kwasuvaswa mikokola ona mithekethi. Kula kwi miti minene kwasuvaswa mikokola ona mithekethi.

Tafsiri

Ninaposhangilia Hivi

Vile unaona nikishangilia hivyo, vile unaona nikishangilia hivyo, sikulala nyumbani. Vile unaona nikishangilia hivyo vile unaona nikishangilia hivyo sikulala nyumbani. Nilikuwa kwenye kilumi (aina ya ngoma ya kiasili inayochezwa kwa namna ya ibada kwa Mungu na miungu) nikiombea jamii. Nilikuwa kwenye kilumi

nikiombea jamii. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea amani. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea amani. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea mvua. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea mvua. Nilikuwa kwenye kilumi nyumbani kwa Mutava. Nilikuwa kwenye kilumi nyumbani kwa Mutava. Ndiko kwenye **miti mikubwa** kunakotengenezwa mikokola na mithekethi (aina ya kifaa cha kukoroga uji unapoendelea kupika. Ndiko kwenye **miti** mikubwa kunakotengenezwa mikokola na **mithekethi** (aina ya kifaa cha kukoroga uji unapoendelea kupika).

Katika wimbo *Undu Ukwona Ngisilila uu* (Ninaposhangilia hivi), mwimbaji anaelezea kwamba usiku uliotangulia hakulala kwa maana alikuwa kwenye shughuli ya ngoma ya *kilumi* akiombea mvua, amani na jamii. *Kilumi* ni ngoma maalum iliyoandaliwa na kucheza kwa njia ya ibada katika jamii ya Wakamba. Kwenye ngoma hii, wahusika walimtolea Mungu sadaka za aina mbalimbali huku zikiandamana na maombi yao. Wimbo huu unapitisha ujumbe wa imani ya jamii ya Wakamba katika Mungu. Hivyo, jamii hii ina imani kwamba wanastahili kumwomba Mungu wao wakati wote hata katika vipindi vya taabu na matatizo. Matatizo yenyewe ni kama vile ukosefu wa mvua, vita, njaa na kiu miongoni mwa mengine. Hivyo, inaaminika kuwa Mungu Muumbaji ndiye suluhisho la matatizo yao. Hivyo, jazanda zinazojitokeza hapa ni **miti minene (miti mikubwa)** na **mithekethi** (kifaa cha jikoni kinachoundwa kwa mbao kinachotumika kukorogea uji unapoupika). Jazanda zenyewe zinarejelea mafanikio yanayotokana na Mungu baada ya kumtambua na kumpa ibada ya sifa.

Ufuatao ni mfano mwingine wa wimbo wa kiasili wa Kikamba katika hafla ya kidini:

NA.17. Tuthii Kithembeoni

*Ukilai ithyonze tuthi kithembeoni, Ukilai ithyonze tuthi kithembeoni. Tukathembee Ngai mbua yue. Tukathembee Ngai mbua yue. Syana syukile, syana syokote **malenge** kivulanio kya **nzuu na mboso**. Tumukathe Ngai Mulungu. Ukilai ithyonze tuthi kithembeoni. TukathembeeNgai, Ngai Mumbi Ngai Mwatuangi. Ula wauisye mbua nundu wa kuthembewa. Ngai nitwooka ithemboni twiwe. Ngai nitwooka ithemboni twiwe. Noituekea mavityo maitu we Mumbi waitu. Noituekea mavityo maitu we Mumbi waitu. Ngai waitu*

nataiwe. Ngai waitu nataiwe. Ngai waitu Mumbi, Ngai Mwatuangi niwaile kutaiwa. Ngai waitu Mumbi, Ngai Mwatuangi niwaile kutaiwa. Ngai tuekea mavityo maitu we Mumbi waitu. Ngai tuekea mavityo maitu we Mumbi waitu.

Tafsiri

Twendeni Madhabahuni

Amkeni sote twende madhabahuni, amkeni sote twende madhabahuni. Tukamwabudu Mungu mvua inyeshe. Tukamwabudu Mungu mvua inyeshe. Watoto wainuke, watoto waokote **maboga**, mchanganyiko wa **mbaazi** na **maharagwe**. Tumtukuze Mungu muumbaji. Inukeni nyote twende kwenye madhabahu, tukamwabudu Mungu, Mungu Muumbaji aliyeinyesha mvua alipoabudiwa. Mungu tumekuja madhabahuni, tusikize. Mungu tumekuja madhabahuni, tusikize. Na utusamehe makosa yetu ewe muumbaji wetu. Mungu wetu atukuzwe, Mungu wetu atukuzwe. Mungu wetu Muumbaji, Mungu Muumbaji anastahili kutukuzwa. Mungu wetu Muumbaji, Mungu Muumbaji anastahili kutukuzwa. Mungu tusamehe makosa yetu ewe Muumba wetu. Mungu tusamehe makosa yetu ewe Muumba wetu.

Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anaanza kwa kuwarai wasikilizaji wake ili waende madhabahuni wakamwabudu Mungu ili mvua inyeshe. Mwimbaji anatamani kuona wakivuna vyakula vya kila aina kama vile maboga, mbaazi na maharagwe. Kupitia kwa wimbo wenyewe, mwimbaji anapitisha imani yake na ya jamii yake kwamba Mungu Muumbaji ndiye anayenyeshwa mvua anapoabudiwa. Vilevile, mwimbaji anatusawiria hali inavyokuwa wakati wa ibada. Hapa, mwimbaji anaomba Mungu awasamehe makosa yao na kuyasikia maombi wanapoomba. Maneno **malenge (maboga) nzuu (mbaazi)** na **mboso (maharagwe)** yamejitokeza kama jazanda zinazorejelea mafanikio na baraka zinazotuandama tunapomwomba na kumwamini Mwenyezi Mungu.

Kwenye hafla za kidini za jamii ya Wakamba, waimbaji huimba nyimbo za kiasili za kidini zinazofumbata itikadi ya kidini kijazanda. Jazanda hizo hubeba ujumbe wa kidini kama vile umuhimu wa kumwabudu Mungu, madhara ya kutomwabudu pamoja na umuhimu wa kuzingatia maadili.

4.1.1.4 *Syathi sya mathiko* (Hafla za mazishi)

Katika jamii ya Wakamba, mazishi ni sherehe inayofanyika kwa watu walioachwa na mpendwa wao kupitia kifo. Sherehe za aina hii huanza pindi tu mhusika anapoaga dunia hadi pale atakapopumzishwa kaburini. Hivyo, katika hafla hizi, uwasilishaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba za mazishi hupewa kipau mbele. Kwa mujibu wa wanajamii husika, nyimbo za aina hii hurejelewa kama *Iio*. Kutokana na maelezo hayo, *Iio* au mbolezi huimbwa wakati wa huzuni na katika miktadha ya mazishi. Mara nyingi, nyimbo za kiasili za Kikamba za mazishi huimbwa kama njia ya kumlilia aliyeaga dunia. Vilevile, nyimbo za mazishi huimbwa katika hali ya kuomboleza na waliofiwa. Wakati mwingine, nyimbo hizi huhusisha sifa za mtu aliyeaga dunia. Hapa, mhusika aliyetuacha humiminiwa sifa kutokana na ufanisi, mienendo au matendo yake mazuri. Nyimbo zenyewe zinaweza kusimulia sifa nzuri za aliyetuacha, faraja kwa walioachwa pamoja na ukwasi aliokuwa nao mhusika.

Kwa mujibu wa uchunguzi huu, nyimbo hizi huwa na dhima ya kijamii pamoja na ya kisaikolojia. Kisaikolojia, nyimbo hizi huimbwa kwa nia ya kuondoa huzuni na mihemko, inayoweza kutatiza afya ya waombolezaji. Dhima ya kijamii nayo inadhihirika pale ambapo nyimbo hizi huimbwa ili kuonyesha umoja wa kijamii katika shughuli ya uombolezaji. Katika hali hii, waimbaji huashiria kwamba wanalia na kuomboleza pamoja na jamii iliyoachwa na mpendwa wao. Kwa kawaida, mbolezi za Kikamba huhusisha masuala kama vile mauti, makiwa, utengano kati ya aliyekufa na waliohai, pamoja na maneno ya faraja na utulizo kwa waliofiwa. Katika jamii ya Wakamba, mauti huwa miongoni mwa mambo mazito wanayokabiliana nayo katika safari ya maisha. Kwa mujibu wa wanajamii hiyo, baadhi ya watoto walipewa majina ya wanajamii waliofariki kama ishara ya heshima kwao. Vilevile, wafu walizikwa

katika maeneo ya karibu na nyumbani. Kwa wale waliotoa maagizo ya mazishi yao kabla ya kukumbana na mauti, maagizo hayo yalizingatiwa.

Hapo awali, kabla ya majilio ya dini ya Kikristo, iliaminika kwamba kifo ni kama njia ya uendelezaji wa uhai miongoni mwa Wakamba. Hivyo, kwa mujibu wa jamii hii kifo hakibadilishi wala kukomesha uhai au mwenendo wa mtu. Badala yake, kifo husababisha mabadiliko katika hali ya mtu ambapo tunapata dhana ya ‘mababu walioaga dunia’. Dhana hii inarejelea watu walioaga dunia, lakini wanaendelea kuishi miongoni mwa wanajamii na kuwasiliana na familia zao. Wafu walizikwa na kuagwa kwa heshima ili kuepukana na laana. Iliaminika kwamba hali hii ilizuia mfu asiwe roho wa kurandaranda pindi tu anapoaga dunia. Iliaminika kuwa kutowaheshimu wafu kungesababisha wafu hao kutopumzika kwa amani, hali ambayo ingewafanya wawe roho wa kurandaranda, waliokuwa hatari kwa watu walio hai. Kwa mujibu wa jamii ya Wakamba, mtu mzee alipofariki, wanajamii walipaswa kumchinja fahali ili kusherehekea. Nyimbo zilizotarajiwa kuimbwa katika kipindi au sherehe ile ya maombolezi zilijawa na huzuni ambapo walio hai waliwasilisha hisia zao kutokana na kuachwa na mpendwa wao.

Baada ya sherehe ya mazishi, sadaka za vinyweo zilimwagwa kwenye kaburi. Haya yalitekelezwa na wazee ili kuwafurahisha *aimu* (mababu waliokufa) ili wakubali kuipokea roho ya aliyekufa katika ulimwengu wa kiroho. Hapa, nyimbo na densi ziliwasilishwa kwa maana iliaminika kwamba hii ilikuwa sherehe ya kujipatia muungano na utambulisho wa kijamii. Vilevile, walimrai yule mfu asije akasababisha balaa au tatizo kwa wale waliobaki hai. Baada ya mazishi husika, tambiko la utakaso lilitokelezwa kwa kutumia mmea maalum unaoitwa *mutaa*. Hili lilifanywa kama ishara ya kuwatakasa wanafamilia kutokana na unajisi huu katika kipindi husika. Vilevile, ni baada ya mazishi ambapo wanafamilia walitarajiwa kunyoa nywele zao

kwani waliamini kuwa uhai umekolea sana katika nywele. Kunyoa nywele kuliashiria kifo huku kumea tena kwa nywele kukiashiria uimarishaji wa uhai. Ufuatao ni mfano wa wimbo wa kiasili wa Kikamba ulioimbwa kwenye hafla ya mazishi:

NA. 18. Mathiko Kyunduani

*Andu asu mwi Kivwese, Mutito wa Ndei Maamba mwi kuu mwii ma Makindu nimwasya ndongosya Mundu wisikie muno. Nimutavya nguma ti mbesa Ndile Kalembe niwathi uthumua Kyunduani Akamba ala me nguma mundu yake mbene Keka **kivila** mundu kusakuuwa vatiele andu ana Kalembe atevo*

Tafsiri

Mazishi Kyunduani

Enyi watu wa Kibwezi, Mtito Andei, Maamba na popote mlipo watu wa Makindu mmempoteza kiongozi mtu maarufu sana nawaambia umaarufu si pesa Ndile Kalembe ameenda kupumzika Kyunduani Wakamba walio na umaarufu wao binafsi Kando na **kiti** mtu kuchaguliwa wamebaki watu wanne bila kumhesabu Kalembe.

Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anazungumzia kifo na mazishi ya mwendazake Kalembe Ndile. Mwimbaji anamsifu mwendazake kwamba alikuwa kiongozi mwema na maarufu. Mwimbaji anaeleza kwamba umaarufu si pesa bali umaarufu wa mtu unategemea namna alivyo yeye, yaani tabia na mienendo yake. Hapa, jazanda inayojitokeza ni **kivila (kiti)**.

Mfano mwingine wa wimbo wa kiasili wa Kikamba unaowasilishwa kwenye hafla ya mazishi ni kama ufuatao:

NA. 19. Kikw'u ni Musyimi

*Kikwu ni **musyimi ute tei**. Ni **muvtani ute tei**. Okaa kwosa kila kiseo. Na kutia mwene na kimeto kitathimika. Osaa ala aseu, ala avoo alau. Ala ma kwikwatwa Misyini yoo. Kikw'u ni musyimi na muvtani. Kikw'u ni musyimi na ndomiiasya ala aseu nduani kana misyini ona nguthuni. Asyima mwendwa wa andu ni kana amonuve*

Tafsiri

Kifo ni Mwindaji

Kifo ni **mwindaji asiye huruma**. Ni **mnyang'anyi asiyekuwa na huruma**. Huja kuchukua kile chema. Na kumwacha mwenyewe na

huzuni isiyopimika. Huchukua wale wazuri, walio wapole na wakarimu. Wanaotegemewa nyumbani mwao. Kifo ni mwindaji na mnyang'anyi. Kifo ni mwindaji na havumiliani na wale wazuri kijijini au nyumbani au kwenye halaiki. Humwinda mpendwa wa watu ili awaumize kwa uchungu.

Umbo la muktadha wa wimbo huu ni mazishi au matanga. Wimbo wenyewe unakilinganisha kifo na mwindaji asiyekuwa na huruma. Katika muktadha wa uwindaji kwenye jamii ya Wakamba, mwindaji humlinda na kumlenga mnyama aliye mnono, mzuri na wa kupendeza machoni. Hivyo, mwindaji huenda msituni akiwa amejihami vilivyo ili kulitafuta windo lake. Kwa hivyo, mwindaji husika huwa hatari kwa wanyama wa porini na ambapo huwashambulia na kuwaua ili apate nyama. Mwindaji husika hutekeleza kazi yake pasi na huruma kwa viumbe hao wa porini. Kwa kawaida, mwindaji huwa hana huruma kwa wanyama anaowalinda. Wanyama hao wanapojitokeza tu, mwindaji huwafuma kwa mshale, bora apate nyama. Vivyo hivyo, ndivyo alivyo anayewanyang'anya watu vitu vyao. Kwenye wimbo huu kifo kinafananishwa na mwindaji kwa maana huja kunyakua watu wazuri na ambapo wapendwa wao huachwa na huzuni tele. Hivyo, wimbo huu unawasilisha itikadi ya mauti kuwa kifo ni uwindaji na unyang'anyi unaosababisha utengano kati ya watu na wapendwa wao. Jazanda zinazojitokeza hapa ni *musyimi ute tei* (mwindaji asiye na huruma) na *muvtani ute tei* (mnyang'anyi asiye na huruma) ambazo zimetumika katika kufumbata itikadi ya mauti.

Kwa hivyo, hafla za mazishi kwenye jamii ya Wakamba hushirikisha uimbaji wa nyimbo za kiasili za mazishi. Nyimbo zenyewe hufumbata itikadi ya mauti kijazanda kwenye jamii hiyo. Mara nyingi, nyimbo za kiasili za Kikamba za mazishi huhusiana na maana ya kifo, huzuni, faraja na maisha baada ya kifo. Ujumbe unaohusiana na mauti hauwasilishwi tu moja kwa moja bali hufumbatwa kwenye jazanda mbalimbali zinazohitaji ufumbuzi.

4.1.1.5 *Syathi sya mutwaano* (Hafla za ndoa)

Syathi sya Mutwaano (**hafla za ndoa**) ni hafla zinazohusiana na masuala ya ndoa na mapenzi. Ndoa huchukuliwa kuwa hatua muhimu sana miongoni mwa jamii ya Wakamba. Hivyo, kila mwanajamii hutarajiwa kuo au kuolewa pindi tu anapofikia umri wa kufanya hivyo. Hii huchukuliwa kama njia ya kipekee ya kuendeleza vizazi vyao. Hasa katika kipindi cha hapo awali, kwa wale ambao hawakuo au kuolewa walichukuliwa kuwa waliotengwa au waliolaaniwa. Vivyo hivyo, ndivyo walivyochukuliwa wanawake waliojifungua watoto nje ya ndoa. Kwa hakika, iwapo mtu angeaga dunia kabla ya kuo au kuolewa huku akiwa amefikisha umri husika, angepigwa mateke kwa jivu kwenye sehemu yake ya nyuma huku maneno fulani yakitamkwa. Hili lilifanywa ili kuhakikisha kwamba hakutawahi kuwepo na watu wa aina hiyo tena kwenye jamii hiyo. Hii ni kwa sababu ndoa na familia zilikuwa njia pekee za kuhakikisha uendelezaji wa jamii. Hivyo, katika jamii ya Wakamba, dhana ya utawa haikuwepo.

Lilikuwa jukumu la wazazi kumtafutia mwanao mchumba. Jamii hii ilikuwa na sifa za mienendo ya kitabia iliyotengewa msichana aliyekuwa anatarajiwa kuolewa. Hizi ni kama vile kuwa mwenye bidii na mwenye tabia njema. Bwana arusi mtarajiwa aliporidhishwa na bibiarusi mtarajiwa, babake angeitembelea familia ya msichana kwa mazungumzo ya kuwasilisha pendekezo lao. Ili ndoa ikubalike rasmi, jamii ya bwana arusi mtarajiwa ilitarajiwa kutekeleza mambo kadha wa kadha kwa mujibu wa utamaduni wa jamii husika.

Sherehe za ndoa ni miongoni mwa hafla zinazohusisha uimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba katika jamii husika. Kwenye jamii ya Wakamba, sherehe ya ndoa isiyoshirikisha uimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba si kamilifu. Hali hii inafafanua umuhimu wa nyimbo husika katika sherehe ya aina hiyo. Hii ni kwa

sababu uimbaji wa nyimbo hizo huhusishwa katika kila hatua ya desturi inayofanywa. Kwa mfano, sherehe ya mwanzo ya ndoa hurejelewa kama *ntheo*. Sherehe ya *Ntheo* huwa shughuli muhimu miongoni mwa jamii ya Wakamba. Sherehe hii huendelezwa na familia ya bwana arusi mtarajiwa. Hii ni sherehe inayohusisha hali ya mchumba wa kiume kudhihirishia jamii ya wakwe watarajiwa kwamba yuko tayari kumchumbia na baadaye kumwoa binti yao. Katika sherehe husika, bwana arusi mtarajiwa hutarajiwa kuleta mbuzi wasiopungua watatu ambapo kati yao, mmoja anafaa kuwa wa kiume na ambaye hajahasiwa. Hata hivyo, idadi ya mbuzi hao inaweza kuzidi watatu bora tu iwe nambari ambayo haiwezi kugawanywa kwa mbili. Kwenye hafla hii, mbuzi ndume huchinjwa na bwana arusi au ndugu yake bwana arusi mtarajiwa. Pindi tu damu ya mbuzi huyo inapomwagika chini, ndipo inapokubalika rasmi kuwa bibi arusi mtarajiwa keshanza kuwa sehemu ya familia ya bwana arusi mtarajiwa. Katika kipindi hiki, nyimbo za kiasili za Kikamba za ndoa huimbwa ili kumsifu mwanaume huyo kwa ukakamavu wake huku akimkaribisha mchumba wake kwenye ulimwengu wa majukumu na katika familia yao. Kupitia kwa nyimbo husika, mwanaume huyo hushauriwa kuasi tabia za ujanani huku akishauriwa kutilia mkazo uwajibikaji kama kichwa cha familia yake. Vilevile, bibiarusi mtarajiwa pia hupewa mawaidha anuai kupitia nyimbo hizo.

Kabla ya kukamilika kwa sherehe hiyo hasa katika kipindi cha hapo awali, wanandoa watarajiwa walishirikishwa katika kula sehemu ya nyama nyepesi itwayo *Kikonde* iliyotolewa kwa mbuzi aliyechinjwa. Hii ilikuwa ishara kwamba wangeendelea kuitunza ndoa yao. Baada ya hayo, mchakato wa kutoa mahari ulianza ambapo majadiliano ya vitu vilivyotarajiwa yalifanyika kwa msingi wa kirafiki. Kwa kuukamilisha mchakato huu, familia ya bibi arusi iliwaandalia wageni wake pamoja na wanakijiji sherehe ya kukata na shoka. Hapa, familia hii ilimchinja fahali

aliyehasiwa aliyerejelewa kama *ilute*. Katika hali hii, nyimbo za kiasili za Kikamba za ndoa ziliimbwa pia. Nyimbo hizi ziliwapongeza na kuwasherehekea wanandoa wapya waliohusika. Ni wakati huu ambapo marika wa bibi arusi walienda nyumbani kwa bibi arusi na kuimba nyimbo za huzuni kwamba mmoja wao alikuwa amewaacha. Nyimbo mbalimbali pia ziliimbwa kama ishara ya kumwomba Mungu na mababu waliofariki wawabariki wanandoa waliohusika. Ukamilifu wa sherehe hii huashiria kwamba bibi arusi ameruhusiwa rasmi kujiunga na jamii ya bwana arusi anayemchumbia.

Vilevile, sherehe nyingine inayofuatia ni ya makubaliano ya, na ulipaji wa mahari. Hapa, jamii zote mbili huja pamoja na kujadiliana kuhusu mahari itakayolipwa kwa wazazi wa bibi arusi mtarajiwa. Pia, ni wakati huu ambapo kiasi fulani cha mahari hulipwa kama ishara ya shukrani kwa wazazi wa binti anayehusika. Hata hivyo, ulipaji wa mahari hufanyika kulingana na uwezo walionao wanajamii wa bwana arusi. Hivyo, haiwi lazima kuilipa mahari hiyo kwa siku au mara moja tu. Baadhi ya wanajamii huilipa mahari hiyo mara kwa mara tu kulingana na uwezo wao.

Iwapo wimbo ulitungwa na kuimbwa katika muktadha au hafla ya sherehe ya ndoa, wimbo huo unaweza kuorodheshwa kama *Wathi wa Mutwaano* yaani wimbo wa ndoa. Kwa kawaida, wimbo wa kiasili wa Kikamba wa ndoa uliotungwa na kuimbwa katika sherehe ya ndoa huwasilisha mawazo yanayohusiana na ndoa, mapenzi, pamoja na ushauri kwa wanandoa wanaohusika. Mara nyingi, ushauri wenyewe huhusiana na namna wanandoa hao wawili wanavyoweza kuifanikisha ndoa yao na kuishi kwa furaha. Hivyo, jamii ya Wakamba huainisha *Mbathi sya Mutwaano* kama nyimbo zinazozungumzia masuala ya ndoa na mapenzi, na ambazo huimbwa katika hafla au muktadha wa ndoa. Nyimbo zinazoimbwa katika hafla hii zinasherehekea mila ya

mwenye maringo. Ndivyo nahisi kuongea mimi, nikificha mtoto mtu mzima na siwezi kumwona mwingine mwenye maringo. Sipendi mtu mwenye vituko, hawa watu wa kwetu, ana vituko, mtu mkosa tabia njema, mwenye vituko. Nataka niambiwe, ana vituko, mtu mzima na siwezi kumtazama mwenye maringo.

Nimetoka mbali, nimetoka mbali na sasa nataka **kitanda** nilale. Nimetoka mbali, nimetoka mbali na sasa nataka kitanda nilale. Nimetoka mbali, nimetoka mbali na sasa nataka kitanda nilale. Nimetoka, mbali, nimetoka mbali, na sasa nataka kitanda nilale. Nimetoka mbali, nimetoka mbali na sasa nataka kitanda nilale. Serikali imeinua mikono ujue familia si rahisi hutafutwa kwa taabu. Mutanu songa Mutanu songa tafadhali mtoto uonekane ama niifungue **mikwa** (aina ya kamba zilizo pana kuliko kamba za kawaida).

Nilikutana na mtoto Mutanu akanisalimu na kuniuliza hivi, mtu wangu, ninapeanwa, umetoka wapi? Nimetoka kumtafuta Mutanu, aolewe ee asante. Nilikutana na mtoto Mutanu akanisalimu na kuniuliza hivi, mtu wangu, ninapeanwa, umetoka wapi? Nimetoka kumtafuta Mutanu, aolewe ee asante. Nasemaje? Sina mengi, na sina mtu wangu, ama kwa ufupi uko hapa. Lakini uliniacha, tembea kwanza lakini natafakari nitakuja tena.

Ni wewe uliniacha mtoto, ni wewe uliniacha nikitangatanga. Ni wewe uliniacha mtoto, ni wewe uliniacha nikitangatanga. Nimeuarifu moyo wangu, Mutanu rudi. Ni wewe uliniacha mtoto, ni wewe uliniacha nikitangatanga. Ni wewe uliniacha mtoto, ni wewe uliniacha nikitangatanga. Nimeuarifu moyo wangu, Mutanu rudi. Mutanu rudi tafadhali **mtoto** uonekane ama nizifungue **kamba pana**.

Katika kifungu cha kwanza, mwimbaji anatusimulia kuhusu mapenzi yake kwa Mutanu. Anaeleza kwamba anahisi kuyaweka wazi mapenzi yake kwa Mutanu ambaye sasa ni mtu mzima. Anamlinganisha Mutanu na wasichana wengine wenye vituko, tabia mbaya na utovu wa nidhamu ambapo anakata shauri kwamba hawezi kumpata mwingine kama Mutanu. Kwenye kifungu cha pili, mwimbaji anatusawiria hali ambapo anamrai Mutanu asonge mbele ili amwonyeshane mbele ya familia au jamii yake. Anasema kuwa ametoka mbali na hivyo anahitaji kitanda apumzike. Katika kifungu cha tatu, tunasawiriwa hali ambapo Mwimbaji na Mutanu wamo katika mazungumzo. Mutanu anamwuliza mpenziwe ametoka wapi huku mhusika huyu akijibu kwamba ametoka katika shughuli za kumtafuta (Mutanu). Hapa,

shughuli ya kumtafuta Mutanu inarejelea uwajibikaji na maandalizi yanayohitajika kwa kijana wa kiume kabla ya kupata jiko. Kwa mfano, kijana wa kiume hana budi kujiandaa na mahari atakayomlipia mke mtarajaiwa. Hapa, mwimbaji anaeleza kwamba Mutanu ndiye aliyemwacha akitangatanga ingawa hajapata mpenzi mwingine. Hivyo, mwimbaji anaeleza Mutanu kuwa moyo wake hu tayari kumpokea kwa sababu hajawahi kumpata mpenzi mwingine.

Kupitia wimbo huu, mwimbaji anawasilisha itikadi kuhusu ndoa. Wimbo wenyewe unawasilisha ujumbe kwamba wanandoa hawana budi kuwa wavumilivu na wanaopendana katika mahusiano yao. Yaani, changamoto za ndoa zipo nyingi ila lazima wapendane na kuvumiliana kwa hali na mali. Tukio la Mutanu kumngojea mpenziwe hata wakati alipomwacha, linaashiria ustahimilivu wa hali ya juu kwamba hata kama wametengana, yapo matumaini kwamba watarudiana hata kama itachukua muda. Kwa hivyo, kupitia kwa wimbo husika mwimbaji anamrai mpenziwe amrudie. Hapa, tunaeleza namna ambavyo mwimbaji huyu alijitahidi kumtafuta mpenzi wake Mutanu. Utafutaji huu unaweza kurejelea hali ya kujiandaa kama vile kutafuta mahari, au kubadili mienendo iliyomfanya mpenziwe amwache. Jazanda zinazojitokeza hapa ni *silikali* (serikali), *mikwa* (Kamba pana), *selia* (sheria) na *kana* (mtoto) ambapo zimeifumbata itikadi ya ndoa kwamba ni taasisi muhimu miongoni mwa wanajamii.

Mfano mwingine wa wimbo wa kiasili unaowasilishwa katika hafla za ndoa ni kama ufuatao:

NA. 21. Kilyambu

Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kuukya ii Kilyambu. Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kuukya ii Kilyambu. Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kuukya ii Kilyambu. Kala kamwana, Kilyambu, kala kanini, Kilyambu, kakwike nesa, Kilyambu, ila twikomana Kilyambu. Kala kanini,

*Kilyambu ila twikomana Kilyambu kakwike nesa, Kilyambu. Na ngoma nisikukunwa kyama ngwika, ii nisyikukunwa kyama ngwika, nitatite kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. Na ngoma nisikukunwa kyama ngwika, ii nisyikukunwa kyama ngwika, nitatite kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. Yii nisyikukunwa ya mundu ungi, nitatite kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. nitatite kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. Nenda ngoma **Mutanu** akitwawa yiya nenda kiliko Mutanu yiya nenda kiliko wa Mwangangi. Nenda ngoma Mutanu akitwawa yiya nenda kiliko Mutanu yiya nenda kiliko wa Mwangangi. Mwiitu wa musee, ni museo sana aendaa na **ngali**. Akithi **Ilovi**, aendaa na ngali. Akithi **Mombasa**, aendaa na ngali.*

Tafsiri

Kilyambu

Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kumekucha ii Kilyambu. Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kumekucha ii Kilyambu. Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kumekucha ii Kilyambu. Yule kijana, Kilyambu, yule mdogo, Kilyambu, akutendee wema, Kilyambu, mkikutana, Kilyambu. Yule mdogo, Kilyambu, mkikutana, Kilyambu akutendee wema, Kilyambu. Na ngoma zitachezwa kama ambavyo ninafanya, ndio zitachezwa kama nifanyavyo, nimejaribu kawayaya, ngoma ya chandarua. Na ngoma zitachezwa kama ambavyo ninafanya, ndio zitachezwa kama nifanyavyo, nimejaribu kawayaya, ngoma ya chandarua. Ndio zitachezwa ya mtu mwingine, nimejaribu kawayaya, ngoma ya chandarua. Nataka ngoma **Mutanu** akiolewa yiya! Nataka akili Mutanu yiya! Nataka akili wa Mwangangi. Nataka ngoma Mutanu akiolewa yiya! Nataka akili Mutanu yiya! Nataka akili wa Mwangangi. Binti wa mzee ni mzuri sana husafiri kwa **gari**. Akienda **Nairobi**, huenda kwa gari. Akienda **Mombasa**, huenda kwa gari.

Wimbo huu umewasilishwa kwenye umbo la muktadha wa sherehe ya ndoa au arusi.

Kupitia kwa wimbo *Kilyambu*, mwimbaji anasimulia kuhusu kijana Kilyambu aliyemchumbia msichana anayeitwa Mutanu. Hapa, Kilyambu anaelezwa kwamba kumekucha na hamna budi kujiandaa kwa maana ni siku yake ya kuozwa msichana Mutanu. Vilevile, kupitia kwa wimbo husika Mutanu anashauriwa kuwa awe mwenye hekima na akili katika ndoa anayoikusudia kuanza. Aidha, mwimbaji anamsifia bi arusi mtarajiwa kuwa yeye ni mwema na mwenye maadili. Jina **Mutanu** (**mwenye furaha**) limetumika kijazanda kurejelea hali iliyomo kwa wanandoa wanaoishi bila mvurugano. Wimbo wenyewe umewasilishwa kijazanda. Jazanda nyingine

zinazodhihirika hapa ni pamoja na *ngali (gari)*, *Mwambasa (Mombasa)* na *Ilovi (Nairobi)* ambapo zimetumika katika kuifumbata itikadi ya ndoa kwamba furaha, amani, uaminifu na upendo ni mambo muhimu kwenye ndoa. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa Mutanu ni mzuri sana na mwenye maadili mema kwa sababu hata anapoenda Mombasa au Nairobi, yeye husafiri kwa gari. Mienendo ya Mutanu imewasilishwa kwa namna ya safari. Kwa kawaida, mtu anaposafiri kwa gari, hufika akiwa msafi na salama. Hata hivyo, mtu anaposafiri kwa miguu, hufika akiwa mchafu na aliyejaa vumbi kila mahali. Pia, usafiri wa miguu wakati mwingine huhatarisha maisha ya mhusika ambapo huenda akashambuliwa na wanyama wa mwituni au watu hatari. Hali hii ni tofauti kwa mtu anayeabiri gari. Yeye huhisi yu salama. Hivyo, usafiri wa gari umetumika kijazanda kurejelea maadili mema ya Mutanu.

Tazama mfano mwingine ufuatao wa wimbo unaowasilishwa kwenye hafla za ndoa:

NA.22. Sikala

*Manguleti nikwita ngikwita, ngwititye **sikala** ukambata na ung'endu ngasokota yakwa na ngekia **mwaki** na ngainia uvuta. Manguleti nikwita ngikwita, ngwititye sikala ukambata na ung'endu ngasokota yakwa na ngekia mwaki na ngainia uvuta. Uambatite sikala Manguleti, umbatite niki tukoonana. Uambatite sikala Manguleti, umbatite niki tukoonana. Na teka sikala, ndumiwe **kisevu** kya kwiyonaa ngusisimukye. Na teka sikala, ndumiwe kisevu kya kwiyonaa ngusisimukye. Mwa Susu nde ngui, susu nde ngui aume ii neteelaa e ivungulu. Mwa Susu nde ngui, susu nde ngui aume ii neteelaa e ivungulu.*

*Kisaayoni, **Kisaayoni**, aume yina mwaki, ii yina mwaki nayo yavoa, seuvya nyeki ii kwaua mkuo. Kisaayoni, Kisaayoni, aume yina **mwaki**, ii yina mwaki nayo yavoa, seuvya nyeki ii kwaua mkuo. Kitemu mukwona, ni kya susu akandumia kingi. Onakyo ni kyakwa, ni kya susu akandumia kingi. **Kitemu** mukwona, ni kya susu akandumia kingi. Onakyo ni kyakwa, ni kya susu akandumia kingi. Kitemu mukwona, ni kya susu akandumia kingi. Ambii ata? Ndikaasembe, Ndikese uthekwa, yiya ni kiseo akandumia kingi. Mwa susu nde ngui, susu nde ngui aume netelae e ivungulyu.*

Tafsiri

Sigara

Manguleti nakuita nakuita, nimekuomba **sigara** ukaninyima tu kwa ukaidi, nikaikunja yangu na kuiwasha **moto** nikaanza kuivuta. Manguleti nakuita nakuita, nimekuomba sigara ukaninyima tu kwa ukaidi, nikaikunja yangu na kuiwasha nikaanza kuivuta. Umeninyima sigara Manguleti, umeninyima kwa nini? Tutaonana. Umeninyima sigara Manguleti, umeninyima kwa nini? Tutaonana. Na kando na sigara, nimeshonewa **kisevu** cha kujionea fahari nikusisimue. Na kando na sigara, nimeshonewa kisevu cha kujionea fahari nikusisimue. Nyanya yangu hachezi, nyanya hachezi jamani nangojea tu. Nyanya yangu hachezi, nyanya hachezi jamani nangojea tu.

Pale kwenye **kisaayo** (aina ya mti) Pale kwenye kisaayo (aina ya mti), jamani ina **moto**. Nayo ikizimika, andaa nyasi, kuutua mzigo. Pale kwenye kisaayo (aina ya mti) Pale kwenye kisaayo (aina ya mti), jamani ina moto. Nayo ikizimika, andaa nyasi, kuutua mzigo. **Kitemu** mnachokiona, (aina ya vazi la kale) ni cha nyanya atanishonea kingine. Hata nacho ni changu, ni cha nyanya atanishonea kingine. Kitemu mnachokiona, (aina ya vazi la kale) ni cha nyanya atanishonea kingine. Aliniambiaje? Nisikimbie, nisije nikachekwa, hicho ni kizuri atanishonea kingine. Nyanya hana mzaha, nyanya hachezi nasubiri tu

Wimbo wa *Sikala* (Sigara) ni wa kimafumbo. Hii ni kwa sababu mwimbaji anazungumzia hali ambapo mhusika Manguleti amemnyima sigara. Baada ya kunyimwa sigara, mwimbaji anaeleza kwamba ameitafuta sigara yake na kisha kuiwasha na kuanza kuivuta. Aidha wimbo huu unazungumzia namna mabinti wanastahili kujitunza hadi watakapoolewa. Kwenye wimbo huu, msichana Manguleti amesawiriwa kama mfano bora kwa wasichana wenzake. Kwa mujibu wa jamii ya Wakamba, ni ukiukaji wa kimaadili kujihusisha na tendo la ndoa kabla ya kuo au kuolewa. Hivyo, hii ndiyo maana tunaelezwa kwamba Manguleti amemnyima mwenzake sigara kwa maana hangetaka kuyakiuka maadili.

Hali ya mwimbaji kuiwasha sigara yake, inarejelea kwamba yeye ana mke. Hivyo, aliponyimwa uhusiano wa kimapenzi na Manguleti, alirejea kwa mkewe, aliyemtimizia mahitaji yake. Kupitia wimbo huu, wanajamii wanaonywa dhidi ya

kuwa na mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa na pia kabla ya ndoa. Jazanda zinazojitokeza hapa ni **sikala** (sigara), **mwaki** (moto), **kitemu** (aina ya vazi la **kiasili**). Jazanda ya sigara inarejelea ngono. Hivyo, jazanda husika zimeifumbata itikadi kuhusu ndoa kwamba ni muhimu kwa vijana kuzingatia ubikira kwenye maisha ya kabla ya kuingia kwenye ndoa. Pia, mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa yamekejeliwa.

Tazama mfano huu pia:

NA. 23. Uka Usuvie Utwae

*Ii niutavya vate kuvuvuana, kana ka mama uka usuvie utwae. Ii niutavya vate kuvuvuana, kana ka mama uka usuvie utwae. Ii niutavya vate kuvuvuana, kana ka mama uka usuvie utwae. Niutavya vate kukia kindu, kana ka mama ii uka usuvie utwae. Niutavya vate kukia kindu, kana ka mama ii uka usuvie utwae. Niuiwe **ngate**, vamwe na **kyavati** ii, Niuiwe ngate, vamwe na kyavati ii kana ka mama uka usuvie utwae.*

Tafsiri

Njoo Uitunze Ndoa

Ndio, nakwambia pasipokuchanganyikiwa, **mtoto wa mama** njoo utunze ndoa. Ndio, nakwambia pasipokuchanganyikiwa, mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Ndio, nakwambia pasipokuchanganyikiwa, mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Ndio, nakueleza pasipo kuogopa lolote mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Ndio, nakueleza pasipo kuogopa lolote mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Umepikiwa **mikate**, njoo utunze ndoa. Umepikiwa **chapati**, njoo utunze ndoa.

Kwenye muktadha wa jamii ya Wakamba, mwanamke anapolewa huandaliwa mapochopocho. Hii inakuwa ishara ya makaribisho katika jamii husika. Katika wimbo *Uka Usuvie Utwae* (Njoo Uitunze Ndoa), mwimbaji anawasilisha ujumbe kwa dadake. Anamweleza kwamba aje aitunze ndoa. Katika muktadha wa wimbo huu, wimbo wenyewe umemlenga mwanamke ambaye alikuwa amekwisha itoroka ndoa yake. Anamweleza kuwa ameandaliwa mapochopocho, chapati na mikate na hivyo basi hana budi kuja kuitunza ndoa hiyo. Mapochopocho haya ya aina ya chapati na mikate yametumika kijazanda kurejelea makaribisho kwenye ndoa. Yaani, hali hii ina

maana kuwa mwanandoa mwenzake (wa kiume) yu tayari kuungana naye ili kuidumisha taasisi hii muhimu ya ndoa. Kupitia wimbo huu, mwimbaji anawarai wanawake wawajibike katika kuzitunza ndoa zao. Anawashauri kuwa japo ndoa ina changamoto zake, ndoa pia ina umuhimu wake na hawana budi kuitunza. Kwenye wimbo *Uka Usuvie Utwae* (Njoo Uitunze Ndoa) tunapata jazanda **kana ka mama (mtoto wa mama) mikate (mikate)** na **chapati (kyavati)** zinazoendeleza itikadi ya ndoa.

Mumbe ni mfano mwingine wa wimbo wa kiasili wa Kikamba unaowasilishwa katika hafla za ndoa na arusi:

NA. 24. Mumbe

Natumie nduu na kana kanini ketawa Mumbe, kanengie kivalua kyumu kakamanthie uki wa ngilu. kanengie kivalua kyumu kya umantha uki wa ngilu. Wa tata nduthi Thua ii, wa tata ndukatike lumba. Wa tata nduthi Thua ii, wa tata ndukatike lumba.

Nakitise nguli muundani iyovete suluali na waitha ongela kamisi na lesa, ongela sikwati na waitha. Ongela kamisi na lesa, ongela sikwati na waitha. Nayu ninooka nguungule Yosi nguka, avai wa tata wa Munyalo ndungethesye Koki wa Munyalo, uuke ukwisa umbakia.

Nekiitwe kamisini vandu ndoneka, sindiliani uu ta ni nondo. Nekiitwe kamisini vandu ndoneka, sindiliani uu ta ni nondo. Kii kyakwa ni kinengo, kii kyakwa ni kinengo nanengiwa ni Mulungu niw'a muyo ngwina.

Tafsiri

Mumbe (Aliyeumbwa akaumbika)

Nilifanya urafiki na mtoto mdogo aitwaye Mumbe. Alinipa kibarua cha kutafuta **asali mwitu** (aina ya mdudu anayeunda asali mwitu). Ndugu yangu nenda Thua, ndugu yangu cheza rhumba. Ndugu yangu nenda Thua, ndugu yangu cheza rhumba.

Nilipata **nyani shambani** akiwa amejifunga **suruali** na uzi wa **waitha** (aina ya mti), ongeza **kamisi** na **kanga**, ongeza **sikati** na waitha. Na sasa nimekuja nikubembeleze Yosi nikija, jamani ndugu yangu wa Munyalo msalimu Koki wa Munyalo, uje kabla ya kunjengea.

Nilikuwa nimeingizwa kwenye kamisi singeonekana, kwenye sindiria kama **matiti**. Nilikuwa nimeingizwa kwenye kamisi

singeonekana, kwenye sindiria kama matiti. Hii yangu ni zawadi, nilipewa na Mola na hufurahia ninapoimba.

Wimbo wa *Mumbe* ni wa kiasili wa Kikamba wa kimapenzi. Kupitia kwake, mwimbaji anasimulia namna alivyoanzisha uhusiano wa kimapenzi na binti anayeitwa Mumbe. Hata hivyo, binti huyu alimpa kibarua kigumu cha kutafuta asali mwitu inayoandaliwa na wadudu waitwao *ngilu*. Hata hivyo, katika ile shughuli ya kutafuta asali mwitu, mhusika alipatana na nyani shambani akiwa amevalia mavazi ya kike. Kisha mhusika alikuwa amefichwa ndani ya yale mavazi yaliyovaliwa na yule nyani. Hivyo, anapoimba, amejitambua na ndiposa amerudi kumwomba mpenziwe Mumbe amkubali ili wafunge pingu za maisha pamoja.

Wimbo huu umewasilishwa kimafumbo. Kwa kawaida, asali mwitu huwa haipatikani kwa urahisi. Hii ni kwa sababu wadudu wenyewe hawapatikani popote pale. Hivyo, neno asali mwitu limetumika kijazanda kurejelea uhadimu wa ndoa kamilifu, ustahimilivu na juhudi zinazohitajika katika utunzaji wa ndoa. Pia, hali ya kufichwa kwenye mavazi ya kike imetumika kurejelea hadaa za anasa na maisha zinazozikumba ndoa nyingi. Kwa mfano, tunaenezwa kuwa mwimbaji alikuwa amefichwa ndani ya yale mavazi, yaani sindiria na kamisi. Hali hii inaonyesha namna ambavyo baadhi ya wanandoa hulaghaiwa na wanawake nje ya ndoa, hali inayowafanya wazitelekeze ndoa zao. Vilevile, msamaha katika ndoa unasisitizwa pale ambapo mhusika anamwomba Mumbe warudishe mahusiano yao kama yalivyokuwa hapo awali. Kwa ujumla, wimbo huu umewasilishwa kimafumbo ambapo unajihusisha na itikadi ya ndoa, yaani namna ambavyo si rahisi kuipata. Itikadi yenyewe imefumbatwa katika jazanda ***uki wa ngilu*** (asali mwitu), ***nguli*** (nyani), ***muundani*** (shambani).

Tazama mfano ufuatao pia:

NA. 25. Nzambi wa Mutunga

*Ndumbinguie wa musyi, ndumbinguie wa Mutunga ndumbinguie wa musyi. Ndumbinguie wa musyi, ndumbinguie wa **Mutunga** ndumbinguie wa musyi. Na ndumbinguie, wa Mutunga ii na ndumbinguie wamusyi. **Nzambi** nzele wivia ku? Ni yakwa ya kuela **ndia**, ngatava na ngathamba Nzambi **nzele** wivia ku? Nzambi nzele wivia ku? Ni yakwa ya kuela **ndia**, ngatava na ngathamba Nzambi nzele wivia ku?*

***Simu** yaumie, simu yaumie Masaku twamikwatie na twooka. Simu yaumie, simu yaumie Masaku twamikwatie na twooka. Aume mwakwata livoti mwaisye ata? Mwindavya. Mbande **mutunda**, ni waki? Wai wa mavatano. Aume mwakwata livoti mwaisye ata? Mwindavya. Mbande mutunda, ni waki? Wai wa mavatano.*

*Nzambi ndaumie ii Kangundo akwete Wayua ii na kwoko, ii wa Mutunga ndasyoke. Nzambi ndaumie ii Kangundo akwete Wayua ii na kwoko, ii wa Mutunga ndasyoke. Ukwaithya **ndata** yaki? Iyaayi ndata ya uwe. Ukwaithya ndata yaki? Iyaayi ndata ya uwe. Ukwete nzele yaki? Iyaayii nzele ya uwe. Ukwete **nzele** yaki? Iyaa yii nzele ya uwe.*

Tafsiri

Nzambi wa Mutunga

Nifungulie wa nyumbani, nifungulie wa Mutunga, nifungulie wa nyumbani. Nifungulie, wa Mutunga nifungulie wa nyumbani. **Nzambi** unapeleka **kata** wapi? Ni yangu ya kupima maji kwenye **kidimbwi**, ninachota na kisha kuoga. Nzambi unapeleka kata wapi? Ni yangu ya kupima maji kwenye bwawa la kuogelea, ninachota maji na kisha kuoga. Nzambi unapeleka kata wapi?

Simu ilipigwa, simu ilipigwa kutoka Machakos tuliipokea na tukaja. Simu ilipigwa, simu ilipigwa kutoka Machakos tuliipokea na tukaja. Wazee mlipoipokea ripoti mlisemaje? Mniambie. Nipande **mtunda**, ni wa nini? Ulikuwa wa mapatano.

Nzambi alitoka Kangundo akiwa amemshika Wayua mkono, ndio wa Mutunga arudi. Nzambi alitoka Kangundo akiwa amemshika Wayua mkono, ndio wa Mutunga arudi. Unatingiza **fimbo** ya nini? iyaayi! Fimbo ya uganga. Unatingiza **fimbo** ya nini? Iyaayi! Fimbo ya uganga. Umeshika **kata** ya nini? Iyaayi! **kata** ya uganga.

Katika wimbo *Nzambi wa Mutunga*, mwimbaji anasimulia kuhusu mhusika Nzambi wa Mutunga aliyekuwa ameolewa Kangundo. Inaelezwa hapa kwamba Nzambi alitoka huko akiwa amemshika Wayua (pengine ni mwanaye) mkononi. Hivyo, ni baada ya kuzipokea habari hizi ambapo mwimbaji amekuja kumchukua mhusika huyu ambaye pengine ni mpenziwe au jamaa wa mumewe. Katika kifungu cha pili,

tunaelezewa kuhusu mapatano ya wazee kuhusu hali hii. Hivyo, mapatano yanaafikiwa ili Nzambi wa Mutunga airejeele ndoa yake.

Kwa kawaida, katika hali ya maisha ya jamii ya Wakamba, upandaji wa mti unaozaa huwa ni ishara ya matumaini mpya, Katika mahusiano ya ndoa iliyokuwa imesambaratika, upandaji wa mti unaozaa matunda hurejelea matumaini ya kunawiri kwa ndoa husika. Hapa, tunaelezwa mhusika Nzambi ameshika kata. Anapoulizwa ni ya nini, anaeleza kwamba kata hiyo ni yake ya kupima kima cha maji **kidimbwini**, kisha anaitumia katika kuchota maji ya kujimwagilia anapooga. Hivyo, neno **ndia (kidimbwi)** limetumika kurejelea utegemevu. Yaani, ili ndoa inayorejelewa idumu, Nzambi anategemewa sana. Nzambi ana wajibu mkubwa katika kuidumisha ndoa husika. Hata ingawa imesambaratika, akitekeleza wajibu wake vilivyo, ndoa hiyo haina budi kusimama. Hivyo, wimbo wenyewe umeifumbata itikadi ya ndoa kupitia jazanda kama vile **ndia (kidimbwi)**, **nzele (kata)**, **ndata (fimbo)**, **simu (simu)**, jina **Mutunga** (anayerudisha) na **mutunda (mtunda)**.

Tavitha ni mfano mwingine wa wimbo uliowasilishwa kwenye hafla ya ndoa. Angalia wimbo wenyewe hapo chini:

NA.26. Tavitha (Tavitha)

Eka nzingithye ileve, Eka nzingithye ileve yaema ninuke ngakomele kwitu. Eka nzingithye ileve, Eka nzingithye ileve yaema ninuke ngakomele kwitu. Na wingulya isyitwa na wingulya isyitwa tanye nguvingusya ninye nguvinguiwa ngenuka kaloko. Na wingulya isyitwa na wingulya isyitwa tanye nguvingusya ninye nguvinguiwa ngenuka kaloko.

*Auuwaa! ninewie ukiwetwa mwa ai kindu wakwa ii ngwendete ii. Auuwaa ninewie ukiwetwa mwa ai kindu wakwa ii ngwendete ii. Tavitha ii wai wakwa ii na wandia, Tavitha ii wai wakwa ii na wandia, Tavitha ii wai wakwa ii na wandia, ninamanyie ukandia na ukuthi ukwete **nduume** na unamikisya **ivindi**. Naungamisye Tavitha ii anambia We! Naungamisye Tavitha ii anambia We! Naungamisye Tavitha ii anambia We! Naungamisye Tavitha ii anambia We! Ndweke ungulya*

mwaka uu ti ta ula ungi nyie ni mukaa mwalimu na ndinenaa na ivisi. Ni mukaa mwalimu na ndinenaa na ivisi. Ni mukaa mwalimu na ndinenaa na ivisi. Ni mukaa mwalimu na ndinenaa na ivisi.

Tafsiri

Tavitha

Wacha nitingize **ileve** (aina ya kifaa kinachochezwa wakati wa ngoma ya kitamaduni) nikishindwa niende nyumbani kwetu nilale huko. Wacha nitingize ileve nikishindwa niende nyumbani kwetu nilale huko. Na unaniuliza jina, na unaniuliza jina, sio mimi nitabisha bali ni mimi nitafunguliwa nitaenda nyumbni asubuhi. Na unaniuliza jina, na unaniuliza jina, sio mimi nitabisha bali ni mimi nitafunguliwa nitaenda nyumbni asubuhi.

Auuwaa! Nilisikia ukisengenywa jamani, eti mpenzi wangu nakupenda. Auuwaa! Nilisikia ukisengenywa jamani, eti mpenzi wangu nakupenda. Tavitha ulikuwa wangu na ukaniacha. Tavitha ulikuwa wangu na ukaniacha. Tavitha ulikuwa wangu na ukaniacha. Tavitha ulikuwa wangu na ukaniacha. Nilijua utaniacha na utembe ukilishikilia ndume na ukalirushia **mfupa**. Nilimsimamisha Tavitha akaniambia We! Nilimsimamisha Tavitha akaniambia We! Nilimsimamisha Tavitha akaniambia We! Nilimsimamisha Tavitha akaniambia We! Wacha kuniuliza mwaka huu si kama ule mwingine mimi ni **mke wa mwalimu** na siongei na vijana wavulana, ni mke wa mwalimu na siongei na vijana wavulana

Kwenye wimbo wa *Tavitha*, mwimbaji anasimulia kuhusu mpenziwe Tavitha. Anaeleza namna anavyompenda Tavitha. Mwimbaji anaeleza kwamba alimpenda msichana huyu kwa moyo wake wote. Hata hivyo, inaonekana kwamba Tavitha alimwacha mpenziwe na kisha kuolewa na mwanaume mwingine ambaye ni **mwalimu**. Hapa, neno mwalimu limetumika kijazanda kuashiria mwanajamii yeyote aliye katika kiwango cha juu na pengine ana mali na pesa. Tunaelezwa kwamba mwimbaji alikisia kuwa Tavitha angemwacha, kwa sababu pengine yeye ni maskini. Hivyo, neno **ivindi** (mfupa) linarejelea ushawishi wa mali na pesa. Kwa mujibu wa wimbo, Tavitha alionekana akiwa amemshika mkono **beberu** aliyemrushia **mfupa** na kumnasa. Neno **beberu** linamaanisha mbuzi wa kiume aliyekomaa. Neno lenyewe linaashiria mwanaume mwenye ushawishi wa pesa na mali. Yaani, kutokana na ushawishi wa uwezo wa pesa na mali wa beberu anayerejelewa, Tavitha alimwacha

mpenziwe na kuishia kuolewa na mhusika huyo. Kwa hivyo, baada ya kunaswa na beberu huyo, Tavitha hataki mahusiano yake na mwimbaji husika. Hii ni kwa sababu sasa yeye ni mke wa mwalimu na kiwango chake si sawa na mpenzi wake wa zamani. Wimbo huu unasawiri hali halisi ya baadhi ya ndoa na mahusiano ya kimapenzi katika ulimwengu wa sasa. Hivyo, mwimbaji anaonekana akihuzunika ingawaje anakiri kwamba alikisia kwamba mpenzi wake huyo angemwacha. Mwimbaji anawasilisha itikadi kuhusu ndoa kwamba mara nyingi hukumbwa na changamoto. Baadhi ya changamoto husika ni za ukosefu wa hela na mali ambapo huenda zikasababisha talaka na utengano. Itikadi yenyewe imefumbatwa kwenye jazanda **ivindi (mfupa)**, **nduume** (beberu) na **mukaa mwalimu** (mke wa mwalimu).

Mfano mwingine wa wimbo unaoimbwa katika hafla ya ndoa ni kama ufuatao:

NA. 27. Mundu Mwiu e Kiliko (mtu mweusi ni mwenye akili)

*Iyaa iyaa! mundu mwiu e kiliko ui na umanyi ii na kwakya ayukila athekete yaa! niw'o mumbile. Iyaa iyaa! mundu mwiu e kiliko ui na umanyi ii na kwakya ayukila athekete yaa! niw'o mumbile. Umaaluka kaloko na kaniki ka muthemba katumitwe kitene na kwovwa utene. Umaaluka kaloko na **kaniki** ka muthemba katumitwe kitene na kwovwa utene. Niyova **leso** uu ta mundu wa tene ula weyovaa kaniki aendete wathini kukuna mukanda kwa!kwa!kwa!kwa! Niyova leso uu ta mundu wa tene ula weyovaa kaniki aendete wathini kukuna mukanda kwa!kwa!kwa!kwa! Niyova leso uu ngalungala nesa ta mundu mueni mwakomana nziani ukaungama nesa ukamba kumwiloela mundu wi kiliko syitwa yake etawa **Mbete, Mbete ya kwoko** ta nikunyamasya nikilya ngomete ngamililikana ngaina kuia ii! Na Mbete akambona ngakethya wa Mwende. Mbete akambona ngakethya wa Mwikali. Tyuu **vevi** tyuu twi suoo. Moko na Mwende nduthi ukime Mukyondo Mukyondo mbai ili, Mukyondo mbai ili wiitwe naka mbee ndena **mundu** ndumbongele nzakame.*

Tafsiri

Mtu Mweusi ni Mwenye Akili

Iyaa iyaa! mtu mweusi ana akili na maarifa na kunapopambazuka anaamka akicheka yaa! ndiyo maumbile. Iyaa iyaa! mtu mweusi ana akili na maarifa na kunapopambazuka anaamka akicheka yaa! ndiyo maumbile. Utoke asubuhi na mapema ukijifunga **kaniki** (aina ya vazi la kitamaduni) ka aina fulani kalikoshonwa kikale na kufungwa

kikale. Nitajifunga **leso** hivi kama mtu wa kale aliyejifunga kaniki akielekea kwenye densi kucheza **mukanda** (aina ya ngoma ya kitamaduni iliyochezwa) kwa!kwa!kwa!kwa! Nitajifunga **leso** hivi kama mtu wa kale aliyejifunga kaniki akielekea kwenye densi kucheza **mukanda** (aina ya ngoma ya kitamaduni iliyochezwa) kwa!kwa!kwa!kwa! Najifunga leso hivi, ninakaa wima kama mtu mgeni mkikutana njiani unasimama vizuri unamtazama kwanza, mtu mwenye hekima, jina lake ni **Mbete, Pete ya mkono** inanisumbua. Nikiwa nimelala naikumbuka na kisha ninaanza kulia ii! Naye Mbete akaniona nikamsalimu wa Mwende, Mbete akaniona nikamsalimu wa Mwikali, ndiye huyu **mtoto** ndiye huyu leo. Mikono juu na Mwende nenda umtwange Mukyondo, Mukyondo mbari mbili ukiwa umeambiwa na wanawake kuwa hana **mtu**, si uniongeze damu.

Mwimbaji anaanza kwa kueleza kuwa mtu mweusi/Mwafrika ni mwenye akili na maarifa. Anaendelea kusema kwamba kunapopambazuka, ni maumbile ya mwafrika kuwa na furaha tu. Hali hii inaonyesha umuhimu wa ustahimilivu katika maisha hata wakati wa changamoto. Mwimbaji anammiminia Mbete sifa husika. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anaelezea namna alivyompenda msichana anayelitwa Mbete. Anaelezea namna mapenzi yake kwake yalivyomfanya alie kila alipomwaza. Anaeleza kuwa hakuwa na habari kwamba binti huyu alikuwa ameshampata mpenzi wake. Kwa hivyo, alipatwa na mshtuko mkubwa alipobaini ukweli ulivyokuwa. Wimbo huu umewasilisha itikadi kuhusu ndoa na mapenzi kwamba iwapo unampenda mtu, mjulishe. Hamna haja kumpenda mtu kisirisiri na kisha anapopata mchumba ndipo unajitokeza kukiri mapenzi yako kwake. Kwa mfano, iwapo mwimbaji husika angekiri mapenzi yake kwa Mbete kwa wakati uliofaa, huenda wangukuwa wapenzi. Hata hivyo, kutokana na kuchelewa chelewa, amempata mwana si wake. Pia, tunajifunza kuwa katika ndoa, udongo uwahi ungali maji. Hivyo, maneno **mundu (mtu)**, **vevi (mtoto)**, **mbete ya kwoko (pete ya mkono)** na **mbete (pete)** yametumika kijazanda ili kuwasilisha itikadi ya ndoa kwamba inahitaji watu wanaopendana au wenye mapenzi.

Utafiti huu umedhihirisha kuwa hafla za ndoa za jamii ya Wakamba huambatanishwa na nyimbo za kiasili za Kikamba za ndoa. Nyimbo zenyewe hufumbata masuala mbalimbali yanayohusiana na ndoa kijazanda. Masuala hayo ni mapenzi, ndoa, talaka na ubikira. Hivyo, itikadi ya ndoa hufumbatwa kupitia jazanda mbalimbali kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba.

4.1.1.6 *Syathi sya kusyawa kwa syana* (Hafla za kuzaliwa kwa watoto)

Uendelezaji wa jamii ya Wakamba ni jambo muhimu katika jamii husika. Lengo hili huafikiwa tu kupitia kujifungua na kuongezeka. Hivyo, kumpata mtoto lilichukuliwa na huchukuliwa kuwa baraka kubwa kutoka kwa Mungu. Jambo hili huonekana kuwa baraka kubwa kwa wanandoa wote. Hasa katika kipindi cha hapo awali, kuolewa kwa mwanamke yeyote kulikuwa na maana ya kupata watoto. Kwa hivyo, utasa ulichukuliwa kuwa ishara ya laana kutoka kwa miungu na mababu waliofariki. Hivyo, iliaminika kuwa tatizo hili lilitokana na uvunjaji wa mwiko au miiko fulani katika jamii husika. Wakati mwingine, ilipotokea kwamba mwanamke hangeweza kupata watoto kabisa, mumewe aliruhusiwa kuoia mwanamke mwingine ambaye angemzalia watoto. Hivyo, ndoa kati ya wanawake wengi ziliruhusiwa kuwa kama suluhisho la tatizo la utasa. Kwa upande mwingine, ilipotokea kwamba mwanaume katika ndoa hakuwa na uwezo wa kuzalisha, mwanamke katika ndoa husika aliruhusiwa kupata watoto nje ya ndoa. Hata hivyo, sadaka ziliweza kutolewa ili kuwafurahisha na kuwatuliza *aimu* (roho za mababu waliokwisha fariki). Katika jamii ya Wakamba, mama mjamzito alitunzwa vilivyo. Kwa mfano, hakuruhusiwa kufanya kazi nzitonzito. Vivyo hivyo, hawakuruhusiwa kuhudhuria hafla fulani za kitamaduni hasa zile zilizohitaji uchezaji au densi. Hii ni kwa sababu hali hii ingeathiri ujauzito husika. Vilevile, kina mama wajaazito hawakuruhusiwa kwenda karibu na makaburi ambapo iliaminika kuwa kufanya hivyo kungekuwa njia moja ya kumshirikisha mtoto

mtarajiwa katika huzuni. Pia, ulikuwa mwiko kwa mtu yeyote akiwemo mumewe, kumchapa mwanamke hasa alipokuwa mjamzito.

Baada ya mtoto kuzaliwa katika jamii ya Wakamba, kilichofuatia kilikuwa kipindi cha furaha na kusherehekea. Kipindi hiki kiliwasilishwa kupitia uimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba. Mtoto wa kiume alikaribishwa kwa kelele zilizofululiza kwa muda mrefu kuliko ilivyokuwa mtoto msichana alipozaliwa. Nyimbo zilizoimbwa zingemsifu mama kwa kazi njema aliyoifanya. Vilevile, wangemsifu mtoto aliyezaliwa kupitia kwa nyimbo husika. Katika hali hii, nyimbo mbalimbali ziliimbwa ili kumkaribisha katika jamii hiyo. Vilevile, nyimbo hizo zilinuiwa kumshukuru Mungu kwa kumwezesha mama kujifungua salama.

Siku kumi na nne baada ya kujifungua, mama alipitishwa katika tambiko la utakaso lililorejelewa kama *kuuswa*. Hii ni kwa sababu iliaminika kwamba kipindi cha ujauzito kilihusishwa na unajisi fulani. Ilimbidi mama huyo anyoe nywele zake ambapo ilikuwa ishara ya kukubalika tena na kuanza upya katika jamii inayohusika. Katika michakato hii yote, nyimbo zilitumika katika kuwasilisha hisia za wanajamii. Kisha, sherehe ya kumpa mtoto jina ilifuatia ambapo mtoto alipewa majina kwa mujibu wa mila na desturi za jamii hiyo. Utafiti huu umebaini kuwa nyimbo za kiasili za Kikamba zilienziwa kwenye jamii hii ambapo ziliwasilishwa katika tukio hili. Hebu angalia mifano hii ya nyimbo zilizowasilishwa katika hafla ya sherehe ya kuzaliwa kwa watoto:

NA. 28. Kyathi no Vala

*Iyaii yayai! kyathi no vala vala wandavisye wambiie ningoka kuathima mwana ii na **kaindo** ngyuka. Iyaii yayai! kyathi no vala vala wandavisye wambiie ningoka kuathima mwana ii na kaindo ngyuka. Yii mwana ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa mwingi. Yii mwana ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa mwingi. **Wa tata** ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa*

mwingi. Wa tata ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa mwingi.

Tafsiri

Miadi ni Ileile

Iyaaiii, aiii! miadi ni ile ile, vile ulivyoniambia uliniambia utakuja kumbariki mtoto na **kakitu** ukija. Iyaaiii aiii! miadi ni ile ile, vile ulivyoniambia uliniambia nitakuja kumbariki mtoto na kitu nikija. Ee! mtoto nyamaza nikubembeleze, nikubembeleze ulale nina raha nyingi. Ee! mtoto nyamaza nikubembeleze, nikubembeleze ulale nina raha nyingi. **Wa baba** nyamaza, nikubembeleze, nikubembeleze ulale nina raha nyingi.

Wimbo wa Kyathi no Vala (Miadi ni ile ile) unasimulia kuhusu wahusika wawili, mmoja akiwa mwimbaji wa wimbo husika. Hivyo, mwimbaji anamkumbusha mwenzake kuwa miadi ni ile ile kwamba alihahidi kuja kumwona na kumbariki mtoto wake. Kupitia kwa wimbo huu, waimbaji wanaonekana kuwa wenye furaha baada ya mwenzao kufanikiwa kupata mtoto. Wimbo huu uliwasilishwa katika umbo la muktadha wa sherehe ya kuzaliwa kwa mtoto. Wimbo wenyewe umewasilisha itikadi ya uzazi na malezi kwamba Watoto ni mali ya jamii na hivyo kuzaliwa kwao humfurahisha kila mwanajamii. Vilevile, inadhihirika hapa kwamba malezi ya Watoto ni jukumu la wanajamii na wala si jukumu la mtu mmoja. Itikadi yenyewe imefumbatwa katika jazanda kama vile **kaindo (kakitu)** na **Wa tata (Wa baba)**

Wimbo ufuatao pia uliwasilishwa kwenye hafla ya sherehe ya kuzaliwa kwa mtoto:

NA. 29. Inyaa Mwana na Ithea Mwana

Inyaa mwana iyi, na ithea mwana iyi, ethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka. Inyaa mwana iyi, na ithea mwana iyi, ethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka. Inyaa mwana iyi, na ithea mwana iyi, ethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka. Ngyuka na ngyuka kethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka. Ngyuka na ngyuka kethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka.

*Kasilisili mwana ii inyaa mwana nukumbenda inyaa mwana akusye ikanda nakwa ainenga ngusye kwata mukwa ulumitye ndukandekye nimandane. Kasilisili mwana ii inyaa mwana nukumbenda inyaa mwana akusye **ikanda** nakwa ainenga ngusye kwata **mukwa** ulumitye ndukandekye nimandane.*

Tafsiri

Mama na Baba Mtoto

Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija.
 Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija.
 Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija.
 Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija.
 Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija.
 Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija.
 Nikija na nikija, kama mtoto ni wangu nifungulie nikija. Nikija na
 nikija, kama mtoto ni wangu nifungulie nikija

Kasilisili mwana ii mama mtoto ee mama mtoto ananihitaji, mama
 mtoto avute **kamba** na kisha anipe nivute shika **kamba pana** vizuri
 usiniachilie nianguke. Kasilisili mwana ii mama mtoto ee mama
 mtoto ananihitaji, mama mtoto avute kamba na kisha anipe nivute
 shika Kamba pana vizuri usiniachilie nianguke.

Kupitia kwenye wimbo *Inyaa Mwanaa Ithea Mwana* (Mama na Baba Mtoto),
 mwimbaji anaomba afunguliwe mlango kwa maana yuko pale karibu, akiwa njiani
 kuja kumwona mtoto aliyezaliwa. Anaeleza kuwa kama mtoto ni wake basi
 afunguliwe mlango aingie. Maelezo haya yanapitisha itikadi kuhusu uzazi na malezi
 kwamba mtoto ni mali ya jamii. Yaani, mwimbaji anakaribishwa kwa kufunguliwa
 mlango kwa sababu mtoto ni wake kama mwanajamii Mkamba.

Katika kifungu cha pili, mwimbaji anatusawiria hali inavyokuwa wakati wa
 kujifungua. Katika kipindi cha awali, akina mama wajawazito walizalia nyumbani
 kwa msaada wa wakunga. Kuna namna walivyoshikilia kamba ya kawaida au kamba
 pana iliyofungiwa kwenye paa la nyumba wakati wa uzalishaji. Kupitia wimbo huu,
 mwimbaji anamweleza mama mtoto ashikilie kamba vizuri asije akahatarisha maisha
 yake au ya mtoto anayezaliwa. Hivyo, maneno **ikanda (kamba)** au **mukwa (kamba
 pana)** yametumika kurejelea ustahimilivu unaoambatana na uzazi na malezi. Yaani,
 ukosefu wa ustahimilivu huenda ukasababisha madhara kama vile mauti. Wimbo
 wenyewe umewasilishwa kijazanda ili kusimulia umuhimu wa umoja wa kijamii na
 ustahimilivu katika uzazi na malezi. Wimbo huu unaeleza mchango wa mkunga,

wanajamii na mama pia katika kujifungua, kutunza na kulea watoto wanaoaminika kuwa mali ya jamii. Hivyo, itikadi hii imefumbatwa kwenye jazanda kama vile ***mukwa (Kamba pana)*** na ***Ikanda (Kamba)***

Imedhihirika kwamba hafla za kuzaliwa kwa watoto huhusisha nyimbo zinazowasilisha masuala ya uzazi na malezi kijazanda. Hivyo, masuala haya husawiriwa kijazanda ambapo ufasiri mwafaka huhitajika ili ujumbe unaohusika ueleweke.

4.1.1.7 *Syathi sya wia wa ikundi (Hafla za kazi za makundi ya watu)*

Katika jamii ya Wakamba, baadhi ya watu hujiunga katika makundi ya kijamii ili kusaidiana kutekeleza kazi mbalimbali. Hii ni kwa sababu kazi inapofanywa na mtu mmoja huwa ya kuchosha, ngumu na ya kukinaisha mhusika. Hivyo, ili kuepukana na matatizo ya aina hii, wanajamii wanaoishi katika maeneo fulani huunda makundi ambayo kwayo wanasaidiana kutekeleza kazi mbalimbali katika jamii hiyo. Miongoni mwa kazi zinazotekelezwa na wanajamii husika ni pamoja na kulima, kuvuna mazao shambani, kuchunga mifugo, kusuka vikapu, kukusanya kuni, kuezeka paa la nyumba, ufinyanzi, ujenzi wa nyumba, uchongaji na uhotaji wa maji miongoni mwa nyingine. Katika hali ya kutaka kupunguza uchovu, ulegevu, ugumu na uzito wa kazi husika, uimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba huhusishwa. Vilevile, uimbaji wa nyimbo hizi huirahisisha kazi inayofanywa pamoja na kuwatia motisha wanaofanya kazi hiyo. Hivyo, katika baadhi ya vijiji, kazi zinazofanywa kimakundi mara nyingi huwa hafla muhimu inayohusisha uimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba.

Utafiti huu umegundua kwamba katika jamii ya Wakamba, hasa katika kipindi cha kabla ya miaka ya 1990, makundi mbalimbali yaliundwa ili kusaidiana katika kazi ya kutayarisha mashamba, kupanda mbegu pamoja na kulima mashamba. Kwa mfano,

makundi yanayorejelewa kama *mwethya* (umoja) au *myethya* (wingi) yaliweza kuundwa katika majira mbalimbali. Makundi haya yalihusisha wanajamii waliokuja pamoja ili kusaidia mwanajamii mwenzao katika kazi kama vile kulima au kutayarisha mashamba. Hivyo, lilikuwa jukumu la mwenye shamba au aliyeomba kusaidiwa kwa kazi husika kuwatarishia chakula cha kutosha wanapoendelea na kazi. Makundi haya yaliweza kushirikisha wanaume na wanawake pamoja, au yakaweza kuundwa kiumri au kijinsia. Hivyo, tunapata *myethya/milaso* ya vijana wa kike pekee, vijana wa kiume pekee, kina mama na wazee pekee. Mara nyingi, kazi kama vile za kufyeka vichaka ili kuandaa mashamba zilihusisha *myethya/milaso* ya Wazee huku kazi kama vile za upanzi, uvunaji na kuezeka paa za nyumba kwa nyasi zilihusisha wanawake. Hii ni kutokana na mtazamo wa kijinsia kwamba baadhi ya kazi zinafaa kutekelezwa na wanawake huku nyingine zikihusishwa na wanaume. Hata hivyo, kazi kama vile ya kulima au kuondoa magugu shambani ilihusisha makundi ya jinsia zote mbili.

Pamoja na hayo, kuna makundi ya *nzeve* yaliyoundwa kwa nia ya kusaidiana kazi hasa za shambani. *Nzeve* ilihusisha wanajamii waliokuwa tayari kusaidiana katika kazi moja maalum. Kwenye kundi hili, waliweka sheria zilizohusiana na utekelezaji wa kazi zao. Sheria hizi zilihusu kwa mfano kazi watakayoitekeleza, muda watakaouchukua kwa kila mshirika, wakati watakaokutana na kuanza kazi husika, miongoni mwa mambo mengine. Hivyo, ikitokea kwamba mwanakikundi mwenzao amekiuka sheria husika, alitozwa ada fulani, ikitegemea makubaliano ya wanakikundi husika. Wananzeve walitekeleza kazi zao kwa zamu, kwamba kila mwanakikundi alikuwa na zamu yake ya kusaidiwa kazi husika.

Wakati mwingine, lilikuwa jukumu la watoto na wajukuu au wanajamii kuja pamoja na kuwasaidia wazazi wao wazee katika kazi mbalimbali hasa za shambani. Kwa

mfano, ikitokea kwamba nyanya au babu ana wajukuu au wanao, mara nyingi hawa ndio waliowasaidia katika kutekeleza kazi husika. Hili lilitokana na imani ya jamii ya Wakamba kwamba kuwasaidia wazazi kwa vyovyote vile ni njia mojawapo ya kujipatia baraka na pia kuepukana na laana. Hivyo, washiriki wa makundi haya mara nyingi huimba nyimbo za kiasili za Kikamba za kazi huku wakiendelea na kazi zao. Pia, kuna nyimbo huimbwa kuandamana na kazi mbalimbali miongoni mwa jamii ya Wakamba. Nyimbo zinazoimbwa katika muktadha wa aina hii hurejelewa kama *Mbathi sya Wia* na kwa Kiswahili nyimbo za kazi. Hivyo, *Mbathi sya Wia* ni nyimbo zinazoimbwa katika hafla za kikazi. Tazama mifano ifuatayo ya nyimbo za kiasili za Kikamba zinazowasilishwa katika hafla za kikazi:

NA. 30. Kaveti Kaanu

*Kaveti kaanu mbua ni mbiingu, Kaveti kaanu mbua ni mbiingu, ndwose **kathungi**, kamulo na kavelu na uyaangia muundani kaveti kaanu mbua ni mbiingu. Syana iyamba kuvuna ii mbemba sya tumikeve twili. Syana iitonya kuvuna **mbemba** sya selekali mbaitu ii mwaka umwe tumikeve twili.*

Tafsiri

Kamwanamke Kazembe

Kamwanamke kazembe mvua imenysha, Kamwanamke kazembe mvua imenysha, chukua **kiondo**, **jembe** na **mbegu** na kisha uelekee **shambani** Kamwanamke kazembe mvua imenysha. Watoto hawawezi shibishwa na mahindi ya serikali jamani mwaka mmoja mikebe miwili, Watoto hawawezi shibishwa na **mahindi** ya serikali jamani mikebe miwili kwa mwaka mzima. Kamwanamke kazembe mvua imenysha.

Wimbo wa *Kaveti Kaanu* (Kamwanamke Kazembe) ni wimbo unaoimbwa hasa wakati wa majira ya mvua. Hivyo, umbo la muktadha wa wimbo huu ni katika kazi za shambani. Wimbo wenyewe umelengwa kwa mwanamke mzembe asiyependa kazi. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anamhimiza mwanamke mzembe ajitahidi afanye kazi ya upanzi shambani. Anaeleza kwamba chakula cha msaada huwa kidogo na hakiwezi kuwahimili yeye na watoto na hivyo basi hana budi kujitahidi shambani.

Mwimbaji anamweleza mwanamke husika kwamba achukue *kathungi* (kiondo), *kamulo* (jembe) na *kavelu* (mbegu) na kisha aelekee *muundani* (shambani) kwa maana mvua imekwisha nyesha. Hapa, maneno *kathungi* (kiondo), *kamulo* (jembe) na *kavelu* (mbegu) yametumika kijazanda kurejelea nyenzo za kazi. Vilevile, neno *muundani* (shambani) linarejelea maeneo ya kazini. Kupitia jazanda hizi, wanajamii wanahimizwa wajitahidi katika kazi wanazozifanya. Hivyo, mwimbaji anakemea tabia za uvivu na uzembe katika maisha. Anahimiza uwajibikaji hasa kwa wanawake walioolewa. Wimbo wenyewe unapitisha itikadi ya bidii kazini kwamba wanawake hawana budi kujitahidi. Hata hivyo, wimbo huu unawasilishwa mwelekeo wa kitaasubi za kiume kwamba wanawake ndio wanaostahili kuwajibika kwenye kazi za shambani. Maoni yangu ni kuwa, wazazi wa jinsia zote hawana budi kuwajibika kwenye kazi za aina hii kwa maana mchango wa kila mtu awe mke au mume ni muhimu. Hivyo, kina mama pekee wasiwe wa kulaumiwa wakati mambo hayaendi vyema katika jamii. Hivyo, itikadi hii imefumbatwa kijazanda kupitia maneno kama vile *kathungi* (kiondo), *kamulo* (jembe), *muundani* (shambani), *mbeu* (mbegu) na *mbemba sya silikali* (mahindi ya serikali).

Angalia wimbo ufuatao:

NA.31. Muika wia Nukunwe

Yii muika ii wia nukunwe, kasi nukunwe waemwa utungwe na musyi. Ve ndeke ikwitwa Manyali ikukua Konza ii nake Songola Manyali akakua andu ma wia. Yii muika ii wia nukunwe, kasi nukunwe waemwa utungwe na musyi ve ndeke ikwitwa Manyali ikukua Konza ii nake Songola Manyali akakua andu ma wia. Onake Sungula Manyali akakua andu ma wia. Onake Sungula Manyali akakua andu ma wia.

Tafsiri

Vijana Kazi Itekelezwe

Eee vijana, kazi ifanywe, kazi ifanywe na ukishindwa urudishwe nyumbani. Kuna **ndege** inaitwa Manyali, inabeba watu **Konza**, naye

Songola Manyali atabeba watu wa kazi. Eee vijana, kazi ifanywe, kazi ifanywe na ukishindwa urudishwe nyumbani. Kuna **ndege** inaitwa Manyali, inabeba watu Konza, naye Songola Manyali atabeba watu wa kazi. Naye Songola Manyali atabeba watu wa kazi.

Wimbo wa *wia Nukunwe* (Vijana Kazi Itekelezwe) ni wimbo unaohusu utekelezaji wa kazi. Wimbo wenyewe umewasilishwa katika umbo la muktadha wa kikazi. Mwimbaji anawahimiza vijana kuifanya kazi kwa bidii. Hivyo, wimbo huu unawalenga vijana au watu waliopewa kazi fulani wawajibike na kuitekeleza kwa bidii. Inaelezwa hapa kwamba kutotia bidii kazini huenda kukasababisha mtu kuipoteza kazi husika. Hivyo, juhudi ni muhimu kazini. Itikadi ya bidii kazini imewasilishwa kupitia fumbo la usafirishaji ambapo wahusika wenye bidii tu ndio watakaosafirishwa. Hivyo, itikadi ya bidii kazini imefumbatwa kwenye jazanda **ukuwa (ubebwaji), ndeke (ndege) na Konza.**

Tazama wimbo ufuatao pia:

NA. 32. Kavuli Vula

Kavuli vula mwee witu. Kavuli vula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. Kavuli vula mwee witu. Kavuli vula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. Ngima yumaa kwi kuthie, ii vulavula mwee witu. Isandi yumaa kwi kukime ii vula vula mwee witu Kinaa kyumaa kwi kuthie ii vula vula mwee witu. Nikilya nathia kakautwa, nikilya nathia kakautwa nila imutengea ya kivetu yukilasya kwoko ta ikwaunya Kavuli vula mwee witu.

Tafsiri

Kavuli Twanga Mawele

Kavuli twanga mawele yetu, Kavuli twanga **mawele** yetu. Ninakaa hapa uwanjani nikitwangatwanga mawele yetu. Ninakaa hapa uwanjani nikitwangatwanga mawele yetu. Kavuli twanga mawele yetu, Kavuli twanga mawele yetu. **Ugali** hupatikana kwa kusiaga mawele, twanga twanga mawele yetu. **Isandi** (aina ya chakula cha kitamaduni) hupatikana baada ya kusaga mawele, twanga twanga mawele yetu. **Kinaa** (aina ya chakula cha kitamaduni) hupatikana kwa kusiaga mawele, twanga twanga mawele yetu. Unga inapungua kadri ninaposiaga, unga inapungua kadri ninaposiaga. Yule mwanamke mzembe ndiye anapunguza).

Katika wimbo *Kavuli Vula Mwee* (Kavuli Twanga Mawele), mwimbaji anatusawiria maandalizi na matumizi ya chakula cha kiasili cha mawele. Baada ya kuvuna mawele, mawele hayo huhitaji kutwangwa ili kuyatenganisha na uchafu usiohitajika. Hivyo, katika hali hii, mwimbaji anamhimiza mhusika ajitahidi katika kuyatwanga. Ni baada ya kuyatenganisha mawele na uchafu ambapo tunaweza kusiaga mawele hayo ili kupata unga. *Ngima* (Ugali), *isandi* (aina ya chakula cha kiasili) na *Kinaa* (aina ya chakula cha kiasili) hutokana na unga iliyosiagwa. Hivyo, aina hizi za vyakula hupatikana kutokana na bidii katika kazi ya maandalizi. Kupitia jazanda husika, mwimbaji anawasilisha ujumbe kwamba juhudi zinahitajika katika kazi yoyote ile. Kwa ujumla, mtaka cha mvunguni sharti ainame ndio ujumbe mkuu katika wimbo huu. Wimbo wenyewe unapitisha itikadi kuhusu kazi kwamba hamna budi kujitahidi kazini. Itikadi hii imefichwa kwenye jazanda kama vile *Kavuli (anayetwanga)*, *mwee (mawele)* na *ngima (ugali)*.

Watu wengi wanaofanya kazi pamoja huunda hafla ya kazi ya kikundi. Hafla za aina hii hushirikisha uimbaji wa nyimbo za kiasili za kikazi zinazowasilisha itikadi ya kazi kijazanda. Hivyo, kupitia jazanda mbalimbali, waimbaji huwasilisha masuala kama vile umuhimu wa kazi, bidii kazini pamoja na madhara ya uzembe miongoni mwa wanajamii.

4.1.2 Hafla Zisizo Rasmi

Kwa upande mwingine, hafla zisizokuwa rasmi ni zile ambazo hazijapangwa, kuagizwa au kuratibiwa. Hivi ni sawa na kusema kwamba, hafla hizi hujitokeza tu kighafla bila kupangwa. Yaani, uimbaji wa nyimbo za kiasili unaweza kutokea bila kuwepo na mpango wa awali kwamba ungekuwepo. Hafla zinazoorodheshwa katika kategoria hii ni matukio ya uwasilishaji katika hafla kama vile mtu anapojipata akiimba huku akifanya kazi peke yake, mhadumu wa mtoto anapoimba huku akimlea

au kumwongoa mtoto au hata watoto wanaposhiriki michezo yao wanajipata wakiimba nyimbo husika.

4.1.2.1 *Syathi sya wia wa mundu umwe* (Hafla za kazi ya mtu mmoja)

Hafla ya kazi ya mtu mmoja inajitokeza pale ambapo mtu mmoja ndiye anafanya kazi fulani. Miongoni mwa kazi zinazotekelezwa katika jamii hii ni pamoja na kulima, kuvuna mazao shambani, kuchunga mifugo, kusuka vikapu, kukusanya kuni, kuezeka paa la nyumba, ufinyanzi, ujenzi wa nyumba, uchongaji na uhotaji wa maji miongoni mwa nyingine. Mara kwa mara, wanajamii hii hushirikisha uimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba wanapofanya kazi mbalimbali, hata inapofanywa na mtu mmoja. Kwa mfano, ni kawaida kumpata mwanamke Mkamba akiimba nyimbo husika anapoendelea na kazi kama vile kusaga mtama, kuchota maji, kulima au kukusanya kuni. Hivyo, nyimbo zozote za kazi huweza kuimbwa na mtu mmoja pekee au hata zikaimbwa na makundi ya watu wakifanya kazi.

4.1.2.2 *Syathi sya kuongola syana* (Hafla za kuwaongoa watoto)

Hafla za uongoaji watoto hujitokeza pale ambapo huimbwa katika shughuli ya kumwongoa mtoto. Kwa mfano, kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wakamba, kina mama hutekeleza kazi mbalimbali zikiwemo za shambani. Inapotokea kwamba mama mtoto anakwenda mahali, mbali na mtotowe, nyimbo hizi huimbwa na mlezi ili ambembeleze mtoto husika alale au anyamaze iwapo analia. Hivyo, dhima ya nyimbo hizi huwa ni kumwongoa au kumtuliza mtoto, huku hafla yenyewe ikiwa ni ya malezi. Kwa kawaida, watoto huweza kulia kama ishara ya njaa, kiu, maumivu, au pia hamu ya kutaka kumwona mamake. Hivyo, inapotokea kwamba mtoto ameanza kulia, ni jukumu la mlezi kumwambia mtoto yule nyimbo za kumtuliza pamoja na kumfanya alale huku wakiendelea kumsubiri mamake. Katika jamii ya Wakamba, mara nyingi watoto waliachwa na ndugu zao wakubwa au walezi wengine. Katika hali kama hizi,

huenda ikawa mama ameenda shambani au kahudhuria shughuli nyingine muhimu. Hivyo, inapotokea kwamba mtoto ameanza kulia, mlezi hana budi kumwambia mtoto yule nyimbo za kumbembeleza ili anyamaze. Wakati mwingine, mtoto huimbiwa nyimbo hizo ili aweze kulala huku wakimsubiri mama yake afike. Ufuatao ni mfano wa wimbo wa kiasili wa Kikamba ulioimbwa katika hafla ya kuwaongoa Watoto:

NA. 33. Lulu Mwana

*Lulu mwana, koma twithukiisye ee Aa mwaitu mayuka aa Maithingithya **syaamba** aa Mailonzanya ii Mailonzanya No ta maliu ii no ta masuni lulu mwana aaa*

Tafsiri

Lulu Mwana

Lulu mwana, lala tusikilize ee, aakina mama wakija aa, wakitingiza **syaamba** (aina ya ala ya muziki inayovaliwa mguuni)aa, wakipiga kelele ee, wakipiga kelele ee, ni kama ndege ii lulu mwana aaa.

Wimbo wa *Lulu Mwana* huimbwa katika hali ya kumwongoa mtoto mdogo ili alale au anyamaze, awache kulia. Huu ni wimbo unaoimbwa kwa namna ya kuuteka umakinifu wa mtoto ambapo baadaye hushikwa na usingizi na kulala. Wimbo huu unapitisha itikadi kuhusu malezi. Hapa, neno **syaamba** limetumika kijazanda kurejelea kelele inayopigwa na mtoto anapolia.

Ufuatao ni mfano mwingine wa wimbo uliowasilishwa katika hafla ya kumwongoa mtoto:

NA. 34. Ndukilye Mwana

*Lulu mwana ndukilye mwa ndukese kulika ni mbiti. Lulu mwana ndukilye mwa ndukese kulika ni mbiti. Lulu mwana nduvindye mwa mbiti yina maeo moi. Lulu mwana ndukilye mwa ndukese kulika ni **nbiti**. Lulu mwana ndukome mwa, asyai maende muundani. Lulu mwana ndukilye mwa ndukese kulika ni mbiti.*

Tafsiri

Mwana Nyamaza

Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na **fisi**. Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na fisi. Lulu mwana tulia we! Fisi ana

meno makali. Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na fisi. Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na fisi. Lulu mwana lala we! Wazazi waende shambani. Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na fisi. Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na fisi.

Wimbo wa *Ndukilye Mwana* (Mwana Nyamaza) unaimbwa kwa nia ya kumwongoa au kumnyamazisha mtoto. Hapa, mwimbaji anamweleza mtoto anayehusika anyamaze ili asije akaliwa na fisi. Inavyodhihirika ni kwamba, wimbo huu unalengwa kwa mtoto anayelia na aliyeachwa na mlezi baada ya wazazi kwenda kwenye shughuli kama vile za shambani. Hapa, mwimbaji anamweleza kwamba kuna mnyama anayeitwa fisi na ambaye ni hatari. Hivyo, anajulishwa kuwa asiponyamaza ataliwa na mnyama husika. Kwa kuuimba wimbo huu, ni njia moja ya kumnyamazisha mtoto husika ili asiendeleo kulia. Vilevile, hii ni njia mojawapo ya kumfahamisha mtoto mazingira aliyomo ulimwenguni, kwamba kuna usalama na pia kuna hali za hatari maishani. Wimbo wenyewe unapitisha itikadi ya malezi kwamba ni jambo na wajibu muhimu miongoni mwa wanajamii. Jazanda inayojitokeza hapa ni neno *fisi*.

4.1.2.3 Syathi sya unywi wa nzovi (Hafla za ulevi)

Hafla kama hizi huenda zikajitokeza mahali popote tu katika jamii husika. Kwa mfano, unaweza kupatana na mlevi njiani, sokoni au hata kwenye barabara kuu huku akiendelea kuimba nyimbo za kiasili za Kikamba kiulevi ulevi. Pamoja na hayo, wakati mwingine utawapata walevi vilabuni wakiendelea kulewa na kuimba nyimbo wanazozifahamu au wanazoziskia zikiimbwa humo kwenye maeneo wanamouziwa pombe. Hivyo, iwapo uwasilishaji wa aina hii haujaratibiwa kwa njia yoyote, hafla zake basi zitasalia kuwa zisizo rasmi. Utafiti huu pia umebaini kuwa walevi wanaweza kuimba nyimbo zozote za kiasili wanazozifahamu, ziwe za kikazi, kishujaa, au hata za kidini.

4.1.2.4 *Syathi sya ithau ya syana* (Hafla za michezo ya watoto)

Katika jamii ya Wakamba, mara nyingi michezo ya watoto huambatanishwa na nyimbo. Hivyo, watoto huimba nyimbo zikiwemo za kiasili za Kikamba wanapocheza. Kama ilivyo katika jamii nyingine za Kiafrika, watoto Wakamba hucheza michezo yao inayoambatanishwa na nyimbo wakati wa mchana na hata wakati wa jioni baada ya shughuli za siku. Hasa katika kipindi cha hapo awali kabla ya majilio ya elimu ya kisasa, watoto walicheza, kusimuliana hadithi, kufumba na kufumbiana mafumbo, kutega na kutegua vitendawili, miongoni mwa mengine. Haya yalifanywa hasa wakati wa jioni baada ya shughuli za siku. Vilevile, watoto Wakamba hucheza michezo mbalimbali kama vile kuruka kamba, kujificha na kutafutana, n.k. Kwa kawaida, baadhi ya michezo ya watoto huandamana na nyimbo. Nyimbo hizi zinazotungwa na kuimbwa na watoto katika michezo yao hurejelewa kama *Mbathi sya Ithau ya Syana* yaani nyimbo za michezo ya watoto. Hivyo, nyimbo hizi huimbwa katika miktadha inayohusisha uchezaji wa watoto. Tazama mifano ifuatayo ya nyimbo za kiasili za Kikamba zinazoimbwa katika hafla za michezo ya watoto:

NA. 35. *Natwaie Valua*

Natwaie valua kwa tata ii na waia nziaani ii. Natwaie valua kwa tata ii na waia nziaani ii, Natwaie valua kwa tata ii na waia nziaani ii. Natwaie valua kwa tata ii nawaia nziaani ii. Indi tiwe, indi tiwe, indi tiwe, indi niwe.

Tafsiri

Nilipeleka Barua

Nilipeleka **barua** kwa baba na ikapotelea njiani. Nilipeleka barua kwa baba na ikapotelea njiani. Nilipeleka barua kwa baba na ikapotelea njiani. Lakini si wewe, si wewe, si wewe na ni wewe.

Kupitia wimbo NA.35. *Natwaie Valua (Nilipeleka Barua)*, mwimbaji anasimulia namna alivyoipoteza barua fulani aliyokuwa akiipelekea babake. Wimbo huu huimbwa na watoto wakiuambatanisha na mchezo fulani wa kukimbia na

kukimbizana. Neno **valua (barua)** limetumika kurejelea ujumbe muhimu. Wimbo wenyewe unawasilisha umuhimu wa uwajibikaji katika malezi. Yaani, Watoto wanastahili kuwajibika na majukumu wanayopewa wanapoendelea kukua. Hivyo, jazanda inayojitokeza hapa ni **valua (barua)**.

Tazama mfano huu pia:

NA. 36. Na Muyo Ndwalasya

*Na muyo ndwalasya, na muyo ndwalasya kethia niwalasya ndikoma ni **kyalya**. Na muyo ndwalasya, na muyo ndwalasya kethia niwalasya ndikoma ni **kyalya**. Na muyo ndwalasya, na muyo ndwalasya kethia niwalasya ndikoma ni **kyalya**. Na syana mwiiw'a ata ii? Ii twiiw'a muyo tuyosa **kikombe**. Alimu mwiiw'a ata ii? Ii twiiw'a muyo tuyosa **kikombe**. Asyai mwiiw'a ata ii? Ii twiiw'a muyo tuyosa **kikombe**.*

Tafsiri

Furaha Haiumi

Utamu hauumi, utamu hauumi kama ungekuwa unauma singeweza kulala kwa sababu ya **maumivu**. Utamu hauumi, utamu hauumi kama ungekuwa unauma singeweza kulala kwa sababu ya maumivu. Utamu hauumi, utamu hauumi kama ungekuwa unauma singeweza kulala kwa sababu ya maumivu. Watoto mnahisi vipi? Tunafurahia tukichukua tuzo. Walimu mnahisi vipi? Tunafurahia tukichukua **tuzo**. Wazazi mnahisi vipi? Tunafurahia tukichukua tuzo.

Na Muyo Ndwalasya (Utamu Hauumi) ni wimbo unaoimbwa kuelezea furaha isiyokuwa na kifani aliyo nayo mwimbaji. Kupitia wimbo huu, mwimbaji anaonekana kuwa na furaha kubwa inayotokana na ushindi wake katika mashindano fulani. Mwimbaji anaeleza kwamba ana furaha isiyokuwa na kifani kwa maana wametuzwa. Hivyo, kama furaha ingepimika kwa mizani au kama ingekuwa inasababisha maumivu, yeye hangelala kutokana na maumivu hayo. Hivyo, ni wimbo unaoimbwa na watoto katika shughuli ambapo kulikuwepo na mashindano fulani na ambapo wao ndio wameibuka washindi na kisha wakatuzwa. Kwa hivyo, wimbo huu unaendeleza itikadi ya kazi kwamba ni muhimu kujitahidi kwa lolote tunalolifanya. Maneno

kikombe (tuzo) na **kyalya (maumivu)** yametumika kijazanda ili kufumbata itikadi husika.

Tazama mfano mwingine wa wimbo uliowasilishwa kwenye hafla ya michezo ya watoto:

NA. 37. Osa Kindu Wikye Kingi

Nuu ula twimutuma, nuu ula twimutuma, nuu ula twimutuma?

Na nduku twimutuma, na Nduku twimutuma, na Nduku twimutuma.

Ukakethye andu Nduku, Ukakethye andu Nduku, Ukakethye andu Nduku.

*Osa **kindu** wikye kingi, Osa kindu wikye kingi, Osa kindu wikye kingi.*

Ai ai isokote, isokote isokote, isokote isokote.

Ai ai isokote, isokote isokote, isokote isokote.

Tafsiri

Chukua Kitu Urushe Kingine

Ni nani tutamtuma, ni nani tutamtuma, ni nani tutamtuma?

Na Nduku tunamtuma, na Nduku tunamtuma, na Nduku tunamtuma?

Ukawasalimu watu Nduku, Ukawasalimu watu Nduku, Ukawasalimu watu Nduku.

Chukua **kitu**, urushe kingine, Chukua kitu, urushe kingine, Chukua kitu, urushe kingine.

Ee Ee, cheza, cheza cheza, cheza cheza

Ee Ee, cheza, cheza cheza, cheza cheza.

Huu ni wimbo wa watoto unaoambatanishwa na uchezaji fulani wanapoendelea kucheza. Wakati mwingine, wimbo wenyewe huimbwa na watoto mbele ya hadhira ya watu wazima au watoto wenzao ili kuwaburudisha tu ambapo si lazima pawepo na ujumbe maalum.

Angalia mfano huu pia:

NA. 38. Tingilingili

*Tingilingili, tingilingili, **ng'ombe sya utuku** syuyawa utuku tingilingili.*

*Tingilingili, tingilingili, ng'ombe sya nau syuyawa utuku nula **mukavi** akanywe iia tingilingili.*

Tingilingili, tingilingili, ng'ombe sya utuku syuyawa utuku tingilingili.

Tingilingili, tingilingili, ng'ombe sya nau syuyawa utuku nula mukavi akanywe iia tingilingili.

Tingilingili, tingilingili, ng'ombe sya nau syuyawa utuku tingilingili.

Tafsiri

Tingilingili

Tingilingili, tingilingili, **ng'ombe wa usiku** wanaibwa usiku tingilingili, tingilingili.

Tingilingili, tingilingili, **ng'ombe wa baba** wanaoibwa usiku na yule **Mmaasai**, akanywe maziwa, tingilingili, tingilingili.

Tingilingili, tingilingili, ng'ombe wa baba wanaoibwa usiku tingilingili, tingilingili.

Tingilingili, tingilingili, ng'ombe wa baba wanaoibwa usiku na yule **Mmasai**, akanywe maziwa, tingilingili, tingilingili.

Tingilingili, tingilingili, ng'ombe wa baba wanaoibwa usiku tingilingili, tingilingili.

Wimbo wa Tingilingili ni wimbo unaoimbwa na watoto wanapocheza. Mwimbaji anaeleza kwamba **ng'ombe wanaoibwa** usiku, hupotea usiku pia. Anaendelea kueleza namna **ng'ombe** waliomilikiwa na babake walivyoibwa na Wamaasai wakati wa usiku. Kupitia jazanda **ng'ombe wa baba** mwimbaji anapitisha ujumbe kwamba **mali ipatikanayo kwa wizi**, hupotea kwa njia hiyo hiyo ya wizi. Hivi ni kumaanisha kuwa, mwizi anapoiba hata yeye huipoteza mali hiyo kwa kuibiwa. Wimbo huu unarejelea muktadha wa kihistoria kwenye jamii ya Wakamba. Katika kipindi cha hapo kale, jamii ya Wamaasai na Wakamba zilishiriki kwenye mashambulizi na wizi wa mifugo mara kwa mara hasa kwenye maeneo ya mipakani.

Wimbo huu unawasilisha itikadi kuhusu ufisadi kwamba haufai. Wimbo wenyewe umebeba ujumbe wa wizi wa mifugo katika jamii ya Wakamba. Kupitia wimbo huu, mwimbaji anasimulia namna baba yake huibiwa ng'ombe ambao huishia kumnufaisha mwizi husika, kutoka kwa jamii jirani ya Wamaasai. Mwizi huyo hunufaika kwa kupata maziwa huku babake akienda hasara kubwa kutokana na tukio lile. Hata hivyo, mwimbaji anaeleza kwamba ng'ombe wanaoibwa usiku wataibiwa vivyo hivyo tu na

wala mwizi anayehusika hatofaidi kamwe. Hivyo, wimbo huu unapitisha itikadi ya kisiasa kwamba ufisadi haufai. Hivyo, *ng'ombe sya tata (ng'ombe wa baba)* na *ng'ombe sya utuku* (ng'ombe wanaoibwa usiku) ni maneno yaliyotumika kijazanda kurejelea mali ya wizi ambayo haifaidi.

4.1.2.5 *Syathi sya uvithukii/kau* (Hafla ya mashambulizi/vita)

Hapo zamani, wanajamii Wakamba walikuwa na vita vya kuviziana vya mara kwa mara kati yao na jirani zao kama vile Wamasai na Wagikuyu. Wavamizi Wamaasai walirejelewa kama *Akavi* au *Iloikop*. Pamoja na hayo, pamekuwepo na uvamizi na wizi wa mifugo kati ya jamii ya Wakamba na jamii ya Wasomali. Hali hii imekuwa ikijirudiarudia mara kwa mara hasa katika maeneo ya mpakani. Hivyo, nyimbo za kiasili za Kikamba hazijaitenga na masuala haya. Kwa hivyo, nyimbo za aina hii zinahusiana na hafla za kimashambulizi. Ifuatayo ni mifano ya nyimbo zilizowasilishwa katika hafla za vita/mashambulizi:

NA. 39. Ngulu wa Ngao

Nguluuu iii Ngulu Mwelela Nguluuuui Ngulu Mwaiwaa. Nguluuu iii Ngulu Mwelela Nguluuuui Ngulu wa Kasimbili. Iwe Ngulu, wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. Malenge meene mwatemangie, no mukaiva, Ngulu wa Ngao, iwe Ngulu wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. Malenge meene mwatemangie, no mukaiva, Ngulu wa Ngao, iwe Ngulu wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. Ngulu, wa Ngao, Ngulu, wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili.

Tafsiri

Ngulu wa Ngao

Nguluuu iii Ngulu Mwelela Nguluuuui Ngulu Mwaiwaa. Nguluuu iii Ngulu Mwelela Nguluuuui Ngulu wa Kasimbili. Iwe Ngulu, wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. **Maboga** ya wenyewe mlioyakatakata, mtalipa tu. Maboga ya wenyewe mlioyakatakata, mtalipa tu Ngulu wa Ngao, wewe Ngulu wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. Ngulu wa Ngao, wewe Ngulu wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. Ngulu, wa Ngao, Ngulu, wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili.

Wimbo huu unasimulia mhusika anayeitwa Ngulu wa Ngao na wenzake ambao ni wapiganaji. Mwimbaji anawaeleza kuwa watalipia maboga ya wenyewe waliyoyakatakata shambani. Kupitia wimbo teule, mwimbaji anawahimiza wahasika kuwa hodari na tayari kupambana. Anawaeleza kwamba huenda wapinzani wao wakarejea kulipiza kisasi, hivyo ni muhimu kuwa waangalifu na tayari wakati wote. Wimbo wenyewe umeimbwa wakati wa vita ili kusesitiza ushujaa na uzalendo. Kwa ujumla, wimbo wenyewe unazungumzia vita vya kuviziana vilivyokuwepo awali kati ya jamii ya Wakamba na Wamaasai au Wagikuyu. Wimbo wenyewe unapitisha itikadi kuhusu vita kwamba wapiganaji hawana budi kuwa wenye ujasirig. Itikadi hii imefumbatwa kijazanda. Kwa mfano, mwimbaji anawasifu wapiganaji kuwa walikatakata maboga ya wenyewe ambapo ni ishara ya ushindi. Hata hivyo, kwa wakati huo huo anawahimiza wawe jasiri na wakakamavu wakati wowote adui anaweza kurudi kulipiza kisasi. Hivyo, neno **malenge matemangiwe (maboga yaliyokatwakatwa)** limetunmika kijazanda kuashiria **uharibifu** unaotokana na vita. Mwimbaji anawasilisha ujumbe kwamba vita havifai kwa lolote. Hii ni kwa sababu hata wanapoibuka washindi, adui anaweza rudi kulipiza kisasi wakati wowote. Hivyo, vita na mashambulizi haviwanufaishi wanaohusika.

NA. 40. Ngune Kithuki

Ngune kithuki mutambo ukaye, Ngune kithuki mutambo ukaye. Musumali niwaleile na ng'ombe. Ekwatya ii Mbiki ni ngulu mbiingi. Ekwatya ii Mbiki ni ngulu mbiingi. Teka Misi waleile Veveloni mwa umiloni wa syua mwa Elisavethi tavya munene nake atume watho ngwaithangye mukau wilingile ii iya u mututu uu ng'ombe ii sya ndia sya kwinukya kioko vayi undu ekai tuthi utwa nzuke Musumali niwaleile na ila ingi.

Niwanengie ndata yayu, nengi naendie kithekani ta mbusya, ngithi ukwama Kalisa nde ngua. Kitheka ki munyambu ii na mbusya ii o ili tunamanzaa inaa. Syangomisye Kalisa ii nde ngua, kitheka ki minyambu na mbusya o ili tunamanzaa inaa.

Tafsiri

Nipige Mbiu

Nipige **mbiu mtambo** utoe sauti, Nipige mbiu **mtambo** utoe sauti. Msomali amekatalia na ng'ombe. Anadhani mimi Mbiki nina maringo mengi. Anadhani mimi Mbiki nina maringo mengi. Kama Misi hangelinda Veveloni, upande wa Mashariki jamani Elisavathi, mwambie mkubwa naye atoe amri nipige mbiu isikike ii iya! Hivi vita, hawa ng'ombe wa wajinga wanaoibiwa asubuhi, hamna neno wacheni twende tukaonane nao, tujue bivu na bichi Msomali amekatalia na wale wengine.

Alinipa **fimbo** jamani, kisha nilienda kichakani kama **kifaru**. Nilikwama Garisa bila mavazi. Kichaka kilicho na **simba** na vifaru, ng'ombe wawili tuliokuwa tukiwatafuta wakapotea. Walinifanya nilale Garisa bila mavazi. Kichaka kilicho na simba na kifaru, wawili tuliokuwa tukiwatafuta wakapotea.

Wimbo huu unatusawiria uvamizi na wizi wa mifugo kati ya jamii ya Wakamba na Wasomali. Mwimbaji anaeleza namna walivyoshambuliwa na kuibiwa ng'ombe ambapo waliwafuata washambulizi wao lakini hawakufaulu. Mwimbaji anasema kwamba alihangaika na kutembea hadi misituni mjini Garisa lakini hakufaulu kuwapata ng'ombe aliokuwa akiwatafuta. Vilevile, wimbo huu unamsifu mhusika Misi kwa ujasiri na ukakamavu wake uliomfanya azuie wizi huo kwenye upande wa Mashariki. Hivyo, wimbo wenyewe unawasisisha itikadi ya vita na mashambulizi kwamba wahusika hawana budi kuwa jasiri na wakakamavu. Itikadi hii imefumbatwa kijazanda kwenye maneno kama vile *ndata (fimbo)*, *mbusya (kifaru)*, *minyambu (simba)* na *kithuki (mbiu)*.

Wimbo ufuatao pia uliimbwa kwenye hafla ya vita:

NA. 41. Nzoka ya Mukelele

Kakiti ukathua ta mukala ii. Kakiti ukathua ta mukala ii. Taambukya kwoko ngutwile mata ii pu! Ndyi kyeni syoka syoka Kakiti ii ukathua ta Mukala. Taambukya ingi, pu! Ndyi kyeni syoka syoka Kakiti ii ukathua ta Mukala

Nzoka ni ya uthwii ii nzoka, ya mukelele. Nzoka ni ya uthwii ii nzoka, ya mukelele. Aume mwisila va ni nzoka? Ya mukelele. Iveti mwisila va ni nzoka, ya mukelele. Nzoka ni ya mumo nzoka, ya

mumo. Nzoka ni ya mumo nzoka, ya mumo. Aume mwisila va ni nzoka? Ya mumo, iveti mwisila va ni nzoka, ya mumo.

*Katiia kutava we umaala utave indo. Aaaa! umaala utave indo. Katiia kutava we umaala utave indo. Aaaa!umaala utave indo. Nzoka ni ya kutava we umaala utave **ng'ombe**, Aaaa! umaala utave ng'ombe. Nzoka ni ya kutava we umaala utave indo, Aaaa! umaala utave **indo**.*

Tafsiri

Nyoka Maridadi

Kakiti utatajirika kama Mgalla ee. Kakiti utatajirika kama Mgalla ee. Nyoosha mkono nikutemee **mate** pu! Sina mkosi geuka Kakiti ee utatajirika kama Mgalla. Nyoosha tena pu! Sina mkosi geuka Kakiti ee utatajirika kama Mgalla.

Nyoka ni wa utajiri huyu nyoka, maridadi. Nyoka ni wa utajiri huyu **nyoka maridadi**. Wanaume mtapitia wapi juu ya huyu nyoka? Maridadi. Wamama mtapitia wapi juu ya nyoka? Maridadi. Nyoka ni wa nehema huyu nyoka, wa nehema. Nyoka ni wa nehema huyu nyoka, wa nehema. Wanaume mtapitia wapi juu ya huyu nyoka? Wa nehema. Wamama mtapitia wapi juu ya nyoka? wa nehema.

Harakisha kuchota wewe toka uchote mifugo. Aaaa! toka uchote mifugo. Harakisha kuchota wewe toka uchote mifugo. Nyoka ni wa kuchota wewe toka uchote **ng'ombe**, Aaaa! toka uchote ng'ombe. Nyoka ni wa kuchota wewe toka uchote ng'ombe, Aaaa! toka uchote **mifugo**.

Wimbo huu unatusawiria hali ilivyokuwa kabla ya wapiganaji wa jamii ya Wakamba kutoka kwenda kuwavamia na kuwaibia wanajamii majirani kama vile Wasomali. Imedhihirika hapa kwamba nabii/mganga alishirikishwa katika shughuli hii ambapo alitabiri kwanza juu ya kufanikiwa au kutofanikiwa katika shughuli husika. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anaeleza hali ambapo anamtaka Kakiti anyooshe mikono yake aitemee mate kama ishara ya kuibariki na kuikabidhi shughuli yao kwa Mungu ile wasipate mikosi safarini. Baada ya kumtemea mate, mwimbaji (nabii) anamweleza mhusika kwamba kuna nyoka maridadi amejitokeza. Kwa mujibu wa mwimbaji, nyoka mwenyewe ni ishara ya utajiri, nehema, baraka na mafanikio. Hivyo, Kakiti na wavamizi wenzake wanaelezwa kwamba ni nafasi yao ya kwenda kuchota mali ya aina ya ng'ombe na mifugo wengine ili watajirike kama Mgalla. Hivyo, wimbo huu

umeimbwa katika umbo la muktadha wa uvamizi. Wimbo wenyewe unapitisha itikadi ya vita kwamba kabla ya kwenda vitani walimshirikisha Mungu kwa njia ya maombi ambapo aliwajibu kwa njia mbalimbali.

Kwa mfano, kwenye wimbo, nyoka maridadi anajitokeza ambapo ni ishara kwamba watafanikiwa kwenye shughuli zao za uvamizi. Vilevile, wasikilizaji wanafahamishwa kwamba ni muhimu kujua majira na wakati, yaani kuna wakati wa kushambulia na pia upo wakati wa kutofanya mashambulizi. Pia, ujasiri unasisitizwa kwa washambulizi kupitia wimbo huu. Kutokana na maelezo hayo, itikadi ya vita inawasilishwa kijazanda kupitia maneno kama vile *nzoka ya mukelele (nyoka maridadi)*, *mata (mate)*, *indo (mifugo)* na *ng'ombe (ng'ombe)*.

Imedhihirika hapa kwamba nyimbo zinazoimbwa katika hafla za vita au mashambulizi zinahusiana na masuala ya vita, mashambulizi, ujasiri na ulipizaji kisasi. Masuala haya hufumbatwa kijazanda na huendeleza itikadi ya vita.

4.2 Uchanganuzi wa Jazanda katika Nyimbo za Kiasili za Kikamba

Sehemu hii imechunguza jazanda mbalimbali zinazojitokeza katika nyimbo za kiasili za Kikamba zinazowasilishwa kwenye hafla maalum zilizadiliwa katika sehemu 4.1. Uchanganuzi wa jazanda umeongozwa na nadharia ya Jazanda Dhanifu. Nadharia hii inadai kwamba katika ufasiri wa maana za jazanda, tunafaa kuzingatia nyanja mbili ambazo ni Uwanja asilia (A) na Uwanja Lengwa (B). Hivyo, ufasiri wa maana za jazanda unahusisha uhamishaji wa sifa za uwanja asilia (A) hadi uwanja lengwa (B). Kutokana na maelezo hayo, uwanja (A) unaweza kutajwa kwa kurejelea uwanja (B). Hivyo, kila ufafanuzi wa kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba umechunguzwa kwa kuangazia uhusiano uliopo kati ya uwanja asilia na uwanja

lengwa. Uchanganuzi umezingatia jazanda zinazotumika katika NZK kwenye hafla mahsusi.

4.2.1 Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Tohara

Utafiti huu umetambua kwamba NKK zinazowasilishwa kwenye hafla za Tohara hufumbata itikadi kuhusu tohara kijazanda. Zifuatazo ni baadhi ya jazanda hizo:

i) Jazanda ya *muti mumu* (Mti uliokauka)

Muti uu ni mumu

Mti huu umekauka/umekomaa

Mboo za watahiriwa ziko tayari kwa utu uzima

Katika wimbo *Kwa sisya Wone (Angalia Uone)*, mwimbaji ambaye ni ngariba anaeleza kuhusu mti uliokomaa au kukauka. Katika hali hiyo, anawauliza watahiriwa ili aukate ambapo wanamruhusu kupitia kwa wimbo huohuo. Hivyo, wimbo wenyewe umewasilishwa kijazanda ambapo ngariba analinganisha uume wa watahiriwa na mti uliokomaa au kukauka. Mhimili wa ukawaida wa jazanda unashikilia kwamba uzoefu wa maelezo ya kijazanda huimarisha maana za kimsingi katika akili za wazungumzaji wa lugha yoyote inayohusika. Hivyo, Jazanda ya *muti mumu* (mti uliokauka) imetumika katika wimbo huu ili kuibua itikadi ya tohara kwamba watahiriwa wanatarajiwa kuwa wenye ujasiri kabla na baada ya kupashwa tohara. Vilevile, watahiriwa wanajuzwa kwamba baada ya tohara watakuwa wamehitimu kupata jiko kwani watakuwa wamekomaa kiasi cha kufanya hivyo. Sifa za mti uliokomaa zinamwezesha msikilizaji kupakua sifa zifuatazo:

Mti uliokomaa (Uwanja Asilia A)

Ni mmea

Umekomaa

Tayari kwa mazao


Mboo za Watahiriwa (Uwanja Lengwa B)

Ni sehemu ya mwili

zimekomaa

Tayari kwa utu uzima

Hivyo, *mti uliokomaa* ndio uwanja asilia A, huku mboo za watahiriwa zikiwa uwanja lengwa B. Angalia mchoro huu:



Kielelezo 4.1: Fasiri ya Jazanda ya *Muti Mumu* (Mti uliokomaa)

ii) Jazanda ya *mbilano* (Kazi)

*Ala matesi **mbilano***

Wasiojua **kazi**

Wasiojiweza **kingono/kimapezi**

Kupitia kwa wimbo **NA.1. Kwa Sisy Wone (Angalia Uone)**, mwimbaji anawaeleza watahiriwa kwamba wasiwe na woga kama wajinga wa milimani wasiojua **kazi**. Mhimili wa umbo dhanifu la jazanda unashikilia kwamba jazanda ni tukio la lugha linalotumia maneno ili kuwasilisha maana. Hivyo, neno **kazi** limetumika kijazanda kuwasilisha maana ya **ngono**. Kutokana na hali ya kutotaka kufananishwa na wajinga wa milimani, watahiriwa wanatarajiwa kuwa jasiri wanapotahiriwa. Maarifa ya kimsingi kuhusiana na kazi yanaiwezesha akili ya msikilizaji kuzipakua sifa zifuatazo:

Kazi (Uwanja Asilia A)

Ni shughuli ya kimwili au kiakili

Huhitaji nguvu

Huhitaji weledi

Ngono/mapenzi (Uwanja Asilia B)


Ni shughuli ya kihisia na kimwili

Huhitaji nguvu

Huhitaji weledi

Hapa, neno *kazi* ndio uwanja asilia A huku neno *ngono* likiwa uwanja lengwa B.

Tazama mchoro ufuatao:



Kielelezo 4.2: Fasiri ya Jazanda ya Mbilano (Kazi)

iii) Jazanda ya *matila ma kiimani* (Wajinga wa milimani)

Ta matila ma kiimani ala matesi mbilano

Kama *wajinga wa mlimani* wasiojua *kazi*

Kama *Wakikuyu* ambao hawajiwezi *kimapenzi*

Katika wimbo *Kwa Sisy Wone (Angalia Uone)*, ngariba anawahimiza watahiriwa wasiogope kutahiriwa. Anawaeleza kwamba wasiogope kama **wajinga wa milimani** wasiojua **kazi**, yaani **ngono/mapenzi**. Watahiriwa kwa kuchelea kufananishwa na “wajinga kutoka milimani” wanajikaza na kutoonyesha dalili zozote za woga. Mhimili wa tatu wa NJD unaeleza kwamba ufasiri wa jazanda unahusisha kuelewa uzoefu halisi pamoja na mifumo ya kimaumbile na mielekeo ya mtumiaji wa lugha anayehusika. Kutokana na uzoefu halisi wa Wakamba, *wajinga wa milimani* kwenye wimbo huu ni Wakikuyu kwa sababu wanaishi sehemu zenye milima kinyume na Wakamba wanaoishi sehemu tambarare. Katika muktadha wa utamaduni wa Wakamba, watu wa milimani yaani Wakikuyu wanachukuliwa kuwa wavivu na

ambao hawajiwezi kimapenzi (Wathome, 2009). Hivyo, akili ya msikilizaji inapakua sifa zifuatazo kuhusiana na nyanja hizi mbili:

Wajinga wa Milimani (Uwanja Asilia A)


Ni binadamu
Ni wazembe
Wasiojua kazi

Wakikuyu (Uwanja Asilia B)

Ni binadamu
Ni wazembe
Wasiojua kazi ya ngono

Kutokana na maelezo yaliyopo hapo juu, *wajinga wa milimani* ndio uwanja asilia A.

Uwanja huu ndio unaomwelekeza msikilizaji kwenye uwanja lengwa B, ambao ndio ufasiri wa jazanda inayohusika. Jazanda yenyewe imeifumbata itikadi ya tohara, ndoa na mapenzi. Mchoro ufuatao ni muhtasari wa maelezo haya:



Kielelezo 4.3: Fasiri ya Jazanda ya *Matila ma Kiimani* (Wajinga wa Milimani)

iv) Jazanda ya *munyambu* (Simba)

Munyambu nuukiva
Simba ananguruma
Ngariba yuko tayari

Kauli iliyopo hapo juu ni ya kijazanda. Hii ni kwa sababu sifa za mnyama zinalinganishwa na za binadamu. Huu ni ulinganishaji wa sifa kati ya uwanja wa wanyama na ule wa kibinadamu. Katika wimbo *Munyambu nuukiva*, mwimbaji anamlinganisha simba na ngariba. Katika hali ya kawaida, simba ni mnyama mkali

ambaye anaogopwa na binadamu kwa ukali wake. Hivyo, msanii anamlinganisha ngariba na simba ili aweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo kwa kufahamu kwamba, wanajamii wanamwamini na wanamthamini kwa kazi yake. Watahiriwa wanafahamishwa kwamba ngariba huyo mkali asiogopwe kwa sababu aliyemualika ni baba na hivyo, hawezi kuwadhuru kwa lolote. Kwa mujibu wa NJD, uundaji, ufasiri na uelewekaji wa jazanda huhusisha mchakato wa kiutambuzi pamoja na uhamishaji wa maana kwa mujibu wa maarifa ya kimsingi ya kila siku kuhusiana na mazingira yanayohusika. Hivyo, maarifa ya kimsingi kwenye mazingira haya ya tohara yanamwongoza msikilizaji katika kutambua kwamba simba anayerejelewa hapa si mwingine ila ngariba anayewatahiri vijana kwenye manthari ya uimbaji. Hivyo, sifa za simba zinaiwezesha akili ya msikilizaji kuzipakua sifa zifuatazo kuhusu ngariba:

Simba (Uwanja Asilia A)


Ni mnyama
Ni jasiri
Ni mkali
Huishi porini
Ni mweledi mawindoni

Ngariba (Uwanja Lengwa B)

Ni binadamu
Ni jasiri
Ni mkali
Huishi nyumbani
Ni mweledi wa kutahiri

Hivyo, neno *simba* ndilo uwanja asilia A, huku *ngariba* likiwa uwanja lengwa B. Jazanda hii imeifumbata itikadi ya tohara kwamba ngariba hana budi kuwa mweledi kwenye ujuzi wa kutahiri. Vilevile, inadhihirika kwamba watahiriwa hawana budi kuwa jasiri katika kipindi cha na baada ya tohara.

Tazama mchoro huu:



Kielelezo 4.4: Fasiri ya Jazanda ya *Munyambu* (Simba)

v) Jazanda ya *ndiani* (Kidimbwini)

Mwaikwa niwalika Ndiani

Mtahiriwa ameingia **Kidimbwini**

Mtahiriwa hana budi kujitegemea

Kupitia kwa wimbo *Mwaikwa niwalika Ndiani* (**Mtahiriwa ameingia Kidimbwini**), mwimbaji anaeleza kwamba mtahiriwa ameingia katika kidimbwi. Muktadha wa uwasilishaji wa wimbo huu umetuongoza katika kufahamu kwamba neno *ndiani* (kidimbwini) limetumika kijazanda kurejelea hali ya **kujitegemea**. Katika hali ya kawaida kwenye jamii ya Wakamba, kidimbwi hutumiwa na vijana katika kuogelea. Hivyo, anayejibwaga kwenye kidimbwi lazima awe na uwezo wa kuogelea pamoja na kukabiliana na changamoto za uogeleaji. Kwa hivyo, mwogeleaji hutegemea uwezo na ustadi wake wa kuogelea pale kidimbwini. Katika muktadha huu, maarifa ya kimsingi kuhusu kidimbwini yanamwezesha msikilizaji kufahamu kwamba maana inayokusudiwa hapa ni utegemevu. Hivyo, mwimbaji anazilinganisha sifa za kidimbwini na zile za hali ya kujitegemea. Hivyo, kidimbwini ndio uwanja asilia (A)

huku hali ya kujitegemea ikiwa Uwanja Lengwa (B). Kutokana na maelezo hayo, sifa za kidimbwini zinaiwezesha akili ya msikilizaji kuzipakua sifa za hali ya kujitegemea akilini mwake. Kwa hivyo, akili ya msikilizaji inapakua sifa zifuatazo kuhusiana na kidimbwini na hali ya kujitegemea:


Kidimbwini (Uwanja Asilia A)

Ni mkusanyiko wa maji
Huogelewa na wahusika
Mhusika hutegemea weledi wake
Huwafaidi wahusika

Utegemevu (Uwanja Lengwa B)

Ni hali dhahania
Hudhihirishwa na wahusika
Mhusika hutegemea weledi wake
Huwafaidi wahusika

Sifa za mfanano kati ya kidimbwini na utegemevu ni kwamba mhusika hunufaika kutokana na weledi wake wa kujitegemea. Tazama mchoro ufuatao:



Kielelezo 4.5: Fasiri ya Jazanda ya *Ndiani* (Kidimbwini)

Jazanda yenyewe imeifumbata itikadi ya tohara kwamba baada ya kupashwa tohara, mtahiriwa hana budi kuwajibika na kujitwika majukumu ya watu wazima. Hii ni kwa sababu baada ya kupashwa tohara, mtahiriwa huvuka kutoka utotoni hadi utu uzima.

vi) Jazanda ya *kaindo* (Kakitu)*Ve kaindo kala ngumanza.*Kuna **kakitu** ninakatafuta*Mwimbaji anatafuta mke*

Katika wimbo *Kaindo*, tunaielezwa kwamba mwimbaji ana kakitu anakokatafuta. Inaelezwa kwamba aidha msichana Mulekye, Vaati au Kanyaa ndio wamekaficha. Hapa, kakitu kenye hakajabainika ni ka aina gani. Maarifa ya kimsingi yanatuwezesha kutambua kuwa kinachotafutwa kimo kwenye mhusika wa kike. Kwa hivyo, neno *kakitu* limetumika kijazanda ili kurejelea mke. Jazanda hii inalinganisha sifa za kakitu na zile za mke. Hapa, kakitu ndiko uwanja asilia (A) huku binadamu (mke) akiwa uwanja lengwa (B). Hivyo, sifa za kakitu zinaiwezesha akili ya msikilizaji kuzifikia sifa za mke akilini mwake. Kutokana na maelezo hayo, akili ya msikilizaji inapakua sifa zifuatazo kuhusiana na *kakitu* anakokatafuta na *mke*:

Kakitu (Uwanja asilia A)

Ni kitu

Si bayana

Ni chenye manufaa

Kamefichwa na wahusika wa kike

Mke (Uwanja lengwa B)


Ni binadamu

Ni bayana

Manufaa ya kumtunza mumewe

Ni wa kike

Jazanda ya *kaindo* nahamisha sifa za kakitu hadi kwa sifa za mke. Hivyo, baadhi ya sifa za kakitu husika ambao ndio uwanja asilia (A) zimetumika kwa kubaini sifa za mke, ambaye ndiye uwanja lengwa (B). Kutokana na uchanganuzi huu, upo mfanano kati ya kakitu na mke. Mfanano wenyewe ni kwamba kakitu kamefichwa na wahusika wa kike huku mke akiwa ni wa kike pia. Mchoro ufuatao unawasilisha maelezo haya:



Kielelezo 4.6: Fasiri ya Jazanda ya *Kaindo* (Kakitu)

Jazanda hii imetumika kuwasilisha itikadi ya ndoa na tohara miongoni mwa Wakamba. Wimbo wenyewe unaimbwa katika hafla ya tohara. Hivyo, walengwa wasikilizaji ni vijana wa kiume waliopashwa tohara. Kwa mfano, inaaminika kuwa tohara ni ishara ya kwamba wamekomaa na kuhitimu kupata jiko. Hivyo, kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wakamba, kijana anapopashwa tohara huwa amepita kiwango cha utoto hadi utu uzima. Kwa hivyo, hana budi kupata mke mwema wa kufunga ndoa naye. Hii ni kwa sababu ndoa huchukuliwa kuwa njia pekee ya kuiendeleza jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hivyo, itikadi ya ndoa inapitishwa kwamba ndoa ni kitu kizuri na kwa hivyo apataye mke hupata kitu kinachoenziwa na wanajamii.

vi) Jazanda ya *mwatu* (Mzinga)

Ukwa mwatu uno nukutha na ndwina uki.

Huu mzinga una nyuki wengi na kumbe hamna asali.

Msichana yupo lakini hajakomaa kimapenzi.

Hapa, tunaeleza kuhusu mzinga ambao una nyuki wengi lakini ndani yake hamna asali, yaani asali yenyewe haipo au imo katika hali ya maandalizi. Jazanda hii

inalinganisha sifa za kifaa kinachohifadhi nyuki wanaoandaa asali na sifa za binadamu. Mzinga, ukiwa katika umbo lisilokuwa la kibinadamu ndio uwanja asilia (A), huku binadamu msichana akiwa uwanja lengwa (B). Sifa za mzinga zinamwezesha mfasiri kuzifikia sifa za binadamu anayerejelewa akilini. Hivyo, ubongo wa mfasiri unapakua sifa zifuatazo kuhusiana na nyanja husika:

Mzinga (Uwanja asilia A)


Ni chombo
Asali tamu huhifadhiwa

Una manufaa

Kijana (Uwanja lengwa B)

Ni binadamu
Huhifadhi burudani kwa
mpenziwe (katika ndoa)
Ana manufaa

Angalia mchoro huu unaowasilisha maelezo yaliyopo hapo juu:



Kielelezo 4.7: Fasiri ya Jazanda ya *Mwatu* (Mzinga)

Kwa mujibu wa ufasiri uliopo hapo juu, jazanda ya mzinga imetumika kuwasilisha itikadi ya tohara, ndoa na mapenzi. Hapa, vijana watahiriwa wanaonywa dhidi ya kujiingiza kwenye mahusiano ya kimapenzi na wasichana wadogowadogo. Hii ni kwa sababu ndoa si ya watoto bali ni ya watu wazima waliokomaa kimwili na kiakili.

viii) Jazanda ya *nyuki mbingi* (Nyuki wengi)

Mwatu nukutha na ndwina uki

Mzinga una *nyuki wengi* lakini hauna asali


Kijana *amekua kimaumbile* lakini hajakomaa kimapenzi

Kwa mujibu wa katiba nchini Kenya (2010), miaka ya utotoni huanzia kuzaliwa hadi umri wa kabla ya miaka kumi na minane. Hata hivyo, Watoto hukua kwa namna tofauti kutegemea maumbile yao. Kuna wale wanaokua polepole huku wengine wakikua harakaharaka. Hivyo, baadhi ya vijana huonekana wakubwa hasa katika umri wa kubaleghe. Ni katika muktadha huu ambapo mwimbaji wa wimbo *Mwatu* (mzinga) ameimba wimbo husika. Hapa, mwimbaji anaeleza hali ambapo mzinga unaonekana kuwa na nyuki wengi ilhali ndani yake hamna asali. Kwa kawaida, ufugaji wa nyuki huhusisha kifaa kinachorejelewa kama mzinga. Kifaa chenyewe hutumika kama hifadhi ya nyuki, ambao ndio huandaa asali ndani ya mzinga. Hivyo, lazima pawepo nyuki kwanza ili asali ipatikane kwenye mzinga. Katika wimbo huu, mwimbaji anatusawiria hali ambapo nyuki wapo, lakini asali haipo. Mhimili wa maarifa ya kimsingi ya nadharia ya JD inatuongoza kufahamu kwamba neno **nyuki wengi** limetumika kijazanda kurejelea **ukuaji wa kimaumbile**. Hapa, ina maana kuwa vijana wanaorejelewa wamekua kimwili lakini bado ni wabichi, yaani wao ni Watoto. Jazanda hii imetumika kupitisha itikadi ya tohara, ndoa na mapenzi. Itikadi zenyewe zinapitishwa kupitia mielekeo kadha. Kwanza, inaaminika kwamba watahiriwa hawafai kujihusisha na matendo ya unajisi bali wanastahili kuwa waadilifu. Hivyo, mtahiriwa yeyote anayejihusisha kimapenzi na mtoto hana budi kukabiliana na mkono wa sheria. Pili, watahiriwa huhitimu kuo au kuolewa baada ya kupashwa tohara. Hata hivyo, ni marufuku kwao kuwao au kuolewa na Watoto walio chini ya miaka 18. Vilevile, inaaminika kwamba ndoa ni ya watu wawili wazima wenye jinsia tofauti na ambao wamekubaliana kuishi kama mume na mke. Hivyo,

kwa yeyote atakayemlazimisha mtu yeyote kimapenzi atakuwa anakiuka sheria. Hivyo, wimbo wenyewe unawaonya vijana dhidi ya unajisi.

Kutokana na maelezo hayo, jazanda ya **nyuki wengi** imetumika kurejelea hali ya **ukuaji wa kimaumbile**. Hivyo, **nyuki wengi** ndio uwanja asilia A, huku **ukuaji wa kimaumbile** ukiwa uwanja lengwa B. Kwa hivyo, akili ya msikilizaji inapakua sifa zifuatazo kuhusiana na nyanja husika:

Nyuki wengi (Uwanja Asilia A)	Ukuaji wa kimaumbile (Uwanja Lengwa B)
Ni wadudu	Ni hali
Ni halisi	Ni dhahiri
Huonekana	Ishara ni dhahiri (k.m; ukuaji wa matiti, sehemu za siri, n.k)
Ni wengi	Una ishara nyingi
Angalia mchoro ufuatao:	



Kielelezo 4.8: Fasiri ya Jazanda ya *Nzuki Mbingi* (Nyuki Wengi)

ix) Jazanda ya *Uki* (asali)

Mwatu nukutha na ndwina uki

Mzinga una nyuki wengi lakini hauna **asali**

Msichana amekua lakini hajakomaa/hawezi kutosheleza kimapenzi

Hapa, mwimbaji anatusawiria hali ambapo mzinga una nyuki lakini hamna **asali**.


Hivyo, muktadha wa uimbaji wa wimbo huu unatuelekeza kufahamu kwamba wimbo wenyewe umewasilishwa kijazanda. Hivyo, neno **uki (asali)** limetumika kijazanda kurejelea hali ya **kutosheleza kimapenzi**. Jazanda hii imeifumbata itikadi ya ndoa na

mapenzi kwamba ni kitu kizuri ila imetengewa watu wazima ambao wamekomaa kiumri na kimaumbile. Hivyo, mapenzi si ya watoto na kwamba yeyote anayejihusisha kingono na watoto anafaa kuchukuliwa hatua za kisheria. Hivyo, akili ya msikilizaji inapakua sifa zifuatazo:

Asali (uwanja asilia A)	Utoshlezaji wa kimapenzi (Uwanja lengwa B)
Ni kitu	Ni tendo
Ni tamu	una raha zake
Ni nadra kupatikana	Ni nadra kupatikana
Hutamanisha wahusika	Hutamanisha wahusika

Katika hali hii, sifa za uwanja asilia A, *asali* zinaiwezesha akili ya msikilizaji kuzitambua sifa za uwanja lengwa B, *utoshlezaji wa kimapenzi*.

Angalia mchoro ufuatao unaowasilisha maelezo haya:



Kielelezo 4.9: Fasiri ya Jazanda ya *Uki* (Asali)

x) Jazanda ya *ngaku* (aina ya mnyama anayewala nyuki)

Kai nzuki syiminwa ni ngaku.

Kumbe nyuki wanaangamizwa na **ngaku**.

Vijana wanaangamizwa na **wabakaji/Wanyanyasaji**.

Jazanda hii inapatikana katika wimbo *Mwatu (Mzinga)*. Hapa, tunachorewa picha ya nyuki wanaoangamizwa na mnyama anayeitwa *ngaku*. Hivyo, badala ya nyuki

kufikia lengo lao la kuandaa asali, wanaangamizwa kabla ya wakati wao. Hapa, maarifa ya kimsingi yanaisaidia akili ya mfasiri kutambua kuwa wimbo wenyewe unazungumzia dhuluma za kijinsia na ubakaji. Hivyo, mwimbaji anapitisha ujumbe kwamba masuala ya ndoa na mapenzi yanafaa kuhusisha watu waliokomaa na wala si watoto. Hivyo, nyuki hapa wanarejelea vijana ambao hawajakomaa. Vijana hawa wanadhulumiwa katika jamii, tendo ambalo linapingwa vikali na ni kinyume cha maadili ya jamii husika. Hivyo, wabakaji/wadhalimu hao ndio wanaorejelewa kama *ngaku* (mnyama anayewala nyuki). Wadhalimu hawa huwahadaa na kuwadhulumu kingono vijana wandogo, wa kike au wa kiume wasije wakazifikia ndoto zao. Hivyo, mwimbaji anawaonya dhidi ya matendo ya aina hiyo kwa maana siku moja mkono wa sheria utawafikia.


Hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu, **ngaku** ni Uwanja asilia (A) huku **wanyanyasaji/wabakaji** ukiwa Uwanja lengwa (B). Upo mchakato ambao kupitia kwake sifa za *ngaku* zinalinganishwa na za wabakaji/wadhalimu. Katika mchakato husika, ubongo wa mfasiri unapakua sifa zifuatazo za Nyanja husika:

Ngaku (Uwanja asilia A)

Ni mnyama
Ni wadhalimu
Hudhulumu nyuki
Ni waovu

Wabakaji/Wanyanyasaji (Uwanja lengwa B)

Ni binadamu
Ni wadhalimu
Hudhulumu binadamu
Ni waovu



Kielelezo 4.10: Fasiri ya Jazanda ya Ngaku (Aina ya mnyama anayewala Nyuki)

Kwa mujibu wa uchanganuzi huu, sio sifa zote za uwanja asilia (A) zinazoambatanishwa na sifa za uwanja lengwa (B). Hivyo, sifa nyinginezo ambazo hazionyeshi ulinganifu wowote kati ya nyanja husika zinaachwa zikiwa fiche.

4.2.2 Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Kazi

i) Jazanda ya *tumikeve twili* (Mikebe miwili Mindogo)

Mwaka umwe tumikeve twili.


Mikebe miwili mindogo kwa mwaka mzima.

Chakula cha msaada hakitoshi.

Kauli iliyopo hapo juu ni ya kijazanda. Hii ni kwa sababu sifa za vifaa mikebe miwili zinalinganishwa na za chakula cha msaada. Jazanda yenyewe inapatikana katika wimbo *Kaveti Kaanu*. Hapa, mwimbaji anapitisha itikadi ya kazi kwamba ni muhimu kujitahidi kazini. Mwimbaji anaeleza kwamba mwanamke mvivu anafaa kuchangamka na kujitahidi kikazi shambani ili aweze kuikimu familia yake. Anaeleza kwamba chakula cha msaada wa serikali hakitoshi kuikimu familia kwa maana huwa kidogo sana. Kwa kawaida hasa wakati wa njaa na kiangazi, serikali hujitolea kutoa chakula cha msaada kwa wanajamii walioathirika. Hivyo, chakula cheneyewe

hugawanywa kwa kupima kwa kutumia mikebe ili kila mwanajamii agawiwe sawa na mwenzake. Hivyo, neno mikebe miwili midogo ni jazanda inayorejelea chakula cha msaada ambacho hakiwezi kutosha ikilinganishwa na kile kinachopatikana mtu anapojituma kazini shambani. Hivyo, mfasiri wa wimbo anapakua sifa zifuatazo kutokana na jazanda husika:

Mikebe Miwili (Uwanja asilia A)	Chakula cha Msaada (Uwanja lengwa B)
Ni kifaa	Ni chakula
Ni midogo	Ni chache
Haitoshi	Hakitoshi
Hupima Chakula	Hupimwa kwa mikebe



Kielelezo 4.11: Fasiri ya Jazanda ya *Tumikeve Twili* (Mikebe Miwili)

ii) Jazanda ya *kathungi* (kiondo), *kamulo* (jembe) na *kavelu* (mbegu)

Osa kathungi, kamulo, kavelu na uyangiia muundani

Chukua *kiondo, jembe, mbegu* na uelekee shambani


Chukua *nyenzo muhimu* za kazini

Kupitia kwenye wimbo *Kaveti Kaanu* (Kamwanamke kazembe), mwimbaji anatusawiria majira ya mvua ambapo anawasilisha ujumbe wake kwa mwanamke mzembe. Anamweleza kwamba mvua imeshanyesha na kwamba mwanamke huyu

hana budi kuchukua vifaa na mbegu zinazohitajika ili aelekee shambani kwenda kupanda. Katika jamii ya Wakamba, wapanzi hasa wanawake huzihifadhi mbegu zao kwenye **kathungi (kiondo)**. Vilevile, wapanzi hao hutumia **kamulo (jembe)** katika kulima na kupalilia **kavelu (mbegu)** husika. Katika muktadha wa kikazi, maneno **kiondo, jembe, mbegu** yametumika kijazanda kurejelea **nyenzo muhimu** za kikazi. Hivyo, kazi inaweza kuwa ya kibiashara, kiofisi, kitaaluma, n.k. Kwa mfano, ikiwa ni kazi ya kibiashara, mtaji na bidhaa za biashara zitahitajika. Vilevile, kwenye sekta ya elimu, mwalimu atahitajika kuchukua vifaa kama vile chaki, kalamu, ratiba ya kazi, n.k na kuelekea shuleni na kisha darasani ambapo ndipo maeneo yake ya kazi. Kwa hivyo, jazanda zenyewe ndizo uwanja asilia A huku **nyenzo muhimu** ikiwa ndio uwanja lengwa B.

Jazanda hii imeifumbata itikadi ya kazi kwamba ni muhimu na kila mwanajamii hana budi kujitahidi. Jazanda yenyewe imetumika katika kukashifu na kukejeli uzembe miongoni mwa wanajamii. Tazama sifa zifuatazo za nyanja mbili zinazohusika:

Kiondo, jembe na mbegu (Uwanja Asilia A)	Nyenzo muhimu (Uwanja Asilia B)
Ni vifaa vya ukulima	Ni vifaa vya kazini
Ni muhimu shambani	Ni muhimu kazini
Zina manufaa	Zina manufaa
Hurahisisha ukulima	Hurahisisha kazi



Kielelezo 4.12: Fasiri ya Jazanda za Kathungi (Kiondo), Kamulo (Jembe) na Kavelu (Mbegu)

iii) Jazanda ya *muundani* (Shambani)

Osa kathungi, kamulo, kavelu na uyang'ia *muundani*

Chukua kiondo, jembe na mbegu na uelekee *shambani*

Chukua nyenzo muhimu za kazi na uende kwenye *maeneo ya kazini*

Jazanda ya *muundani* inajitokeza katika wimbo *Kaveti Kaanu* (Mwanamke **mzembe**). Mwimbaji anamlenga mwanamke mzembe ambapo anamshauri achukue vifaa muhimu kama vile kiondo, jembe na mbegu halafu aende shambani na kujitahidi kazini. Hivyo, neno shambani hapa limetumika kijazanda kuashiria **maeneo ya kazini**. Hivyo, kazi ni za aina mbalimbali. Kupitia jazanda hii, mwimbaji ameifumbata itikadi ya kazi kwamba ni muhimu kwa wanajamii. Vilevile, inadhihirika hapa kwamba wanajamii hawana budi kujitahidi kazini. Hivyo, tabia za uvivu na uzembe ni kinyume na desturi za Wakamba na hivyo zinakashifiwa. Kwa hivyo, akili ya msikilizaji inapakua sifa zifuatazo:


Shambani (Uwanja Asilia A)

Kazi hutekelezwa
Mbegu hupandwa
Mazao huvunwa
Faida kwa mhusika

Maeneo ya Kazi (Uwanja Lengwa B)

Kazi hutekelezwa
Raslimali huwekezwa
Mazao hupatikana
Faida kwa mhusika

Hapa, uwanja asilia A, *shambani* unalinganishwa na uwanja lengwa B *maeneo ya kazini*. Maeneo ya kazini inamaanisha mahali popote ambapo mtu anafanya kazi. Hivyo, kazi ni kazi, bora isikiuke sheria za nchi. Kwa hivyo, kila mwanajamii ni sharti azingatie bidii kazini ndiposa aweze kufaulu.

**Kielelezo 4.13: Fasiri ya Jazanda ya *Muundani* (Shambani)****iv) Jazanda ya *ndeke* (ndege)**

Ve ndeke ikwitwa Manyali ikakua andu ma wia
Kuna **ndege** inaitwa Manyali itabeba watu wenye bidii
Mafanikio yatatokana na bidii kazini


Jazanda hii imejitokeza katika wimbo *Muika wia nukunwe* (Vijana kazi itekelezwe). Hapa, uwanja asilia **Ndege** unalinganishwa na uwanja lengwa **Mafanikio**. Huu ni ulinganishaji wa sifa kati ya uwanja wa chombo cha usafiri wa angani na ule wa matokeo ya juhudi za kibinadamu. Hivyo, katika ufasiri wa kauli hii, akili ya mfasiri hupakua sifa zifuatazo kuhusiana na Nyanja hizo mbili husika:

Ndege (Uwanja asilia A)

Ni chombo
Husafirisha
Toka chini hadi juu
Huhitaji rubani
Juhudi muhimu

Mafanikio (Uwanja lengwa B)

Ni matokeo
Hupandisha
Toka chini hadi juu
Huhitaji mhusika
Juhudi muhimu

**Kielelezo 4.14: Fasiri ya Jazanda ya *Ndeke* (Ndege)**

Jazanda hii imetumika katika kuendeleza itikadi ya kazi katika jamii ya Wakamba.

Hapa, wanajamii wanahimizwa wajitahidi kazini kwa maana juhudi huzaa mafanikio.

v) Jazanda ya *kavuli* (anayetwanga)

Kavuli vula mwee witu.

Kavuli twanga mawele yetu.

Kavuli ni mwenye jitihada kazini.

Kutokana na wimbo *Kavuli Vula Mwee witu*, tunaipata jazanda ya **Kavuli**. Jazanda hii imetumika katika kuendeleza itikadi ya kazi katika jamii ya Wakamba. Hivyo, utafiti huu umetambua kwamba jina *Kavuli* ni la kimajazi linalomaanisha anayetwanga mawele. Neno hili ni jazanda inayorejelea mtu yeyote anayefanya kazi kwa bidii. Hivyo, mhusika Kavuli amepewa jina hilo kwa mujibu wa sifa zake za kutwanga kazi vilivyo na ambapo mwimbaji anayehusika anamhimiza aendelee kufanya hivyo. Kwa

hivyo, mtu anayehitaji mafanikio hana budi kujitahidi katika lolote analolifanya.


Tazama fasiri zifuatazo:

Kavuli (Uwanja Asilia A)

Ni binadamu
Hutwanga mawele
Ana bidii

Mwenye Jitihada (Uwanja Lengwa B)

Ni binadamu
Hutwanga kazi
Ana bidii



Kielelezo 4.15: Fasiri ya Jazanda ya Kavuli (Anayetwanga)

vi) Jazanda ya *ngima* (Ugali)

Ngima yumaa kwi kuthie.

Ugali hupatikana kwa kusiaga mawele

Mafanikio hupatikana baada ya kujitahidi.

Pamoja na hayo, neno *ngima* (ugali) limetumika kama ishara inayorejelea mafanikio ya wanaofanya kazi kwa bidii. Hapa, chakula hiki kinalinganishwa na mafanikio yanayotokana na juhudi kazini. Mwimbaji anawahimiza wanajamii waendeleo kujituma kazini kwa maana mtaka cha mvunguni sharti ainame. Hivyo, mtu anayehitaji mafanikio hana budi kujitahidi katika lolote analolifanya. Jazanda hii inahamisha sifa za ugali na zile za mafanikio. Kwa hivyo, baadhi ya sifa za ugali ambayo ndiyo uwanja asilia (A) zimetumika katika kuzifikia sifa za mafanikio, ambayo ndiyo uwanja lengwa (B). Hivyo, msikilizaji anafahamishwa kwamba


mafanikio mazuri ya kikazi hutokana na juhudi za anayehusika. Kutokana na maelezo hayo, akili ya mfasiri inapakua sifa zifuatazo za nyanja hizi mbili:

Ugali (Uwanja Asilia A)

Aina ya chakula
Hushibisha
Hutokana na bidii kazini

Mafanikio (Uwanja Lengwa B)

Aina ya matokeo
Huridhisha
Hutokana na bidii kazini



Kielelezo 4.16: Fasiri ya Jazanda ya *Ngima* (Ugali)

Katika ufasiri wa maana ya jazanda hizi, sifa za uwanja asilia (A) zenye mfanano na uwanja lengwa (B) ndizo zinazohusishwa katika uhamishaji husika.

4.2.3 Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Kidini

i) Jazanda za *malenge* (Maboga), *NzUU* (Mbaazi) na *Mboso* (Maharagwe)

Syana syokote malenge kivulanio kya nzUU na mboso.

Watoto waokote **maboga**, mchanganyiko wa **mbaazi** na **maharagwe**.

Jamii ipate **mafanikio**.

Wimbo wa *Tuthii kithembeoni* (Twendeni Madhabahuni) unaendeleza itikadi ya kidini. Hapa, wanajamii wanahimizwa wamwabudu Mungu ambaye ndiye chanzo cha aidha mafanikio au matatizo yao. Hivyo, imedhihirika hapa kwamba kumwabudu Mungu kunaweza kuwasababishia mafanikio huku kutomtambua au kutomwabudu kukipelekea matatizo kama vile kiangazi au ukosefu wa mvua. Hivyo, **maboga**,


mbaazi na maharagwe ni aina ya vyakula vinavyopatikana mvua inaponyesha vizuri. Taswira hii ya msimu wa kiangazi na mvua imetumika kijazanda ili kurejelea umuhimu wa kumwabudu Mungu. Kutokana na maelezo hayo, maneno maboga, baazi na maharagwe ndio Uwanja Asilia A unaotuwezesha kutambua **mafanikio** ambayo ndiyo Uwanja Lengwa B. Hapa, sifa za aina hizi za vyakula zinalinganishwa na sifa za mafanikio ambapo tunapata fasiri zifuatazo:

Maboga, mbaazi na maharagwe (U. Asilia A)

Aina ya chakula cha kiasili
Ibada na imani ni muhimu

Mafanikio (Uwanja Lengwa B)

Aina ya matokeo
Ibada na Imani ni muhimu



Kielelezo 4.17: Fasiri ya Jazanda za *malenge* (Maboga), *Nzuu* (Mbaazi) na *Mboso* (Maharagwe)

4.2.4. Jazanda zinazojitokeza kwenye NKK zinazowasilishwa katika Hafla za Ndoa na Arusi

i) Jazanda ya *katanda* (Kitanda)

Nauma kwasa nayu ningwenda katanda ngome.

Nimetoka mbali na sasa nataka kitanda nilale.

Nimetoka mbali na sasa nataka ndoa.

Jazanda ya **Katanda** inajitokeza katika wimbo *Mutanu*. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anatusimulia uchovu alio nao kutokana na safari ndefu ya kumtafuta mpenziwe Mutanu ambaye alikuwa amemwacha. Hapa, hali ya kuanzisha familia inawasilishwa kwa njia ya safari ambapo safari yenyewe huwa ni ndefu, yenye mapito na huhitaji uvumilivu. Hivyo, neno katanda limetumika kama ishara ya ndoa. Hii ni baada ya mwimbaji kumpata mpenzi aliye tayari kufunga pingu za maisha naye. Kupitia kwa jazanda hii, mwimbaji anapitisha itikadi ya ndoa na mapenzi kwamba mtu anapooa au kuolewa anatarajiwa awe na utulivu fulani wa kimaisha. Japo ndoa ina changamoto zake katika kupanda na kushuka, wanandoa huhitajika wawe na utulivu na kuvumiliana namna walivyo. Hii ni sawa na kusema kwamba hakuna ndoa au mapenzi yasiyokuwa na dosari, ila wahusika huhitajika kuelewana na kuungana ili kukamilishana. Hivyo, wanandoa ndio wanaoidhibiti na kuihimili ndoa hiyo husika. Kutokana na maelezo hayo, sifa za **Kitanda** ambao ndio uwanja Asilia A zinalinganishwa na za **ndoa** ambao ndio uwanja lengwa B. Ulinganishaji huu unamwezesha mfasiri kuzipakua sifa zifuatazo kuhusiana na Nyanja hizi:


Kitanda (Uwanja Asilia A)

Ni kifaa
Hulaliwa
Huhimili wahusika
Huwatuliza wahusika

Ndoa (Uwanja Lengwa B)

Ni mahusiano
Hudhibitiwa
Huhimili wahusika
Huwatuliza wahusika

Angalia mchoro ufuatao:



Kielelezo 4.18: Fasiri ya Jazanda ya *Katanda* (Kitanda)

ii) Jazanda ya *ngali* (Gari)

Ni museo sana aendaa na ngali

Ni mzuri sana husafiri kwa **gari**.

Mutanu ni mwaminifu.

Kupitia kwa wimbo Kilyambu, tunapata jazanda ya Gari. Hapa, tunasimuliwa kuhusu kijana Kilyambu ambaye amemchumbia msichana aitwaye Mutanu. Hapa, tunaelezwa kwamba msichana huyu ni mzuri sana kwa maana yeye husafiri kwa **gari** kila anapoenda popote. Hivyo, tabia na mienendo ya msichana huyu imesimuliwa kwa namna ya safari. Taswira hii inatupatia picha halisi ya vijana wanapotembea mtaani. Kwa mfano, kwa wale wasiokuwa na maadili hupata nafasi ya kujihusisha katika mahusiano mabaya kila wanapotembea. Hii ni kwa sababu kila mara wao hupatana na watu waovu walio tayari kuathiri na kuharibu mienendo yao bora. Hivyo, hali ya uaminifu inasawiriwa kupitia kwa neno **gari**, ambapo tunaelezewa kuwa Mutanu husafiri kwalo kila mara.

Hivyo, msichana huyu hujapata nafasi ya kujinajisi kwa njia yoyote. Kupitia kwa jazanda hii, mwimbaji anapitisha itikadi ya ndoa na mapenzi kwamba vijana

wanastahili kuvumilia hadi pale watakapolewa ili wajihusishe na masuala ya tendo la ndoa. Hivyo, kulingana na utamaduni wa jamii ya Wakamba, ni marufuku kwa vijana hasa wasichana kujihusisha na mapenzi au tendo la ndoa kabla ya ndoa. Kutokana na maelezo hayo, ubikira ni suala lililotiliwa na linatiliwa maanani sana kwenye jamii hiyo. Kwa hivyo, neno **gari** ambalo ni chombo cha usafiri ndio Uwanja Asilia A huku neno **uaminifu** likiwa Uwanja lengwa B. Kutokana na maelezo hayo, ubongo wa mfasiri unapakua sifa zifuatazo kuhusiana na **gari** na pia **uaminifu**:

Gari (Uwanja asilia A)

Ni chombo cha usafiri

Hutunza (abiria)


Usafi (kimwili)

Uaminifu (Uwanja lengwa B)

Ni aina ya tabia

Hutunza (ndoa)

Usafi (kitabia)



Kielelezo 4.19: Fasiri ya Jazanda ya Ngali (Gari)

iii) Jazanda ya *sikala* (Sigara)

Ngwititye sikala

Nimekuomba **sigara**

Mwimbaji anaomba *tendo la ndoa*

Jazanda hii inajitokeza katika wimbo *Sikala*. Jazanda yenyewe imetumika katika kuendeleza itikadi ya ndoa na mapenzi. Kupitia kwenye wimbo huu, tunaelezwa


namna ambavyo mwimbaji amemwomba msichana Tavitha sigara bila mafanikio. Hivyo, neno sigara limetumika kijazanda kurejelea tendo la ndoa. Hapa, maarifa ya kimsingi yanatuwezesha kutambua kwamba kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wakamba, msichana hafai kujihusisha na tendo la ndoa kabla ya kuolewa. Hivyo, mwimbaji anajaribu kuwasilisha ujumbe kwamba tendo la ndoa ni la wale walio katika ndoa pekee. Hii ndiyo sababu inayomfanya mhusika wa kike Tavitha kumnyima mwenzake wa kiume uhusiano wa aina hiyo. Vijana wanahimizwa kusalia mabikira hadi pale watakapooa au kuolewa. Jazanda hii inazilinganisha sifa za sigara na zile za tendo la ndoa. Hapa, sigara ambayo ni miongoni mwa madawa yanayovutwa ndio Uwanja Asilia (A) huku tukio la tendo la ndoa likiwa Uwanja Lengwa (B). Hivyo, sifa za aina hii ya dawa inayovutwa zikitupatia sifa za tendo husika. Ubongo wa mfasiri basi unapakua sifa zifuatazo kuhusiana na sigara na pia tendo la ndoa:

Sigara (Uwanja Asilia)

Ni dawa inayovutwa
Huburudisha kihisia
Hutuliza kiu fulani

Tendo la Ndoa (Uwanja Lengwa)

Ni tendo linalofanywa
Huburudisha kihisia
Hutuliza kiu fulani



Kielelezo 4.20: Fasiri ya Jazanda ya *Sikala* (Sigara)

iv) Jazanda ya *ngate* (Mikate) na Kyavati (Chapati)

Niuiwe ngate vamwe na kyavati.

Umepikiwa **mikate** pamoja na **chapati**.

Umekaribishwa kwa mikono miwili.

Kwa kawaida, jamii ya Wakamba huichukulia arusi na ndoa kuwa shughuli muhimu. Hivyo, kwenye hafla za aina hii, wanandoa husika huandaliwa mapochopocho kama ishara ya makaribisho katika familia ya bwana arusi. Hivyo, sherehe huandaliwa ambapo wanajamii wote hutarajiwa kushiriki katika kushangilia na kuwakaribisha wanandoa katika hatua hii muhimu ya kuanza ndoa katika maisha yao. Kupitia wimbo *Uka usuvie utwae (Njoo uitunze ndoa)*, mwimbaji anamweleza mke mtarajiwa aje aitunze ndoa yake. Hivyo, mwimbaji anawasilisha itikadi ya ndoa kwamba ni muhimu wanandoa wawajibike katika kuitunza ndoa yao. Kwa hivyo, neno **mikate** limetumika kijazanda kurejelea **makaribisho** makubwa. Mwimbaji anamweleza bibi arusi kuwa ameandaliwa mikate na chapatti na hivyo hana budi kuitunza ndoa. Hivyo, anajaribu kuwasilisha ujumbe kwamba binti huyu amekaribishwa katika ile jamii mpya na basi ni sharti awajibike katika kuitunza ndoa yake. Kutokana na maelezo hayo, akili ya mfasiri inapakua sifa zifuatazo kuhusu Nyanja hizi mbili:

Mikate na Chapati (Uwanja Asilia A)

Ni aina ya chakula

Ni tamu


Huandaliwa

Makaribisho (Uwanja Lengwa B)

Ni hali ya kumpokea mtu

Hufurahisha

Huandaliwa



Kielelezo 4.21: Fasiri ya Jazanda ya *Ngate* (Mikate)

v) Jazanda ya *uki wa ngilu* (Asali mwitu)

Umantha uki wa ngilu.

Kutafuta **asali mwitu**.

Kuwa na **uwajibikaji**

Kupitia kwenye wimbo *Mumbe*, mwimbaji anasimulia namna alivyompata mpenzi aitwaye Mumbe. Hata hivyo, mpenziwe alimpatia kibarua kigumu cha kutafuta asali mwitu ambapo alienda maeneo mbalimbali akifanya hivyo. Kwa kawaida, asali mwitu huandaliwa na wadudu wadogo wadogo na ambao hawapatikani kwa urahisi msituni. Hivyo, ni nadra sana kuipata asali mwitu. Kwa mtu anayehitaji kuipata, hana budi kuwa mvumilivu na aliye tayari kupitia na kushinda changamoto mbalimbali. Hivyo, mwimbaji anatumia neno **asali mwitu** kama jazanda ili kuwasilisha itikadi ya ndoa kwamba si rahisi. Anaeleza kwamba kama ilivyo vigumu kuipata asali mwitu, ndivyo ilivyo katika kuitunza ndoa. Kwa hivyo, mwimbaji anawajulisha wanandoa kwamba hawana budi kuwajibika na kuzilipia gharama ndoa zao. Gharama zenyewe ni pamoja na kuwa mwenye uvumilivu na uwajibikaji. Kwa hivyo, japo ndoa si rahisi, inahitaji uvumilivu, uwajibikaji na maelewano miongoni mwa wanaohusika. Kwa mujibu wa


maelezo hayo, akili ya mfasiri inapakua sifa zifuatazo kuhusu uwanja asilia na uwanja lengwa:

Asali mwitu (Uwanja Asilia A)

Ni aina ya chakula
Ni nadra sana kupatikana
Uvumilivu muhimu

Uwajibikaji (Uwanja Lengwa B)

Ni sifa ya kitabia
Ni nadra sana kuwa nayo
Uvumilivu muhimu



Kielelezo 4.22: Fasiri ya Jazanda ya *Uki wa Ngilu* (Asali Mwitu)

vi) Jazanda ya *mutunda* (Mtunda)

Mbande mutunda, ni waki? Wai wa mavatano.

Nipande **mtunda**, ni wa nini? Ulikuwa wa mapatano.

Nizingatie mapatano/makubaliano.

Jazanda hii inadhahirika katika wimbo *Nzambi wa Mutunga*. Jazanda yenyewe imetumika kuwasilisha itikadi ya ndoa. Inadhahirika kwamba ndoa huwa imejaa changamoto hapa na pale. Hata hivyo, marekebisho na mapatano ni muhimu katika kusuluhisha changamoto zinazohusika. Hapa, tunaelezwa kuhusu mhusika wa kike Nzambi ambaye walikosana na mumewe na kisha akarudi kwao yaani kwa wazazi wake. Hivyo, mwimbaji anaimba katika muktadha wa mazungumzo ili kuleta

mapatano kati ya wanandoa hao wawili. Kulingana na wimbo huo, wana kikao wamekubaliana kuwa Nzambi arudi kwa mumewe. Hivyo, tunaelezwa kwamba imekubalika kwamba wazee wapande mtunda ambao ni ishara ya makubaliano au mapatano yaliyoafikiwa. Hivyo, neno **mtunda** limetumika kama jazanda inayorejelea **mapatano** hayo.


Tazama ufasiri ufuatao:

Mtunda (Uwanja Asilia A)

Ni mmea
Huzaa matunda
Ni ishara ya matumaini

Mapatano (Uwanja Lengwa)

Ni makubaliano
Huleta mwanzo mpya
Ni ishara ya matumaini



Kielelezo 4.23: Fasiri ya Jazanda ya *Mtunda* (Mtunda)

4.2.5. Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Kuzaliwa kwa Watoto

i) Jazanda ya *kaindo* (Kakitu)

*Kuathima mwana ii na **kaindo** ngyuka.
Kumbariki mtoto na **kakitu** nikija.
Kumletea mtoto **zawadi**.*

Jazanda ya Kaindo inajitokeza katika wimbo *Kyathi no Vala* (Miadi ni ileile). Wimbo wenyewe unawasilisha itikadi ya uzazi na malezi. Katika wimbo huu, mwimbaji anaanza kwa kubisha hodi huku akielezea kwamba alikuwa ameahidi kuwa angekuja kumbariki mtoto na kakitu. Kwenye jamii ya Wakamba, kuzaliwa kwa mtoto huwa ni ishara ya kuendelea kwa jamii hiyo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mujibu wa utamaduni wa jamii hii, mtoto ni mali ya jamii. Hivyo, mtoto anapozaliwa jamii husherehekea na kumzawadi mama pamoja na mtoto aliyezaliwa. Hali hii huwa ishara ya kuwajibika kijamii kuhusiana na malezi ya mtoto anayehusika. Ni katika muktadha huu ambapo neno **kakitu** linafasiriwa kuwa **zawadi**. Kutokana na maelezo hayo, akili ya mfasiri inapakua sifa hizi kuhusiana na nyanja mbili zinazohusika:

Kakitu (Uwanja Asilia A)

Ni kitu

Si bayana


Hutumika kwa njia mbalimbali

Zawadi (Uwanja Lengwa B)

Ni kitu

Si bayana

Huzawadiwa kwa mhusika



Kielelezo 4.24: Fasiri ya Jazanda ya *Kaindo* (Kijitu)

ii) Jazanda ya *mukwa* (Kamba pana) na *ikanda* (kamba)

Kwata mukwa ulumitye ndukandekye nimandane.

Shika **kamba pana** vizuri usiniachilie nianguke.

*Kuwa na **ustahimilivu**.*

Mukwa (Kamba pana) na *Ikanda* (kamba) ni jazanda zinazojitokeza katika wimbo *Inyaa mwana na Ithea mwana* (Mama na baba mtoto). Mwimbaji anaanza kwa kubisha hodi kisha anasimulia mazingira ya kuzaliwa kwa mtoto. Hivyo, anaeleza namna ambavyo wakunga humsaidia mama anapojifungua. Kwa kawaida, kamba pana au kamba ya kawaida hutumika katika shughuli hiyo ambapo kuna namna fulani kamba hiyo hushikiliwa na mkunga pamoja na mama anayejifungua. Kamba husika huhitaji uvumilivu mkubwa kwa sababu si rahisi kuishikilia. Hapa, mwimbaji anaeleza hatari iliyopo katika shughuli ya kujifungua. Hivyo, mwimbaji anaeleza kuwa Kamba husika isiposhikwa kwa uangalifu huenda mkunga, mama au mtoto anayezaliwa akaanguka. Hivyo, jazanda ya **mukwa** imetumika katika kuendeleza itikadi ya uzazi kwamba mzazi na hasa mama huyahatarisha maisha yake ili mtoto apatikane. Hivyo, mzazi hana budi kuwa na **ustahimilivu** na uangalifu mkubwa katika uzazi na malezi ya watoto katika jamii. Hivyo, iwapo ameweza kustahimili uchungu huo wa kujifungua, hana budi kujitahidi katika malezi pia. Tazama fasiri zifuatazo:

Kamba pana (Uwanja Asilia A)

Hutumika na mama na mkunga

Huhitaji ukakamavu


Si rahisi kulishikilia

Ustahimilivu (Uwanja Lengwa B)

Huhitajika wakati wa kujifungua

Huhitaji ukakamavu

Si rahisi kuudumisha



Kielelezo 4.25: Fasiri ya Jazanda za *Mukwa* (Kamba Pana) na *Ikanda* (Kamba)

4.2.6 Jazanda zinazojitokeza kwenye NKK zinazowasilishwa katika Hafla za kisiasa

i) Jazanda ya *nzele ikithambwa* (Kata inayooshwa)

Nzambi akithambya nzele ii ya kuthamba.

Nzambi akiosha **kata** ya kuoga.

Kiongozi mpya akiuondoa **ufisadi** uliopo.

Jazanda ya *nzele* (kata) imejitokeza katika wimbo *Nzambi akithambya Nzele*. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anatuchorea picha ya mhusika Nzambi akiosha kata. Katika hali ya kuiosha kata hiyo, tunaeleza kuhusu watu wanaonung'unika huku kando kwamba anaharibu wakati, maji hayatoshi, na mambo mengine kama hayo. Hivyo, mwimbaji anawauliza kwa nini wanung'unike? Anataka wampe mhusika nafasi ili aifanye na kuikamilisha kazi yake vizuri. Kutokana na maelezo hayo, mfasiri anatambua kwamba taswira ya uoshaji wa kata inayosawiriwa hapa inarejelea hali ya kuuondoa ufisadi uliotekelwa na viongozi tangulizi. Hivyo, mwimbaji anawarai wasikilizaji wampe muda kiongozi mpya na kisha kazi yake itaonekana kwa mujibu wa wakati. Mwimbaji anaitaka hadhira iache kulalamika kwamba kiongozi mpya hajafanya kazi wanayoitarajia. Hivyo, wimbo wenyewe ni wa kisiasa na unapitisha


itikadi ya kisiasa. Kutokana na maelezo hayo, wimbo wenyewe umewasilishwa kijazanda ambapo unazungumzia ufisadi uliokuwa unatekelezwa na viongozi tawala tangulizi. Hivyo, maarifa haya ya kimsingi yanaisaidia akili ya mfasiri kutambua uwanja asilia na uwanja lengwa katika kifungu hiki cha kijazanda. Kwa hivyo, tukio la kuosha kata ndilo uwanja asilia (A) huku tukio la kuondoa ufisadi likiwa uwanja lengwa (B). Hivyo, upo mchakato ambao kupitia kwake, sifa za uoshaji wa kata zinalinganishwa na uondoaji wa ufisadi. Katika mchakato husika, ubongo wa mfasiri unapakua sifa zifuatazo za Nyanja husika:

Uoshwaji wa Kata (Uwanja Asilia)

Ni kuondoa uchafu
Si kazi rahisi
Huhitaji ustahimilivu
Tazama mchoro ufuatao:

Uondoaji wa Ufisadi (Uwanja Lengwa)

Ni kuondoa uozo wa kijamii
Si kazi rahisi
Huhitaji ustahimilivu



Kielelezo 4.26: Fasiri ya Jazanda ya *Kuthambya Nzele* (Uoshwaji wa Kata)

ii)Jazanda ya *nzele yi kiko* (Kata chafu)

Kuthambya **nzele**

Kuosha **kata**

Kuna **ufisadi**

Kauli hii inajitokeza kwenye wimbo *Nzambi akithambya nzele* (Nzambi akiosha kata). Hapa, tunaelezewa kwamba Nzambi anaosha kata. Hivyo, maarifa ya kimsingi yanatuwezesha kufahamu kwamba kata inayooshwa ni chafu. Hivyo, kata inayorejelewa hapa ni chafu na bila shaka ipo haja ya kuiosha kama anavyofanya mhusika Nzambi. Kwa hivyo, kata chafu imetumika kijazanda kurejelea ufisadi unaoendelezwa na viongozi tawala. Kwa mujibu wa uchanganuzi huu, kata chafu ndio uwanja asilia A huku ufisadi ukiwa uwanja lengwa B. Sifa zifuatazo zinadhihirika kuhusiana na Nyanja hizi:

Kata chafu (Uwanja asilia A)

Ni kifaa cha jikoni

Hukwaruzwa kinapooshwa

Haipendezi


Ufisadi (Uwanja lengwa B)

Ni uovu

Kuna mkwaruzano unapoondolewa

Haupendezi

Angalia mchoro huu:



Kielelezo 4.27: Fasiri ya Jazanda ya *Nzele yi Kiko* (Kata Chafu)

iii) Jazanda ya *simba ii syi ngunyu* (Simba wenye Makucha)

Simba ii syi ngunyu nitwasyelile.

Simba wenye kucha tushazikatakata.

Tushaitambua mienendo ya wanasiasa maarufu na wafisadi.

Jazanda ya **simba wenye makucha** inatokea katika wimbo *Munuve*. Mwimbaji anaanza kwa kumweleza mhusika Munuve kuwa asiwe na hofu bali aingie kwenye kinyang'anyiro cha kupigania ubunge. Anamweleza kwamba kwa wale **simba wenye makucha**, asiwaogope kwani wameshazikatakata kucha hizo. Kwa kawaida simba wenye makucha huwa hatari sana. Wao huweza kuwashambulia na kuwanyanyasa wanajamii. Simba wenye makucha ni neno lililotumika hapa kurejelea viongozi au wanajamii wabaya, fisadi na wanaowanyanyasa wanajamii. Mwimbaji anawasilisha ujumbe kwamba wamekwisha tambua mbinu zao mbaya wanazozitumia ili kuingia uongozini. Hivyo, mbinu mwafaka ya kuwaondoa mamlakani ni kukosa kuwapigia kura. Hivyo, kukosa kuwapigia kura kunalinganishwa na kuwakata kata makucha yao. Hivyo, neno simba wenye makucha hapa limetumika kijazanda kuashiria wanasiasa wafisadi. Anaposema kwamba wameshayakatakata makucha yao, anarejelea hali ya kuutambua uongo na uovu wao pamoja nakutokuwa tayari kuwapigia kura tena wanasiasa hao. Kutokana na maelezo hayo, jazanda hii imetumika katika kuwasilisha itikadi ya kisiasa kwamba uongo na ulaghai wa wanasiasa una mwisho, yaani njia ya mwongo ni fupi. Hivi ni sawa na kusema kwamba wanajamii wanafaa kujiepusha na kuwapigia kura wanasiasa wabaya, fisadi na walaghai kura. Tazama fasiri zifuatazo kwa mujibu wa uwanja Asilia na Uwanja Lengwa:

Simba wenye kucha (Uwanja Asilia A)

Ni hatari

Hushambulia viumbe


Ni wanyanyasaji

Wanasiasa Wafisadi (Uwanja Lengwa B)

Ni hatari

Hushambulia mali ya uma

Ni wanyanyasaji



Kielelezo 4.28: Fasiri ya Jazanda ya *Simba ii syi Ngunyu* (Simba wenye Makucha)

iv) Jazanda ya *nzou* (Ndovu)

Usumbi aume ni nzou.

Jamani urais ni ndovu.

Cheo cha Urais hunyemelewa kwa hekima.


Jazanda hii inatokana na wimbo *Usumbi ni Nzou* (Urais ni ndovu). Jazanda yenyewe imetumika katika kuendeleza itikadi ya kisiasa. Hapa, mwimbaji anaeleza namna utafutaji wa cheo cha urais ulivyo mgumu. Hivyo, mwimbaji anatusawiria muktadha wa uwindaji ambapo uwindaji wa ndovu unalinganishwa na ule wa urais. Mwimbaji anawahimiza wanasiasa kuwa makini na wenye hekima katika shughuli zao za kisiasa. Hivyo, jazanda hii inahamisha sifa za uwindaji wa ndovu hadi kwa utafutaji wa cheo cha urais. Kwa hivyo, baadhi ya sifa fulani za ndovu ambaye ndiye uwanja asilia A, zinatumika katika kupakua sifa za urais, ambao ndio uwanja lengwa B. Hivyo, akili ya mfasiri inapakua sifa zifuatazo kuhusiana na nyanja hizi mbili:

Uwindaji wa Ndovu (Uwanja Asilia A)

Ni mnyama anayehusika
Hunyemelewa kimakini
Hekima ni muhimu
Si rahisi

Utafutaji wa Urais (Uwanja Lengwa B)

Ni cheo kinachohusika
Hunyemelewa kimakini
Hekima ni muhimu
Si rahisi



Kielelezo 4.29: Fasiri ya Jazanda ya Nzou (Ndovu)

v)Jazanda ya ng'ombe sya mutavo (Ng'ombe wa wizi)

Ng'ombe sya mutavo syendaa na ungi

Ng'ombe wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia

Mali inayomilikiwa kupitia kwa ufisadi au wizi hutoroshwa kwa wizi pia

Jazanda ya **Ng'ombe sya mutavo (Ng'ombe wa Wizi)** inajitokeza katika nyimbo mbili ambazo ni **Tingilingili (Tingilingili)** na **Muvisi Ungi (Kijana Mwingine)**. Kwenye nyimbo hizi zote, tunaelezwa kwamba ng'ombe wanaopatikana kutokana na wizi hupotea vivyo hivyo. Hivyo, hawawafaidi wezi wanaohusika kwa maana wezi wengine huja kuwaiba. Mhimili wa tatu wa nadharia ya Jazanda Dhanifu unasisitiza uhamishaji wa maana kwa mujibu wa maarifa ya kimsingi ya kila siku kuhusiana na mazingira yanayohusika. Katika muktadha wa kihistoria ya jamii ya Wakamba, palikuwepo mashambulizi ya mara kwa mara kati ya jamii mbali mbali zinazopatikana mipakani.


Katika mashambulizi hayo, jamii iliyoshambuliwa ilinyang'anywa mali kama vile ng'ombe, mbuzi na vitu vinginevyo. Mara kwa mara, ilitokea kwamba jamii iliyonyang'anywa pia ilijitahidi kulipiza kisasi kwa kukujia mali hiyo hiyo pamoja na mali nyingine iliyomilikiwa na wahusika. Hivyo, ilibainika kwamba ng'ombe waliomilikiwa kwa njia hii ya wizi hawakuwafaidi wanajamii husika kwa maana

waliibiwa na kuwafaidi watu wengine kwengineko. Kwa hivyo, uwanja asilia (A) hapa ni *ng'ombe wa wizi*, huku uwanja lengwa (B) ukiwa *mali ya wizi au ufisadi*. Kutokana na maarifa haya ya kimsingi kwenye akili ya mfasiri, msikilizaji ataifasiri jazanda yenyewe kwa kutambua sifa zifuatazo:

Ng'ombe sya Mutavo (Uwanja asilia A) Mali ya Wizi/ufisadi (Uwanja lengwa B)

Ni wanyama	Huhusisha wanyama na vitu vinginevyo pia
Hupatikana kwa wizi/ufisadi	Hupatikana kwa wizi/ufisadi
Hupotea kwa njia hiyo ya wizi tu	Hupotea kwa njia hiyo ya wizi tu
Haimnufaishi mhusika	Haimnufaishi mhusika

Angalia mchoro ufuatao unaotoa muhtasari wa maelezo hayo:



Kielelezo 4.30: Fasiri ya Jazanda ya Ng'ombe sya Mutavo (Ng'ombe wa Wizi)

vi) Jazanda ya kaletiu (redio)

Ninye (Mwini) kaletiu

Mimi (mwimbaji) ndiye karedio

Mwimbaji ni mpashanaji wa habari/ujumbe


Jazanda hii inalinganisha sifa za chombo cha habari na binadamu. Redio, ikiwa katika umbo lisilokuwa la kibinadamu ndio uwanja asilia (A), huku binadamu Mwimbaji

akiwa uwanja lengwa (B). Sifa za aina ya chombo cha habari zinamwezesha mfasiri kuzifikia sifa za binadamu anayerejelewa akilini. Hivyo, ubongo wa mfasiri unapakua sifa zifuatazo kuhusiana na nyanja husika:

Redio (Uwanja asilia A)
 Ni chombo cha habari
 Hutumika kwa utangazaji
 Hupashana habari/ujumbe
 Ni muhimu katika jamii

Mwimbaji (Uwanja lengwa B)
 Ni binadamu
 Ni mwimbaji
 Hupashana habari/ujumbe
 Ni muhimu katika jamii

Angalia mchoro huu:



Kielelezo 4.31: Fasiri ya Jazanda ya *Kaletio* (Redio)

4.2.7 Jazanda zinazojitokeza kwenye NKK zinazowasilishwa katika Hafla za Mazishi

i) Jazanda ya *kivila* (Kiti)

Keka kivila mundu kusakuuwa

Kando na **kiti** mtu kuchaguliwa.

Kando na **cheo** Kalembe alikuwa mwenye utu.

Jazanda ya **kiti** imejitokeza katika wimbo NA. 18. *Mathiko Kyunduani* (Mazishi Kyunduani). Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anasimulia kuhusu mwenzake


Kalembe Ndile. Anaeleza kwamba mwenzake alikuwa mtu wa watu na mwenye umaarufu wake. Hivyo, mwimbaji anamsifu mwenzake kupitia wimbo huu wa mazishi. Inadhihirika hapa kwamba neno kiti limetumika kijazanda kumaanisha **cheo**. Hivyo, sifa za kiti ambacho ndicho Uwanja Asilia A, zinatumika katika kufafanua sifa za Uwanja Lengwa B, cheo. Tazama sifa zinazopakuliwa na ubongo wa mfasiri kuhusiana na Nyanja hizi mbili:

Kiti (Uwanja Asilia A)

Ni kifaa
Hukaliwa
Huhimili mhusika

Cheo (Uwanja Lengwa B)

Ni uongozi
Hudhibitiwa
Huhimili mhusika



Kielelezo 4.32: Fasiri ya Jazanda ya Kivila(Kiti)

ii) Jazanda ya *Musyimi ute tei* (mwindajii asiyekuwa na huruma)

Kikw'u ni musyimi ute tei

Kifo ni mwindaji asiyekuwa na huruma

Kifo husababisha ukiwa na utengano kwa waliofiwa

Katika wimbo NA. 19. mwimbaji anakilinganisha kifo na mwindaji asiyekuwa na huruma. Katika muktadha wa jamii ya Wakamba, uwindaji wa porini hufanywa na

wawindaji waliojihami kwa silaha kama vile uta na mishale. Kwa kawaida, wawindaji hutafuta windo la mnyama aliye na afya na mnono. Anapojitokeza, mwindaji humfuma mshale mnyama huyo bila huruma, bora atimize lengo lake la kupata nyama. Hali hii basi inalinganishwa na kifo kinachowapokonya watu wpendwa wao bila huruma. Wafiwa huachwa katika hali ya maumivu, ukiwa na utengano kati yao na aliyewaacha. Hivyo, jazanda hii imetumika katika kuiendeleza itikadi inayohusiana na mauti. Ujumbe unaopitishwa hapa ni kwamba mauti husababisha uchungu, ukiwa na utengano kwa waliofiwa. Wanajamii hunyang'anywa mpendwa wao kwa lazima ambapo huwa hawana uwezo wa kulizuia jambo hilo. Kwa hivyo, akili ya mtafiti inazipakua sifa zifuatazo kuhusiana na jazanda husika:

Mwindaji asiye na huruma (Uwanja Asilia A)


Ni binadamu
Ni katili
Hana huruma
Huwalenga wanyama
Huleta utengano
Huleta ukiwa

Kifo (Uwanja Lengwa B)

Ni tukio
Ni katili
Hakina huruma
Huwalenga wanyama na watu
Huleta utengano
Huleta ukiwa

Hapa, sifa zinazohusiana katika nyanja hizi mbili ndizo uhamishwa kutoka uwanja Asilia A hadi katika Uwanja Lengwa B.

Tazama kielelezo kifuatacho:



Kielelezo 4.33: Fasiri ya Jazanda ya *Musyimi ute tei* (Mwindaji asiye na huruma)

iii) **Jazanda ya *Muvutani ute tei* (mnyang'anyi asiyekuwa na huruma)**

Kikw'u ni muvutani ute tei

Kifo ni mnyang'anyi asiyekuwa na huruma

Kifo husababisha ukiwa na utengano kwa waliofiwa

Jazanda ya *Muvutani ute tei* (mnyang'anyi asiyekuwa na huruma) inajitokeza katika wimbo NA. 19. Katika kauli iliyopo hapo juu, kifo kinalinganishwa na mnyang'anyi asiyekuwa na huruma. Katika hali ya kawaida, wanyang'anyi huwapokonya watu vitu vyao kwa lazima na bila matarajio. Wakati wa unyang'anyi, mwizi hapigi ripoti kuwa atakuja kukunyang'anya. Pia, baada na hata wakati wa kunyang'anywa, mwathiriwa huachwa katika hali ya uchungu na hata upweke. Katika muktadha huu, kifo kinalinganishwa na mnyang'anyi. Hivyo, akili ya mfasiri itapakua sifa zifuatazo kuhusiana na dhana hizi mbili:

Mnyang'anyi asiye na huruma (Uwanja Asilia A) Kifo (Uwanja Lengwa B)

Ni binadamu

Hana huruma

Hunyang'anya

Huleta maumivu


Ni tukio

Hakina huruma

Hunyang'anya

Huleta maumivu

Tazama kielelezo hiki:



Kielelezo 4.34: Fasiri ya Jazanda ya *Muvutani ute tei* (mnyang'anyi asiyye na huruma)

4.2.8 Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Michezo ya Watoto

i) Jazanda ya *Ng'ombe sya utuku* (Ng'ombe wa usiku)

Jazanda ya *Ng'ombe sya utuku* (Ng'ombe wa usiku) inajitokeza katika wimbo NA.

38. *Tingili Tingili*. Kupitia wimbo husika, mwimbaji anaeleza kuhusu ng'ombe wa babake wanaoibiwa nyakati za usiku. Anaeleza kwamba Ng'ombe hao huwa wanaibiwa na Wamaasai ili waweze kunufaika kwa kupata maziwa. Hata hivyo, anaeleza kwamba Ng'ombe wa aina hiyo hupotea vivyohivyo. Yaani, vitu vya wizi hupotea kwa njia hiyo hiyo ya wizi. Hivi ni kumaanisha kwamba mali ya wizi haifai.

Akili ya mfasiri inapakua sifa zifuatazo:

Ng'ombe wa usiku (Uwanja Asilia A)

Ni wanyama

Huibiwa

Hanufaishi

Hawafai

Angalia kielelezo kifuatacho:


Mali ya Wizi (Uwanja Lengwa B)

Ni vitu na wanyama

Huibiwa

Hainufaishi

Haifai

**Kielelezo 4.36: Fasiri ya Jazanda ya Ng'ombe sya utuku (Ng'ombe wa usiku)****4.2.9 Jazanda kwenye NKK katika Hafla za Vita****i) Jazanda ya *Malenge matemangiwe* (Maboga yaliyokatwakatwa)**

Maarifa ya kimsingi yanaturejesha kwenye muktadha wa kihistoria katika jamii ya Wakamba. Hapo kale, jamii ya Wakamba ilishiriki kwenye vita vya kuviziana na wizi wa mifugo kati yao na jamii jirani kama Wamaasai na Wagikuyu. Kwenye mashambulizi yao, walisababisha uharibifu kama vile wa mimea mashambani. Ni katika muktadha huu ambapo wimbo huu umeimbwa. Mwimbaji anamweleza Ngulu wa Ngao ujumbe wake. Ngulu wa Ngao ni mmoja wa wapigananji wa jamii ya Wakamba. Hivyo, anaelezwa kwamba watalipia maboga ya wenyewe waliyoyakatakata. Hivyo, neno maboga limetumika kurejelea uharibifu unaotokana na


vita. Mwimbaji anatumia neno hilo kijazanda kuwasilisha ujumbe kwamba vita havifai na wala havimnufaishi yeyote. Hii ni kwa sababu wapiganaji husika hawakunufaishwa na maboga husika, bali nia yao ilikuwa kusababisha hasara tu kwa maadui zao. Maarifa ya kimsingi yanamsaidia mfasiri katika kupakua sifa zifuatazo:

Maboga yaliyokatwakatwa (Uwanja Asilia A)

Ni mmea
Vita vimehusika
Uharibifu upo
Ni hasara
Hayafai
Tazama kielelezo hiki:

Uharibifu (Uwanja Lengwa B)

Ni matokeo
Vita vimehusika
Uharibifu upo
Ni hasara
Haufai



Kielelezo 4.37: Fasiri ya Jazanda ya Malenge matemangiwe (Maboga yaliyokatwakatwa)

4.3 Hitimisho

Sura ya nne imepambanua hafla mbalimbali za kijamii ambamo NZK huwasilishwa. Imedhihirika kuwa hafla hizi zinaweza kuwa rasmi au zisizo rasmi kutegemea iwapo zimeratibiwa na jamii zima ya Wakamba au watu binfasi. Hafla hizi huweza kuwa rasmi au zisizo rasmi. Hafla rasmi ni zile ambazo uwasilishaji wa nyimbo za kiasili za

Kikamba huwa umepangwa, kuagizwa na wakati mwingine kuratibiwa. Mfano ni sherehe za ndoa, sherehe za tohara, mikutano ya kisiasa pamoja na ile ya kidini. Kwa upande mwingine, hafla zisizo rasmi ni zile ambazo uwasilishaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba haujapangwa au kuratibiwa. Mfano ni kama vile wakati mama anaimba nyimbo za kiasili za Kikamba huku akiendelea kulima shambani au akisaga mtama.

Aidha, jazanda mbalimbali zinazotumika katika NZK zimechanganuliwa kwa msingi wa Nadharia ya Jazanda Dhanifu. Ni bayana kuwa ufasiri wa maana ya jazanda kwenye NZK hutegemea muktadha ambamo nyimbo hizo zinawasilishwa.

Sura inayofuata inahakiki itikadi zinazofumbatwa na jazanda ambazo zimetumika katika nyimbo za kiasili za Kikamba.

SURA YA TANO

UHAKIKI WA ITIKADI ZILIZOFUMBATWA KIJAZANDA KWENYE

NYIMBO ZA KIASILI ZA KIKAMBA

5.0 Utangulizi

Sura hii ya tano inalenga kutimiza lengo la tatu la uhakiki wa itikadi mbalimbali zilizofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Uchunguzi huu wa itikadi umeongozwa na nadharia ya Itikadi kwa mujibu wa Van Djik (1998). Van Djik anaifasili itikadi kuwa maumbo ya kimsingi ya utambuzi wa kijamii. Maumbo yenyewe huundwa kwa maadili teule ya kijamii na kitamaduni. Hivyo, maadili yenyewe hupangwa kwa muundo wa kiitikadi unaowakilisha ufafanuzi wa kikundi fulani. Kwa hivyo, mtafiti wa fasihi hana budi kuchunguza uamilifu wa kiitikadi katika utanzu wa fasihi unaohusika.

5.1 Itikadi Zilizofumbatwa Kijazanda katika Nyimbo za Kiasili za Kikamba

Mohamed (1995), anaeleza kwamba itikadi ya mtunzi hutegemea mambo kama vile alizaliwa wapi, alikulia katika mazingira ya aina gani, ana imani ipi ya kidini na nafasi ya kiuchumi kati ya mengineyo. Kwa kuwa mwanadamu ndiye huiumba na kuiwasilisha kazi ya fasihi, utunzi wake huathiriwa na mazingira ya kijamii ambamo huchota malighafi(fani) ya utunzi na masuala (maudhui) anayoyaanzia katika utungo wake.

Kwa hivyo, mtunzi akiwa sehemu ya jamii yake huathirika sana na itikadi ambazo jamii yake inazingatia katika utunzi wake. Van Dijk (1998) anathibitisha ukweli huu anaposema kwamba itikadi huwa za kijamii. Kwa hivyo, mtunzi wa nyimbo za kiasili za Kikamba hana budi kuzingatia itikadi za jamii yake katika utunzi wake ili kazi zake ziwe faafu kwa jamii lengwa. Kama mwalimu wa jamii yake msanii yeyote yule huwa ana jukumu la kuelimisha jamii yake mintarafu ya itikadi hizo. Utafiti huu

umetambua kwamba katika jamii ya Wakamba, zipo itikadi za aina mbalimbali na ambazo hupitishwa kwenye nyimbo zao za kiasili. Hivyo, nyimbo za kiasili za Kikamba huwasilisha itikadi mbalimbali zilizofumbatwa kijazanda. Itikadi zenyewe zinahusu masuala kama vile tohara, kazi, ndoa na mapenzi, utamaduni, malezi, mauti na siasa.

5.1.1 Itikadi kuhusu Tohara

Tohara ni upasuaji mdogo wa kukata au kuondoa govi, yaani ngozi inayofunika ncha ya uume. Hivyo, tohara inaweza kufanyika kutokana na sababu za kiutamaduni, kidini au kiafya. Kwa mujibu wa utamaduni wa Wakamba, tohara ni hatua muhimu katika maisha ya jamii. Hatua hii ndiyo kivukio cha kutoka kwenye kiwango cha utotoni hadi utu uzima. Hivyo, itikadi kuhusiana na tohara hudhihirika katika nyimbo za kiasili za Kikamba za tohara au nyiso. Nyiso za Kikamba huimbwa katika hafla za tohara. Nyimbo hizi hubeba mafunzo mbalimbali kwa watahiriwa. Kwa mfano, katika wimbo *Na. 4. **Kaindo** (Kijitu)* tunaelezwa kwamba mwimbaji ana kakitu anakokatafuta. Inaelezwa kwamba aidha wasichana **Mulekye**, **Vaati** au **Kanyaa** ndio wamekaficha. Angalia ubeti ufuatao:

*Ve **kaindo** kala ngumanza kana niwe uvithite na ndandavasya ngumanza. Ve kaindo kala ngumanza Kana niwe uvithite, Na ndandavasya ngumanza. Kanyaa niwe uvithite, Na ndandavasya ngumanza. Ve kaindo kala ngumanza kana niwe uvithite na ndandavasya ngumanza. **Kanyaa** niwe uvithite, Na ndandavasya ngumanza. Ve kaindo kala ngumanza kana niwe uvithite na ndandavasya ngumanza **Vaati** niwe uvithite, na ndandavasya ngumanza. Ngutavye niwe uvithitei, na ndandavasya ngumanza. Ngutavye niwe uvithitei, na ndandavasya ngumanza. **Mulekye** niwe uvithite, na ndandavasya ngumanza.*

Tafsiri

Kuna **kijitu** ninachokitafuta, sijui kama ndiye amekificha, na haniambii nikikitafuta. Kuna kijitu ninachokitafuta, Sijui kama ndiye amekificha na haniambii nikikitafuta. Kanyaa ndiye amekificha na haniambii nikikitafuta. Kuna kakitu ninachokitafuta, sijui kama ndiye amekificha, na haniambii nikikitafuta. **Kanyaa** ndiye

amekificha , na haniambii nikikitafula. Kuna kijitu ninachokitafula, sijui kama ndiye amekificha, na haniambii nikikitafula **Vaati** ndiye amekificha, na haniambii nikikitafula. **Mulekye** ndiye amekificha , na haniambii nikikitafula.

Kutokana na ubeti uliopo hapo juu, maarifa ya kimsingi yanatuwezesha kutambua kuwa kinachotafutwa kimo kwenye mhusika wa kike. Anayekitafula ni mhusika mtahiriwa wa kiume. Pia, mwimbaji mtahiriwa anakisia kuwa anachokitafula kimefichwa na mhusika wa kike, aidha Kanyaa, Mulekye au Vaati. Hivyo, majina ya kike **Kanyaa**, **Mulekye** na **Vaati** yametumika kijazanda kuashiria **mwanamke**. Vilevile, neno **kaindo** limetumika kijazanda kurejelea ndoa, ambapo akipata mke atakuwa amekwishaipata. Hivyo, mwimbaji anatafula **mwanamke** anayefaa ili afunge **ndoa** naye awe **mke** wake. Wimbo wenyewe unapitisha itikadi inayohusu ndoa na tohara. Jazanda hizi zinadhahirisha itikadi ya Wakamba kwamba tohara ndiyo njia ya pekee inayowapa vijana kibali cha kuoa. Hivyo, tohara ni kitu kizuri kinachokubalika na jamii. Ni utamaduni unaoenziwa na jamii.

Pia, wimbo wa **NA. 1. Sisy Wone** (Angalia Uone) unapitisha itikadi ya tohara.

Tazama kifungu kifuatacho:

Mwaiki: *Muti uu ni mumu. Muti uu ni mumu. Umite nza na nthini nomwiu. Ninguutila!* Watahiriwa: *Tila*

Mwaiki: *Ninguutila*

Aikwa: *Tila*

Mwaikwa: *Ekai ukia ta matila ma kiimani matesi mbilano*

Tafsiri:

Ngariba: Mti huu umekauka. **Mti** huu umekauka. Umekauka nje lakini ndani ni mbichi Nitaukata Watahiriwa: Ukate

Ngariba: Nitaukata

Watahiriwa: Ukate

Ngariba: Wacheni kuogopa Kama **wajinga wa milimani** wasiojua **kazi**.

Kutokana na kifungu hiki, ngariba ambaye ndiye mwimbaji anaeleza kuhusu *mti uliokauka* nje lakini ndani ni mbichi. Ngariba anaendelea kusema kwamba atakata mti huo ambapo watahiriwa kupitia wimbo huo huo wanamruhusu kuukata. Kisha, anawashauri wasiwe na woga kama *wajinga wa milimani* ambao hawajui kazi. Hapa, mwimbaji anazilinganisha *mboo za watahiriwa* na *mti uliokomaa* au *kukauka*. Anaeleza kwamba mti unaorejelewa hapa umekauka nje lakini ndani bado ni *mbichi*. Hivyo, *mbichi* unaorejelewa hapa ni ile hali ya mtahiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha, ambayo ni ishara ya kuiendeleza jamii. Kwa hivyo, mwimbaji anapitisha itikadi ya tohara kwamba baada ya kupashwa tohara, mtahiriwa huwa amehitimu kuoa na kushiriki kitendo cha ndoa ili kuiendeleza jamii inayohusika. Kupitia kwa wimbo huu, watahiriwa wanahimizwa wasiwe na woga kama wale *wajinga wa milimani* wasiojua *kazi*. Hivyo, neno wajinga wa milimani linarejelea Wakikuyu ambao wanaishi sehemu za milimani kinyume na Wakamba wanaoishi maeneo tambarare.

Wakamba huwachukulia Wakikuyu kuwa wavivu na ambao hawajiwezi kimapenzi (Wathome, 2009). Pamoja na hayo, neno *mbilano (kazi)* hapa limetumika kama ishara ya tendo la ndoa. Hivyo, watahiriwa wanashauriwa wawe jasiri kabla na hata baada ya tohara. Vilevile, wanahimizwa kwamba wasiwe waoga katika masuala ya kimapenzi kwenye ndoa kwa maana hiyo ndiyo njia ya pekee ya kupata watoto na hatimaye kuiendeleza jamii.

Vilevile, itikadi ya tohara inadhihirika katika wimbo **NA. 5. Mwatu** (Mzinga) uliowasilishwa kwenye hafla ya tohara. Angalia kifungu kifuatacho:

Ukwa mwatu uno nukutha na ndwina uki mwinawa mwatu uno nukutha na ndwina uki ,mwatu uno nukutha na ndwina nzuki mwinawa kai syiminwa ni ngaku mwatu usu nduuisiasya. Ukwa mwatu uno nukutha na ndwina uki mwinawa mwatu uno nukutha na ndwina nzuki mwinawa kai syiminwa ni ngaku mwatu usu nduuisiasya

Tafsiri

Unajua huu **mzinga** unaonekana kama una **nyuki wengi** na kumbe hamna **asali** kaka yangu, huu **mzinga** unaonekana kama una **nyuki wengi** na kumbe hamna **asali** kaka yangu, kumbe nyuki wanaangamizwa na **ngaku** (aina ya mnyama anayewaangamiza nyuki), hujauchunguza mzinga vizuri. Unajua huu mzinga unaonekana kama una nyuki wengi na kumbe hamna **asali** kaka yangu, kumbe nyuki wanaangamizwa na ngaku hujauchunguza mzinga vizuri.

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Itikadi ni maadili (Van Djik, 1998). Mhimili huu unashikilia kwamba itikadi ni mifumo ya utambuzi wa kijamii ambayo inaweza kutathminiwa. Yaani, itikadi huweka msingi wa maamuzi kuhusu kilicho kizuri au kibaya na pia hutoa mwongozo wa kimsingi wa mtazamo na maingiliano ya kijamii. Hivyo, inachukuliwa kuwa vijenzi vikuu vya itikadi ni maadili ya kijamii-kitamaduni kama vile ukweli, haki, wema na usawa miongoni mwa mengine. Kwenye kifungu kilichopo hapo juu, tunaelezwa kuhusu **mzinga** ambao una **nyuki wengi** lakini hamna **asali**. Mwimbaji anaeleza pia kwamba nyuki hao wanaangamizwa na **ngaku**. Hivyo, badala ya nyuki kufikia lengo lao la kuandaa asali, wanaangamizwa wangali wachanga. Kwa hivyo, taswira tunayochorewa katika wimbo huu ni ya kijazanda inayorejelea dhuluma za kijinsia na ubakaji. Hivyo, **nyuki** hapa wanarejelea **vijana** ambao hawajakomaa. Vijana wanaorejelewa hapa wanadhulumiwa kimapenzi katika jamii iliyojawa na **ngaku**, yaani wabakaji. Hivyo, unyanyasaji wa aina hii ni kinyume cha maadili ya jamii ya Wakamba. Kwa hivyo, wimbo wenyewe unawaonya vijana watahiriwa dhidi ya dhuluma za kijinsia ambapo mwimbaji anawafahamisha kuwa sasa wao ni watu wazima wanaopaswa kuwajibika katika jamii. Hapa, matendo maovu ya unyanyasaji wa kimapenzi yanakashifiwa huku maadili ya haki za watoto na vijana zikisisitizwa. Hivyo, vijana wanatarajiwa kudumisha maadili kwa maana wanategemewa kwa kiwango kikubwa katika jamii. Haya ni kwa mujibu wa imani ya

Wakamba kwamba wavulana hutahiriwa ili kuingizwa katika kundi la wanaume wanaopaswa kuwajibika katika jamii.

Neno *asali* limetumika kijazanda kurejelea *utoshelezaji wa kimapenzi*. Hivyo, usemi kwamba ‘mzinga una nyuki wengi lakini hamna asali’ una maana kwamba japo vijana wanaweza kudhihirisha ukuaji wa kimaumbile, bado hawajakomaa kiasi cha kushirikishwa kwenye vitendo vya kimapenzi. Haya yanalandana na Katiba ya nchi ya Kenya (2010) kwamba umri wa kabla ya miaka kumi na minane ni wa watoto. Hivyo, ni kinyume cha sheria ya nchi hii kushirikiana kimapenzi na mtoto. Hii ndiyo maana mwimbaji anawashauri watahiriwa kwamba wakivunja sheria hiyo wataangukiwa na kesi.

Itikadi ya tohara inadhihirika pia kwenye wimbo *Na. 2. Munyambu Nuukiva* (Simba ananguruma). Wimbo wenyewe unaeleza kuhusu *simba* anayenguruma na ambaye amelikwa na baba. Hivyo, mwimbaji anawashauri watahiriwa kuwa wasitetemeke kwa maana simba huyo ameitwa na baba.

Tazama kifungu hiki:

*Munyambu nuukiva. Munyambu nuukiva wi Ukavi. Ni nau uwitie
Munyambu nuukiva. Ni nau uwitie. Sisy ndukalilie. Ni nau uwitie*

Tafsiri:

Simba anaguruma. Simba anaguruma akiwa Ukavi. Ni baba aliyemwita. Simba anaguruma. Ni baba aliyemwita. Chunga usitetemeke. Ni baba aliyemwita.

Katika kifungu kilichopo hapo juu, mwimbaji anamlinganisha *simba* na **ngariba**.

Katika hali ya kawaida, simba ni mnyama mkali ambaye anaogopwa na binadamu kwa ukali wake. Hivyo, msanii anamlinganisha ngariba na simba ili aweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo kwa kufahamu kwamba, wanajamii wanamwamini na wanamthamini kwa kazi yake. Watahiriwa wanafahamishwa kwamba ngariba huyo

mkali asiogopwe kwa sababu aliyemualika ni baba na hivyo, hawezi kuwadhuru kwa lolote. Kwa hivyo, jazanda ya *simba* imetumika kufumbata itikadi ya tohara kwamba ni hatua muhimu na inayofaa kuenziwa Wakamba. Vile vile, uchungu wanaouhisi watahiriwa ni ishara ya mambo magumu na changamoto za maisha zinazowasubiri katika hatua ya utu uzima. Hivyo, inaaminika kwamba changamoto zenyewe zinahitaji ujasiri, ukakamavu na uvumilivu wa kutosha. Yaani, maisha ya uwajibikaji si ya waoga na wanaovunjika mioyo kwa haraka.

Pamoja na hayo, wimbo **NA. 3. Mwaikwa niwalika Ndiani** (*Mtahiriwa ameingia Kidimbwini*) unapitisha itikadi ya tohara. Angalia ubeti ufuatao:

Onthe: *Mwaikwa ii*
Mwaikwa: *Mwaikwa ii*
Onthe: *Yu niwalika ndiani*
Mwaikwa: *Yu niwalika ndiani*
Onthe: *Ndiani ya kulungilwa.*
Mwaikwa: *Mwaikwa niwalika ndiani*

Tafsiri

Wote: Mtahiriwa ii
Mtahiriwa: Mtahiriwa ii
Wote: Sasa ameingia **kidimbwini**.
Mtahiriwa: Sasa ameingia kidimbwini
Wote: Kidimbwi cha kujitegemea.
Mtahiriwa: Mtahiriwa umeingia kidimbwini.

Kupitia kwa wimbo huu, inaelezwa kwamba mtahiriwa ameingia kidimbwini. Van Dijk (1998) anasisitiza mhimili wa nne wa nadharia yake. Mhimili wenyewe ni wa maumbo. Mhimili wa maumbo unashikilia kwamba maumbo yanarejelea uwakilishaji wa kiakili wa tajriba za kibinafsi kuhusu shughuli, matukio au hali maalum. Hivyo, maumbo huwakilisha ufahamu wetu wa shughuli na matukio mengine pamoja na wahusika wa matukio hayo. Vilevile, maumbo huwakilisha maoni yetu maalum ya kibinafsi. Kutokana na maarifa yetu ya kimsingi, neno *kidimbwini* limetumika kijazanda. Katika hali ya kawaida kwenye mazingira ya Wakamba, kidimbwi ni

mkusanyiko wa maji yenye kina kirefu na ambamo vijana na watu wazima huogelea. Hivyo, ufanisi au kutofauli kwa mwogeleaji hutegemea weledi na ujuzi wake kuhusu shughuli ya kuogelea. Hivyo, iwapo mwogeleaji ana ujuzi wa kutosha, yeye hufaulu na kutoka majini salama salimini. Hata hivyo, ukosefu wa stadi za uogeleaji huenda ukampelekea mwogeleaji katika kuzama majini, huku ndoto yake ya kuogelea na kutoka majini salama ikizimwa.

Hivyo, mwimbaji anailinganisha *hali ya uogeleaji* na hali ya *utegemevu* ambapo mtahiriwa anakabiliana nayo. Mwimbaji anaifumbata itikadi ya tohara kijazanda kwenye wimbo teule. Hivyo, mwimbaji anawasilisha imani za itikadi hii kwamba baada ya kupashwa tohara, mtahiriwa hutoka utotoni wa kuwategemea wazazi na kisha anaanza kujitegemea mwenyewe. Hivyo, inaaminika kwamba baada ya tohara vijana hawana budi kuwajibika na kujitwika majukumu ya watu wazima kama inavyostahili kwenye jamii ya Wakamba. Hivyo, tohara ni kivukio cha kutoka utotoni kwenda kwenye utu uzima.

5.1.2 Itikadi kuhusu Kazi

Kazi ni shughuli anayoifanya mtu. Shughuli yenyewe inaweza kuhusisha juhudi za kiakili na kimwili ili kufikia lengo au matokeo fulani. Katika jamii ya Wakamba, zipo kazi za aina mbalimbali. Kazi zenyewe ni kama vile kulima, kutwanga mawe, kusaga unga, kuvuna mazao shambani, kuanika mizinga na kuchunga mifugo miongoni mwa nyingine. Hivyo, kazi ni sehemu muhimu ya maisha ya Wakamba na huchukua nafasi kubwa katika nyimbo zao za kiasili. Utafiti huu umetambua kwamba itikadi ya kazi inadhihirika katika baadhi ya nyimbo za kiasili za Kikamba za kikazi. Akizungumzia nadharia ya Itikadi, Van Djik (1998) anaeleza kwamba mhimili wa tatu wa nadharia hii ni mielekeo ya itikadi. Mielekeo yenyewe hushikiliwa na washirika wa kundi fulani la kijamii. Kupitia kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba

hasa za kikazi, itikadi ya kazi hufumbatwa kijazanda. Itikadi hiyo hujengwa kwa mielekeo mbalimbali. Kwa mfano, kupitia kwenye wimbo NA. 30. *Kaveti Kaanu* (Kamwanamke Kazembe), mwimbaji anasimulia kuhusu mwanamke mzembe. Mwimbaji anatoa ushauri kwa mwanamke huyu kwamba mvua imenyeshwa na bila shaka hana budi kuchukua **kathungi (kiondo)**, **kamulo (jembe)** na **kavelu (mbegu)** na kisha aelekee shambani. Inaelezwa hapa kwamba watoto hawawezi kushiba chakula cha serikali cha **mikebe miwili** na hivyo anafaa kwenda shambani aifanye kazi ili aikimu familia yake. Angalia sehemu ifuatayo ya wimbo huu:

*Kaveti kaanu mbua ni mbiingu, Kaveti kaanu mbua ni mbiingu, ndwose **kathungi, kamulo na kavelu** na uyaangiia muundani kaveti kaanu mbua ni mbiingu. Syana iyamba kuvuna ii mbemba sya tumikeve twili. Syana iitonya kuvuna **mbemba sya selekali** mbaitu ii mwaka umwe **tumikeve twili**.*

Tafsiri

Kamwanamke kazembe mvua imenyeshwa, Kamwanamke kazembe mvua imenyeshwa, chukua **kiondo, jembe na mbegu** na kisha uelekee shambani Kamwanamke kazembe mvua imenyeshwa. Watoto hawawezi shibishwa na mahindi ya serikali jamani mwaka mmoja mikebe miwili, Watoto hawawezi shibishwa na **mahindi ya serikali** jamani **mikebe** miwili kwa mwaka mzima. Kamwanamke kazembe mvua imenyeshwa.

Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anapitisha itikadi ya kazi kwamba ni muhimu kujitahidi kazini. Mwimbaji huyu anaeleza kwamba mwanamke mvivu anafaa kuchangamka na kujitahidi kikazi **shambani** ili aweze kuikimu familia yake. Anaeleza kwamba chakula cha msaada wa serikali hakitoshi kuikimu familia kwa maana huwa kidogo mno. Hivyo, neno *tumikeve twili* (mikebe miwili mindogo) ni jazanda inayorejelea **chakula cha msaada** ambacho hakiwezi kutosha ikilinganishwa na kile kinachopatikana mtu anapojituma kazini shambani. Jazanda hii imetumika kuwasilisha itikadi ya kazi kwamba ina manufaa makubwa kwa wanajamii. Hivyo, tabia za uzembe na kutowajibika zinakemewa vikali kupitia kwa wimbo huu.

Katika jamii ya Wakamba, wapanzi hasa wanawake huzihifadhi mbegu zao kwenye **kathungi (kiondo)**. Vilevile, wapanzi hao hutumia **kamulo (jembe)** katika kulima na kupalilia **kavelu (mbegu)** husika. Katika muktadha wa kikazi, maneno **kiondo, jembe, mbegu** yametumika kijazanda kurejelea **nyenzo muhimu** za kikazi. Hivyo, kazi inayorejelewa hapa inaweza kuwa ya kibiashara, kiofisi, kitaaluma, n.k. Kwa mfano, ikiwa ni kazi ya kibiashara, mtaji na bidhaa za biashara zitahitajika. Vilevile, kwenye sekta ya elimu, mwalimu atahitajika kuchukua vifaa kama vile chaki, kalamu, ratiba ya kazi, n.k na kuelekea shuleni na kisha darasani ambapo ndipo maeneo yake ya kazi. Kwa hivyo, neno **muundani** (shambani) limetumika kijazanda kuashiria **maeneo ya kazi**. Jazanda hizi zote zimetumika katika kuifumbata itikadi ya kazi kwamba kazi ni muhimu na kila mwanajamii hana budi kujitahidi. Jazanda zenyewe zimetumika katika kukashifu na kukejeli uzembe miongoni mwa wanajamii.

Japo neno *Kaveti kaanu* (Kamwanamke kazembe) limetumika kijazanda kuashiria mwanajamii yeyote mwenye uzembe, mwimbaji wa wimbo huu anamsawiri mwanamke kwa njia isyofaa. Kwa mfano, neno *Kaveti kaanu* (Kamwanamke kazembe) limetumika kwa namna ya kuidunisha jinsia ya kike. Hivyo, matumizi ya “kamwanamke” badala ya “mwanamke” yanaibua hali ya kumdunisha mhusika anayelengwa kwenye wimbo. Pamoja na hayo, wimbo wenyewe unapitisha itikadi ya kazi kwamba kazi za shambani zinafaa kushughulikiwa na wanawake. Yaani, mwelekeo unaowasilishwa hapa ni kwamba ni jukumu la mwanamke kushughulikia familia yake shambani ili wasihangaike kwa kukosa chakula. Hali hii inathibitisha maelezo ya Strobel (1979) kwamba kwa mujibu wa tamaduni nyingi za Kiafrika, mwanamke amepewa nafasi ya pili chini ya mwanamume katika mfumo wa kuumeni. Hivyo, maoni ya mtafiti ni kwamba mume na mke hawana budi kuwajibika na kushughulika shambani pamoja ili kuikimu familia yao. Hivyo, kazi za aina hii

zinafaa kuwahusisha wazazi wote wawili. Hivi ni sawa na kusema kwamba, iwapo tatizo kama vile la njaa limetokea katika familia, mwanamke asiwe wa kulaumiwa peke yake kwa maana ndoa ni ya wawili na bila shaka wote hawana budi kuwajibika.

Itikadi ya kazi inajitokeza katika wimbo **NA. 31. Muika Wia Nukunwe** (Vijana Kazi Itekelezwe) pia. Kupitia kwa wimbo huu, vijana wanaelezwa kwamba wafanye kazi kwa bidii ambapo yule atakayeshindwa atarudishwa nyumbani. Mwimbaji anatusawiria kuhusu **ndege** fulani inayoitwa Manyali itakayowasafirisha wafanyikazi wenye bidii. Hivyo, neno **ndege** limetumika kijazanda kurejelea **mafanikio** yanayotokana na juhudi kazini. Hivyo, jazanda yenyewe imetumika katika kuendeleza itikadi ya kazi katika jamii ya Wakamba. Hapa, wanajamii wanahimizwa wajitahidi kazini kwa maana juhudi huzaa maendeleo na mafanikio makubwa. Angalia kifungu kifuatacho:

Yii muika ii wia nukunwe, kasi nukunwe waemwa utungwe na musyi. Ve ndeke ikwitwa Manyali ikukua Konza ii nake Songola Manyali akakua andu ma wia. Yii muika ii wia nukunwe, kasi nukunwe waemwa utungwe na musyi ve ndeke ikwitwa Manyali ikukua Konza ii nake Songola Manyali akakua andu ma wia. Onake Sungula Manyali akakua andu ma wia. Onake Sungula Manyali akakua andu ma wia.

Tafsiri

Eee vijana, kazi ifanywe, kazi ifanywe na ukishindwa urudishwe nyumbani. Kuna **ndege** inaitwa Manyali, inabeba watu Konza, naye Songola Manyali atabeba watu wa kazi. Eee vijana, kazi ifanywe, kazi ifanywe na ukishindwa urudishwe nyumbani. Kuna **ndege** inaitwa Manyali, inabeba watu Konza, naye Songola Manyali atabeba watu wa kazi. Naye Songola Manyali atabeba watu wa kazi.

Katika wimbo **NA. 32. Kavuli Vula Mwee Witu** (Kavuli Twanga Maweale), itikadi ya kazi inadhihirika kupitia jazanda *ngima* (ugali), *isandi* (chakula cha kiasili kinachotokana na unga ya mtama) na *kinaa* (chakula cha kiasili kutokana na maweale). Kwa kawaida, ili chakula cha ugali kipatikane, juhudi nyingi huhitajika. Kwa mfano, ipo kazi ya kupanda mahindi au maweale shambani, kuyapalilia, kuyavuna,

kuyatenganisha na uchafu na pia kusiaga mahindi au mawele husika. Tunaposiaga mawele tunapata unga inayotumika katika kupikia ugali. Hivyo, bila bidii hakuna ugali, wala mafanikio yoyote kazini. Hapa, mwimbaji anamlenga mhusika Kavuli ambapo anamrai aendelee kujitahidi katika kutwanga mawele. Anaendelea kumweleza kwamba vyakula vya aina mbalimbali hupatikana baada ya kujitahidi kazini.

Kwa mfano, mwimbaji anaeleza kwamba ugali hupatikana baada ya kutwanga mawele. Hivyo, maneno *ngima* (ugali) *isandi* (chakula cha kiasili kinachotokana na unga ya mtama) na *kinaa* (chakula cha kiasili kutokana na mawele) yametumika kama ishara ya mafanikio ya wanaofanya kazi kwa bidii. Hapa, *kinaa*, *isandi* na *ugali* ni vyakula vinavyolinganishwa na mafanikio yanayotokana na juhudi kazini. Hivyo, wanajamii wanahimizwa waendeleo kujituma kazini kwa maana mtaka cha mvunguni sharti ainame. Hivyo, mtu anayehitaji mafanikio hana budi kujitahidi katika lolote analolifanya. Tazama kifungu kifuatacho cha Wimbo **NA.32**:

Wimbo NA.32

***Kavuli** vula mwee witu. Kavuli vula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. Kavuli vula mwee witu. Kavuli vula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. **Ngima** yumaa kwi kuthie, ii vulavula mwee witu. **Isandi** yumaa kwi kukime ii vula vula mwee witu **Kinaa** kyumaa kwi kuthie ii vula vula mwee witu. Nikilya nathia kakautwa, nikilya nathia kakautwa nila imutengea ya kiveti yukilasya kwoko ta ikwaunya Kavuli vula mwee witu.*

Tafsiri

Kavuli twanga mawele yetu, Kavuli twanga mawele yetu. Ninakaa hapa uwanjani nikitwangatwanga mawele yetu. Ninakaa hapa uwanjani nikitwangatwanga mawele yetu. Kavuli twanga mawele yetu, Kavuli twanga mawele yetu. **Ugali** hupatikana kwa kusiaga mawele, twanga twanga mawele yetu. **Isandi** (aina ya chakula cha kitamaduni) hupatikana baada ya kusaga mawele, twanga twanga mawele yetu. **Kinaa** (aina ya chakula cha kitamaduni) hupatikana

kwa kusiaga mawele, twanga twanga mawele yetu. Unga inapungua kadri ninaposiaga, unga inapungua kadri ninaposiaga. Yule mwanamke mzembe ndiye anapunguza).

5.1.3 Itikadi kuhusu Dini

Dini ni imani maalumu ya kumwamini na kumtii Mungu wa haki. Dini inahusiana na mambo ya kiroho kwamba kuna muumba aliyeumba ulimwengu huu na kwamba ndiye mtawala wa vyote vilivyomo. Hivyo, dhana ya dini inarejelea imani kuhusu Mungu au miungu ambayo huchukuliwa kuwa ni ukweli na wanaoiamini dini inayohusika. Kwa hivyo, itikadi ya kidini inajihusisha na masuala ya kidini kama vile imani, uwepo wa viumbe vikuu kama vile Mungu, miongoni mwa mengine. Utafiti huu umetambua kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba husheheni itikadi ya kidini. Nyimbo zinazosheheni itikadi hizi mara nyingi huwasilishwa katika hafla za kidini kama vile *kilumi*. Kwa mfano, itikadi hii inajitokeza kwenye wimbo *NA. 16. Undu Ukwona ngisilila uu* (Ninaposhangilia Hivi). Tazama ubeti huu:

*Niwee kilumini ngivoyea muuo, Niwee kilumini ngivoyea muuo.
Niwee kilumini ngivoyea mbua, Niwee kilumini ngivoyea mbua.
Niwee kilumini kwa Mutava musyi, Niwee kilumini kwa Mutava musyi.
Kula kwi **miti** minene kwasuvaswa **mikokola** ona **mithekethi**.
Kula kwi miti minene kwasuvaswa mikokola ona mithekethi.*

Tafsiri

Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea amani. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea mvua. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea mvua. Nilikuwa kwenye kilumi nyumbani kwa Mutava. Nilikuwa kwenye kilumi nyumbani kwa Mutava. Ndiko kwenye **miti** mikubwa kunakotengenezwa mikokola na mithekethi (aina ya kifaa cha kukoroga uji unapoendelea kupika. Ndiko kwenye miti mikubwa kunakotengenezwa **mikokola** na **mithekethi** (aina ya kifaa cha kukoroga uji unapoendelea kupika).

Katika kifungu kilichopo hapo juu, inaelezwa kwamba usiku uliotangulia mwimbaji hakulala nyumbani kwa maana alikuwa ameenda kwenye *kilumi*. *Kilumi* ni aina ya ibada inayowasilishwa kwenye jamii ya Wakamba kama maombi kwa Mungu. Katika jamii hii, wanamrejelea Mungu kama *Ngai Mumbi* anayeaminika kuwa muumba wa

ulimwengu na vyote vilivyomo. Hafla ya *kilumi* huaminika kuwa njia mojawapo ya kuwasiliana na Mungu pamoja na roho za mababu walioaga dunia. Katika hafla ya aina hii, tambiko na sadaka hutolewa kwa Mungu. Shughuli hii ya *kilumi* iliandaliwa wakati wa changamoto au majanga kama vile njaa na kiangazi. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anaeleza kwamba alikuwa amehudhuria hafla ya *kilumi* kwa nia ya kuiombea mvua, jamii na amani. Inaelezwa kwamba alikokuwa ameenda kuomba kuna *miti* mikubwamikubwa inayotumika katika kuchongea vifaa kama vile *mithekethi* na *mikokola*.

Hivyo, maneno *miti* (miti) *mithekethi* na *mikokola* (aina ya vifaa vya jikoni vinavyochongwa kutokana na miti) yametumika kijazanda kurejelea *manufaa* yanayotokana na kumwabudu Mungu. Wimbo huu unapitisha itikadi ya kidini kwamba Mungu pekee ndiye hunyesha au kunyima mvua na vitu vyote vizuri. Hivyo, Mungu anapofurahishwa na wanajamii huwanyeshea mvua ambapo mavuno ya aina mbalimbali hupatikana kwa wingi. Hata hivyo, matendo ya wanajamii yanapomkasirisha Mungu, husababisha majanga kama vile njaa na kiangazi. Hivyo, kupitia wimbo teule, mwimbaji anatusawiria kipindi ambacho kina ukosefu wa mvua. Hivyo, anawarai wanajamii waende kwenye *kilumi* ili wamwabudu Mungu ndiposa aweze kuinyesha mvua. Anaeleza kwamba kule alikohudhuria ile hafla ya ibada kuna miti mikubwamikubwa. Hivyo, maneno *miti*, *mithekethi* na *mikokola* yametumika kama jazanda inayorejelea *mafanikio* yanayotokana na kumwabudu Mungu. Yaani, mwimbaji anapitisha mwelekeo wa itikadi ya kidini kwamba kila mwanajamii anastahili kumtambua na kumwabudu Mungu kila wakati.

Pia, itikadi ya kidini imejitokeza katika wimbo **NA.17. Tuthii kithembeoni** (Twendeni Madhabahuni). Itikadi yenyewe imefumbatwa katika jazanda *malenge* (*maboga*), *nzuu* (*baazi*) na *mboso* (*maharagwe*). Angalia kifungu kifuatacho:

*Ukilai ithyonze tuthi kithembeoni, Ukilai ithyonze tuthi kithembeoni. Tukathembee Ngai mbua yue. Tukathembee Ngai mbua yue. Syana syukile, syana syokote **malenge** kivulanio kya **nzuiu** na **mboso**. Tumukathe Ngai Mulungu. Ukilai ithyonze tuthi kithembeoni. TukathembeeNgai, Ngai Mumbi Ngai Mwaturangi. Ula wauisye mbua nundu wa kuthembewa. Ngai nitwooka ithemboni twiwe. Ngai nitwooka ithemboni twiwe. Noituekea mavityo maitu we Mumbi waitu. Noituekea mavityo maitu we Mumbi waitu. Ngai waitu nataiwe. Ngai waitu nataiwe. Ngai waitu Mumbi, Ngai Mwaturangi niwaile kutaiwa. Ngai waitu Mumbi, Ngai Mwaturangi niwaile kutaiwa. Ngai tuekea mavityo maitu we Mumbi waitu. Ngai tuekea mavityo maitu we Mumbi waitu.*

Tafsiri

Amkeni sote twende madhabahuni, amkeni sote twende madhabahuni. Tukamwabudu Mungu mvua inyeshe. Tukamwabudu Mungu mvua inyeshe. Watoto wainuke, watoto waokote **maboga**, mchanganyiko wa **baazi** na **maharagwe**. Tumtukuze Mungu muumbaji. Inukeni nyote twende kwenye madhabahu, tukamwabudu Mungu, Mungu Muumbaji aliyeinyesha mvua alipoabudiwa. Mungu tumekuja madhabahuni, tusikize. Mungu tumekuja madhabahuni, tusikize. Na utusamehe makosa yetu ewe muumbaji wetu. Mungu wetu atukuzwe, Mungu wetu atukuzwe. Mungu wetu Muumbaji, Mungu Muumbaji anastahili kutukuzwa. Mungu wetu Muumbaji, Mungu Muumbaji anastahili kutukuzwa. Mungu tusamehe makosa yetu ewe Muumba wetu. Mungu tusamehe makosa yetu ewe Muumba wetu.

Wanajamii wanahimizwa kwenda madhabahuni ili kumwabudu Mungu ambaye ndiye chanzo cha aidha mafanikio au matatizo yao. Hivyo, imedhihirika hapa kwamba kumwabudu Mungu kunaweza kuwasababishia mafanikio huku kutomtambua au kutomwabudu kunasababisha matatizo kama vile kiangazi au ukosefu wa mvua. Hivyo, **maboga**, **baazi** na **maharagwe** ni aina ya vyakula vinavyopatikana mvua inaponyesha. Taswira hii ya msimu wa kiangazi na mvua imetumika kijazanda ili kurejelea umuhimu wa kumwabudu Mungu.

Itikadi ya dini pia inajitokeza katika wimbo **NA. 12. Ngai wa Nzou nowe wa Nduti** (Mungu wa Ndovu ndiye Mungu wa Siafu). Tazama kifungu kifuatacho:

*Ii Ngai ndamamaa Mulungu ndakomaa Ngai ula wa **nzou** nowe wa **nduti** Ngai nowe usu Ngai ula wa athwii nowe ukusuviaa asuviaa ngya isu Ngai ndamamaa Ngai ula wa matu nowe ukusuviaa twindo tula twi nzi twi nzi ta nduti Ngai niwe usuviaa **nzungu***

Tafsiri

Ee Mungu halali Mungu hasinzii Mungu yule wa **ndovu** ndiye wa **siafu** Mungu ndiye huyo, Mungu yule wa matajiri ndiye anayekulinda yeye hulinda maskini hao Mungu halali Mungu wa mbinguni ndiye akulindaye viumbe wadogowadogo walio hapa duniani Mungu ndiye hulinda **siafu**

Kwenye wimbo huu, inaelezwa kwamba Mungu wa ndovu ndiye Mungu wa siafu na kwamba Mungu hasinzii wala halali. Hivyo, itikadi ya kidini imewasilishwa kupitia maneno siafu na ndovu ambayo yametumika kijazanda. Kwa kawaida, ndovu ni mnyama wa porini na ambaye ni mkubwa sana. Naye siafu ni mdudu mdogo sana anayetambaa ardhini. Hivyo, katika hali ya kawaida, ndovu anaweza kumdharau siafu kutokana na ukweli kwamba yeye ni mkubwa kinyume na siafu ambaye ni mdogo kupindukia. Hivyo, neno *ndovu* hapa limetumika kurejelea tabaka la juu la matajiri na wanaojiweza huku neno *siafu* likitumika kurejelea tabaka la chini la maskini na wale wasiojiweza. Hapa, inaelezwa kwamba Mungu hana upendeleo. Mungu anawapenda na kuwajali watu wote kwa njia sawa, wawe maskini au tajiri. Hivyo, itikadi hii ya kidini inajengwa na imani kwamba Mungu sio kama binadamu. Yeye huwashughulikia watu wote bila kuzingatia misingi yao ya kitabaka. Wanajamii wanahimizwa kutozingatia tofauti za kitabaka kwa maana utabaka ni mojawapo wa mambo ambayo hayampendezi Mungu.

5.1.4 Itikadi kuhusu Ndoa na Mapenzi

Ndoa ni muungano kati ya mwanamume na mwanamke kuishi pamoja kama mume na mke hadi kifo kiwatenganishe. Kwa mujibu wa maelezo haya, katika ndoa, watu wawili wa jinsia tofauti hutakiwa kuungana na kupendana hadi mwisho. Akizungumzia dhana hii, Senkoro (1982) anaeleza kwamba taasisi ya ndoa ni jambo muhimu na la lazima katika jamii. Wanajamii Wakamba huichukulia ndoa kuwa taasisi muhimu katika maisha ya kila mwanajamii. Hivyo, vijana walihimizwa kua

au kuolewa baada ya kupashwa tohara. Kwa kawaida, jamii ya Wakamba huichukulia arusi na ndoa kuwa shughuli muhimu. Hivyo, kwenye hafla za aina hii, wanandoa husika huandaliwa mapochopocho kama ishara ya makaribisho katika familia ya bwana arusi. Hivyo, sherehe huandaliwa ambapo wanajamii wote hutarajiwa kushiriki katika kushangilia na kuwakaribisha wanandoa katika hatua hii muhimu ya kuanza maisha mapya ya ndoa. Nyimbo za kiasili za Kikamba zimeipa itikadi ya ndoa kipaumbele. Nyimbo hizi zinaibainisha ndoa kama kiungo muhimu cha jamii. Kwa mfano, wimbo **NA. 23. Uka Usuvie Utwae** (Njoo Uitunze Ndoa) ni mojawapo wa nyimbo za kiasili za Kikamba zinazopitisha itikadi ya ndoa. Tazama kifungu kifuatacho:

*Li niutavya vate kuvuvuana, kana ka mama uka usuvie utwae. Li niutavya vate kuvuvuana, kana ka mama uka usuvie utwae. Li niutavya vate kuvuvuana, kana ka mama uka usuvie utwae. Niutavya vate kukia kindu, kana ka mama ii uka usuvie utwae. Niutavya vate kukia kindu, kana ka mama ii uka usuvie utwae. Niuiwe **ngate**, vamwe na **kyavati** ii, Niuiwe **ngate**, vamwe na **kyavati** ii kana ka mama uka usuvie utwae.*

Tafsiri

Ndio, nakwambia pasipokuchanganyikiwa, mtoto wa mama njoo uitunze ndoa. Ndio, nakwambia pasipokuchanganyikiwa, mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Ndio, nakwambia pasipokuchanganyikiwa, mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Ndio, nakueleza pasipo kuogopa lolote mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Ndio nakueleza pasipo kuogopa lolote mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Umepikiwa **mikate**, njoo utunze ndoa. Umepikiwa **chapati**, njoo utunze ndoa.

Katika kifungu kilichopo hapo juu cha wimbo *Uka Usuvie Utwae* (Njoo Uitunze Ndoa), mke mtarajiwa anaelezwa aje aitunze ndoa yake. Hivyo, mwimbaji anawasilisha itikadi ya ndoa kwamba mwanamke ana wajibu mkubwa wa kuitunza ndoa yake. Kwa kawaida, chapati na mikate ni miongoni mwa vyakula vinavyoandaliwa kwenye hafla mbalimbali katika jamii ya Wakamba. Kwa hivyo, maneno *ngate (mikate)* na *kyavati (chapati)* yametumika kijazanda kurejelea **makaribisho** makubwa katika jamii ya bwana arusi. Mwimbaji anamweleza bibi

arusi kuwa ameandaliwa mikate na chapati na hivyo hana budi kuitunza ndoa. Hivyo, anajaribu kuwasilisha ujumbe kwamba binti huyu amekaribishwa katika ile jamii mpya na basi ni sharti awajibike katika kuitunza taasisi hii muhimu. Hata hivyo, maoni ya mtafiti ni kwamba utunzaji wa ndoa unawahusisha wanandoa wote wawili. Hivyo, mume na mke hawana budi kuwajibika katika ndoa. Hivi ni sawa na kusema kwamba utunzaji wa ndoa usiegeme kwenye upande mmoja. Yaani, isiwe kwamba ndoa inapofeli mwanamke ndiye wa kulaumiwa. Hii ni kwa sababu kila mwanandoa ana mchango wake katika ndoa inayohusika na hivyo, mwanandoa yeyote awe mke au mume anaweza kufeli. Hivyo, ni muhimu wanandoa wawajibike katika kuitunza ndoa yao.

Pamoja na hayo, itikadi ya ndoa inajitokeza katika wimbo **NA. 25. Nzambi wa Mutunga**. Angalia ubeti ufuatao:

*Simu yaumie, simu yaumie Masaku twamikwatie na twooka. Simu yaumie, simu yaumie Masaku twamikwatie na twooka. Aume mwakwata livoti mwaisye ata? Mwindavya. Mbande **mutunda**, ni waki? Wai wa mavatano. Aume mwakwata livoti mwaisye ata? Mwindavya. Mbande mutunda, ni waki? Wai wa mavatano.*

Tafsiri

Simu ilipigwa, simu ilipigwa kutoka Machakos tuliipokea na tukaja. Simu ilipigwa, simu ilipigwa kutoka Machakos tuliipokea na tukaja. Wazee mlipoipokea ripoti mlisemaje? Mniambie. Nipande **mtunda**, ni wa nini? Ulikuwa wa mapatano.

Katika wimbo huu, mwimbaji anaeleza kuhusu mhusika wa kike Nzambi ambaye walikosana na mumewe na kisha akarudi kwa wazazi wake. Hivyo, mwimbaji anaimba katika muktadha wa mazungumzo ili kuleta mapatano kati ya wanandoa hao wawili. Kulingana na wimbo huu, wanakikao wamekubaliana kuwa Nzambi arudi kwa mumewe. Hivyo, tunaelezwa kwamba imekubalika kwamba wazee wapande *mutunda* (mti unaozaa matunda) ambao ni ishara ya *makubaliano* au *mapatano* yaliyoafikiwa. Imebainika hapa kwamba ndoa huwa imejaa changamoto mbalimbali.

Wakizungumzia suala hili, Boss (1988), Van (1989) na Benokraitis (1993) wanaeleza kwamba changamoto ni jambo la kawaida katika mahusiano yoyote ya wanadamu. Aidha, namna changamoto hizo zinavyoshughulikiwa huweza kuimarisha au kuzorotesha zaidi mahusiano hayo. Kwa hivyo, marekebisho na mapatano ni muhimu katika kusuluhisha changamoto za ndoa. Hapa, itikadi ya ndoa imefumbatwa kwenye jazanda *mutunda* inayoashiria *mapatano*.

Pia, itikadi ya ndoa na mapenzi inadhihirika katika wimbo **NA. 24. Mumba**. Tazama kifungu hiki:

*Natumie nduu na kana kanini ketawa **Mumba**, kanengie kivalua kyumu ngakamanthie uki wa ngilu. kanengie kivalua kyumu kya umantha **uki** wa **ngilu**. Wa tata nduthi Thua ii, wa tata ndukatike lumba. Wa tata nduthi Thua ii, wa tata ndukatike lumba.*

Tafsiri

Nilifanya urafiki na mtoto mdogo aitwaye **Mumba**. Alinipa kibarua cha kutafuta **asali mwitu** (aina ya mdudu anayeunda asali mwitu). Ndugu yangu nenda Thua, ndugu yangu cheza rhumba. Ndugu yangu nenda Thua, ndugu yangu cheza rhumba.

Katika wimbo *Mumba (Aliyeumbwa akaumbika)*, mwimbaji anasimulia namna alivyompata mpenziwe aitwaye Mumba. Hapa, mwimbaji anaeleza kwamba mpenziwe alimpatia kibarua kigumu cha kutafuta asali mwitu. Mwimbaji husika alitembelea maeneo mbalimbali akijaribu kulitimiza ombi la mpenziwe la kutafuta asali mwitu. Kwenye harakati zake za kutafuta asali mwitu, mwimbaji anakiri kwamba hakuwahi kumpata msichana ambaye alimpenda kama vile alivyompenda Mumba. Asali mwitu ni aina ya asali inayoandaliwa msituni na wadudu wadogo waitwao *ngilu*. Hivyo, asali yenyewe huwa nadra sana kupatikana. Imetambuliwa hapa kwamba mwimbaji ametumia neno **asali mwitu** kama jazanda ili kuwasilisha itikadi ya ndoa kwamba si rahisi. Anaeleza kwamba kama ilivyo vigumu kuipata asali mwitu, ndivyo ilivyo katika kuitunza ndoa na mapenzi. Kwa hivyo, mwimbaji

anawajulisha wanandoa kwamba hawana budi kuwajibika katika kuitunza na kuiendeleza taasisi ya ndoa miongoni mwao. Hivyo, japo ndoa si rahisi, inahitaji uvumilivu, ukakamavu, uwajibikaji na maelewano miongoni mwa wanaohusika.

Pamoja na hayo, itikadi ya ndoa na mapenzi inajitokeza katika wimbo *Na. 20. Mutanu*. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anatusimulia uchovu alio nao kutokana na safari ndefu ya kumtafuta mpenziwe Mutanu ambaye alikuwa amemwacha.

Angalia kifungu kifuatacho:

*Nauma kwasa nauma kwasa nayu ningwenda katanda ngome.
Nauma kwasa nauma kwasa nayu ningwenda katanda ngome.
Nauma kwasa nauma kwasa nayu ningwenda **katanda** ngome.
Nauma kwasa nauma kwasa nayu ningwenda katanda ngome.
Nauma kwasa, nauma kwasa, nayu ningwenda katanda ngome.
Silikali niyookilya moko umanye musyi wi vinya umanzawa na thina
Mutanu songa Mutanu songa **kana** mwa woneke kana nithasye
mikwa. Silikali niyookilya moko umanye musyi wi vinya umanzawa
na thina Mutanu songa Mutanu songa kana mwa woneke kana
nithasye **mikwa***

Tafsiri

Nimetoka mbali, nimetoka mbali na sasa nataka **kitanda** nilale.
Nimetoka mbali, nimetoka mbali na sasa nataka kitanda nilale.
Nimetoka mbali, nimetoka mbali na sasa nataka kitanda nilale.
Nimetoka, mbali, nimetoka mbali, na sasa nataka kitanda nilale.
Nimetoka mbali, nimetoka mbali na sasa nataka kitanda nilale.
Serikali imeinua mikono ujue familia si rahisi hutafutwa kwa taabu.
Mutanu songa Mutanu songa tafadhali **mtoto** uonekane ama
niifungue **mikwa** (aina ya kamba zilizo pana kuliko kamba za
kawaida).

Katika wimbo huu, hali ya kuanzisha familia inawasilishwa kwa njia ya safari ambapo safari yenyewe huwa ni ndefu, yenye mapito na huhitaji uvumilivu. Hivyo, neno **katanda** limetumika kama ishara ya ndoa. Hii ni baada ya mwimbaji kumpata mpenzi aliye tayari kufunga pingu za maisha. Kupitia kwa jazanda hii, mwimbaji anapitisha itikadi ya ndoa na mapenzi kwamba mtu anapooa au kuolewa anatarajiwa awe na utulivu fulani wa kimaisha. Japo ndoa ina changamoto zake katika kupanda na kushuka, wanandoa huhitajika kuvumiliana. Hii ni sawa na kusema kwamba hakuna

ndoa au mapenzi yasiyokuwa na dosari, ila wahusika huhitajika kuelewana na kuungana ili kukamilishana. Hivyo, wanandoa ndio wanaoidhibiti na kuihimili ndoa yao.

5.1.5 Itikadi kuhusu Ubikira

Ubikira ni hali ya kuwa bikira. Ni ile hali ya kutomjua mwanamume au mwanamke kimwili. Katika jamii ya Wakamba, ubikira ulithaminiwa sana hasa kwa vijana wa kike. Vijana hawa walihimizwa kuutunza ujana wao hadi pale watakapohitimu kuwa mume na mke na kuanzisha ndoa. Hivyo, kutokana na hali hii, wasichana waliopata mimba au kujifungua nje ya ndoa walidharauliwa sana. Iliaminika na inaaminika kwamba ni jukumu la kila kijana kujitunza na kuutunza ubikira hadi pale atakapopata jiko. Hivyo, kwa mujibu wa jamii ya Wakamba, tendo la ndoa linafaa kuhifadhiwa kwa wanandoa pekee. Kama zilivyo itikadi zingine, itikadi ya ubikira imepewa kipau mbele katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Kwa mfano, itikadi ya ubikira inajitokeza katika wimbo **NA. 22. Sikala**. Angalia kifungu kifuatacho:

*Manguleti nikwita ngikwita, ngwititye **sikala** ukambata na ung'endu ngasokota yakwa na ngekia **mwaki** na ngainia uvuta. Manguleti nikwita ngikwita, ngwititye sikala ukambata na ung'endu ngasokota yakwa na ngekia mwaki na ngainia uvuta. Umbatite sikala Manguleti, umbatite niki tukoonana. Umbatite sikala Manguleti, umbatite niki tukoonana. Na teka sikala, ndumiwe **kisevu** kya kwiyonaa ngusisimukye. Na teka sikala, ndumiwe kisevu kya kwiyonaa ngusisimukye. Mwa Susu nde ngui, susu nde ngui aume ii neteelaa e ivungulu. Mwa Susu nde ngui, susu nde ngui aume ii neteelaa e ivungulu.*

Tafsiri

Manguleti nakuita nakuita, nimekuomba **sigara** ukaninyima tu kwa ukaidi, nikaikunja yangu na kuiwasha **moto** nikaanza kuivuta. Manguleti nakuita nakuita, nimekuomba sigara ukaninyima tu kwa ukaidi, nikaikunja yangu na kuiwasha nikaanza kuivuta. Umeninyima sigara Manguleti, umeninyima kwa nini? Tutaonana. Umeninyima sigara Manguleti, umeninyima kwa nini? Tutaonana. Na kando na sigara, nimeshonewa **kisevu** cha kujionea fahari nikusisimue. Na kando na sigara, nimeshonewa kisevu cha kujionea fahari nikusisimue. Nyanya yangu hachezi, nyanya hachezi jamani

nangojea tu. Nyanya yangu hachezi, nyanya hachezi jamani
nangojea tu.

Katika wimbo huu, tunaelezwa namna ambavyo mwimbaji amemwomba msichana *Manguleti* sigara bila mafanikio. Inaelezwa kwamba baada ya kunyimwa *sigara* alitafuta yake akaiwasha na kisha akaanza kuivuta. Anaeleza kwamba sigara yake imeshika *moto*. Sigara iliyowashwa na mhusika inarejelea mkewe. Hivyo, aliponyimwa mahusiano ya kimapenzi na *Manguleti*, alienda kwa mkewe ambaye alimtosheleza mahitaji yake. Hivyo, neno *sigara* limetumika kijazanda kurejelea *tendo la ndoa*. Pia, neno *mwaki* (moto) limetumika kuashiria hisia ya kutaka *kutoshelezwa kimapenzi*. Kwa hivyo, wimbo *Sikala* umewasilishwa kijazanda kurejelea hali ya vijana wa kiume kutaka kuingiliana na wale wa kike kimapenzi. Tukio la *Manguleti* kumnyima mwenzake *sigara* limetumika kuwasilisha itikadi ya ubikira. Hapa, maarifa ya kimsingi yanatuwezesha kutambua kwamba kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wakamba, msichana hafai kujihusisha na tendo la ndoa kabla ya kupata jiko. Hivyo, mwimbaji anawasilisha ujumbe kwamba tendo la ndoa ni la wale walio katika ndoa pekee. Hii ndiyo sababu inayomfanya mhusika wa kike *Manguleti* kumnyima mpenziwe wa kiume uhusiano wa aina hiyo. Vijana wanahimizwa kusalia mabikira hadi pale watakapooa au kuolewa. Hivyo, tendo la ndoa linafaa kuhifadhiwa hadi pale wahusika wawili wa jinsia tofauti watakapohitimu kuwa mume na mke.

Pamoja na hayo, itikadi ya ubikira inawasilishwa kupitia kwenye wimbo **NA. 21.**

Kilyambu. Tazama kifungu hiki:

*Na ngoma nisikukunwa kyama ngwika, ii nisyikukunwa kyama
ngwika, nitatite kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. Yii nisyikukunwa
ya mundu ungi, nitatite kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. nitatite
kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. Nenda ngoma Mutanu akitwawa
yiya nenda kiliko Mutanu yiya nenda kiliko wa Mwangangi. Nenda
ngoma Mutanu akitwawa yiya nenda kiliko Mutanu yiya nenda kiliko*

wa Mwangangi. Mwiitu wa musee, ni museo sana aendaa na ngali. Akithi Ilovi, aendaa na ngali. Akithi Mombasa, aendaa na ngali.

Tafsiri

Na ngoma zitachezwa kama ambavyo ninafanya, ndio zitachezwa kama nifanyavyo, nimejaribu kawayu, ngoma ya chandarua. Ndio zitachezwa ya mtu mwingine, nimejaribu kawayu, ngoma ya chandarua. Nataka ngoma Mutanu akiolewa yiya! Nataka akili Mutanu yiya! Nataka akili wa Mwangangi. Nataka ngoma Mutanu akiolewa yiya! Nataka akili Mutanu yiya! Nataka akili wa Mwangangi. Binti wa mzee ni mzuri sana husafiri kwa gari. Akienda Nairobi, huenda kwa gari. Akienda Mombasa, huenda kwa gari.

Hapa, tunasimuliwa kuhusu kijana Kilyambu ambaye amemchumbia msichana aitwaye Mutanu. Inaelezwa kwamba msichana huyu ni mzuri sana kwa maana yeye husafiri kwa gari kila anapoenda popote. Hivyo, tabia na mienendo ya msichana Mutanu imesimuliwa kwa namna ya safari. Taswira hii inatupa picha halisi ya vijana wanapotembea mitaani. Kwa mfano, kwa wale wasiokuwa na maadili hupata nafasi ya kujihusisha katika mahusiano mabaya kila wanapotembea. Hii ni kwa sababu kila mara wao hupatana na watu waovu walio tayari kuathiri na kuharibu mienendo yao bora. Hivyo, hali ya usafi wa kitabia inasawiriwa kupitia kwa neno gari, ambapo tunaelezwa kuwa Mutanu husafiri kwalo kila mara. Hivyo, msichana huyu hajapata nafasi ya kujinajisi kwa njia yoyote. Kupitia kwa jazanda hii, mwimbaji anapitisha itikadi ya ubikira kwamba vijana wanastahili kuvumilia hadi pale watakapoolewa au kuoia ili wajihusishe na masuala ya tendo la ndoa. Hivyo, kulingana na utamaduni wa jamii ya Wakamba, ni marufuku kwa vijana kujihusisha na tendo la ndoa kabla ya ndoa. Kutokana na maelezo hayo, ubikira ni suala lililotiliwa na linatiliwa maanani sana kwenye jamii ya Wakamba.

5.1.6 Itikadi kuhusu Utamaduni

Utamaduni ni uzoefu wa kimaisha wa watu fulani. Kwa kawaida, neno hili huleta michakato ya kijamii ambayo huiwezesha jamii hiyo kujieleza na kujitambulisha

pamoja na kufanya shughuli za kila siku. Hivyo, utamaduni unarejelea imani, tabia au ufahamu unaopokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Ufahamu huu huyashirikisha makundi ya watu na huhusisha vitu vyote ambavyo ni milki yao kama wahusika wa jamii hiyo. Kwa hivyo, utamaduni huhusisha vitu halisi, mawazo, thamani, mielekeo pamoja na mipangilio ya kitabia katika jamii husika. Hivyo, utamaduni haupitishwi kibayolojia bali hupokezwa kupitia uzoefu wa jamii inayohusika. Kwa hivyo, dhima ya kitamaduni ya nyimbo za kiasili za Kikamba huhusisha uhifadhi na upitishaji wa tamaduni za jamii inayohusika.

Kwa mfano, nyimbo za kiasili za Kikamba ni urithi wa kitamaduni kwenye jamii ya Wakamba. Hivyo, nyimbo zenyewe zina wajibu mkubwa katika ukuzaji wa utamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwenye jamii hii. Nyimbo za kiasili za Kikamba hutokana na msukumo wa nguvu fulani unaowaelekeza wanajamii katika kuufahamu vyema utamaduni wao. Hali hii huhakikisha uhifadhi wa utamaduni huo. Utafiti huu umetambua kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba zimekuwa kama nyenzo ya kueneza utamaduni wa jamii ya Wakamba. Hivyo, nyimbo za kiasili za Kikamba ni nyenzo muhimu inayohusika katika kupitisha itikadi ya utamaduni wa Wakamba kwa wanajami. Kwa mfano, itikadi hii inajitokeza katika wimbo **NA. 11.**

Kithio kya Mukamba (Utamaduni wa Mkamba). Angalia ubeti huu:

*Kithio twatiie kyonze vyu kithio kitu Syokimau letiu, letiu Kaundi, Athiani, Musyi, Kyeni, Mbaitu Mwenge mukilye kililimbi twai na mwathani mwathani wa ukamba **Syokimau** kithio tukituungie Mukamba akuthuka ambiaa kwasya ni musomu ni mutangiie ndyendaa siasa ndyendaa kithio ni mutangiie na usu mundu ukathi umwithie akumiswa mayini malikile ku e mutangiie? Wamwithia Mombasa niwe **Bakari** niwe **Juma Juma** mukamba mwenda ndini syonze Mukamba ndusyoke syoka kithioni umanyiswe undu*

Tafsiri

Utamaduni tuliuaacha wote kabisa utamaduni wetu Syokimau redio, redio Kaundi Athiani, Musyi, Kyeni, Mbaitu Mwenge muinue kiwango. Tulikuwa na nabii nabii wa Ukambani **Syokimau**

tuurejeshe utamaduni. Mkamba akianza kupotoka huanza kwa kusema kwamba nimesoma, nimeokoka sipendi siasa sipendi utamaduni nimeokoka na huyo mtu utampata akitolewa mapepo yaliingilia wapi akiwa ameokoka? Ukimpata Mombasa ndiye **Bakari**, ndiye **Juma**, Juma Mkamba mpenda dini zote Mkamba si urudi rudi kwenye utamaduni ufundishwe jambo

Katika wimbo huu, tunaielezwa kwamba tumeuacha utamaduni na ni muhimu turudi kule tulikouachia. Mwimbaji anaeleza namna ambavyo Wakamba wamekegeuka na kuzibugia dini za kigeni na kisha kuusahau utamaduni wao. Hivyo, mwimbaji anawarai Wakamba wazingatie utamaduni wao kwa maana una umuhimu wake kwa vizazi vijavyo. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anaomba kwamba utamaduni huu ukuzwe na kuendelezwa kupitia kwenye vyombo vya habari vya Ukambani kama vile Musyi FM, Syokimau FM na Kaunti FM miongoni mwa vingine. Anawarai watangazaji kama vile Mwenge wa Musyi FM wachangie katika shughuli hizo za ukuzaji wa utamaduni wa Wakamba. Kwa hivyo, wimbo huu unapitisha itikadi ya utamaduni kwamba ni jambo muhimu linalofaa kuzingatiwa na Wakamba. Vilevile, mwimbaji anazungumzia athari ya majilio ya wageni katika utamaduni wa Wakamba. Kwa mfano, anaeleza kwamba wanajamii Wakamba wameathiriwa na dini za kigeni kiasi kwamba wameuacha utamaduni wao huku wakiupokea utamaduni wa kigeni. Hivyo, mwimbaji husika anaeleza kuwa majilio ya dini zingine hayamaanishi kuwa Wakamba wazitupilie mbali tamaduni zao na kisha kubugia zile za kigeni. Hapa, mwimbaji anaeleza kwamba jamii nyingine kama vile Wapokomo na Wamasai wangali wanashikilia tamaduni zao. Hivyo, maneno *Bakari* na *Juma* ni majina ya kiislamu yaliyotumika kijazanda kurejelea *ukengeushi* unaowakumba Wakamba wakaacha utamaduni wao. Jazanda hizi zimetumika kuupinga ukengeushi ili Wakamba waukumbatie na kuuonea fahari utamaduni wao. Maoni ya mtafiti ni kwamba uzoefu, tabia, vitendo na imani za kitamaduni zilizopitwa na wakati ndizo zinazofaa kutupiliwa mbali. Hivyo, utamaduni unaofaa hauna budi kukuzwa,

kuendelezwa na kuzingatiwa na wanajamii. Van Djik (1998) anaeleza kwamba itikadi imegawanywa katika kategoria mbalimbali. Hivyo, nyenzo ni mojawapo wa kategoria hizo. Kwa hivyo, utamaduni ni nyenzo muhimu kwa Wakamba na hamna budi kuuzingatia..

Pamoja na hayo, imegunduliwa hapa kwamba itikadi ya utamaduni imewasilishwa katika wimbo **NA. 11. Kithio kya Mukamba** (Utamaduni wa Mkamba) kupitia usimulizi wa kihistoria. (Tazama ubeti uliopo hapo juu). Wimbo huu unataja visa na matukio yanayohusishwa na mashujaa wa kitamaduni na kihistoria. Mfano ni kama vile, mwimbaji anasimulia kuhusu mhusika wa kihistoria anayeitwa **Syokimau**. Kwa mujibu wa Kareithi (2012), jina Syokimau linarejelea nabii tajika katika jamii ya Wakamba. Kihistoria, nabii Syokimau alitabiri kuhusu majilio ya wageni (watu weupe) pamoja na ujenzi wa reli na gari moshi katika maeneo ya Afrika.

Katika utabiri wake, inadaiwa kwamba Syokimau aliona nyoka mrefu sana aliyekuwa anatema moto na moshi na ambaye alitambaa kutoka kwenye eneo moja la maji hadi kwenye eneo lingine. Pamoja na hayo, ndani mwake mlitoka watu weupe ambao mazungumzo yao yalikuwa kama sauti za nyuni au ndege. Watu hao walibeba mioto mifukoni mwao, popote walipoenda. Unabii wake ulitimia mnamo karne ya ishirini ambapo ujenzi wa reli ya Uganda- Kenya ulikamilika. Reli hii ilitoka Mombasa hadi Kisumu. Watu aliokuwa anawaona ni wazungu waliozungumza Kiingereza na ambao walibeba viberiti mifukoni mwao. Vilevile, Syokimau alitabiri kuhusu ukoloni. Hapa, aliwaambia wanajamii wenzake kuwa watu hawa weupe wangewapiga sana, wachukue ardhi yao pamoja na kuwalazimisha waache utamaduni na miungu yao huku wakiwalazimisha kumwabudu Mungu wao. Unabii huu ulitimia mnamo mwaka wa 1844 baada ya majilio ya wamishenari kama wale wa Kijerumani Dkt. Ludwig Krapf na Johannes Rebmann nchini Kenya. Hivyo, neno *Syokimau* limetumika

kijazanda kurejelea mashujaa wa kitamaduni na wa kihistoria ambao hawafai kusahaulika kama sehemu ya utamaduni wa Wakamba.

Utafiti huu umetambua kwamba itikadi ya utamaduni imefumbatwa katika wimbo

NA. 27. *Mundu Mwiu e Kiliko* (Mtu mweusi ni mwenye Akili). Angalia kifungu kifuatacho:

*Iyaa iyaa! mundu mwiu e kiliko ui na umanyi ii na kwakya ayukila athekete yaa! niw'o mumbile. Iyaa iyaa! mundu mwiu e kiliko ui na umanyi ii na kwakya ayukila athekete yaa! niw'o mumbile. Umaaluka kaloko na kaniki ka muthemba katumitwe kitene na kwovwa utene. Umaaluka kaloko na **kaniki** ka muthemba katumitwe kitene na kwovwa utene. Niyova lesu uu ta mundu wa tene ula weyovaa kaniki aendete wathini kukuna **mukanda** kwa!kwa!kwa!kwa! Niyova lesu uu ta mundu wa tene ula weyovaa kaniki aendete wathini kukuna mukanda kwa!kwa!kwa!kwa!*

Tafsiri

Iyaa iyaa! mtu mweusi ana akili na maarifa na kunapopambazuka anaamka akicheka yaa! ndiyo maumbile. Iyaa iyaa! mtu mweusi ana akili na maarifa na kunapopambazuka anaamka akicheka yaa! ndiyo maumbile. Utoke asubuhi na mapema ukijifunga **kaniki** (aina ya vazi la kitamaduni) ka aina fulani kalikoshonwa kikale na kufungwa kikale. Nitajifunga lesu hivi kama mtu wa kale aliyejifunga kaniki akielekea kwenye densi kucheza **mukanda** (aina ya ngoma ya kitamaduni iliyochezwa) kwa!kwa!kwa!kwa! Nitajifunga lesu hivi kama mtu wa kale aliyejifunga kaniki akielekea kwenye densi kucheza **mukanda** (aina ya ngoma ya kitamaduni iliyochezwa) kwa!kwa!kwa!kwa!

Katika wimbo uliotajwa hapo juu, mwimbaji anaanza kwa kueleza kwamba mtu mweusi ni mwenye akili na maarifa. Inaelezwa pia kwamba kunapokucha anaamka akicheka na kufurahia na hayo ndiyo maumbile yake. Mwimbaji anaendelea kueleza namna atakavyojiandaa kwa ajili ya kukutana na mpenzi wake aitwaye Mutanu. Anaeleza namna atakavyojifunga *kaniki* (aina ya vazi la kitamaduni) kama mtu wa kale aliyejifunga akielekea kwenye densi ya *mukanda* (aina ya ngoma ya kitamaduni iliyochezwa na kuwaburudisha wanajamii). Hivyo, inaelezwa kwamba mhusika huyu atapendeza sana kwa namna atakavyokuwa amevalia mavazi ya kitamaduni. Kupitia

kwenye wimbo huu, mwimbaji anayasifu mavazi ya kitamaduni kwamba ni ya kupendeza. Hivyo, anayaonea fahari mavazi yenyewe ambapo anadai kwamba atayavaa siku yake muhimu ya kukutana na mpenzi wake. Hivyo, maneno *kaniki* (aina ya vazi la kitamaduni) na *mukanda* (aina ya ngoma ya kitamaduni iliyochezwa ili kuwaburudisha wanajamii) yametumika kijazanda kurejelea *vifaa*, *mavazi* na *mapambo ya kitamaduni*. Kupitia jazanda hizi, mwimbaji anapitisha itikadi ya utamaduni kwamba ni jambo la kuonea fahari. Hivyo, utamaduni ni nyenzo muhimu inayofaa kuenziwa, kukuzwa na kuhifadhiwa.

5.1.7 Itikadi kuhusu Malezi

Malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki. Hivyo, ni mbinu zinazohusishwa katika kuwalea na kuwakuza watoto kutoka kiwango kimoja hadi kingine maishani. Malezi huhusisha ukuzaji na utunzaji wa watoto kimwili, kiafya, kiroho, kiakili, kihisia na hata kijamii miongoni mwa mengine. Kezilahabi (1971) anaeleza kwamba katika utamaduni wa kijadi, ndoa huchukuliwa kuwa imekamilika inapokuwa na watoto na hasa wa kiume ambao huchukuliwa kama nguzo ya kijamii.

Hivyo, katika jamii ya Wakamba, inaaminika kuwa mtoto ni mali ya jamii na kila mwanajamii ana wajibu wake katika kuwakuza watoto wa jamii husika. Hata hivyo, jukumu kubwa la malezi ya mtoto huegemea kwenye wazazi wa mtoto anayehusika. Hivyo, baba na mama wa mtoto wanatarajiwa kuwa karibu naye na kumkuza kwa njia inayofaa. Wazazi wanatarajiwa kumkuza mtoto kwa mujibu wa tamaduni na maadili ya Wakamba. Hata hivyo, inapotokea kwamba wazazi wa mtoto wameaga dunia au hawapo tena, watu wa karibu kiukoo kama vile shangazi, amu, babu na nyanya ndio huliendeleza jukumu hilo.

Utafiti huu umebainisha kwamba itikadi ya malezi imefumbatwa kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Kwa mfano, itikadi ya malezi imewasilishwa kupitia wimbo **NA. 28. Kyathi no Vala** (Miadi ni ileile). Angalia ubeti huu:

*Iyaii yayai! kyathi no vala vala wandavisye wambiie ningoka kuathima mwana ii na **kaindo** ngyuka. Iyaii yayai! kyathi no vala vala wandavisye wambiie ningoka kuathima mwana ii na kaindo ngyuka. Yii mwana ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa mwingi. Yii mwana ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa mwingi. Wa tata ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa mwingi. Wa tata ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa mwingi.*

Tafsiri

Iyaaiii, aiii! miadi ni ile ile, vile ulivyoniambia uliniambia utakuja kumbariki mtoto na **kitu** ukija. Iyaaiii aiii! miadi ni ile ile, vile ulivyoniambia uliniambia nitakuja kumbariki mtoto na kitu nikija. Ee! mtoto nyamaza nikubembeleze, nikubembeleze ulale nina raha nyingi. Ee! mtoto nyamaza nikubembeleze, nikubembeleze ulale nina raha nyingi. Wa baba nyamaza, nikubembeleze, nikubembeleze ulale nina raha nyingi.

Katika wimbo **NA. 28. Kyathi no Vala** (Miadi ni ileile) mwimbaji anaanza kwa kubisha hodi huku akielezea kwamba alikuwa ameahidi kuwa angekuja kumbariki mtoto na *kakitu*. Kwenye jamii ya Wakamba, kuzaliwa kwa mtoto huwa ni ishara ya kuendelea kwa jamii hiyo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mujibu wa utamaduni wa jamii hii, mtoto ni mali ya jamii. Hivyo, mtoto anapozaliwa jamii husherehekea na kumzawadi mama pamoja na mtoto aliyezaliwa. Hali hii huwa ishara ya kuwajibika kijamii kuhusiana na malezi ya mtoto anayehusika. Hivyo, hali hii inaonyesha kwamba jamii pia inapaswa kuwajibika katika malezi ya watoto wa jamii. Hivyo, neno kaindo (*kakitu*) limetumika kijazanda kurejelea zawadi yoyote kwa mtoto anayesherehekewa kuzaliwa kwake. Hivyo, itikadi inayowasilishwa hapa ni ya malezi kwamba watoto ni wa jamii na kila mwanajamii ana jukumu la kuwalea watoto hao.

Tukio la wanajamii la kumtembelea mama na mtoto aliyezaliwa linaashiria upendo na mapenzi yao kwa mtoto ambaye ndiye mwanajamii mgeni. Tukio hili ni njia mojawapo ya kumkaribisha mtoto anayehusika katika jamii. Akizungumzia hoja hii, Boss (1998) anaeleza kwamba watoto hujifunza kupenda na kupendwa katika familia walimozaliwa. Kwa hivyo, Wakamba wanaamini ni vigumu kwa mtu ambaye hakupata kupendwa utotoni mwake kuweza kuonyesha upendo kwa wengine.

Pamoja na hayo, itikadi ya malezi inajitokeza katika wimbo *Na. 29. Inyaa mwana na Ithea mwana* (Mama na baba mtoto). Angalia sehemu ifuatayo ya wimbo huu:

*Kasilisili mwana ii inyaa mwana nukumbenda inyaa mwana akusye ikanda nakwa ainenga ngusye kwata mukwa ulumitye ndukandekye nimandane. Kasilisili mwana ii inyaa mwana nukumbenda inyaa mwana akusye **ikanda** nakwa ainenga ngusye kwata **mukwa** ulumitye ndukandekye nimandane.*

Tafsiri

Kasilisili mwana ii mama mtoto ee mama mtoto ananihitaji, mama mtoto avute **kamba** na kisha anipe nivute shika **kamba pana** vizuri usiniachilie nianguke. Kasilisili mwana ii mama mtoto ee mama mtoto ananihitaji, mama mtoto avute kamba na kisha anipe nivute shika mukwa vizuri usiniachilie nianguke.

Kupitia kwa wimbo uliotajwa hapo juu, mwimbaji anaanza kwa kubisha hodi na kisha anasimulia mazingira ya kuzaliwa kwa mtoto. Hivyo, anaeleza namna ambavyo wakunga humsaidia mama anapojifungua. Kwa kawaida, *kamba pana* hutumika katika shughuli hiyo ambapo kuna namna fulani kamba hiyo hushikiliwa na mkunga pamoja na mama anayejifungua. Hapa, mwimbaji anaeleza hatari iliyopo katika shughuli ya kujifungua. Hivyo, mwimbaji anaeleza kuwa kamba husika isiposhikwa kwa uangalifu huenda mkunga, mama au mtoto anayezaliwa akaanguka. Hivyo, jazanda ya **mukwa** (Kamba pana) imetumika katika kuendeleza itikadi ya uzazi na malezi kwamba mzazi na hasa mama huyahatarisha maisha yake ili mtoto apatikane.

Hivyo, mzazi hana budi kuwa na **ustahimilivu** na uangalifu mkubwa katika uzazi na malezi ya watoto katika jamii.

Hivyo, iwapo ameweza kustahimili uchungu huo wa kujifungua, hana budi kujitahidi katika malezi pia. Vilevile, hali ya wanajamii kumtembelea mama mzazi ni ishara kwamba malezi ya mtoto yanashirikisha wanajamii wote. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa utamaduni wa Wakamba, mtoto ni mali ya jamii na hivyo jamii yenyewe ina wajibu wake kwenye malezi ya mtoto anayehusika.

5.1.8 Itikadi kuhusu Siasa na Uongozi

Siasa ni mtazamo unaofuatwa na kundi au jamii fulani ambao ni msingi wa kuendesha uchumi, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya jamii hiyo. Hivyo, siasa ni matukio yote yanayohusiana na utawala au uongozi wa nchi au eneo fulani. Matukio haya pia hushirikisha mijadala inayohusiana na uwezo wa vyama vya kisiasa. Pia, dhana hii ya siasa inarejelea mpango wa matukio yanayohusiana na kufanya maamuzi ya kimamlaka katika makundi fulani ya watu. Uongozi nao ni hali ya kuwa na mamlaka juu ya nchi, sehemu ya nchi au maisha ya watu katika jamii fulani. Kwa mujibu wa utafiti huu, itikadi ya siasa na uongozi inadhihirika kwa njia mbalimbali katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Kwa mfano, **NA. 7. Nzambi akithambya Nzele** (Nzambi akiosha Kata) ni wimbo unaopitisha itikadi ya siasa na uongozi. Tazama kifungu kifuatacho:

Nzambi akithambya nzele ii ya kuthamba ii we wimwia ii undu uu ni waki? Nzambi akithambya nzele. Nzambi akithambya nzele ii ya kuthamba ii we wimwia ii undu uu ni waki? Nzambi akithambya nzele. Ekai umwia ii wa Katuta ii, Nzambi akithambya nzele. Ndanaumyai mundu uu Katuta? Nzambi akithambya nzele. Ekai ukulya ii ai kuyi na mbua ii niki? Nzambi akithambya nzele. Mukulasya ii mundu uu watata ii Nzambi akithambya nzele.

Tafsiri

Nzambi akiosha **kata** ya kuogea ee wewe unamwambia eti hivi ni kwa nini? Nzambi akiosha kata. Nzambi akiosha kata ya kuoga ee wewe unamwambia eti hivi ni kwa nini? Nzambi akiosha kata. Wacheni kumwambia ee eti wa Katuta, Nzambi akiosha kata. Hajaitoa ewe mtu wa Katuta, Nzambi akiosha nzele. Wacheni kuuliza eti na hakuna mvua kwa nini? Nzambi akiosha kata. Mnauliza mtu huyu mtoto wa babangu, Nzambi akiosha kata.

Katika wimbo huu, mwimbaji anatuchorea picha ya mhusika Nzambi anayeosha kata.

Katika hali ya kuiosha kata, tunaeleza kuhusu watu wanaonung'unika na kusemezana kwamba mhusika Nzambi anaharibu wakati, maji hayatoshi na mambo mengine kama hayo. Hivyo, mwimbaji anawauliza kwa nini wanung'unike? Mwimbaji anawataka wampe mhusika nafasi ili aifanye na kuikamilisha kazi yake vizuri.

Mtafiti anatambua kwamba itikadi ya siasa na uongozi imepitishwa kwenye wimbo huu kijazanda. Kwa mfano, taswira ya *uoshwaji wa kata* inayosawiriwa hapa imetumika kijazanda ili kurejelea hali ya *kuuondoa ufisadi* uliotekelezwa na viongozi tawala tangulizi. Hivyo, mwimbaji anawarai wasikilizaji wampe muda kiongozi mpya na kisha kazi yake itaonekana kwa mujibu wa wakati. Mwimbaji anaitaka hadhira iache kulalamika kwamba kiongozi mpya hajafanya kazi waliyoitarajia. Hivyo, wimbo wenyewe unawasilisha itikadi ya siasa na uongozi kwamba viongozi wanafaa kujiepusha na ufisadi katika shughuli zao za uongozi. Vilevile, inabainika kwamba uongozi imara unahitajika katika jamii. Hata hivyo, hadhira inafahamishwa kwamba uongozi imara unahitaji uvumilivu wa hali ya juu pamoja na busara isiyokuwa na kifani. Kwa hivyo, neno *kata inayooshwa* limetumika kijazanda ambamo itikadi ya siasa na uongozi imefumbatwa.

Vilevile, itikadi ya siasa na uongozi inajitokeza katika wimbo *Na. 8. Munuve*. Angalia kifungu kifuatacho:

*Munuve tata ii manya ukia kindu **simba** ii syi ngunyu nitwasyelile.
 Munuve tata ii manya ukia kindu **simba** ii syi ngunyu nitwasyelile.
 Munuve tata ii manya ukia kindu **simba** ii syi ngunyu nitwasyelile.
 Munuve tata ii manya ukia kindu **simba** ii syi ngunyu nitwasyelile.*

Tafsiri

Munuve baba, ee usiogope chochote **simba wenye makucha** tushayakatakata. Munuve baba, ee usiogope chochote **simba wenye makucha** tushayakatakata. Munuve baba, ee usiogope chochote **simba wenye makucha** tushayakatakata.

Mwimbaji anaanza kwa kumweleza mhusika Munuve kuwa asiwe na hofu bali aingie kwenye kinyang'anyiro cha kupigania ubunge. Anaendelea kumweleza Munuve kwamba asiwaogope wale **simba wenye makucha** kwa maana wao (raia) wameshayakatakata makucha hayo. Hivyo, neno *simba wenye makucha* hapa limetumika kijazanda kuashiria *wanasiasa wafisadi*. Hivyo, anaposema kwamba wameshayakatakata makucha hayo, anarejelea hali ya kuutambua uongo, ujanja na ufisadi wao pamoja na kutokuwa tayari kuwapigia kura wanasiasa hao. Mwimbaji anaweka wazi uovu wa viongozi waliotangulia huku akiwaonya wanajamii kwamba wasirudie makosa ya kuwateua viongozi wa aina hiyo. Hali hii inaafikiana na maelezo ya Eagleton (1991) kwamba ung'amuzi wa uongo unafaa kuwekwa wazi ili wanajamii husika wajitambue na kisha kujinasua kutokana na unyanyasaji unaotekelezwa na tabaka tawala. Kutokana na maelezo hayo, jazanda ya *simba ii syi ngunyu (simba wenye makucha)* imetumika katika kuwasilisha itikadi ya kisiasa kwamba uongo na ulaghai wa wanasiasa una mwisho, yaani njia ya mwongo ni fupi. Hivi ni sawa na kusema kwamba wanajamii wanafaa kujiepusha na kuwapigia kura viongozi wabaya, fisadi na walaghai. Wanajamii wanahimizwa kuzingatia uadilifu wa viongozi wanapofanya maamuzi ya watakaowapigia kura.

Itikadi ya siasa na uongozi inadhihirika katika wimbo **NA. 9. Usumbi ni Nzou** (Urais ni ndovu). Tazama kifungu kifuatacho:

Usumbi aume ni nzou na nzou ngiti ikwamba uu ndithengeeleka isu kila mundu ndove syake na mukuthi Mwambasa Muthama mukevingie. Muvisi ava ndikwona vandu mutathi nzi ino mwina Nduya Muthama kwaambiia a ve Musila, Kiema nginya Charity. Andu onthe matungianiwe ndokta Malombe twambe kumbania mbai Kivutha evo Kivwana Musimba e vau vau na unyuvani wavika ungamya ula ukwenda na ndukaume asu angi. Mundu umwe atwike ngavana kitanda ndukilisya aume eli me vamwe.

Tafsiri

Jamani urais ni ndovu na huwezi kumkaribia ndovu mbwa wakibweka hivyo. Hao, kila mtu afunge wake. Halafu Muthama mwende Mombasa mjifungie. Muvisi sioni popote hamwezi kwenda nchini mkiwa na Nduya Muthama. Kuanzia alipo Musila, Kiema hata Charity watu wote waunganishwe Daktari Malombe. Tuanze kwa kuikusanya jamii ya Mkamba Kivutha akiwepo Kivwana. Musimba akiwa hapo hapo na uchaguzi ukifika simamisha yule unataka na usiwatusi wale wengine. Mtu mmoja awe gavana haupandishi wanaume wawili kwenye kitanda kimoja.

Katika wimbo huu, mwimbaji anaeleza kwamba urais ni ndovu. Hapa, tunasawiriwa hali ya mawindo ya ndovu ambapo kelele za mbwa hazihitajiki. Inaelezwa namna mawindo ya ndovu yalivyo tofauti na ya wanyama wengine. Kupitia wimbo huu, viongozi wanaombwa kuwafunga mbwa wao kwa maana hawahitajiki kwenye mawindo. Vilevile, katika wimbo husika, viongozi wa kisiasa Wakamba wanaombwa wapange mkutano wao peke yao ambapo watahakikisha kuungana na kuwa na utangamano miongoni mwao.

Kutokana na muhtasari wa wimbo wa *Usumbi ni Nzou (Urais ni Ndovu)*, itikadi ya siasa na uongozi inajitokeza kijazanda. Hivyo, itikadi yenyewe imefumbatwa kwenye jazanda mbalimbali ambazo zimetumika. Kwa mfano, mwimbaji anaumithilisha utafutaji wa cheo cha urais na uwindaji wa ndovu. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji analitumia neno *nzou* (ndovu) kijazanda kurejelea cheo cha urais. Mwimbaji anaonyesha imani na mielekeo inayowaongoza wanasiasa na wanajamii Wakamba hasa kuhusiana na siasa na uongozi. Kupitia wimbo huu, mwimbaji anatusawiria muktadha wa uwindaji katika jamii husika. Katika jamii hii, mara nyingi

wawindaji huambatana na mbwa wao mawindoni ili kuwasaidia katika shughuli husika. Kulingana naye, wawindaji huwawinda wanyama wa aina mbalimbali. Hata hivyo, mwimbaji anaeleza kwamba kila mnyama huwindwa kwa namna tofauti. Kwa mfano, mwimbaji huyu anaeleza kwamba unapomwinda ndovu, huna budi kumnyemelea ipasavyo. Anaeleza kwamba uwindaji wa ndovu hahuhitaji ushirikishaji wa kelele za mbwa bali wawindaji wanahitajika kumnyemelea kiumakinifu na kwa uangalifu mkubwa ili waweze kumnasa.

Katika wimbo huu, tunaelezwa namna wanasiasa Wakamba walivyogawanyika katika makundi ambapo hawawezi kumuunga mkono mmoja wao katika shughuli za uwanjaji urais. Hali hii inadhihirisha yaliyozungumziwa na Karl Marx kwamba kwenye uongozi wa kibepari, tabaka la juu hutumia sheria ya ‘gawanya na kisha utawale’ ili kuendeleza shughuli zake za kidhuluma miongoni mwa wanajamii. Hali hii basi ndiyo inayojitokeza kwenye viongozi wa kisiasa Wakamba. Wamegawanywa kupitia siasa na imani potovu. Mwimbaji anasisitiza imani ya Wakamba kwamba kidole kimoja hakiui chawa na hivyo kuna umuhimu wa kuungana.

Hivyo, *kelele za mbwa* hapa ni jazanda inayorejelea *upinzani miongoni mwa wanasiasa Wakamba*, yaani kupingana wenyewe kwa wenyewe. Kupitia kwa jazanda hizi, mwimbaji anapitisha imani yake na ya jamii yake kuwa umoja ni nguvu ila utengano ni udhaifu. Hivi ni sawa na kusema kwamba mwimbaji anasisitiza umoja, muungano na utangamano kati ya viongozi wa kisiasa Wakamba. Hii ni kwa sababu Wakamba wanaamini kuwa iwapo hawawezi kuungana na kusaidiana wao wenyewe, itakuwa vigumu jamii nyingine kuwaunga mkono katika matamano yao ya kisiasa. Yaani, ili mwanasiasa Wakamba afaulu kuwa rais wa nchi, wanasiasa Wakamba hawana budi kumuunga mkono ndiposa wanajamii nyingine wawe na imani naye.

Hivyo, wanasiasa wanaowania nyadhifa mbalimbali za kiuongozi wanahimizwa kuzingatia maadili, umakinifu na ukakamavu katika shughuli zao.

5.1.9 Itikadi kuhusu Utambulisho

Utambulisho ni maelezo ya kutambulisha. Ni ule ukweli wa jinsi kitu au mtu alivyo, yaani yeye ni nani au ni nini. Utambulisho ni zile sifa na imani inayomtofautisha mtu au kundi la watu na wengine katika jamii. Utambulisho ni sifa zinazotumiwa na watu katika kujihusisha na wengine huku wakizitumia sifa hizohizo kujitofautisha na wenzao. Ni ile hali au mienendo inayokibainisha kitu au mtu fulani. Hivyo, utambulisho wa mtu unadhihirika kupitia sifa, imani, tabia, hulka, mwonekano au hata namna anavyojiwasilisha. Utambulisho wa mtu unaweza kuwa wa kisaikolojia, kijinsia, kitaifa kitamaduni au hata kijamii. Kutokana na maelezo hayo, utambulisho wa kijamii basi unahusisha zile sifa zinazowafanya watu waungane pamoja na wale wanaoishi ndani ya mipaka ya jamii yao au wajitofautishe na wengine wanaoishi nje ya mipaka ya jamii yao. Nyimbo za kiasili za Kikamba zimekuwa njia moja ya kuukuza na kuudumisha utambulisho wa jamii ya Wakamba. Kwanza kabisa, lugha ya nyimbo hizi huwa kama mpaka unaowekwa kati ya wanaoielewa na wale wasioielewa. Hivyo, ujumbe na uwasilishaji husika huwa umekusudiwa kundi la jamii inayoielewa lugha hiyo. Hivyo, wanakikundi hao hujitambulisha na lugha na jamii hiyo ya Wakamba. Kwa hivyo, kupitia kwa nyimbo za kiasili za Kikamba wanajamii husika huupata utambulisho wa aina fulani. Hii ni kwa sababu, nyimbo hizi huwatofautisha wanajamii na wanajamii wengine wenye kiwango, umri na pengine hali sawa. Kwa kutumia nyimbo za kiasili za Kikamba, tunaweza kuwarejelea watu hawa kwa urahisi tunapozungumza. Hivyo, nyimbo zenyewe huwa kama alama ya utambulisho miongoni mwa wanajamii husika.

Vilevile, nyimbo za kiasili hazijaachwa nyuma katika kuiwasilisha itikadi ya utambulisho. Kwa mfano, katika wimbo **NA. 13. Kikamba ni kyakwa** (Kikamba ni Lugha yangu), mwimbaji anaonea fahari lugha ya Kikamba huku akidai kwamba hiyo ni lugha yake. Hivyo, anaeleza kwamba lugha ya Kikamba anayoitumia ni ya kimaumbo na si kila mtu anaweza kuielewa. Hapa, mwimbaji anatumia neno *ninachoimba* kijazanda kurejelea ufumbaji uliomo kwenye lugha anayoitumia. Hivyo, mwimbaji anajitambulisha na lugha yake ya Kikamba inayotumiwa na wanajamii Wakamba. Kwa hivyo, itikadi ya utambulisho inadhahirika hapa ambapo wanajamii husika wanahimizwa kuonea fahari lugha yao kwa maana ni sehemu ya utambulisho wao. Hapa, anaeleza umuhimu wa kuifahamu lugha husika ambapo lugha hiyo huwapa wahusika wa jamii hiyo utambulisho fulani. Utambulisho huo ndio unaowatofautisha na wahusika wa jamii nyingine. Tazama kifungu kifuatacho:

*Kikamba kyoomie kyoomie ona tene ona ila kwai nguano teka syathelile aka nimo meesi ndia syikwo mwita. Mundu tyuu mwanake niwauka na ndesi auka utee wa muunda kumanza ki? Ukethia kula ii syiitwa kiitene ii undu ungi syetaw'a kuu ni aa Manandu na Mwangu wa Ivuti **nguano** Kikamba ala maivita metitye kwitya mutino utevo ni andu anini **kila ninaa** ki mwalyuli walyula kii nake e muthinzio wa ngili ili*

Tafsiri

Kikamba kimekuwa kigumu hata kitambo kulipokuwa na uchumba ni vile uliisha tu, wanawake ndio walijua kuwa wapo wajinga wengi. Mtu ni huyu mtanashati amekuja na hajui amekuja kando ya shamba kufanya nini? Ingekuwa kwamba kura hizi zinaitishwa kama kitambo ee kama zilivyoitishwa huku na akina Manandu na akina Mwangu wa Ivuti **uchumba** Kikamba wanaoweza kuzipita wakiwa wameziomba pasi bahati mbaya ni watu wachache. **Ninachoimba (Kikamba)** kinahitaji mfasiri, mfasiri awezaye kufasiri hiki ana zawadi ya elfu mbili

5.1.10 Itikadi kuhusu Mauti

Mauti ni hali ya kumfanya kiumbe kukosa uhai. Ni ile hali ya kuishiwa au kuondokewa na uhai hapa duniani. Hivyo, itikadi ya mauti inahusu imani, mielekeo

na mawazo ya wanajamii kuhusiana na mauti. Utafiti huu umetambua kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba zimekuwa katika msitari wa mbele katika uwasilishaji wa itikadi ya mauti. Kwa mfano, katika wimbo **NA. 18. Mathiko Kyunduani** (Mazishi Kyunduani) mwimbaji anasimulia kuhusu kifo cha mhusika mwanasiasa Kalembe Ndile. Angalia sehemu ifuatayo ya wimbo huo:

*Andu asu mwi Kivwese, Mutito wa Ndei Maamba mwi kuu mwii ma Makindu nimwasya ndongosya Mundu wisikie muno. Nimutavya nguma ti mbesa Ndile Kalembe niwathi uthumua Kyunduani Akamba ala me nguma mundu yake mbene Keka **kivila** mundu kusakuuwa vatiele andu ana Kalembe atevo*

Tafsiri

Enyi watu wa Kibwezi, Mtito Andei, Maamba na popote mlipo watu wa Makindu mmempoteza kiongozi mtu maarufu sana nawaambia umaarufu si pesa Ndile Kalembe ameenda kupumzika Kyunduani Wakamba walio na umaarufu wao binafsi Kando na **cheo** mtu kuchaguliwa wamebaki watu wanne bila kumhesabu Kalembe.

Kupitia wimbo uliotajwa hapo juu, mwimbaji anaeleza namna mauti huwanyanganya watu wapendwa wao. Hapa, mwimbaji anammiminia sifa mwendazake ambapo anaeleza kwamba jamii husika imempoteza kiongozi wa maana na mashuhuri. Vilevile, inaelezwa hapa kwamba mwendazake ameenda kupumzika kwao Kyunduani. Mojawapo wa maumbo ya itikadi ni mielekeo. Kwa hivyo, kupitia wimbo huu tunapata mielekeo mbalimbali inayoijenga itikadi ya mauti katika jamii ya Wakamba. Kwanza kabisa, mauti inachukuliwa kama namna ya kupumzika. Inaaminika kwamba duniani kuna shida na matatizo ya kila aina. Hivyo, mtu anapoaga dunia huwa ni njia mojawapo ya kupumzika. Katika hafla za matanga, wanajamii huwafariji waliofiwa kwa kuwaeleza kwamba mpendwa wao amepumzika na hivyo yupo kwenye pahali pema zaidi ya walioachwa. Vilevile, katika wimbo uliopo hapo juu, tunaelezwa kwamba jamii imempoteza kiongozi mwema. Mauti inaeleweka kama namna ya kumpoteza mpendwa aliyeiaga dunia. Inaaminika mtu

anapoaga dunia ni sawa na kupotea. Hii ni kwa sababu mwenzake harudi tena ulimwenguni wa walio hai akiwa kwenye umbo lake la kimaumbile. Hivyo, kwenye wimbo huu, *kifo* kinalinganishwa na *upotezaji* na *mapumziko* kijazanda. Jazanda zenyewe zimetumika katika kuifumbata itikadi ya mauti. Hata hivyo, kwenye jamii ya Wakamba inaaminika kwamba yapo maisha mengine baada ya hapa duniani. Hii ndio maana zipo dhana za *aimu* (miungu na roho za mababu walioaga dunia). Hivyo, Wakamba huhakikisha kuwa wamewapumzisha wapendwa wao kwa amani. Vilevile, iwapo mwenzake alipendekeza masharti fulani alipokuwa hai, wao huzingatia kuyatimiza. Hivyo, haya yote ni kutokana na imani kwamba wasipoyazingatia huenda wakamkasirisha mwenzake ambapo huishia kutopumzika kwa amani. Hivyo, anapokosa kupumzika kwa amani anakuwa roho wa kurandaranda ambaye ni hatari kwa wanajamii walio hai. Hata hivyo, Imani hizi zimeathiriwa na dini ya Kikristo katika jamii hii ambapo wanaamini kuwa kuna maisha baada ya kifo, ambapo hatima ya mtu hutegemea uhusiano wake na Muumba wake alipokuwa hai.

Katika wimbo **NA. 19.** *Kikw'u ni Musyimi* (Kifo ni Mwindaji) tunapata itikadi ya inayohusiana na mauti. Jazanda *Musyimi ute tei* (Mwindaji asiye na huruma) na *Muvutani ute tei* (Mwizi asiye na huruma). Jazanda hizi zimetumika katika kufafanua maana ya kifo ambapo kinalinganishwa na mnyang'anyi na mwizi asiyekuwa na huruma. Jazanda hizi zinawasilisha uchungu wanaohisi wafiwa baada ya kuachwa na mpendwa wao. Hivyo, kifo ni namna ya kuwatenga na kuwanyang'anya wanajamii wapendwa wao.

Pamoja na hayo, itikadi kuhusiana na mauti imejitokeza katika wimbo **NA. 14.** *Katiba Muuo wa Ndee* (Katiba Amani ya Maeneo ya Mipakani). Hapa, mwimbaji anasimulia matukio ya kihistoria yaliyotokea kwenye maeneo ya mpakani kati ya Wakamba na jamii jirani ya Wasomali. Kupitia kwa wimbo huu, mwimbaji anasimulia namna

Wakamba walivyouawa na Wasomali mashfta waliowashambulia. Inaelezwa hapa kwamba baadhi yao waliuliwa kinyama kama vile kuangamizwa na moto pamoja na familia zao. Hivyo, mwimbaji anawalilia wahusika huku akiomba suluhisho lipatikane ili amani irejee kwenye maeneo ya mipakani.

Kutokana na nyimbo hizi, imedhihirika kwamba jamii ya Wakamba huchukulia mauti kama njia ya utengano kati ya mhusika aliyeaga dunia na wapendwa wake walio hai. Katika jamii ya Wakamba, mauti huwa miongoni mwa mambo mazito wanayokabiliana nayo katika safari ya maisha yao. Hata hivyo, Wakamba huamini kwamba mauti sio mwisho wa maisha kwani wao hushikilia imani kwamba kuna wakati watakapokutana na wale waliowatangulia kwenye ulimwengu mwingine. Hivyo, imani hii ndiyo huwapa wafiwa faraja kwa kujua kwamba huo sio mwisho wao wa kupatana na mpendwa wao, bali kuna matumaini ya kukutana tena. Vilevile, kabla ya majilio ya imani za kigeni, Wakamba waliamini kuwa mtu anapoiaga dunia huwa hajafa bali yeye huungana na roho za mababu walioaga dunia ambapo wao huishi miongoni mwao tu.

5.1.11 Itikadi kuhusu Ufisadi

Ufisadi ni tendo la kuleta maovu au uharibifu katika jamii. Ni uovu wa aina yoyote unaofanywa katika jamii. Kwa mujibu wa utafiti huu, nyimbo za kiasili za Kikamba hazijaachwa nyuma kuhusiana na itikadi ya ufisadi. Kwa mfano, katika wimbo kama vile **NA. 15. *Muvisi ungi*** (Kijana mwingine) mwimbaji analitumia neno **ng'ombe sya mutavo** (ng'ombe wa wizi) kijazanda kurejelea ufisadi unaoendelezwa na baadhi ya wanajamii ili kujinufaisha wenyewe. Maumbo ya muktadha ni kipengee muhimu cha kiitikadi. Hivyo, kwenye muktadha wa kihistoria katika jamii ya Wakamba, kulikuwepo na vita vya uviziaji kati yao na jamii jirani za Kisomali. Katika kipindi cha muda mrefu, hali hii imekuwa ikijitokeza mara kwa mara ambapo wao huvamiana

na kuibiana mifugo kimabavu. Hivyo, ni katika hali hii ambapo mwimbaji anasema kwamba ng'ombe waliopatikana kwa njia hiyo hawawezi kuwafaidi wale waliowaiba. Kulingana naye, hii ni kwa sababu inawezekana kwamba watakuja wezi wengine watakaoiba ng'ombe haohao kutoka kwa mwizi wa kwanza. Hivyo, mwimbaji amelitumia neno *ng'ombe wa wizi* katika muktadha huu kama ishara inayorejelea *mali ya ufisadi na wizi*. Akizungumzia hoja hii, anaeleza kwamba kiongozi yeyote asifurahie uongozi anaoupata kwa njia ya ulaghai kama vile kuwahonga wapigaji kura. Kitendo cha mtu kujipatia kipato kisichokuwa halali yake ni ufisadi pia. Hivyo, ufisadi hauna faida bali hukwamisha maendeleo. Viongozi wanashauriwa kuwa wapigaji kura haohao watahonga na wengine ambapo hatimaye watanyang'anywa uongozi huo kwa njia hiyohiyo. Angalia sehemu ifuatayo ya wimbo **NA. 15**.

Ng'ombe ii sya mutavo syendaa nongi Wavena mundu kiveti na mbesa Umany ukakivenwa uu Sya mutavo syendaa nongi Ng'ombe sya mutavo syendaa nongi Ng'ombe syataviwe usumali Ikaetwe ukamba Isu ng'ombe sikesiwa nangi Sya mutavo syendaa nongi Kitheka wosie utuvite chifu na ngusi Ukaiva kikaung'endye Kithitu kikaingwa Uminiwa andu vyu Kivila wosie uivite andu kuiva kuiva ii Makaivwa nangi nokwikwa o ta Mwau Sya mutavo syendaa nongi.

Tafsiri

Ng'ombe hawa wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia. Ukimnyang'anya mtu mkewe kwa pesa Ujue nawe utanyang'anywa vivyo hivyo wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia **Ng'ombe wa wizi** hutoroshwa kwa wizi pia Ng'ombe walioibiwa Somalia wakaletwa Ukambani hao ng'ombe watakujiwa na wengine wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia Ardhi uliyomiliki kwa kuwahonga chifu na mashahidi Utailipia usiionee kiburi tambiko la 'Kuinga Kithitu' likifanywa wanafamilia wako wataangamia wote cheo ulichokipata kwa kuwalipa watu vilivyo watalipwa na wengine na ufanyiwe kama Mwau wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia.

Kutokana na kifungu kilichopo hapo juu, matukio ya kiufisadi husababisha hasara tupu kwa wanaohusika. Hivyo, mwimbaji husika anashikilia kwamba mwanaume anayemnyang'anya mwenzake mke kutokana na uwezo wake wa kifedha, atafanyiwa vivyo hivyo na mwanaume mwingine atakayekuwa na uwezo mkubwa wa kifedha

zaidi yake. Vivyo hivyo, kwa mtu anayemhonga chifu na mashahidi ili amnyang'anye mwenzake sehemu ya ardhi, atakuja kufanyiwa vivyo hivyo. Hivyo, ujumbe unaowasilishwa hapa ni kwamba apandacho mtu ndicho atakachovuna, yaani ukiwadhulumu wenzako pia nawe utadhulumuwa. Aidha, Wakamba huamini kwamba malipo ya lolote mtu afanyalo ni hapa hapa duniani. Hivyo, ukitenda mema utavuna mema na ukitenda mabaya utavuna mabaya hapa hapa duniani.

Kupitia wimbo **NA. 38. Tingilingili**, mwimbaji anaeleza kuhusu ng'ombe wa babake wanaoibwa usiku na wanajamii Wamaasai. Hapa, mwimbaji anapitisha ujumbe kwamba ng'ombe wanaopatikana kwa njia ya wizi pia hupotea kwa njia hiyo hiyo. Hivyo, itikadi ya ufisadi imefumbatwa kupitia jazanda ya *ng'ombe wa wizi kurejelea mali ya wizi*. Hivyo, mwimbaji anawasilisha msimamo wa Wakamba kwamba ufisadi haufaidi na kwamba apandacho mtu ndicho atakachovuna, kiwe kizuri au kibaya.

Itikadi ya ufisadi inajitokeza kwenye wimbo *Na. 14. Kativa muuo wa Ndee* (Katiba Amani ya Maeneo ya Mipakani). Angalia sehemu ifuatayo ya wimbo huo:

*Mwanaa Mweu Mwikya niwe wi thayu andu ala ma tene vyu maendie mbunge Vuti ndamanya undu wa mashifta Kisini ndukile Twalyulanie **uta uu** Kula kwi ii mbee **uta** tuvindue Mwikya niwisi undu wa mashifta Kisini ndukile wa Mwatha nenda withiwe wa kamitii kau kativa ikusenzwa kundu kula muuo utaakwatikana itheka sya ndee kundu kuu miao isenzwe undu ungi na ti kuu kwitu ni Kenya yonze itheka ii syi ndee ii syenda miao isenzwe undu ungi isu ya ukoloni nditutethasya twaitye mathayu ma andu maitu maingi teka na kuu kuasa o vaa Muniyithya wa Mwinzi woowailwe*

Tafsiri

Watu wa zamani sana walioenda mbungeni mwana wa Mweu Mwikya ni wewe uko hai Vuti hawezi kujua kuhusu mashifta Kisini amka uende kwa gavana tugeuze **huu uta** kulikokuwa mbele, tugeuze **uta** Mwikya unajua kuhusu mashifta Kisini amka wa Mwatha nataka uwe mwanakamati hiyo Katiba ikibadilishwa maeneo ambamo amani haikupatikana maeneo ya mipakani maeneo haya sheria zibadilishwe kwa namna nyingine na si huku kwetu tu, ni Kenya nzima. Maeneo haya yaliyo mipakani yanahitaji sheria zibadilishwe kwa namna nyingine sheria hizi za nyakati za ukoloni

hazitusaidii. Tumepoteza nafsi za watu wengi kando na huko nyuma sana kipindi hiki tu ambapo Munyithya wa Mwinzi aliuliwa.

Inadhihirika kwamba wizi wa mifugo na vita vinavyojitokeza katika maeneo ya mipakani mara kwa mara ni ufisadi mkubwa. Mwimbaji anasimulia namna ufisadi huo umesababisha uharibifu mkubwa miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, inaelezwa kwamba maafa kama vile mauti, huzuni, umaskini ni miongoni mwa matokeo ya ufisadi. Hivyo, mwimbaji anavikashifu vitendo vya ufisadi ambapo wanajamii wanahimizwa kuwa waadilifu. Hivyo, wanajamii Wakamba wanaamini kwamba uadilifu ndio njia pekee ya kuepukana na ufisadi. Vilevile, inapendekezwa kwamba sharia za nchi zibadilishwe na kuundwa zile zitakazoshughulikia wanajamii waliomo kwenye maeneo ya mipakani. Hivyo, neno *uta* limetumika kijazanda kurejelea *katiba* inayohitaji mabadiliko. Hivyo, mwimbaji ana imani kwamba sharia ndiyo njia itakayowanasua kutokana na tatizo wanalokumbana nalo la kiufisadi.

5.2 Hitimisho

Sura hii imehakiki itikadi zilizofumbatwa kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Imebainika kuwa nyimbo za kiasili za Kikamba zilizochunguzwa zinasheheni jazanda ambazo zinafumbata itikadi za Wakamba kuhusiana na masuala ya tohara, kazi, dini, mauti, ndoa na mapenzi, ubikira, utamaduni, malezi, siasa na uongozi. Mbali na kuwasilisha itikadi mahsusi, jazanda pia hutekeleza dhima za kifani katika tungo za kifasihi. Katika sura inayofuata, uamilifu wa jazanda kifani na kimaudhui katika nyimbo za kiasili za Kikamba unatathminiwa.

SURA YA SITA

UAMILIFU WA JAZANDA KIFANI NA KIMAUDHUI KWENYE NYIMBO ZA KIASILI ZA KIKAMBA

6.0 Utangulizi

Sura hii inatimiza lengo la tatu la utafiti huu. Lengo lenyewe linahusiana na tathmini ya uamilifu wa jazanda mahsusi kifani na kimaudhui katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Tathmini ya jazanda imeongozwa na nadharia ya Jazanda Dhanifu. Nadharia hii inaichukulia jazanda kuwa kipengee muhimu cha lugha na ambacho hutekeleza kazi maalum katika matini za kifasihi. Nadharia hii inadai kwamba jazanda ni mchakato wa kiakili ambao kwake dhana moja hueleweka kwa misingi ya dhana nyingine. Kwa msingi huu sura hii inachanganua uamilifu wa jazanda mbalimbali kifani na kimaudhui katika nyimbo za kiasili za Kikamba.

6.1 Uamilifu wa Jazanda Mahsusi Kifani na Kimaudhui kwenye Nyimbo za Kiasili za Kikamba

Fani ni ufundi wa kisanaa katika kazi ya fasihi. Ni mbinu za kiufundi zinazotumiwa na mtunzi kuwasilisha masuala fulani kupitia kwenye kazi yake ya fasihi. Kama anavyoeleza Senkoro (2011), fani na maudhui ni vipengee visivyoweza kutenganishwa. Hii ni kwa sababu vipengee hivi vinaingiliana na kukamilishana. Ni kama pande mbili za sarafu moja. Hivyo, huku maudhui yakijibu swali la ni nini kinachowasilishwa, fani hujibu swali la ni vipi kinavyowasilishwa. King'ei na Kisovi (2005) wanaeleza kwamba fasihi hutumia fani au ufundi fulani wa kimasimulizi ili kuwasilisha maudhui fulani kuambatana na matakwa ya mtunzi. Hivyo, jazanda ni mojawapo ya vipengee vya kifani katika fasihi. Mbali na kufumbata itikadi kama kipengee mojawapo cha maudhui katika NKK, jazanda hutekeleza dhima mahsusi kifani kuhusiana na kile kinawasilishwa kwa upande wa hadhira. Hii ni athari ambayo

humpata msikilizaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba ambamo jazanda hutumika. Haya ni kwa mujibu wa Wamitila (2008). Hivyo, uamilifu wa Jazanda kifani na kimaudhui unadhihirika kama ifuatavyo:

6.1.1 Jazanda Hukuza Maana Inayowasilishwa

Utafiti huu umetambua kwamba jazanda huwasilisha maana fulani. Kwa mujibu wa nadharia ya Jazanda Dhanifu, maana inayowasilishwa na jazanda huunda uhusiano fulani kati ya kitengo lengwa na kitengo asilia katika akili ya msikilizaji, mtazamaj au msomaji. Kwa hivyo, hali hii ndiyo humpa msikilizaji au mtazamaji wa wimbo wa kiasili mtazamo unaohusiana na itikadi inayowasilishwa. Mbinu hii ya kifasihi ya jazanda huipa nguvu lugha ya kishairi na uimbaji. Hili hufanyika kwa kuyakuza mawazo pamoja na kuendeleza uelewa wa msikilizaji wa ujumnbe kwenye wimbo unaohusika. Kwa njia hii, jazanda huweza kurahisisha ufasiri wa ujumbe kama vile kuchora taswira zinazoeleweka na hadhira. Hivyo, taswira hizo huhusisha mambo magumu na yale yaliyo rahisi kueleweka. Kwa mfano:

Ng'ombe sya mutavo syendaa na ungi
Ng'ombe wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia
Mali inayomilikiwa kupitia kwa ufisadi au wizi hutoroshwa kwa wizi pia.

Jazanda hii inalinganisha sifa za ng'ombe wa wizi na zile za mali ya wizi. Hapa, ng'ombe wa wizi (mnyama) ndicho kitengo asilia huku mali ya wizi (Wanyama na vitu vinginevyo) ikiwa kitengo lengwa. Kutokana na uchanganuzi huu, upo mfanano kati ya ng'ombe wa wizi na mali ya wizi. Mfanano wenyewe ni kwamba yote ni mali inayopatikana kwa njia ya ufisadi na pia haiwanufaishi wahusika wanaoiiba. Hivyo, jazanda yenyewe imetumika kuwasilisha itikadi ya ufisadi katika jamii husika. Kwa mujibu wa jazanda hii, mwimbaji ana mtazamo hasi kuhusiana na ufisadi kwamba haufai kitu kwa maana hauna manufaa yoyote. Hapa, mwimbaji anajaribu kuieleza

umma kuhusu madhara yanayosababishwa na ufisadi. Kutokana na maarifa ya kimsingi kwenye akili ya mfasiri, msikilizaji anaifasiri jazanda yenyewe kwa kutambua sifa zifuatazo:

Ng'ombe wa Wizi (Uwanja asilia A)	Mali ya Wizi/ufisadi (Uwanja lengwa B)
Ni wanyama	Huhusisha wanyama na vitu vinginevyo pia
Hupatikana kwa wizi/ufisadi	Hupatikana kwa wizi/ufisadi
Hupotea kwa njia hiyo ya wizi tu	Hupotea kwa njia hiyo ya wizi tu
Haimnufaishi mhusika	Haimnufaishi mhusika

Kwa ufupi, kutokana na kifungu kilichopo hapo juu, dhima ya jazanda ni kukuza itikadi kuwa wizi na ufisadi ni suala lisilofaa kwa wanajamii.

6.1.2 Jazanda Huimarisha kumbukumbu na Kuthabitisha Ujumbe

Jazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba zimetumiwa kukuza na kuthabitisha ujumbe unaowasilishwa na pia kuimarisha kumbukumbu ya hadhira. Hali hii inadhihirika katika jazanda ya **usumbi ni nzou** (urais ni ndovu).

Katika jazanda hiyo, wadhfa wa urais unalinganishwa na ndovu. Msikilizaji wa wimbo anapoisikia jazanda hiyo, sifa za ndovu au picha ya ndovu akilini mwake inahamishwa kwenye dhana ya urais na hivyo kuimarisha kumbukumbu kuhusiana na dhana ya urais. Jazanda hii pia inathabitisha ujumbe kuhusiana na wadhifa wa urais kwamba ni mzito na kwa hivyo, unahitaji umakinifu na nguvu kuutekeleza.

Mfano wa mwingine wa jazanda yenye uamilifu wa aina hii ni: **Ngima yumaa kwi kuthie** (Ugali hupatikana kwa kusiaga mawele). Itikadi inayofumbatwa hapa ni kwamba **mafanikio** hupatikana baada ya kujitahidi. Hapa sifa na picha ya ugali iliyo kwenye akili ya msikilizaji inahamishwa kwenye dhana ya mafanikio ambapo kumbukumbu ya dhana hiyo inamarishwa. Jazanda ya **Ngima (ugali)** pia inathabitisha ujumbe kwamba mafanikio hupatikana baada ya kujitahidi kazini. Hivyo, jazanda ya

ugali inawasilisha itikadi kuhusu kazi kwamba wanajamii hawana budi kufanya bidii kazini ndipo wafanikiwe.

Kwa hivyo, matumizi ya jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba huimarisha itikadi inayowasilishwa kwa kuithabitisha akilini na pia kumwezesha msikilizaji kuhifadhi kumbukumbu ya kinachowasilishwa kwa taswira inayochipuzwa akilini kwa jazanda ya ugali. Hii ni kwa sababu ubongo wake utakuwa umeshirikishwa sana katika ufasiri wa jazanda husika.

6.1.3 Jazanda Huimarisha Ujumi wa Lugha

Matumizi ya jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba huzua urembo fulani wa kisanaa katika lugha. Matumizi ya jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba huzifanya zipendeze masikioni mwa hadhira na kwa hivyo kuvuta makini ya hadhira kwenye ujumbe unaowasilishwa. Tazama mfano ufutao:

***Kavuli vula mwee witu.** (Kavuli twanga mawele yetu).*

Jina **Kavuli** limetumiwa kijazanda na kimajazi kurejelea mtu mwenye bidii kazini. Zaidi ya hayo, jazanda hiyo katika lugha ya Kikamba inaleta wizani na ladha fulani ya kishairi kupitia kwa maneno ***Kavuli vula***. Hapa kuna takriri ya mizani **vu-li** na **vu-la** ambayo inavutia masikioni na kuimarisha burudani ya hadhira hali kadhalika kumbukumbu ya itikadi ya bidii kazini.

Dhima ya ujumi wa lugha inadhihirika pia katika mfano ufuatao:

*Nauma kwasa nayu ningwenda **katanda** ngome* (Nimetoka mbali na sasa nataka **kitanda** nilale.

*Nimetoka mbali na sasa nataka **ndoa**.*

Katika mfano uliopo hapo juu, jazanda ya **kitanda** inatumika kuwasilisha itikadi ya ndoa. Kauli ya kutoka mbali inarejelea mhusika aliyekomaa kihulka na kitanda ni jazanda ya ndoa. Itikadi inayowasilishwa hapa ni kwamba ndoa ni kwa wale

wamekomaa kiakili na kimwili. Jazanda hizi zinachochea taharuki katika hadhira na kwa njia hii kuifanya itafakari kwa kina kutafuta fasiri ya ujumbe uliofumbatwa na jazanda hizo. Hapa, lugha ya kimafumbo inazua ladha ya kisanaa kwenye wimbo wa kiasili.

6.1.4 Jazanda Hukuza Hisia

Matumizi ya jazanda huathiri hisia za hadhira kuhusiana na masuala yanayowasilishwa katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Matumizi ya jazanda huubua picha akilini mwa hadhira na kwa njia hufanya suala linalowasilishwa lieweke kwa urahisi. Kupitia kwa jazanda msikilizaji au mtazamaji wa nyimbo hizi huweza kuhusisha vitu vinavyolinganishwa ambapo hatimaye huweza kuunda picha akilini. Kwa mfano jazanda ya *Simba ii syi ngunyu nitwasyelile*. (**Simba wenye kucha** tushazikatakata) inarejelea *mienendo ya wanasisia fisadi*.

Mwimbaji anatumia jazanda ya *simba wenye kucha* kurejelea viongozi ambao amabo wametumia mamlaka yao vibaya na ambao wameshatupiliwa mbali na wapiga kura. Msikilizaji anahusisha picha ya simba wenye kucha na viongozi fisadi ambao hawastahili kupewa wadhifa wa uongozi. Jazanda hiyo inaibua taswira na hisia ya uoni ambayo inathabitisha itikadi kuhusiana na uongozi katika jamii ya Wakamba. Watu fisadi hawastahili kupewa wadhifa wa uongozi. Jazanda hii inaweza kuiathiri hadhira kichanya kwa kuifanya iwe makini katika harakati za kuchagua viongozi.

6.1.5 Jazanda Husitiri Ujumbe

Wakati mwingine, uwepo wa jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba unaweza kusababisha utata katika maana ya kile kinawasilishwa. Hii ni kwa sababu mwimbaji anaweza kuficha maana kamili za maneno katika jazanda husika. Hivyo, maana za jazanda zinaweza kueleweka tu na hadhira maalum kutokana na msingi fulani wa

maarifa walio nayo. Hivyo, uelewekaji wa jazanda inayohusika hutegemea uzoefu wa mwimbaji na hadhira inayohusika pia. Kwa hivyo, hadhira inapoelewa maana iliyokusudiwa, wao huweza kuburudishwa zaidi na wimbo unaoimbwa lakini kinyume chake pia kinaweza kutokea pale ambapo hadhira inashindwa kufasiri maana iliyofumbatwa na jazanda maalum. Tazama mfano ufuatao:

Muti uu ni mumu (Mti huu umekauka/umekomaa)

Kwenye mfano huo, maneno **mti uliokauka uliokomaa** ni jazanda ambayo inaweza kueleweka vyema na hadhira inayoufahamu muktadha wa tohara katika jamii ya Wakamba inaelewa kuwa kinachorejelewa ni mboo za watahiriwa ambazo zinalinganishwa na mti uliokomaa kumaanisha kuwa watahiriwa sasa wako tayari kujihusisha na masuala ya utu uzima. Hata hivyo, mwanajamii asiyeufahamu muktadha ambamo jazanda hii inatumika huenda akatatizika kufasiri maana fiche kwenye jazanda hiyo na kuishia kueleza maana ya juu juu ya jazanda hiyo.

Mfano mwingine wa jazanda inayosababisha utata wa kimaana ni ufuatao:

*Syana syokote **malenge** kivulanio kya **nzuu** na **mboso**.* (Watoto waokote **maboga**, mchanganyiko wa **baazi** na **maharagwe**.)

Katika wimbo **NA.17. Tuthii Kithembeoni** (Twendeni Madhabahuni) tunapata maneno **Malenge (Maboga)**, **Nzuu (Mbaazi)** na **Mboso (Maharagwe)** ambayo yametumika kijazanda kurejelea dhana ya **mafanikio** yanayotokana na kumwabudu Mungu. Hivyo, hali hii ya dhana nyingi kurejelea dhana moja pia ni utata wa kimaana.

Vilevile, maana ya jazanda ya **ndovu** katika wimbo **NA. 9. Usumbi ni Nzou** (Urais ni **Ndovu**) na wimbo **NA. 12. Ngai wa Nzou nowe wa Nduti** (Mungu wa **ndovu** ndiye Mungu wa siafu) ni tofauti. Neno **ndovu** kwenye wimbo **NA. 9** limetumika kurejelea cheo cha **urais** huku neno hilo likitumika kurejelea **tabaka tawala** katika wimbo **NA. 12.**

Angalia kauli hizi:

NA. 9

Usumbi aume ni nzou.

Jamani urais ni **ndovu**.

Cheo cha Urais hunyemelewa kwa hekima.

NA.12.

Ngai wa nduti nowe wa nzou.

Mungu wa **siafu** ndiye wa **ndovu**.

Mungu wa tabaka tawaliwa (la chini) ndiye Mungu wa tabaka tawala (la juu).

Katika mifano hiyo yote, neno **ndovu** linazua utata wa kimaana. Hii ni kwa sababu neno hilo linaweza kutumika katika kuwasilisha maana tofautitofauti kutegemea muktadha wa wimbo unaowasilishwa. Mbali na kuzua utata kimaana, jazanda kama kipengele cha fani kinakuza tafakuri ya hadhira katika kufumbua maana fiche ambayo huwa ni itikadi maalum inayowasilishwa kisanaa.

6.1.6 Jazanda Hukuza Fikra za Kiuhakiki

Uwepo wa jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba unaweza kumfanya msikilizaji au mtazamaji atafakari zaidi kuhusiana na wimbo unaohusika. Hivyo, matumizi ya jazanda katika nyimbo zinazohusika yanaweza kukuza mijadala na uhakiki wa dhana maalum, hali inayoweza kuibua mtazamo mbadala kuhusu dhana ambazo kidegesturi zimchukuliwa kuwa na maana moja maalum. Kwa maneno mengine, jazanda huchangia katika udenguzi wa maana katika dhana na masuala yanayowasilishwa kwenye wimbo wa kiasili. Kutegemea muktadha ambamo nyimbo za kiasili zinawasilishwa, jazanda zilizomo zinaweza kufasiriwa kwa njia mbalimbali. Hivyo, msikilizaji au mtazamaji husikiliza au kuutazama wimbo unaohusika kwa njia ya kiuhakiki. Uhakiki wenyewe hutokana na hali ya kuutafuta ukweli uliofichika katika jazanda na itikadi zinazowasilishwa kupitia nyimbo zinazohusika.

6.1.7 Jazanda Hupanua maana ya Dhana

Jazanda hutumika katika kupanua dhana fulani kwa kuifafanua zaidi. Wahusika na wasikilizaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba huzingatia zaidi kinacholinganishwa katika wimbo husika. Kwa mfano,

*Mbande **mutunda**, ni waki? Wai wa mavatano.* (Nipande **mtunda**, ni wa nini? Ulikuwa wa mapatano).

Kutokana na mfano huo, dhana ya **Mtunda** inarejelea **mapatano/makubaliano kati ya wanandoa**. Hivyo, kupitia matumizi ya jazanda hii, dhana ya mtunda imepanuliwa kimaana na kimatumizi. Hii ni kwa sababu unaweza kutumia dhana hizi mbili **mtunda** na **mapatano** kurejelea kitu kimoja. Hivyo, dhana inayowasilishwa hapa imekuzwa na kupanuliwa kwa kupewa maana nyingine.

Mfano mwingine niufuatao:

***Munyambu nuukiva (Simba ananguruma)**
Ngariba yuko tayari*

Jazanda ya **simba** katika mfano huo inarejelea **ngariba** katika muktadha wa tohara. Kwa msingi huu, matumizi ya jazanda ya **ngariba** imepanuka kiupeo wa kimatumizi. Mzungumzaji anaweza kutumia istilahi zote mbili; **ngariba** na **simba** kurejelea kitu kimoja.

6.1.8 Jazanda na Uashiriaji

Kutokana na ukweli kwamba jazanda ni ulinganishaji, kitengo kimoja huwa ishara ya kingine. Tunapolinganisha A na B, kitengo B huwasilisha sifa au dhima za kitengo A. Kwa mfano:

*Ve **ndeke** ikwitwa Manyali ikakua andu ma wia* (Kuna **ndege** inaitwa Manyali itabeba watu wa kazi
Mafanikio yanatokana na bidi kazini

Mfano huo unabainisha jazanda ya ndege ambayo inaashiria mafanikio. Hivyo, sifa ya kupaa juu kwa ndege inalinganishwa na mafanikio ambayo ni kufikia kiwango cha juu kimaendeleo. Kwa hivyo, mwimbaji anapotaja kwamba **ndege Manyali** itabeba watu wa kazi anaashiria kwamba mafanikio hupatikana kwa watu walio na bidii kazini na kwa hivyo ni jazanda inayofumbata itikadi ya kufanya kazi kwa bidii maishani ili kupata mafanikio.

Mfano mwingine ni wa jazanda ya **sigara** katika mfano uatao:

*Ngwitivitye **sikala** (Nimekuomba sigara)
Mwimbaji anaomba tendo **la ngono***

Katika mfano huo, sigara ni jazanda inayoashiria tendo la ngono. Kwa hivyo, mhusika wa kiume anamwomba mhusika wa kike (Tavitha) sigara, inaashiria kwamba tendo la ngono ndilo linarejelewa. Hivyo, jazanda hii imetumika katika kuendeleza ujumbe kwamba vijana hawana budi kusalia mabikira hadi pale watakapolewa kirasmi. Hii ni kwa sababu tendo la ngono ni la wanandoa pekee. Jazanda ya Tavitha kunyimana sigara inaashiria kutojikusisha katika tendo la ndoa ambalo ni aina ya uraibu ambao umetengewa wanandoa katika jamii.

6.1.9 Jazanda hutumika kama Tasfida

Mwimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba anaweza kutumia jazanda kurejelea dhana fulani ambazo ni mwiko kuzitaja moja kwa moja. Kwa mfano, jazanda huweza kutumiwa kurejelea mieleleko maalum ya kisiasa, magonjwa sugu pamoja na sehemu nyeti za mwili. Kwa mfano:

*Nzambi akithambya **nzele** ii ya kuthamba. (Nzambi akiosha **kata** ya kuoga.)*

Katika wimbo **NA. 7. Nzambi akithambya nzele (Nzambi akiosha kata)**, mwimbaji anaitumia jazanda **nzele** kurejelea **uondoaji wa uozo** wa kijamii unaotekelezwa na viongozi watangulizi. Hapa suala la ufisadi wa viongozi ni suala nyeti ambalo

wanajamii huogopa kulieleza moja kwa hasa katika harakati za kampeni za kutafuta kura. Kwa hivyo, kutokana na hali hii, mwimbaji hana budi kutumia lugha ya kijazanda ili kupunguza makali ya ujumbe wake hadhira ili itafakari juu ya wale wanastahili kupewa fursa ya uongozi. Kwa kufanya hivi, mwimbaji huuimba wimbo wake kama fumbo linalohitaji kufumbuliwa ndiposa itikadi zinazowasilishwa zipate kueleweka.

Mfano mwingine wa jazanda zinatumika kusafidi lugha ni huu ufuatao:

Ala matesi mbilano (Wasiojua kazi)

Neno *mbilano* (Wasiojua *kazi*) limetumika kijazanda. Jazanda yenyewe inajitokeza katika wimbo **NA. 1. Kwa Sisy Wone (Angalia Uone)**. Hapa, mwimbaji anaitumia jazanda ya *mbilano* kuashiria *tendo la ndoa*. Maeno *tendo la ndoa* ni tasfida inayopunguza makali kihisia na kuepuka aibu ambayo ingezuliwa iwapo maneno halisi yanayorejelea dhana hiyo yangetumiwa. Kwa hivyo jazanda ni kipengele muhimu cha kusafisha lugha zikiwemo nyimbo za kiasili za Kikamba zinazowasilishwa katika hafla mbalimbali za kijamii.

6.2 Hitimisho

Sura ya sita imejadili uamilifu wa jazanda mbalimbali kama kipengee cha kifani na kimaudhui kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Utafiti huu umetambua kwamba jazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba zina dhima mahsusi kifani na kimaudhui. Jazanda huchangia katika kuchora taswira zinazorahisisha uelewa wa itikadi katika nyimbo za Kiasili za Kikamba. Jazanda pia hukuza na kutanua maana ya dhana, kuimarisha kumbukumbu ya itikadi zinazowasilishwa, huimarisha ujumi wa lugha na kukuza hisia za hadhira, husafidi lugha katika NKK, huzua utata wa kimaana na kukuza fikra za kiuhakiki miongoni mwa hadhira. Kwa hivyo, jazanda ni mojawapo

ya tamathali za usemi na mbinu muhimu ya kisanaa ambayo ina uamilifu mkubwa katika kuimarisha ujumi na ujumbe katika nyimbo za kiasili za Kikamba.

SURA YA SABA

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.0 Utangulizi

Utafiti huu umeangazia ufumbaji wa itikadi kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Utafiti wenyewe umewasilishwa kupitia tasnifu hii ambayo imegawika katika sura saba. Sura hii ya saba inapambanua muhtasari wa utafiti, hitimisho pamoja na mapendekezo ya utafiti zaidi.

7.1 Mutasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umeangazia ufumbaji wa itikadi kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Data ya utafiti huu imetokana na nyimbo 41 za kiasili za Kikamba. Hapa, nyimbo zilizosheheni vipengee vya utafiti husika ndizo zilizoteuliwa. Vipengee vyenyewe ni jazanda na itikadi katika nyimbo teule. Sura ya kwanza ndiyo imeweka msingi wa utafiti huu. Hapa, usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti huu yameshughulikiwa. Vilevile, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti na mbinu za utafiti zimejadiliwa. Sura ya pili imeshughulikia msingi wa nadharia pamoja na tahakiki ya maandishi. Nadharia ya Jazanda Dhanifu na Nadharia ya Itikadi ndizo ziliongoza utafiti huu. Nadharia ya Jazanda Dhanifu ilitumika katika uchanganuzi wa jazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba na uamilifu wa jazanda hizo kifani na kimaudhui kwenye nyimbo teule. Nadharia ya Itikadi nayo imeuongoza utafiti huu katika kuhakiki itikadi za Wakamba zinazojitokeza katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Pia, hafla mbalimbali ambamo NKK huwasilishwa zimechunguzwa kwa mwongozo wa Nadharia ya Itikadi. Mapitio ya maandishi yamethibitisha kwamba suala la ufumbaji wa itikadi kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba halikuwa limetafitiwa.

Upambanuzi wa jazanda mahsusi zinazojitokeza katika NKK zinazowasilishwa kwenye hafla maalum umeshughulikiwa katika sura ya tatu. Imegunduliwa kwamba hafla maalum ambamo nyimbo za kiasili za Kikamba huimbwa zinaweza kugawanywa katika makundi mawili makuu; kundi la hafla rasmi na lile la hafla zisizo rasmi. Kila mojawapo wa makundi haya limegawika katika makundi madogo madogo kutegemea shughuli ya hafla husika. Hafla rasmi zinahusisha makundi kama vile *Syathi sya Nzaiko* (Hafla za Tohara), *Syathi sya Siasa* (Hafla za Siasa), *Syathi sya Kithaitho* (Hafla za Kidini), *Syathi sya Mathiko* (Hafla za Mazishi), *Syathi sya Mutwaano* (Hafla za Ndoa), *Syathi sya Kusyawa kwa Syana* (Hafla za Kuzaliwa kwa watoto) pamoja na *Syathi sya Wia wa Ikundi* (Hafla za Kazi za Makundi ya Watu). Kwa upande mwingine, hafla zisizo rasmi zimegawanywa katika makundi kama vile *Syathi sya Wia wa Mundu Umwe* (Hafla za Kazi ya Mtu Mmoja), *Syathi sya Kuongola Syana* (Hafla za Kuongoa Watoto), *Syathi sya unywi wa Nzovi* (Hafla za Ulevi) pamoja na *Syathi sya Ithau ya Syana* (Hafla za Michezo ya Watoto). Utafiti huu umedhihirisha kwamba hafla mbalimbali katika jamii ya Wakamba hushirikisha nyimbo za kiasili ambamo itikadi kuhusu masuala mbalimbali hufumbatwa kijazanda.

Jazanda mahsusi zimepambanuliwa kwenye sura ya tatu. Upambanuzi huu umedhihirisha kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba husheheni jazanda mbalimbali zinazofumbata itikadi za Wakamba kama ifuatavyo: Nyimbo zilizowasilishwa katika hafla za tohara zinadhihirisha jazanda za *Muti Mumu* (Mti uliokauka) inayorejelea mboo za watahiriwa, *Uki* (Asali) inayorejelea utoshelezaji wa kingono, *Kaindo* (Kakitu), *Munyambu* (Simba) inayoashiria ngariba, *Nzuki Mbingi* (Nyuki Wengi) inayomaanisha ukuaji wa kimaumbile, *Ngaku* (aina ya mnyama anayewala nyuki) inayorejelea wabakaji, *Mbilano* (kazi) inayoashiria ngono, *Matila ma Kiimani* (Wajinga wa Milimani) inayorejelea Wakikuyu, *Ndiani* (Kidimbwini) inayoashiria

utegemevu na *Mwatu* (Mzinga) inayorejelea kijana. Itikadi inayowasilishwa na jazanda hizi ni kwamba tendo la ndoa si la Watoto wadogo bali ni watu wazima wanaoruhusiwa kushiriki katika tendo hilo. Hii ni kwa sababu wamekomaa kiakili na kimaumbile na wako tayari kutekeleza majukumu ya watu wazima. Kwa hivyo, jamii ya Wakamba inauenzi ubikira miongoni mwa vijana. Vijana wanahimizwa kujitunza na kujiepusha na mahusiano ya ngono na ubakaji ambayo ni matendo yanayoashiria ukiukaji wa maadili kwenye jamii ya Wakamba. Vilevile, jazanda hizi zinawasilisha ujumbe kwamba mtahiriwa hana budi kuwa jasiri na mwenye kuwajibika katika wadhfa mpya wa maisha ya utu uzima.

Itikadi kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii nayo inawasilishwa kwenye NKK zinazowasilishwa katika hafla za kazi. Itikadi hii imefumbatwa katika jazanda za; *tumikeve twili* (mikebe miwili midogo) inayorejelea chakula cha msaada, *Kathungi* (Kiondo), *kamulo* (jembe) na *Kavelu* (Mbegu) kuashiria nyenzo muhimu za kazi, *Muundani* (Shambani) kuashiria maeneo ya kazini, *Ndeke* (Ndege) kuashiria mafanikio, *Kavuli* (Anayetwanga) kumaanisha mwenye jitihada, *Ngima* (Ugali) kurejelea mafanikio yanayotokana na bidii kazini. Katika jazanda hizi, mwimbaji anawahimiza wanajamii wajitahidi katika kazi wanazofanya. Wanahitajika wawajibike na wala sio kutegemea misaada wala kuombaomba.

Imebainika pia kwamba itikadi inayohusiana na imani katika Mungu na baraka zinazotokana na imani hiyo zinawasilishwa kupitia jazanda. Jazanda za *Malenge* (Maboga), *Nzuu* (Mbaazi) na *Mboso* (Maharagwe), *Miti Minene* (Miti Mikubwa) zinazorejelea dhana ya mafanikio yanayotokana na kumwabudu Mungu. Wanajamii wanahimizwa wamche na kumwabudu Mungu ambaye ni chanzo cha mafanikio maishani mwao.

Vilevile, itikadi kuhusu ndoa na mapenzi imewasilishwa kijazanda katika NKK zinazowasilishwa katika hafla za ndoa na arusi. Itikadi hii inadhihirika kupitia maneno *Katanda* (Kitanda) linaloashiria ndoa, *Ngate* (Mikate) linalomaanisha makaribisho, *Uki wa Ngilu* (Asali Mwitu) linaloashiria uwajibikaji na hata *Mutunda* (Mtunda) linaloashiria mapatano. Kupitia kwa jazanda hizi, wanandoa wanahimizwa wazingatie upendo, ustahimilivu, maelewano, msamaha na uwajibikaji ili kuidumisha taasisi hii ya ndoa. Talaka katika jamii ya jadi ya Wakamba haikuruhusiwa na kwa hivyo wanandoa walipaswa kustahamili changamoto za ndoa maishani mwao mote.

Itikadi inayohusiana na umuhimu wa ubikira nayo inaendelezwa kupitia jazanda ya *Ngali* (Gari) inayomaanisha uaminifu, *Sikala* (Sigara) inayoashiria tendo la ndoa na *Mwaki* (Moto) inayorejelea hisia za kimapenzi. Maneno haya yametumika kijazanda kupitisha ujumbe kwamba tendo la ndoa ni la wanandoa pekee. Hivyo, ni kinyume cha maadili kwa vijana kushiriki katika ngono. Vijana wanahimizwa wajitunze, wawe na kiasi na kujiepusha na unajisi wa aina yoyote. Vilevile, wanandoa wanahimizwa kuwa waaminifu katika ndoa. Hivyo, suala la uaminifu kwenye ndoa limepewa kipau mbele kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba zinazoimbwa katika hafla za ndoa na arusi ambapo suala hilo limefumbatwa kijazanda.

Maneno *Syokimau* (nabii wa kale katika jamii ya Wakamba), *Bakari* (Jina la Kiislamu), *Juma* (Jina la Kiislamu) na *Kaletiu* (Redio) linaloashiria mpashanaji wa habari, yametumika kijazanda kuifumbata itikadi ya utamaduni wa Wakamba. Kupitia jazanda hizi, wanajamii wanaonywa dhidi ya kukegeuka na kuzitupilia tamaduni zao huku wakizipokea zile za kigeni. Wakamba Wanaamini kuwa mwacha mila ni mtumwa na kwa hivyo nyimbo za kiasili za Kikamba zilitungwa na kuimbwa kwenye hafla za kijamii kushinikiza itikadi hii kwa hadhira.

Nayo itikadi ya uzazi na malezi imefumbatwa katika jazanda ya *Kaindo* (Kakitu) inayorejelea zawadi na *Mukwa* (Kamba Pana) inayoashiria ustahimilivu. Ujumbe unaowasilishwa hapa ni kwamba, uzazi na malezi si kazi rahisi. Hivyo, suala la malezi ni jukumu la wanajamii kwa maana watoto ni mali ya jamii. Hata hivyo, jukumu kubwa la malezi ni la wazazi au wanajamii wenye uhusiano wa karibu na mtoto anayehusika.

Pamoja na hayo, itikadi kuhusu siasa na uongozi imefumbatwa katika jazanda *Nzambi* (Huoga/Safi) inayoashiria kiongozi teule, *Nzele* (kata) inayoashiria kiongozi mpya, , *Uthambya wa nzele* (uoshwaji wa kata) unaoashiria uondoaji wa ufisadi, *Simba ii syi ngunyu* (Simba wenye makucha) kuashiria viongozi fisadi na *Nzou* (ndovu) kurejelea cheo cha urais. Jazanda hizi zinawasilisha ujumbe kwamba uongozi si rahisi na hivyo unahitaji umoja na utangamano wa viongozi wanaohusika. Pia, wanajamii wanaonywa dhidi ya kuwateua viongozi wabaya.

Ng'ombe sya mutavo (ng'ombe wa wizi) ni jazanda inayorejelea mali ya wizi. Jazanda hii imetumika kuwasilisha ujumbe kuhusu ufisadi kwamba haufai. Wanajamii wanaonywa dhidi ya ufisadi kwa maana haumfaidi mtu kwa vyovyote na badala yake hukomesha na kudidimiza maendeleo.

Itikadi inayohusiana na mauti inadhihirika kwenye NKK zinazoimbwa kwenye hafla za mazishi. Kwa mfano, maneno *Musyimi ute tei* (Mwindaji asiye na huruma) na *Muvutani ute tei* (mwizi asiye na huruma) yametumika kurejelea hali ya ukiwa na upweke wanaohisi wanajamii baada ya kuachwa na mpendwa wao. Jazanda hizi zinafafanua kifo kama kitu kibaya na ambacho kila mmoja hana budi kujiepusha nacho inapowezekana. Hivyo, ujitiaji kitanzi ni jambo ambalo halifai na limepigwa marufuku miongoni mwa Wakamba.

Sura ya nne imeshughulikia uhakiki wa itikadi za Wakamba zilizofumbatwa kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Utafiti huu umetambua kwamba nyimbo za kiasili za Kikamba hupitisha itikadi mbalimbali kwa hadhira lengwa. Itikadi zenyewe zinahusiana na kazi, dini, ndoa na mapenzi, ubikira, utamaduni, malezi, siasa na uongozi, mauti na ufisadi.

Uchunguzi wa uamilifu wa jazanda kifani na kimaudhui kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba umeangaziwa katika sura ya tano. Imegunduliwa kwamba jazanda hukuza na kuwasilisha maana, huimarisha kumbukumbu na hata kukuza hisia. Vilevile, jazanda nyingine hutumika katika kuimarisha ujumi au urembo wa lugha huku nyingine zikitumika katika kuzua utata kimaana. Jazanda hutumika kupanua maana ya dhana, kuchochea fikra za kiuhakiki, kuashiria maana na pia hutumika kama tasfida kupunguza hisia kali katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Sura ya sita nayo inajadili matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti zaidi kutokana na mahitimisho ya utafiti huu..

7.2 Hitimisho

Utafiti huu umebainisha kuwa nyimbo za kiasili za Kikamba huwasilishwa kwenye hafla mbalimbali zinazoambatana na utamaduni wa jamii ya Wakamba. Hafla zenyewe zinaweza kugawanywa katika; hafla rasmi na hafla zisizo rasmi kutegemea muktadha wa uwasilishaji. Vilevile, nyimbo za kiasili za Kikamba husheheni jazanda mahsusi ambazo hufumbata itikadi ya Wakamba kuhusiana na masuala kama vile ndoa na mapenzi, ubikira, ufisadi, kazi, tohara, mauti, dini na siasa na uongozi. Kisanaa, jazanda hutumika na watunzi wa NKK kutekeleza dhima mbalimbali kama vile: Kujenga taswira ya kile kinawasilishwa ili kieleweka akilini mwa hadhira. Kwa njia hii, ujumbe unaowasilishwa huthabitishwa. Jazanda nyingine hutumika kama tasfida ili kupunguza makali katika nyimbo za kiasili za Kikamba.

Nadharia tulizozitumia katika utafiti huu ni mbili; Nadharia ya Jazanda Dhanifu ambayo imetufaa sana katika upambanuzi wa jazanda na uchunguzi wa uamilifu wa jazanda. Nadharia ya Itikadi imetumika kuhakiki itikadi inayofumbatwa na jazanda na pia kupambanua hafla zinamoimbwa NKK. Matokeo ya utafiti huu yataifaidi taaluma ya fasihi kwa jumla. Matokeo yake ni nyongeza katika fasihi ikiwemo ile ya Kiswahili na Kikamba. Hivyo, tasnifu hii ni rejeleo muhimu kwa wasomi na wa fasihi simulizi ya Kiswahili na ile ya Kikamba.

7.3 Mapendekezo ya Utafiti

Itikadi mbalimbali hufumbatwa kijazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Kwa hivyo, hadhira haina budi kuzifasiri jazanda husika kwa njia mwafaka ili ujumbe uliokusudiwa ueleweke. Hata hivyo, mbali na kusheheni jazanda, nyimbo za kiasili za Kikamba zina ukwasi katika sanaa za utendaji unaofaa kuchunguzwa katika tafiti za usoni. Kwa hivyo, tunapendekeza tafiti zaidi zifuatazo:

Kwanza, tunapendekeza utafiti ufanywe kuhusiana na vipengee vya utendaji vya mandhari, maleba, miondoko na uigizaji. Utafiti wa aina hii ujaribu kubainisha jinsi vipengee hivi vinafanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwenye nyimbo za kiasili. Aidha uchunguzi wa aina hii unaweza kufanywa kwa misingi ya nadharia ya utendaji.

Pili, utafiti unaweza kufanywa kuhusiana na dhima zinazofungamana na matumizi ya vipengee vya utendaji. Utafiti wa aina hii uchunguze uamilifu wa kifani wa vipengee vya utendaji katika nyimbo za kiasili za jamii ya Kikamba au jamii nyinginezo za Kiafrika.

MAREJELEO

- Adorno, T. W., Frenkel-Brunswik, E., Levinson, D. J., & Sanford, R. N. (1950). *The Authoritarian Personality*. New York: Harper.
- Aggrey, W., Chimerah, R., & Karisa, B. (2017). Muundo wa Utenzi wa Wabukusu wa Khuswala Kumuse. *Mulika Journal*, 34(1).
- Althusser, L. (1984). *Essays on Ideology*. London: Verso.
- Althusser, L., & Etienne, B. (1970). *Reading Capital*. London: New Left Books.
- Anderson, D.G. (1988). Power, rhetoric, and the state: a theory of presidential legitimacy, *Review of Politics*, 50 (2): 198-214.
- Anzaldúa, G.(1999). *Borderlands/La Frontera: The New Mestiza*. San Francisco: Aunt Lute Books.
- Babalola, S. A. (1963). *The content and form of Yoruba Ijala*. University of London, School of Oriental and African Studies (United Kingdom).
- Bakhtin, M. M., Emerson, M. H. T. C., & Austin, M. H. Althusser, Louis. (1971). "Ideology and Ideological State Apparatuses." *Lenin and Philosophy and Other Essays*. Trans. Ben Brewster. New York: Monthly Review Press.
- Baran, P. A. (1957). *The political economy of growth*, New York (Monthly Review Press).
- Bascom, W. R. (1981). *Contributions to folkloristics* (Vol. 10). Meerut, India: Folklore Institute: Archana Publications.
- Bascom, W. R. (1954). Four functions of folklore. *The Journal of American Folklore*, 67(266), 333-349.
- Bauman, R. (Ed.). (1992). *Folklore, cultural performances, and popular entertainments: A communications-centered handbook*. Oxford University Press.
- Benokraitis, N.V. (1993). *Marriages and Families: Changes, Choices and Constraints*. Englewood Cliffs, New Jersey: Prentice Hall.
- Boss, P. (1988). *Family Stress Management*. Newbury Park, California: Sage Publications.
- Brunvand, J. H. (2015). *The Taming of the Shrew (Routledge Revivals): A Comparative Study of Oral and Literary Versions*. Routledge.
- Brunvand, J. H. (1981). *The vanishing hitchhiker: American urban legends and their meanings*. WW Norton & Company.
- Cardoso, F. H. (1973). Associated-dependent development: theoretical and practical implications. *Authoritarian Brazil*, 142-176.
- Chase-Dunn, C. (1975). The effects of international economic dependence on development and inequality: A cross-national study. *American Sociological Review*, 720-738.

- Chenenje, S. (2017). *Stylistic Analysis of Kabras Folk Songs* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Chuachua, R. (2011). *Itikadi Katika Riwaya za Shaaban Robert*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taluma za Kiswahili.
- Cuddon, J. A. (2012). *A dictionary of literary terms and literary theory*. John Wiley & Sons.
- Dorson, R. M. (Ed.). (1978). *Folktales told around the world*. University of Chicago Press.
- Eagleton, T. (2007). *Ideology: An introduction*. London, UK: Verso
- Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction*. Minnesota: University of Minnesota Press.
- Eagleton, T. (1976). *Criticism and Ideology: A study in Marxist Literary Theory*. London: NLB.
- Eagleton, T. (1976). *Marxism and Literary Criticism*. London: Methuen.
- Evans, P. B. (1979). *Dependent development: The alliance of multinational, state, and local capital in Brazil*. Princeton University Press.
- Fedders, A., & Salvadori, C. (1980). *Peoples and Cultures of Kenya Trans Africa. Nairobi. REXCOLLINGS London in association with Kenya Tourist Development Co-operation*.
- Finnegan, R. (2012). *Oral literature in Africa* (p. 614). Open Book Publishers.
- Frank, A. G. (1967). Sociology of development and underdevelopment of sociology. *Cahiers Internationaux de Sociologie*, 42(JAN-J), 103-131.
- Freire, A. M. A., & Macedo, D. (1998). *The Paulo Freire Reader*. Cassell and Continuum, 370 Lexington Avenue, New York, NY 10017.
- Freire, P. (1976). *Education, the practice of freedom*. London: Writers and readers Publishing Cooperative. Cited by Maria de Figueiredo-Cowen and Denise Gastaldo, (1995), Paulo Freire at the institute. Institute of Education. University of London.
- Freire, P. (1974). *Education for Critical Consciousness* (London, Sheed and Ward). *Freire Education for Critical Consciousness 1974*.
- Freire, P. (1970). *Pedagogy of the oppressed*, New York (Herder & Herder) 1970.
- Genova, M.K. (2008). *Intimate Relationships, Marriage and Families*, Seventh Edition. New York: McGraw Hill.
- Gottdiener, M. (1985). Hegemony and mass culture: A semiotic approach. *American journal of sociology*, 90(5), 979-1001.
- Gramsci, A. (1985). *Selections From Cultural Writings*. London: Lawrence and Wishart.
- Gramsci, A. (1971). *Selections from the prison notebooks*, edited and translated by Quintin Hoare and Geoffrey Nowell Smith.

- Hymes, D. (1968). The ethnography of speaking. *Readings in the Sociology of Language*, 2, 99-138.
- Hymes, D. (1964). Introduction: toward ethnographies of communication 1. *American anthropologist*, 66(6_PART2), 1-34.
- Hymes, D. (2005). Models of the interaction of language and social life: toward a descriptive theory. *Intercultural discourse and communication: The essential readings*, 1, 4-16.
- Kareithi, A. (July 29, 2012). Syokimau, a place that inspires awe, despair in equal measure. *Standard Digital*. The Standard Group. Retrieved 9 July 2017
- Kavyu, P. N. (1980). *Traditional musical instruments of Kenya*. Kenya Literature Bureau.
- Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Arusha: E.L.B
- Kieti, M. (1999). Myali songs. Social Critique among the Kamba (M.A. Thesis, University of Nairobi).
- Kieti, M. (Ed.). (1990). *Barking, you'll be eaten!: the wisdom of Kamba oral literature*. Phoenix Publ..
- Kilauni, N. W. (2007). *Usasa katika Ngoma ya Itheke* (M.A. Thesis, Kenyatta University).
- Kilonzi, L.A. (1992). Dance and movement: A Study of the factors affecting Step and Dance movement among the Kamba; Kinze. (M.A. Thesis, Kenyatta University).
- Kimilu, D. (1962). *Mukamba wa w'o*. Nairobi: East Africa Literature Bureau.
- Kimondo, G.K. (1997). *Family Law and Succession*. Nairobi: Claripress
- King'ei, K. (2002). Swala la Uana Katika Fasihi ya Kiswahili. Uhakiki wa Utafiti kutoka Kenya katika Utafiti wa Kiswahili. Eldoret: Moi University Press. kur. 87-95
- King'ei, G. K. (1992). Uhakiki wa Nthimo (Methali) za Kikamba:(Kwa Kufuatisha Misingi ya Methali za Kiswahili) (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- King'ei, K., & Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau
- Kobia, J.M. (2008). Taswira za kiuana miongoni mwa Waigembe (Doctoral dissertation, Kenyatta University)
- Kovecses, Z. (2010). *Metaphor: A practical introduction*. Oxford University Press.
- Kövecses, Z. (2003). Language, figurative thought, and cross-cultural comparison. *Metaphor and Symbol*, 18(4), 311–320.
- Kunene, D. P. (1971). *Heroic poetry of the Basotho*. Oxford [Eng.]: Clarendon Press.
- Lakoff, G. (1993). *The contemporary theory of metaphor*. Katika <https://escholarship.org/uc/item/54g7j6zh>

- Lakoff, G., & Johnson, M. (2008). *Metaphors we live by*. University of Chicago press.
- Lakoff, G., & Johnson, M. (1980). The metaphorical structure of the human conceptual system. *Cognitive science*, 4(2), 195-208.
- Lakoff, G., Johnson, M., & Sowa, J. F. (1999). Review of Philosophy in the Flesh: The embodied mind and its challenge to Western thought. *Computational Linguistics*, 25(4), 631-634.
- Loewenstein, K. (1953). Political Systems, Ideologies, and Institutions: The Problem of Their Circulation. *Western Political Quarterly*, 6(4), 689-706.
- Loewenstein, K. (1952). Union of Western Europe: Illusion and Reality--An Appraisal of the Motives: Part II, The. *Colum. L. Rev.*, 52, 209.
- Lord, A. B., Mitchell, S. A., & Nagy, G. (2000). *The singer of tales* (Vol. 24). Harvard University Press.
- Lukacs, G. (1971). *History and Class Consciousness: studies in Marxism*. London: Merlin Press
- Mannheim, K. (1936) *Ideology and Utopia: An Introduction to the Sociology of Knowledge*. New York: Harcourt, Brace and World (Harvest).
- Marx, K. (1973). Karl Marx, Frederick Engels on literature and art, eds. *Lee Baxandall and Stefan Morawski, New York: International General*.
- Marx, K., & Engels, F. (1974). *The German Ideology*. London: Arthur.
- Matei, A. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. O.U.P.
- Matteru, M. (1983). Fasihi. *Makala ya Semina ya Kimataifa*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbiti, J.S. (1991). *Love and Marriage*. London: Longman.
- Mbiti, J. S. (1990). *African religions & philosophy*. Heinemann.
- Mc Laren, P. (2003). *Life in schools: An introduction to critical pedagogy in the foundations of education*. Boston, MA: Allyn and Bacon.
- Mc Laren, P., & McLaren, P. P. D. (1995). *Critical pedagogy and predatory culture: Oppositional politics in a postmodern era*. Psychology Press.
- McLellan, D. (1973). *Karl Marx: His life and thought*. Springer.
- Mengistu, M. (2005). *Map of African literature*. Addis Ababa University.
- Mohamed, S. A. (1995). *Amezidi*. Nairobi: E.A.E.P
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa fasihi*. East African Educational Publishers.
- Msokile, M. (1981). Nafasi ya Nyimbo za Fasihi Simulizi katika Jamii Inavyobadilika. Makala za Semina ya Fasihi Simulizi. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 36-54.
- Mue, E. K. (2013). Maudhui na matumizi ya Lugha katika nyimbo za injili za Rose Muhando (M.A. Thesis, Kenyatta University)

- Musembi, N. (2016). *Mabadiliko ya Maudhui katika Nyimbo za Jando: Mfano kutoka jamii ya Wakamba*. (Doctoral Dissertation, Mount Kenya University)
- Musyoka, E. M. (2012). *Uhakiki wa Kimtindo wa Nyimbo za Mazishi Miongoni Mwa Wakamba* (M.A. Thesis, Kenyatta University)
- Mutwiri, G. (2005). *Mitazamo ya utendakazi wa Nyiso katika jamii ya Watigania* (M.A. Thesis, Kenyatta University)
- Mwai, K.W. (1997). *The Power of Song for Swahili Woman: Contesting social Death* (M.A. Thesis, Kenyatta University)
- National Council for Population and Development. (2013). *Kenya population situation analysis. NCPD and UNFPA*.
- Ndeti, K. (1972). *Elements of Akamba Life*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Ngugi, T. (1972). *Homecoming: Essays on African and Caribbean Literature, culture and politics*. London: Heinemann
- Njogu, K., & Chimera, R. M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na mbinu* (Vol. 1). Jomo Kenyatta Fndtn.
- Njogu, S. (1987). *Maudhui ya mapinduzi katika Riwaya za Visiwani Zanzibar* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Nketia, J. H. K. (1992). *The music of Africa*. London, England: W. W. Norton & Company, Inc.
- Nketia, J. H. K. (1963). *African music in Ghana*. Evanston, IL: Northwestern University Press
- Nkwera, F. V. (1979). *Sarufi na fasihi, sekondari na vyuo*. Tanzania Publishing House.
- Nurse, D & Spear, J. (1984). *The Swahili Reconstructing: The History and Languages of African Societies 1800-1850*. Philadelphia: University of Pennsylvania.
- Nzioki, S. (1982). *People of Kenya. The Akamba*. Nairobi: Evans Brothers.
- Otite, O. (1994). *Sociology: Theory and Applied*. Lagos: Malthouse Press Limited
- Peirce, C. S., & Welby, V. L. (1977). *Semiotic and significs: The correspondence between Charles S. Peirce and Victoria Lady Welby*.
- Saussure, F. M. (2011). *Course in general linguistics*. Columbia University Press.
- Saville-Troike, M. (2003). *The Ethnography of Communication*. Malden. MA: Blackwell Publishing.
- Scholes, R. (1982). *Semiotics and interpretation* (Vol. 465). Yale University Press.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar-es-salaam: Kauttu Limited.
- Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: nadharia na tahakiki*. Dar es Salaam University Press.

- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar-es-Salaam: Press and Publicity Centre.
- Strobel, M. (1979). *Muslim Women in Mombasa; 1890-1975*. New Haven and London: Yale University Press
- The *Constitution of Kenya* (2010). Nairobi: The National Council for Law Reporting.
- Thompson, J.B. (1990). *Ideology and Modern Culture: Critical Social Theory in the Era of Mass Communication*. Stanford, CA: Stanford University Press.
- Titon, J.T. (1992). Music: Folk and Traditional. In Richard Bauman (ed.), *Folklore Cultural Performances and Popular Entertainments*. New York: Oxford University Press.
- Toelken, B. (1986). *Ballads and Folksongs, Folklore Groups and Folklore Genres. An Introduction*. Logan, Utah: Utah University Press.
- TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi: Oxford University Press
- van Dijk, T.A. (1988). *News as Discourse*. Hillsdale, NJ: Erlbaum
- Van Dijk, T.A. (1998). *Ideology: A multidisciplinary Approach*. London. SAGE Publications.
- van Dijk, T.A. (ed.) (1997). *Discourse Studies: A Multidisciplinary Study*, (2 vols). London: Sage.
- Verhaar, J. W. (1975). Dell Hymes, Foundations in Sociolinguistics: An ethnographic approach. Philadelphia: University of Pennsylvania Press, 1974. Pp. x+ 245. *Language in Society*, 4(3), 352-361.
- Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.
- Wanjala, S. (2007). *Nyiso za Wabukusu: Maudhui na Lugha* (M.A, Kenyatta University).
- Wallerstein, I. (1979). *The capitalist world-economy*. Cambridge University Press.
- Wamitila K. W. (2008). *Kichocheo cha Fasihi. Simulizi na Andishi*. Dar-es-Salaam: Press and Publicity Centre.
- Wamitila K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers
- Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wathome, R. (2009). *Mtindo Katika Nyimbo za jamii ya Wakamba wa Masaku ya Kati* (M.A. Thesis, Kenyatta University).
- Wright, W. (1975). *Six Guns and Society: A structural Study of the Western*. University of California Press.

VIAMBATISHO

Kiambatisho 1: Nakala za Nyimbo za Kiasili za Kikamba

NA. 1. Kwa Sisy Wone

Aikwa: *Twauma kuasa. Twauma kuasa ii. Tukite nzaikoni kwa Mutinda. Kwa sisya wone Kwa sisya wone*

Mwaiki: **Muti** uu ni mumu. Muti uu ni mumu. Umite nza na nthini nomwiu. Ninguutila! Watahiriwa: Tila

Mwaiki: *Ninguutila*

Aikwa: *Tila*

Mwaikwa: *Ekai ukia ta matila ma kiimani Matesi **mbilano***

Tafsiri:

Angalia Uone

Watahiriwa: Tumetoka mbali. Tumetoka mbali. Tumekuja jandoni kwa Mutinda. Angalia uone Angalia uone.

Ngariba: Mti huu umekauka. **Mti** huu umekauka. Umekauka nje lakini ndani ni mbichi Nitaukata Watahiriwa: Ukate

Ngariba: Nitaukata

Watahiriwa: Ukate

Ngariba: Wacheni kuogopa Kama **wajinga wa milimani** wasiojua **kazi**.

NA. 2. Munyambu Nuukiva

Munyambu nuukiva. Munyambu nuukiva wi ukavi. Ni nau uwitie Munyambu nuukiva. Ni nau uwitie. Sisy ndukalilie. Ni nau uwitie

Tafsiri:

Simba Ananguruma

Simba ananguruma. Simba anaguruma akiwa ukavi. Ni baba aliyemwita. Simba anaguruma. Ni baba aliyemwita. Chunga usitetemeke. Ni baba aliyemwita.

NA. 3. Mwaikwa Niwalika Ndiani

Onthe: *Mwaikwa ii*

Mwaikwa: Mwaikwa ii

Onthe: *Yu niwalika **ndiani***

Mwaikwa: Yu niwalika ndiani

Onthe: Ndiani ya kulungilwa.

Mwaikwa: Mwaikwa niwalika ndiani

Onthe: Neewua maikulanya Kavila

eya kyau?

Mwaikwa: Neewua maikulanya Kavila

eya kyau?

Tafsiri:

Mtahiriwa Umeingia Kidimbwini

Wote: Mtahiriwa ii

Mtahiriwa: Mtahiriwa ii

Wote: Sasa ameingia **kidimbwini**.

Mtahiriwa: Sasa ameingia kidimbwini

Wote: Kidimbwi cha kujitegemea.

Mtahiriwa: Mtahiriwa umeingia

kidimbwini.

Wote: Nimesikia wakiulizana Kavila

atakula nini?

Mtahiriwa: Nimesikia wakiulizana Kavila atakula nini?

NA.4. Kaindo (Kakitu)

*Ve **kaindo** kala ngumanza kana niwe uvithite na ndandavasya ngumanza. Ve kaindo kala ngumanza Kana niwe uvithite, Na ndandavasya ngumanza. Kanyaa niwe uvithite, Na ndandavasya ngumanza. Ve kaindo kala ngumanza kana niwe uvithite na ndandavasya ngumanza. **Kanyaa** niwe uvithite, Na ndandavasya ngumanza. Ve kaindo kala ngumanza kana niwe uvithite na ndandavasya ngumanza **Vaati** niwe uvithite, na ndandavasya ngumanza. Ngutavye niwe uvithitei, na ndandavasya ngumanza. Ngutavye niwe uvithitei, na ndandavasya ngumanza. **Mulekye** niwe uvithite, na ndandavasya ngumanza.*

Tafsiri:

Kaindo

Kuna **kakitu** ninakatafuta, sijui kama ndiye amekaficha, na haniambii nikikatafuta. Kuna kakitu ninakatafuta, Sijui kama ndiye amekaficha na haniambii nikikatafuta. Kanyaa ndiye amekaficha, na haniambii nikikatafuta. Kuna kakitu ninakatafuta, sijui kama ndiye amekaficha, na haniambii nikikatafuta. **Kanyaa** ndiye amekaficha, na haniambii nikikatafuta. Kuna kakitu ninakatafuta, sijui kama ndiye amekaficha, na

haniambii nikikatafuta **Vaati** ndiye amekaficha , na haniambii nikikatafuta. **Mulekye** ndiye amekaficha , na haniambii nikikatafuta.

NA.5. Mwatu (Mzinga)

Ila wiw'aa ngiweta, ila wiw'aa ngiweta ndeto sya usenyo mwinawa ala usemba wone watungwa na ikwani. Ila wiw'aa ngiweta, ila wi'waa ngiweta ndeto sya usenyo mwinawa ala usemba wone watungwa na ikwani. Ala usemba wone, watungwa na ikwani. Ala usemba wone, watungwa na ikwani.

Nyamu ni ndevelovumendi niyo king'ong'o wona kana ka mundu tata na vinya usembe ndukatumbwe ni ikwani. Ala usemba wone, watumbwa ni ikwani. Wona kana ka mundu tata na vinya wivithe ndukatumbwe ni ikwani. Ala usemba wone, watumbwa ni ikwani.

*Ukwa **mwatu** uno nukutha na ndwina **nzuki** mwinawa mwatu uno nukutha na ndwina nzuki mwinawa kai syiminwa ni **ngaku** mwatu usu nduuisiasya. Ukwa mwatu uno nukutha na ndwina nzuki mwinawa mwatu uno nukutha na ndwina nzuki mwinawa kai syiminwa ni ngaku mwatu usu nduuisiasya.*

Tafsiri:

Mzinga

Unaposikia nikisema, unaposikia nikisema maneno ya kushangaza ndugu yangu mdogo, hebu kimbia uone ukirudisha na kesi. Unaposikia nikisema, unaposikia nikisema maneno ya kushangaza ndugu yangu mdogo, hebu kimbia uone ukirudisha na kesi. Hebu kimbia uone ukirudishwa na kesi. Hebu kimbia uone ukirudishwa na kesi.

Tendo hili linaitwa kunaswa na mtego ukimwona mtoto wa mwenyewe jaribu ujiepushe naye usiangukiwe na kesi. Hebu kimbia uone, utaangukiwa na kesi. ukimwona mtoto wa mwenyewe jaribu ujifiche usiangukiwe na kesi.

Unajua huu **mzinga** unaonekana kama una **nyuki** wengi na kumbe hamna kaka yangu, kumbe nyuki wanaangamizwa na **ngaku** (aina ya mnyama anayewaangamiza nyuki) , hujauchunguza mzinga vizuri. Unajua huu mzinga unaonekana kama una nyuki wengi na kumbe hamna kaka yangu, kumbe nyuki wanaangamizwa na ngaku hujauchunguza mzinga vizuri.

NA.6. Maendeleo ma Wia (Maendeleo ya Kazi)

Iyuu, Uhulu na nowe silikali tutanie silikali na utanu mwingi, silikali ina muuo ngitunga muvea. Miongo thanthatu na itatu nowo twosie usumbi. Ii wambiiwe ii ni Kinyatta ukaatiswa laisi ii mwikilye nimutavye Uulu nukuthukuma athukume na kithito. Iyuu, Uulu na nowe silikali tutanie silikali na utanu mwingi, silikali ina muuo ngitunga muvea. Miongo thanthatu na itatu nowo twosie usumbi. Ii wambiiwe ii ni Kinyatta ukaatiswa laisi ii mwikilye nimutavye Uulu nukuthukuma athukume na kithito.

Ii miongo thanthatu na itatu now'o twosie usumbi. Ii wambiiwe ii ni Kinyatta ukaatiswa laisi ii mwikilye nimutavye Uulu nukuthukuma athukume na kithito. Ii miongo thanthatu na itatu now'o twosie usumbi. Ii wambiiwe ii ni Kinyatta ukaatiswa laisi ii mwikilye nimutavye Uulu nukuthukuma athukume na kithito.

*Iyaaii, Savali nongwenda kuulukya **kikungu** ngome ngiivindua, nonguthingithangya valasa ndia nawina. Niwina nesa Velesi niwina nikue, ngenuka nenda mwa Uhulu ndwose ngethi. Maendeleo kwitu nguluvu twenda ngwatano, maendeleo ma wia. Maendeleo kwitu nguluvu twenda ngwatano, maendeleo ma wia. Ithyonze twenda kwiw'ana, maendeleo ma wia. Uulu twenda kwiw'ana, maendeleo ma wia.*

Tafsiri:

Maendeleo ya Kazi

Iyaa! Uhuru na ndiye serikali tufurahie serikali kwa furaha kubwa. Serikali ina amani natoa shukrani. Sitini na tatu ndio tuliupata uhuru. Ee aliyeanzisha ni Kenyatta kisha akafuatia rais ee, wacha niwaambie, Uhuru atafanya kazi aifanye kwa bidii. Iyaa! Uhuru na ndiye serikali tufurahie serikali kwa furaha kubwa. Serikali ina Amani natoa shukrani. Sitini na tatu ndio tuliupata uhuru. Ee aliyeanzisha ni Kenyatta kisha akafuatia rais ee, wacha niwaambie, Uhuru atafanya kazi aifanye kwa bidii.

Sitini na tatu ndio tuliupata uhuru. Ee aliyeanzisha ni Kenyatta kisha akafuatia rais ee, wacha niwaambie, Uhuru atafanya kazi aifanye kwa bidii. Sitini na tatu ndio tuliupata uhuru. Ee aliyeanzisha ni Kenyatta kisha akafuatia rais ee, wacha niwaambie, Uhuru atafanya kazi aifanye kwa bidii

Iyaaii, Savali nataka kusababisha **vumbi**, nilale nikijigeuza, nitawaguza wanabaraza, nitaimba vilivyo. Nitauimba vizuri Velesi nitauimba (wimbo) hadi nitosheke. Nitaenda nyumbani nitakapohitaji kufanya hivyo, Uhuru pokea salamu. Maendeleo kwetu wanavikundi tunahitaji umoja, maendeleo ya kazi. Sote twahitaji umoja, maendeleo ya kazi. Uhuru twahitaji masikilizano, maendeleo ya kazi.

NA.7. Nzambi Akithambya Nzele (Nzambi Akiosha Kata)

*Nzambi akithambya **nzele** ii ya kuthamba ii we wimwia ii undu uu ni waki? Nzambi akithambya nzele. Nzambi akithambya nzele ii ya kuthamba ii we wimwia ii undu uu ni waki? Nzambi akithambya nzele. Ekai umwia ii wa Katuta ii, Nzambi akithambya nzele. Ndanaumyai mundu uu Katuta? Nzambi akithambya nzele. Ekai ukulya ii ai kuyi na mbua ii niki? Nzambi akithambya nzele. Mukulasya ii mundu uu watata ii Nzambi akithambya nzele.*

Tafsiri:

Nzambi Akiosha Kata

Nzambi akiosha kata ya kuogea ee wewe unamwambia eti hivi ni kwa nini? Nzambi akiosha kata. Nzambi akiosha kata ya kuoga ee wewe unamwambia eti hivi ni kwa nini? Nzambi akiosha kata. Wacheni kumwambia ee eti wa Katuta, Nzambi akiosha kata. Hajaitoa ewe mtu wa Katuta, Nzambi akiosha nzele. Wacheni kuuliza eti na

hakuna mvua kwa nini? Nzambi akiosha kata. Mnauliza mtu huyu mtoto wa babangu, Nzambi akiosha kata.

NA. 8. Munuve

*Munuve tata ii manya ukia kindu **simba** ii syi ngunyu nitwasyelile. Munuve tata ii manya ukia kindu simba ii syi ngunyu nitwasyelile. Munuve tata ii manya ukia kindu simba ii syi ngunyu nitwasyelile. Munuve tata ii manya ukia kindu simba ii syi ngunyu nitwasyelile.*

Mundu ungi ndasyoka mbunge, Mundu ungi ndasyoka mbunge matuku kenda twitunga Munuve. Matuku aa ii twitunga Munuve. Asevuye kisomo, twitunga Munuve. Mwana waitu ii, ndukile utwokoe. Mwana wa Mati ii, ndukile utwokoe.

Twina thina mwingi, twina thina mwingi na ukilitye misyi, ndukile tata ii ndukile utwokoe. Twina thina mwingi, twina thina mwingi na ukilitye misyi, ndukile tata ii ndukile utwokoe. Andu ma Tseikuru tuikwenda mundu masiwa lala twenda ngumbau mundu ta Munuve

Tafsiri:

Munuve

Munuve baba, ee usiogope chochote **simba wenye kucha** tushazikata. Munuve baba, ee usiogope chochote simba wenye kucha tushazikata. Munuve baba, ee usiogope chochote simba wenye kucha tushazikatakata.

Mtu mwingine hawezi kurudi mbungeni, Mtu mwingine hawezi kurudi mbungeni tarehe tisa tutamrudisha Munuve. Tarehe hii ee, tutamrudisha Munuve. Aunde elimu, tutamrudisha Munuve. Mtoto wetu ee, amka utuokoe. Mwana wa Mati ee, amka utuokoe.

Tuna shida nyingi, tuna shida nyingi zimejaajaa humu nyumbani, amka baba amka utuokoe. Tuna shida nyingi, tuna shida nyingi zimejaajaa humu nyumbani, amka baba amka utuokoe. Watu wa Tseikuru hatutaki mtu maziwa lala tunataka jasiri mtu kama Munuve.

NA. 9. Usumbi ni Nzou

*Ni mukwatania wa tene wakutungiania mbai Kuma enzi ya Moi kuvika o vaa Kibaki unaminile utawala tutanambiia **mirugo** kurugania ta mang'oi. Myaka isu twimina na uruga uruga.*

Ngumangano ila mwinasyo ikwiwa ni sya kumanza usumbi usumbi ndwaamanzwa ii nandu kwaandikawa mathi maumange angi. Nasu namo mokile na mithato makeyumie vau mwinatetheka mwiteethya mavisii

*Andu ala mwi ngaliko ino Na ala mwi ngaliko iya mukwona muyonania muyonania winzi mukanyungia unyungia. Ngiti syathi na mukwato nzyima ndyendeeaa mwithi mukove ii **ngiti** li **nyamu** syonze ti sya ngiti **Nzou** ikungiawa ukungiwa.*

*Usumbi aume ni **nzou** na **nzou ngiti** ikwamba uu ndithengeeleka isu kila mundu ndove syake na mukuthi Mwambasa Muthama mukevingie. Muvisi ava ndikwona vandu mutathi nzi ino mwina Nduya Muthama kwaambiia a ve Musila, Kiema nginya Charity. Andu onthe matungianiwe ndokta Malombe twambe kumbania mbai Kivutha evo Kivwana Musimba e vau vau na unyuvani wavika ungamya ula ukwenda na ndukaume asu angi. Mundu umwe atwike ngavana **kitanda** ndukilisya **aume** eli me vamwe.*

*Ninisi ninaananga **ngima** neekia ve **mboka** nauluania vandu vamwe mwiiya vau inywonthe. Ii aa Masika Mutambu Mwendwa wa Mwova wikilye **kiw'u** umathambye. Mathambye meiiya vau monze. Ii mbaa lili ta Akamba ukilai mwaangumangei wathi unokie uilye uu.*

*Andu ala mwi ngaliko ino na ala mwi ngaliko iya mukwona muyonania muyonania **winzi (mwiw'a)** mukanyenya **mithumo**. Ngiti syathi na mukwato **nzyima** ndyendeeaa mwithi mukove ii **ngiti** nyamu syonze ti sya ngiti **nzou** ikungiawa ukungiwa.*

Tafsiri:

Urais ni Ndovu

Mimi ni mpatanishaji wa mbari wa tangu jadi, tangu nyakati za Moi hadi hivi majuzi ambapo Kibaki alikamilishia utawala wake kabla ya kuanza **urukaji** kurukaruka kama punda miaka hiyo tutaimaliza kwa kurukaruka?

Matusi mliyonayo yanasemekana ni ya kutafuta urais urais haujawai tafutwa eti kwa kuwatuma watu waende kuwatusi wengine. Hao nao wainuke kwa hasira kuwatusi wenzao pia. Hapo hamjasaidika mmewasaidia vijana.

Watu mlio upande huu na wale mlio upande ule, vile hamwezi kuonyeshana (mwiba) ulio chini ni kunusa mtanisia urais. Mbwa wakienda mawindoni na hisia za kimapenzi uwindaji haufanyiki Nendeni mkawafunge hawa **mbwa wanyama** wote si wa mbwa **Ndovu** hunyemelewa kunyemelewa

Jamani urais ni **ndovu** na huwezi kumkaribia ndovu **mbwa** wakibweka hivyo. Hao, kila mtu afunge wake. Halafu Muthama mwende Mombasa mjifungie. Muvisi sioni popote hamwezi kwenda nchini mkiwa na Nduuya Muthama. Kuanzia alipo Musila, Kiema hata Charity watu wote waunganishwe Daktari Malombe. Tuanze kwa kuikusanya jamii ya Mkamba Kivutha akiwepo Kivwana. Musimba akiwa hapo hapo na uchaguzi ukifika simamisha yule unataka na usiwatusi wale wengine. Mtu mmoja awe gavana haupandishi **wanaume** wawili kwenye **kitanda** kimoja.

Najua nimeharibu **ugali** nikachanganya na **mboga** nikachanganya pamoja mtakulia hapo nyote. Ee akina Masika Mutambu Mwendwa wa Mwova weka **maji** uwanawishe wanawishe watalia hapo wote. Ee akina fulani kama Wakamba amkeni mkanitusi wimbo ulikuja ukiwa hivyo.

Watu mlio upande huu na wale mlio upande ule vile hamwezi kuonyeshana ulio chini (**mwiba**) mtaramba **visigino**. Mbwa wakienda **mawindoni** na hisia za kimapenzi uwindaji haufanyiki. Nendeni mkawafunge hawa **mbwa** wanyama wote si wa mbwa **ndovu** hunyemelewa kunyemelewa.

11. Kithio kya Mukamba (Utamaduni wa Mkamba)

*Kithio twatiie kyonze vyu kithio kitu Syokimau letiu, letiu Kaundi, Athiani, Musyi, Kyeni, Mbaitu Mwenge mukilye kililimbi twai na mwathani mwathani wa ukamba **Syokimau** kithio tukituungie Mukamba akuthuka ambiaa kwasya ni musomu ni mutangiie ndyendaa siasa ndyendaa kithio ni mutangiie na usu mundu ukathi umwithie akumiswa mayini malikile ku e mutangiie? Wamwithia Mombasa niwe **Bakari** niwe **Juma** Juma mukamba mwenda ndini syonze Mukamba ndusyoke syoka kithioni umanyiswe undu*

*Yila mwewaa mwana kuna **ngua** ti ngua ilinda kanywa nukunawa nzoni syi kanywani niw'o umanaa mwana wa Mukamba syoka kithioni umanyiswe undu. Ona usumbi uu mukumanza muimanye ni wa nzi ti wa matuni na mwiumanza mwi nzi na I nzi nayo I syithio Apokomo I kithio kyoo na kya Masaai nakyo Akamba kyoo kyaendie ku?*

Tafsiri:

Utamaduni wa Mkamba

Utamaduni tuliua cha wote kabisa utamaduni wetu Syokimau redio, redio Kaundi Athiani, Musyi, Kyeni, Mbaitu Mwenge muinue kiwango. Tulikuwa na nabii nabii wa Ukambani **Syokimau** tuurejeshe utamaduni. Mkamba akianza kupotoka huanza kwa kusema kwamba nimesoma, nimeokoka sipendi siasa sipendi utamaduni nimeokoka na huyo mtu utampata akitolewa mapepo yaliingilia wapi akiwa ameokoka? Ukimpata Mombasa ndiye **Bakari**, ndiye **Juma**, Juma Mkamba mpenda dini zote Mkamba si urudi rudi kwenye utamaduni ufundishwe jambo.

Mliposikia mwana piga **nguo** Si nguo rinda, mdomo hupigwa pia soni zimo mdomoni, ndio unaotukanana mwana wa Mkamba rudi kwenye utamaduni ufundishwe jambo. Hata urais huu mnaoutafuta mjue ni wa hapa duniani si wa mbinguni na mnautafuta mkiwa duniani na dunia nayo ina tamaduni Wapokomo wana utamaduni wao na waMaasai Nao Wakamba wao ulienda wapi?

NA. 12. Ngai wa Nzou Nowe wa Nduti (Mungu wa Ndovu Ndiye wa Siafu)

*Ii Ngai ndamamaa Mulungu ndakomaa Ngai ula wa **nzou** nowe wa **nduti** Ngai nowe usu Ngai ula wa athwii nowe ukusuviaa asuviaa ngya isu Ngai ndamamaa Ngai ula wa matu nowe ukusuviaa twindo tula twi nzi twi nzi ta nduti Ngai niwe usuviaa **nzungu***

*Wathi ninia Katutu Mulango ndavye andu Kwa-Siku Ona ala me Ndovoini Ngai ula wa **nguku** nowe wa **nzou** Mulungu ndakomaa Ngilu nunaetiwe atendesye nzi kula kwi **maliko maima** maneekitwe utwike mutendea withie Asumali na Akala menyithya kiw'u kwa Kimanzi yiya ni Ngengi aa Kambua Kitaka Metinda mailye vamwe Nzangi na aa Katembu Mbula withie Kitundu nanga nimwaya kyaliti tondu nimwakata Mbiti wa Mulonzya kalima kangu kulisa kayulisa Ngura ningwate Munenii ii nduku ya Mutwii Mavulya mwalimu ii nguutambua ndwose ngethi nothi ungethesya Malu Mivukoni **Musungu** yu nunaendie Kitui kaundi twina Mukamba.*

Tafsiri:**Mungu wa Ndovu ndiye wa Siafu**

Ee Mungu halali Mungu hasinzii Mungu yule wa **ndovu** ndiye wa **siafu** Mungu ndiye huyo, Mungu yule wa matajiri ndiye anayekulinda yeye hulinda maskini hao Mungu halali Mungu wa mbinguni ndiye akulindaye viumbe wadogowadogo walio hapa duniani Mungu ndiye hulinda **siafu**

Wimbo nauimbia Katutu Mulango niwaambie watu Kwa-Siku hata wale wako Ndovoini Mungu wa **kuku** ndiye wa **ndovu** Mungu halali Ngilu aliletwa anyoroshe nchi palipo na **mashimo** na **mabonde** yaliyowekwa yanyoroke kabisa iwe Wasomali na Wagalla Wananyunyuzia maji kwa Kimanzi jameni. Akina Kambua Kitaka wanashinda pamoja Nzangi na akina Katembu Mbula iwe kwamba mmebahatika kwa maana mmetafuta Mbiti wa Mulonzya hakuna kupanda mlima mwingine, Ngura imeshikwa vilivyo Muneeni ee ndugu ya Mutwii Mavulya mwalimu nakutambua pokea salamu na umsalimu Malu Mivukoni **mzungu** alienda Jimbo la Kitui tuna Mkamba sasa.

NA. 13. Kikamba ni Kyakwa (Kikamba ni Lugha Yangu)

*Kikamba kyoomie kyoomie ona tene ona ila kwai nguano teka syathelile aka nimo meesi ndia syikwo mwita. Mundu tyuu mwanake niwauka na ndesi auka utee wa muunda kumanza ki? Ukethia kula ii syiitwa kiitene ii undu ungi syetaw'a kuu ni aa Manandu na Mwangu wa Ivuti **nguano** Kikamba ala maivita metitye kwitya mutino utevo ni andu anini kila ninaa ki mwalyuli walyula kii nake e muthinzio wa ngili ili*

*Ula undu Makau Vulovesa mwisi wisene na Kithungu, Kikamba nikyakwa niika umuunyulila kunyula kunyula. Nimwisi mutaa ula wa kuathima kasele natulya kathaku vandu kau keyaa vau no keumuathima kioko tene nina muikio. Ngilasya naweta ngwatano ngwiwa ningwitanga **liu** nzi ninaeka kwananga liu wenyu. Nainie ngwatano vandu va mwaka umwe myei ikumi na ili nimanzite ngwatano ya Musila na Kaluki inywonze mwi ngusi na mwaema nethia nethia kilya nine nimaingianisye*

*Mbikilye nzame niyo luka twisi Mukamba athukaa na kwenda nzamithyo. **Maanga** nzamithye **makwasi** nzamithye Mukamba nukwenda usama **manyanya** na ethia ndwimuvata nukusama vyu. Ndumbikilye nzame niyo luka twisi Mukamba athukiaa kwenda usamithwa **Maanga** nzamithye **makwasi** nzamithye Mukamba nukwisa usamithwa utongosya na ethiwa ndwimuvata nukweendee*

*Ndinengawe kindu ai mukambia Wathi uu ni kindu ai kindu ngwenda ndinengawe kindu ona kava inywi mwina musaala na maluvuluvu Mulyungi anoonie kundu kutoneka **nguunguu** yonaa vandu vaasa tyo vaa ve kimba ithyi twona vau*

Tafsiri:**Kikamba Ndiyo Lugha Yangu**

Kikamba kimekuwa kigumu hata kitambo kulipokuwa na uchumba ni vile uliisha tu, wanawake ndio walijua kuwa wapo wajinga wengi. Mtu ni huyu mtanashati amekuja na hajui amekuja kando ya shamba kufanya nini? Ingekuwa kwamba kura hizi zinaitishwa kama kitambo ee kama zilivyoitishwa huku na akina Manandu na akina

Mwangu wa Ivuti **uchumba** Kikamba wanaoweza kuzipita wakiwa wameziomba pasi bahati mbaya ni watu wachache. Ninachoimba kina mfasiri awezaye kufasiri hiki ana zawadi ya elfu mbili

Kama vile mnajua Makau Profesa anajuana na Kiingereza Kikamba ni changu nawagawia kidogo tu kugawa kidogo kidogo tu. Mnajua **mutaa** ule wa kubariki Nimewekelea **Kata** juu pahali hako katalala hapo katawabariki asubuhi na mapema, nina imani. Huwa nikitaja muungano ninaambiwa namwagamwaga **chakula**. Nimeacha kuharibu chakula chenu, niliimba muungano kwa mwaka mmoja miezi kumi na miwili nikitafuta muungano wa Musila na Kaluki nyote ni mashahidi na ikashindikana nikaamua niimbe niwachochee

Niwekee nionje ndiyo lugha tunayoifahamu Mkamba huharibika kwa kutaka kuonjeshwa. **Mihogo** nionjeshe Mkamba anataka kuonja **nyanya** na kama hutamkataza ataonja kabisa Niwekee nionje ndiyo lugha tunayoijua Mkamba huzidi kwa kutaka kuonjeshwa **Mihogo** nionjeshe **viazi vitamu** nionjeshe Mkamba ataonjeshwa uongozi na kama hutamkataza ataendeleaaa

Sipewi kitu eti mtaniambia Wimbo huu ni kitu eti kitu ninataka sipewi kitu hata heri nyinyi Mna mishahara na marupurupu Mulyungi aliona kusikoonekana **kunguru** huona mbali si hapa tu penye mzoga sisi tunaona hapo.

NA. 14. Kativa Muuo wa Ndee (Katiba Amani ya Maeneo ya Mipakani)

*Andu ma ndee twalei kusyoka tusyoke utee o kula myaka miongo itatu na ili a mutai asyae nooka umusomethya kila kitawa sumali shifita ni mundu wa utee mbaitu tea matu nimusomethye. Nzia twatiile o kuula kwa Mweu ivinda ya Manandu andu aa mweewie Mutua wa Kioko aviviswe musyi na andu make. Ukasi mooawa ivinda ya Manandu nzia twoisye ku twatyiiile nzia o kula kwa Mweu ivinda ya Manandu ala mweewie Mutua wa Kioko aviviswe musyi na andu make moonze mooawa ivinda ya Manandu nzia twoisye kuu yu **nzia** isu mukuna kaa kii nditethya niyo tutindiiiaa?*

Asumali siasa twenda tumonie ingi me vaati vyu masamu aa twonaa kau wa ndongoi uimatethesya. Mainatumina makatumina mainatuuaa makatuuaa mumye andu ala anyuue mumye monze vyu musakue angi ona asu muusakua onamo mukaumya Asomali nonaa makatuthinia mainatuthinia makatuthinia mainatuuaa makatutemanga

Manandu akumanzithya undu ula ukwikana na mashifta a mamuvingaa matwitasyaa i kula ona Asomali asu vayi utamaweta ndukakengwe a maendie mbunge monze ni shifita maendaa na Asomali aa ninyee ndawa yamo ninguthi umamina na maemee vau Nyayo twai nake ndeke ii Ngomeni okite umamina na amatii vau ninoonie nzia ukukuluswa andu ala makwithisye

Andu ala ma tene vyu maendie mbunge mwanaa Mweu Mwikya niwe wi thayu Vuti ndamanya undu wa mashifta Kisini ndukile wa Mwatha nenda withiwe wa kamitii kau kativa ikusenzwa kundu kula muuo utaakwatikana itheka sya ndee kundu kuu miao isenzwe undu ungi na ti kuu kwitu ni Kenya yonze itheka ii syi ndee ii syenda miao isenzwe undu ungi isu ya ukoloni nditutethasya twaitye mathayu ma andu maitu maingi teka na kuu kuasa o vaa Munyithya wa Mwinzi woowailwe

Kuma vau ni andu miongo itatu na kenda moae kuma Kaningo kuvika Endau na Mutha ndwi vau ala uwongela no kwongela kungi nuumanya undu ngwasya ndukambuthisye na mwewa ngwina uu mwikasye no ngui ikwamba ta ila ingi. Thii muumbane mawokili na andu ma ndee mwithi muumbane na ngavana na anyuvwa ma ndee musuvie ndee nayo no miao ivandiliswe undu ungi ino ya ukoloni kuvika vau ii nditutethasya.

Tafsiri:

Katiba Amani ya Maeneo ya Mipakani

Watu wa mipakani hebu turudini kule kando kule miaka thelathini na miwili iliyopita wale hamkuwa mmezaliwa nimekuja kuwafundisha kinachoitwa Wasomali Shifta mimi ni mtu wa mpakani jameni tega masikio niwafundishe. Njia tuliachia kule kwa kina Mweu wakati wa Manandu kwa wale mlisosikia Mutua wa Kioko alichomewa nyumba pamoja na watu wake Ukasi wakauawa wakati wa Manandu tuliachia njia huko. Tuliachia njia kule kwa Mweu wakati wa Manandu kwa wale mlisosikia Mutua wa Kioko alichomewa nyumba pamoja na watu wake wote waliuawa wakati wa Manandu tuliachia njia huko. Sasa hiyo **njia** mnapitia Kwa kweli haiwezi kutusaidia ndiyo tutairudia?

Manandu akitafuta namna ya kuwafanyia waliompinga walituitisha hizo kura kwa kisingizio cha kuwamaliza mashifta hakuna mwenye hakuwataja, usidaganywe. Walioenda mbunge wote ni shifta wao huenda kwa madai kuwa Mashifta hawa mimi ndiye dawa yao nitaenda kuwamaliza lakini wameenea hapo. Tulikuwa na Nyayo aliacha ndege yake Ngomeni ila aliwaacha hapo Alikuwa amekuja kuwamaliza ila aliwaacha hapo niliona namna waliofiwa walivyoteseka

Watu wa zamani sana walioenda mbungeni mwana wa Mweu Mwikya ni wewe uko hai Vuti hawezi kujua kuhusu mashifta Kisini amka uende kwa gavana tugeuze **huu uta** kulikokuwa mbele, tugeuze **uta** Mwikya unajua kuhusu mashifta Kisini amka wa Mwatha nataka uwe mwanakamati hiyo Katiba ikibadilishwa maeneo ambamo amani haikupatikana maeneo ya mipakani maeneo haya sheria zibadilishwe kwa namna nyingine na si huku kwetu tu, ni Kenya nzima. Maeneo haya yaliyo mipakani yanahitaji sheria zibadilishwe kwa namna nyingine sheria hizi za nyakati za ukoloni hazitusaidii. Tume poteza nafsi za watu wengi kando na huko nyuma sana kipindi hiki tu ambapo Munyithya wa Mwinzi aliuliwa.

Kuanzia hapo ni watu thelathini na tisa wameuliwa kutoka Kaningo hadi Endau na Mutha iko hapo wale mnaongeza mnaweza kuongeza unajua vile ninasema usinidharau. Na mkisikia nikiimba hivyo, msiseme ni mwimbaji anasema kama wengine nendeni mkusanyike mawokili na watu wa maeneo ya mipakani. Nendeni mkusanyike na magavana na wanajamii wa mipakani mtunze mipakani pia ni sharti sheria zibadilishwe kwa njia nyingine hizi za ukoloni kufikia hapo hizi hazitusaidii.

NA.15. Muviisi Ungi (Kijana Mwingine)

*Ng'ombe ii sya mutavo syendaa nongi wavena mundu kiveti na mbesa umanye ukakivenwa uu Sya mutavo syendaa nongi **Ng'ombe** sya mutavo syendaa nongi Ng'ombe syataviwe usumali ikaetwe ukamba isu ng'ombe sikesiwa nangi sya mutavo syendaa nongi **kitheka** wosie utuvite chifu na ngusi ukaiva kikaung'endye kithitu*

kikaingwa uminiwa andu vyu kivila wosie uivite andu kuiva kuiva makaivwa nangi nokwikwa o ta Mwau sya mutavo syendaa nongi

*Nisoma **ivuku** ndyusoma mundu ekai kwisoma ni wathi ngwina nye na nyie niwina ula undu ukie utuku uilye na ndiweengeesya ve undu wi vaa ukuthinya andu na mayuuweta Maiyu nuuwete. Undu tyuu vaa uuthinya andu na Akamba muyuuweta nuuwete ninye **kaletiu** ka Syokimau nuke ndumusye Akamba*

*Kamwana ti kaa kanini vyu kailite usakuwa kailye nzi ona katanaungama ni kavitie **kilaa** kyumaa nzi na miw'a yakyo kaa kenda utwilwa mata Kalonzo ala utwila wone muvisi ungi tyuu. Mauta ma ng'ombe ulovotye mbokani muuke museo **muti** wa uvosya ndwikiawa mwingi Kivutha Kibwana vena undu ninaw'o Uka Nguni wisie muthinzio **ndila** ngunenge na nundu wi ngavana ninisi nduka nika uminenge Ileli wetewe Makueni. we minista munini Kivwana niwokie ukethania Kyethani uka Nguni wisie muthinzio ndila ngunenge na nundu wi ngavana ninisi nduka nika uminengane Kivutha wetewe Makueni.*

Tafsiri:

Kijana Mwingine

Ng'ombe hawa wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia ukimnyang'anya mtu mkewe kwa pesa ujue nawe utanyang'anywa vivyo hivyo wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia. **Ng'ombe** wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia Ng'ombe walioibiwa Somalia wakaletwe Ukambani hao ng'ombe watakujiwa na wengine wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia. **Ardhi** uliyomiliki kwa kuwahonga chifu na mashahidi utailipia usiionee fahari mila ya 'Kuinga Kithitu' ikifanywa wanafamilia wako wataangamia wote cheo ulichokipata kwa kuwalipa watu vilivyo watalipwa na wengine na ufanyiwe kama Mwau wa wizi hutoroshwa kwa wizi pia

Nasoma **kitabu** sisomi mtu wacheni kujisoma ni wimbo ninaimba mimi nami nitauimba vile ulivyokuja usiku na siwezi kuupotosha kuna jambo hapa linawatatiza watu na hawalitaji Maiyu nitalitaja. Jambo ni hili hapa linawatatiza watu na Wakamba hawalitaji nitalitaja mimi ndiye **karedio** ka Syokimau nije niwaongeleshe Wakamba

Kijana ni huyu mdogo sana anafaa kuchaguliwa akiwa ameketi hata akiwa hajasimama tayari amepita **kilaa** (aina ya mmea wenye miiba) hutoa miiba yake tangu uchangani huyu anahitaji kutemewa mate Kalonzo hebu tema uone. Kijana mwingine ndiye huyu **mafuta** ya ng'ombe umwage kwenye mboga harufu mwafaka **dawa** hainywewi nyingi Kivutha Kivwana niko na jambo njoo Nguni ukujie zawadi **Beberu** nikupatie na kwa maana wewe ni gavana najua huwezi kuja nitatumana Ileli uletewe Makueni wewe naibu minister ulikuja kutembelea Kyethani njoo Nguni ukujie zawadi beberu nikupatie na kwa maana wewe ni gavana najua huwezi kuja nitatumana Kivutha uletewe Makueni.

NA.16. Undu Ukwona Ngisilila Uu (Ninaposhangilia Hivi)

Undu ukwona ngisilila uu, Undu ukwona ngisilila uu Ndinakoma musyi. Undu ukwona ngisilila uu, Undu ukwona ngisilila uu Ndinakoma musyi. Niwee kilumini ngivoyea misyi, Niwee kilumini ngivoyea misyi. Niwee kilumini ngivoyea muuo, Niwee kilumini ngivoyea muuo. Niwee kilumini ngivoyea mbua, Niwee kilumini ngivoyea

mbua. Niwee kilumini kwa Mutava musyi, Niwee kilumini kwa Mutava musyi. Kula kwi miti minene kwasuvaswa mikokola ona mithekethi. Kula kwi miti minene kwasuvaswa mikokola ona mithekethi.

Tafsiri:

Ninaposhangilia Hivi

Vile unaona nikishangilia hivyo, vile unaona nikishangilia hivyo, sikulala nyumbani. Vile unaona nikishangilia hivyo vile unaona nikishangilia hivyo sikulala nyumbani. Nilikuwa kwenye kilumi (aina ya ngoma ya kiasili inayochezwa kwa namna ya ibada kwa Mungu na miungu) nikiombea jamii. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea jamii. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea amani. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea amani. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea mvua. Nilikuwa kwenye kilumi nikiombea mvua. Nilikuwa kwenye kilumi nyumbani kwa Mutava. Nilikuwa kwenye kilumi nyumbani kwa Mutava. Ndiko kwenye miti mikubwa kunakotengenezwa mikokola na mithekethi (aina ya kifaa cha kukoroga uji unapoendelea kupika. Ndiko kwenye miti mikubwa kunakotengenezwa mikokola na mithekethi (aina ya kifaa cha kukoroga uji unapoendelea kupika).

NA.17. Tuthii Kithembeoni (Twendeni Madhabahuni)

Ukilai ithyonze tuthi kithembeoni, Ukilai ithyonze tuthi kithembeoni. Tukathembee Ngai mbua yue. Tukathembee Ngai mbua yue. Syana syukile, syana syokote malenge kivulanio kya nzuu na mboso. Tumukathe Ngai Mulungu. Ukilai ithyonze tuthi kithembeoni. TukathembeeNgai, Ngai Mumbi Ngai Mwatuangi. Ula wauisye mbua nundu wa kuthembewa. Ngai nitwooka ithemboni twiwe. Ngai nitwooka ithemboni twiwe. Noituekea mavityo maitu we Mumbi waitu. Noituekea mavityo maitu we Mumbi waitu. Ngai waitu nataiwe. Ngai waitu nataiwe. Ngai waitu Mumbi, Ngai Mwatuangi niwaile kutaiwa. Ngai waitu Mumbi, Ngai Mwatuangi niwaile kutaiwa. Ngai tuekea mavityo maitu we Mumbi waitu. Ngai tuekea mavityo maitu we Mumbi waitu.

Tafsiri:

Twendeni Madhabahuni

Amkeni sote twende madhabahuni, amkeni sote twende madhabahuni. Tukamwabudu Mungu mvua inyeshe. Tukamwabudu Mungu mvua inyeshe. Watoto wainuke, watoto waokote maboga, mchanganyiko wa baazi na maharagwe. Tumtukuze Mungu muumbaji. Inukeni nyote twende kwenye madhabahu, tukamwabudu Mungu, Mungu Muumbaji aliyeinyesha mvua alipoabudiwa. Mungu tumekuja madhabahuni, tusikize. Mungu tumekuja madhabahuni, tusikize. Na utusamehe makosa yetu ewe muumbaji wetu. Mungu wetu atukuzwe, Mungu wetu atukuzwe. Mungu wetu Muumbaji, Mungu Muumbaji anastahili kutukuzwa. Mungu wetu Muumbaji, Mungu Muumbaji anastahili kutukuzwa. Mungu tusamehe makosa yetu ewe Muumba wetu. Mungu tusamehe makosa yetu ewe Muumba wetu.

NA. 18. Mathiko Kyunduani (Mazishi Kyunduani)

Andu asu mwi Kivwese, Mutito wa Ndei Maamba mwi kuu mwii ma Makindu nimwasya ndongosya Mundu wisikie muno. Nimutavya nguma ti mbesa Ndile Kalembe niwathi uthumua Kyunduani Akamba ala me nguma mundu yake mbene Keka kivila mundu kusakuuwa vatiele andu ana Kalembe atevo

Tafsiri:

Mazishi Kyunduani

Enyi watu wa Kibwezi, Mtito Andei, Maamba na popote mlipo watu wa Makindu mmempoteza kiongozi mtu maarufu sana nawaambia umaarufu si pesa Ndile Kalembe ameenda kupumzika Kyunduani Wakamba walio na umaarufu wao binafsi Kando na cheo mtu kuchaguliwa wamebaki watu wanne bila kumhesabu Kalembe.

NA. 19. Kikw'u ni Musyimi

Kikwu ni musyimi ute tei. Ni muvutani ute tei. Okaa kwosa kila kiseo. Na kutia mwene na kimeto kitathimika. Osa ala ase, ala avoo alau. Ala ma kwikwatwa Misyini yoo. Kikw'u ni musyimi na muvutani. Kikw'u ni musyimi na ndomiiasya ala ase nduani kana misyini ona nguthuni. Asyimaa mwendwa wa andu ni kana amonuve

Tafsiri:

Kifo ni Mwindaji

Kifo ni **mwindaji asiye huruma**. Ni **mnyang'anyi asiye na huruma**. Huja kuchukua kile chema. Na kumwacha mwenyewe na huzuni isiyopimika. Huchukua wale wazuri, walio wapole na wakarimu. Wanaotegemewa nyumbani mwao. Kifo ni mwindaji na mnyang'anyi. Kifo ni mwindaji na havumiliani na wale wazuri kijijini au nyumbani au kwenye halaiki. Humwinda mpendwa wa watu ili awaumize kwa uchungu.

NA. 20. Mutanu

Alililililiiii! Nimutumane ni selia mbene maundu ala me mundu nzyoke na musyi indi ningwisilya undu umwe ndutua. Nimutumane ni selia mbene maundu ala me musyi nzyoke na musyi indi ningwisilya undu umwe ndutua. Niw'o ngwi'wa kunena nyie navitha kana mundu ukuveva na ndyamba kwona musung'wa. Niw'o ngwi'wa kunena nyie navitha kana mundu ukuveva na ndyamba kwona musung'wa. Ndyendaa mundu wina manyamanya, andu aa ma kwitu, wina manyamanya, mundu ute tavia, wina manyamanya, nenda nitavwe wina manyamanya, mundu ukuveva na ndyamba kwona musung'wa)

Nauma kwasa nauma kwasa nayu ningwenda katanda ngome. Nauma kwasa nauma kwasa nayu ningwenda katanda ngome. Nauma kwasa nauma kwasa nayu ningwenda katanda ngome. Nauma kwasa, nauma kwasa, nayu ningwenda katanda ngome. Silikali niyookilya moko umanye musyi wi vinya umanzawa na thina Mutanu songa Mutanu songa kana mwa woneke kana nithasye mikwa. Silikali niyookilya moko umanye musyi wi vinya

NA. 21. Kilyambu (Kilyambu)

*Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kuukya ii Kilyambu. Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kuukya ii Kilyambu. Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kuukya ii Kilyambu. Kala kamwana, Kilyambu, kala kanini, Kilyambu, kakwike nesa, Kilyambu, ila twikomana Kilyambu. Kala kanini, Kilyambu ila twikomana Kilyambu kakwike nesa, Kilyambu. Na ngoma nisikukunwa kyama ngwika, ii nisyikukunwa kyama ngwika, nitatite kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. Na ngoma nisikukunwa kyama ngwika, ii nisyikukunwa kyama ngwika, nitatite kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. Yii nisyikukunwa ya mundu ungi, nitatite kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. nitatite kawayaya aiii ngoma ya kyandalua. Nenda ngoma Mutanu akitwawa yiya nenda kiliko Mutanu yiya nenda kiliko wa Mwangangi. Nenda ngoma Mutanu akitwawa yiya nenda kiliko Mutanu yiya nenda kiliko wa Mwangangi. Mwiitu wa musee, ni museo sana aendaa na **ngali**. Akithi **Ilovi**, aendaa na ngali. Akithi **Mombasa**, aendaa na ngali.*

Tafsiri:

Kilyambu

Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kumekucha ii Kilyambu. Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kumekucha ii Kilyambu. Kilyambu ui, Kilyambu ui, ii kumekucha ii Kilyambu. Yule kijana, Kilyambu, yule mdogo, Kilyambu, akutendee wema, Kilyambu, mkikutana, Kilyambu. Yule mdogo, Kilyambu, mkikutana, Kilyambu akutendee wema, Kilyambu. Na ngoma zitachezwa kama ambavyo ninafanya, ndio zitachezwa kama nifanyavyo, nimejaribu kawayaya, ngoma ya chandarua. Na ngoma zitachezwa kama ambavyo ninafanya, ndio zitachezwa kama nifanyavyo, nimejaribu kawayaya, ngoma ya chandarua. Ndio zitachezwa ya mtu mwingine, nimejaribu kawayaya, ngoma ya chandarua. Nataka ngoma Mutanu akiolewa yiya! Nataka akili Mutanu yiya! Nataka akili wa Mwangangi. Nataka ngoma Mutanu akiolewa yiya! Nataka akili Mutanu yiya! Nataka akili wa Mwangangi. Binti wa mzee ni mzuri sana husafiri kwa **gari**. Akienda **Nairobi**, huenda kwa gari. Akienda **Mombasa**, huenda kwa gari.

NA.22. Sikala (Sigara)

*Manguleti nikwita ngikwita, ngwititye **sikala** ukambata na ung'endu ngasokota yakwa na ngekia **mwaki** na ngainia uvuta. Manguleti nikwita ngikwita, ngwititye sikala ukambata na ung'endu ngasokota yakwa na ngekia mwaki na ngainia uvuta. Umatite sikala Manguleti, umbatite niki tukoonana. Umatite sikala Manguleti, umbatite niki tukoonana. Na teka sikala, ndumiwe **kisevu** kya kwiyonaa ngusisimukye. Na teka sikala, ndumiwe kisevu kya kwiyonaa ngusisimukye. Mwa Susu nde ngui, susu nde ngui aume ii neteela e ivungulu. Mwa Susu nde ngui, susu nde ngui aume ii neteela e ivungulu.*

*Kisaayoni, **Kisaayoni**, aume yina mwaki, ii yina mwaki nayo yavoa, seuvya nyeki ii kwaua mkuo. Kisaayoni, Kisaayoni, aume yina **mwaki**, ii yina mwaki nayo yavoa, seuvya nyeki ii kwaua mkuo. Kitemu mukwona, ni kya susu akandumia kingi. Onakyo ni kyakwa, ni kya susu akandumia kingi. **Kitemu** mukwona, ni kya susu akandumia kingi. Onakyo ni kyakwa, ni kya susu akandumia kingi. Kitemu mukwona,*

ni kya susu akandumia kingi. Ambii ata? Ndikaasembe, Ndikese uthekwa, yiya ni kiseo akandumia kingi. Mwa susu nde ngui, susu nde ngui aume netelae e ivungulyu.

Tafsiri:

Sigara

Manguleti nakuita nakuita, nimekuomba **sigara** ukaninyima tu kwa ukaidi, nikaikunja yangu na kuiwasha **moto** nikaanza kuivuta. Manguleti nakuita nakuita, nimekuomba sigara ukaninyima tu kwa ukaidi, nikaikunja yangu na kuiwasha nikaanza kuivuta. Umeninyima sigara Manguleti, umeninyima kwa nini? Tutaonana. Umeninyima sigara Manguleti, umeninyima kwa nini? Tutaonana. Na kando na sigara, nimeshonewa **kisevu** cha kujionea fahari nikusisimue. Na kando na sigara, nimeshonewa kisevu cha kujionea fahari nikusisimue. Nyanya yangu hachezi, nyanya hachezi jamani nangojea tu. Nyanya yangu hachezi, nyanya hachezi jamani nangojea tu.

Pale kwenye **kisaayo** (aina ya mti) Pale kwenye kisaayo (aina ya mti), jamani ina **moto**. Nayo ikizimika, andaa nyasi, kuutua mzigo. Pale kwenye kisaayo (aina ya mti) Pale kwenye kisaayo (aina ya mti), jamani ina moto. Nayo ikizimika, andaa nyasi, kuutua mzigo. **Kitemu** mnachokiona, (aina ya vazi la kale) ni cha nyanya atanishonea kingine. Hata nacho ni changu, ni cha nyanya atanishonea kingine. Kitemu mnachokiona, (aina ya vazi la kale) ni cha nyanya atanishonea kingine. Aliniambiaje? Nisikimbie, nisije nikachekwa, hicho ni kizuri atanishonea kingine. Nyanya hana mzaha, nyanya hachezi nasubiri tu

NA. 23. Uka Usuvie Utwae (Njoo Uitunze Ndoa)

*Ii niutavya vate kuvuvuana, kana ka mama uka usuvie utwae. Ii niutavya vate kuvuvuana, kana ka mama uka usuvie utwae. Niutavya vate kukia kindu, kana ka mama ii uka usuvie utwae. Niutavya vate kukia kindu, kana ka mama ii uka usuvie utwae. Niuiwe **ngate**, vamwe na **kyavati** ii, Niuiwe ngate, vamwe na kyavati ii kana ka mama uka usuvie utwae.*

Tafsiri:

Njoo Uitunze Ndoa

Ndio, nakwambia pasipokuchanganyikiwa, mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Ndio, nakwambia pasipokuchanganyikiwa, mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Ndio, nakwambia pasipokuchanganyikiwa, mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Ndio, nakueleza pasipo kuogopa lolote mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Ndio nakueleza pasipo kuogopa lolote mtoto wa mama njoo utunze ndoa. Umepikiwa **mikate**, njoo utunze ndoa. Umepikiwa **chapati**, njoo utunze ndoa.

NA. 24. Mumbe (Aliyeumbwa Akaumbika)

Natumie nduu na kana kanini ketawa Mumbe, kanengie kivalua kyumu kakamanthie uki wa ngilu. kanengie kivalua kyumu kya umantha uki wa ngilu. Wa tata nduthi Thua ii, wa tata ndukatike lumba. Wa tata nduthi Thua ii, wa tata ndukatike lumba.

Nakitisyeye nguli muundani iyovete suluali na waitha ongela kamisi na lesa, ongela sikwati na waitha. Ongela kamisi na lesa, ongela sikwati na waitha. Nayu ninooka nguungule Yosi nguka, avai wa tata wa Munyalo ndungethesye Koki wa Munyalo, uuke ukwisa umbakia.

Nekiitwe kamisini vandu ndoneka, sindiliani uu ta ni nondo. Nekiitwe kamisini vandu ndoneka, sindiliani uu ta ni nondo. Kii kyakwa ni kinengo, kii kyakwa ni kinengo nanengiwa ni Mulungu niw'a muyo ngwina.

Tafsiri:

Mumbe (Aliyeumbwa Akaumbika)

Nilifanya urafiki na mtoto mdogo aitwaye Mumbe. Alinipa kibarua cha kutafuta **asali mwitu** (aina ya mdudu anayeunda asali mwitu). Ndugu yangu nenda Thua, ndugu yangu cheza rhumba. Ndugu yangu nenda Thua, ndugu yangu cheza rhumba.

Nilipata **nyani shambani** akiwa amejifunga **suruali** na uzi wa **waitha** (aina ya mti), ongeza **kamisi** na **kanga**, ongeza **sikati** na waitha. Na sasa nimekuja nikubembeze Yosi nikija, jamani ndugu yangu wa Munyalo msalimu Koki wa Munyalo, uje kabla ya kunijengea.

Nilikuwa nimeingizwa kwenye kamisi singeonekana, kwenye sindiria kama **matiti**. Nilikuwa nimeingizwa kwenye kamisi singeonekana, kwenye sindiria kama matiti. Hii yangu ni zawadi, nilipewa na Mola na hufurahia ninapoimba.

NA. 25. Nzambi wa Mutunga (Nzambi wa Mutunga)

Ndumbinguie wa musyi, ndumbinguie wa Mutunga ndumbinguie wa musyi. Ndumbinguie wa musyi, ndumbinguie wa Mutunga ndumbinguie wa musyi. Na ndumbinguie, wa Mutunga ii na ndumbinguie wamusyi. Nzambi nzele wivia ku? Ni yakwa ya kuela ndia, ngatava na ngathamba Nzambi nzele wivia ku? Nzambi nzele wivia ku? Ni yakwa ya kuela ndia, ngatava na ngathamba Nzambi nzele wivia ku?

Simu yaumie, simu yaumie Masaku twamikwatie na twooka. Simu yaumie, simu yaumie Masaku twamikwatie na twooka. Aume mwakwata livoti mwaisye ata? Mwindavya. Mbande mutunda, ni waki? Wai wa mavatano. Aume mwakwata livoti mwaisye ata? Mwindavya. Mbande mutunda, ni waki? Wai wa mavatano.

Nzambi ndaumie ii Kangundo akwete Wayua ii na kwoko, ii wa Mutunga ndasyoke. Nzambi ndaumie ii Kangundo akwete Wayua ii na kwoko, ii wa Mutunga ndasyoke. Ukwaithya ndata yaki? Iyaayi ndata ya uwe. Ukwaithya ndata yaki? Iyaayi ndata ya uwe. Ukwete nzele yaki? Iyaayi nzele ya uwe. Ukwete nzele yaki? Iyaayi nzele ya uwe.

Tafsiri:**Nzambi wa Mutunga**

Nifungulie wa nyumbani, nifungulie wa Mutunga, nifungulie wa nyumbani. Nifungulie, wa Mutunga nifungulie wa nyumbani. **Nzambi** unapeleka **kata** wapi? Ni yangu ya kupima maji kwenye **bwawa la kuogelea**, ninachota na kisha kuoga. Nzambi unapeleka kata wapi? Ni yangu ya kupima maji kwenye bwawa la kuogelea, ninachota maji na kisha kuoga. Nzambi unapeleka kata wapi?

Simu ilipigwa, simu ilipigwa kutoka Machakos tuliipokea na tukaja. Simu ilipigwa, simu ilipigwa kutoka Machakos tuliipokea na tukaja. Wazee mlipoipokea ripoti mlisemaje? Mniambie. Nipande **mtunda**, ni wa nini? Ulikuwa wa mapatano.

Nzambi alitoka Kangundo akiwa amemshika Wayua mkono, ndio wa Mutunga arudi. Nzambi alitoka Kangundo akiwa amemshika Wayua mkono, ndio wa Mutunga arudi. Unatingiza **fimbo** ya nini? Iyaayi! Fimbo ya uganga. Unatingiza **fimbo** ya nini? Iyaayi! Fimbo ya uganga. Umeshika **kata** ya nini? Iyaayi! **kata** ya uganga.

NA.26. Tavitha (Tavitha)

Eka nzingithye ileve, Eka nzingithye ileve yaema ninuke ngakomele kwitu. Eka nzingithye ileve, Eka nzingithye ileve yaema ninuke ngakomele kwitu. Na wingulya isyitwa na wingulya isyitwa tinye nguingusya ninye nguinguiwa ngenuka kaloko. Na wingulya isyitwa na wingulya isyitwa tinye nguingusya ninye nguinguiwa ngenuka kaloko.

Auuwaa! ninewie ukiwetwa mwa ai kindu wakwa ii ngwendete ii. Auuwaa ninewie ukiwetwa mwa ai kindu wakwa ii ngwendete ii. Tavitha ii wai wakwa ii na wandia, Tavitha ii wai wakwa ii na wandia, Tavitha ii wai wakwa ii na wandia, Tavitha ii wai wakwa ii na wandia, ninamanyie ukandia na ukuthi ukwete nduume na unamikisya ivindi. Naungamisye Tavitha ii anambia We! Naungamisye Tavitha ii anambia We! Naungamisye Tavitha ii anambia We! Naungamisye Tavitha ii anambia We! Ndweke ungulya mwaka uu ti ta ula ungi nyie ni mukaa mwalimu na ndinena na ivisi. Ni mukaa mwalimu na ndinena na ivisi. Ni mukaa mwalimu na ndinena na ivisi. Ni mukaa mwalimu na ndinena na ivisi.

Tafsiri:**Tavitha**

Wacha nitingize ileve (aina ya kifaa kinachochezwa wakati wa ngoma ya kitamaduni) nikishindwa niende nyumbani kwetu nilale huko. Wacha nitingize ileve nikishindwa niende nyumbani kwetu nilale huko. Na unaniuliza jina, na unaniuliza jina, sio mimi nitabisha bali ni mimi nitafunguliwa nitaenda nyumbni asubuhi. Na unaniuliza jina, na unaniuliza jina, sio mimi nitabisha bali ni mimi nitafunguliwa nitaenda nyumbni asubuhi.

Auuwaa! Nilisikia ukisengenywa jamani, eti mpenzi wangu nakupenda. Auuwaa! Nilisikia ukisengenywa jamani, eti mpenzi wangu nakupenda. Tavitha ulikuwa wangu na ukaniacha. Tavitha ulikuwa wangu na ukaniacha. Tavitha ulikuwa wangu na ukaniacha. Tavitha ulikuwa wangu na ukaniacha. Nilijua utaniacha na utembe

ukilishikilia ndume na ukalirushia **mfupa**. Nilimsimamisha Tavitha akaniambia We! Nilimsimamisha Tavitha akaniambia We! Nilimsimamisha Tavitha akaniambia We! Nilimsimamisha Tavitha akaniambia We! Wacha kuniuliza mwaka huu si kama ule mwingine mimi ni mke wa mwalimu na siongei na vijana wavulana, ni mke wa mwalimu na siongei na vijana wavulana

NA. 27. Mundu Mwiu E Kiliko (Mtu Mweusi ni Mwenye Akili)

*Iyaa iyaa! mundu mwiu e kiliko ui na umanyi ii na kwakya ayukila athekete yaa! niw'o mumbile. Iyaa iyaa! mundu mwiu e kiliko ui na umanyi ii na kwakya ayukila athekete yaa! niw'o mumbile. Umaaluka kaloko na kaniki ka mthemba katumitwe kitene na kwovwa utene. Umaaluka kaloko na **kaniki** ka mthemba katumitwe kitene na kwovwa utene. Niyova lesu uu ta mundu wa tene ula weyovaa kaniki aendete wathini kukuna mukanda kwa!kwa!kwa!kwa! Niyova lesu uu ta mundu wa tene ula weyovaa kaniki aendete wathini kukuna mukanda kwa!kwa!kwa!kwa! Niyova lesu uu ngalungala nesa ta mundu mueni mwakomana nziani ukaungama nesa ukamba kumwiloela mundu wi kiliko syitwa yake etawa **Mbete**, **Mbete** ya kwoko ta nikunyamasya nikilya ngomete ngamililikana ngaina kuia ii! Na Mbete akambona ngakethya wa Mwendu. Mbete akambona ngakethya wa Mwikali. Tyuu **vevi** tyuu twi suoo. Moko na Mwendu nduthi ukime Mukyondo Mukyondo mbai ili, Mukyondo mbai ili wiitwe naka mbee ndena **mundu** ndumbongele **nzakame**.*

Tafsiri:

Mtu Mweusi ni Mwenye Akili

Iyaa iyaa! mtu mweusi ana akili na maarifa na kunapopambazuka anaamka akicheka yaa! ndiyo maumbile. Iyaa iyaa! mtu mweusi ana akili na maarifa na kunapopambazuka anaamka akicheka yaa! ndiyo maumbile. Utoke asubuhi na mapema ukijifunga **kaniki** (aina ya vazi la kitamaduni) ka aina fulani kalikoshonwa kikale na kufungwa kikale. Nitajifunga lesu hivi kama mtu wa kale aliyejifunga kaniki akielekea kwenye densi kucheza **mukanda** (aina ya ngoma ya kitamaduni iliyochezwa) kwa!kwa!kwa!kwa! Nitajifunga lesu hivi kama mtu wa kale aliyejifunga kaniki akielekea kwenye densi kucheza **mukanda** (aina ya ngoma ya kitamaduni iliyochezwa) kwa!kwa!kwa!kwa! Najifunga lesu hivi, ninakaa wima kama mtu mgeni mkikutana njiani unasimama vizuri unamtazama kwanza, mtu mwenye hekima, jina lake ni **Mbete**, **Pete** ya mkono inanisumbua. Nikiwa nimelala naikumbuka na kisha ninaanza kulia ii! Naye Mbete akaniona nikamsalimu wa Mwendu, Mbete akaniona nikamsalimu wa Mwikali, ndiye huyu **mtoto** ndiye huyu leo. Mikono juu na Mwendu nenda umtwange Mukyondo, Mukyondo mbari mbili ukiwa umeambiwa na wanawake kuwa hana **mtu**, si uniongeze **damu**.

NA. 28. Kyathi no Vala (Miadi ni ile ile)

*Iyaii yayai! kyathi no vala vala wandavisye wambiie ningoka kuathima mwana ii na **kaindo** ngyuka. Iyaii yayai! kyathi no vala vala wandavisye wambiie ningoka kuathima mwana ii na **kaindo** ngyuka. Yii mwana ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa mwingi. Yii mwana ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa*

mwingi. Wa tata ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa mwingi. Wa tata ii vindya, ngwongole, ngwongole ukome nina laa mwingi.

Tafsiri:

Miadi ni Ileile

Iyaaiii, aiii! miadi ni ile ile, vile ulivyoniambia uliniambia utakuja kumbariki mtoto na **kitu** ukija. Iyaaiii aiii! miadi ni ile ile, vile ulivyoniambia uliniambia nitakuja kumbariki mtoto na kitu nikija. Ee! mtoto nyamaza nikubembeleze, nikubembeleze ulale nina raha nyingi. Ee! mtoto nyamaza nikubembeleze, nikubembeleze ulale nina raha nyingi. Wa baba nyamaza, nikubembeleze, nikubembeleze ulale nina raha nyingi.

NA. 29. Inyaa Mwana na Ithea Mwana (Mama na Baba Mtoto)

Inyaa mwana iyi, na ithea mwana iyi, ethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka. Inyaa mwana iyi, na ithea mwana iyi, ethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka. Inyaa mwana iyi, na ithea mwana iyi, ethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka. Inyaa mwana iyi, na ithea mwana iyi, ethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka. Ngyuka na ngyuka kethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka. Ngyuka na ngyuka kethia mwana ni wakwa ndumbinguie ngyuka.

*Kasilisili mwana ii inyaa mwana nukumbenda inyaa mwana akusye ikanda nakwa ainenga ngusye kwata mukwa ulumitye ndukandekye nimandane. Kasilisili mwana ii inyaa mwana nukumbenda inyaa mwana akusye **ikanda** nakwa ainenga ngusye kwata **mukwa** ulumitye ndukandekye nimandane.*

Tafsiri:

Mama na Baba Mtoto

Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija. Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija. Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija. Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija. Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija. Mama mtoto na baba mtoto, kama mtoto ni wangu, nifungulie nikija. Nikija na nikija, kama mtoto ni wangu nifungulie nikija. Nikija na nikija, kama mtoto ni wangu nifungulie nikija.

Kasilisili mwana ii mama mtoto ee mama mtoto ananihitaji, mama mtoto avute **kamba** na kisha anipe nivute shika **kamba pana** vizuri usiniachilie nianguke. Kasilisili mwana ii mama mtoto ee mama mtoto ananihitaji, mama mtoto avute kamba na kisha anipe nivute shika mukwa vizuri usiniachilie nianguke.

NA. 30. Kaveti Kaanu (Kamwanamke Kazembe)

Kaveti kaanu mbua ni mbiingu, Kaveti kaanu mbua ni mbiingu, ndwose kathungi, kamulo na kavelu na uyaangiia muundani kaveti kaanu mbua ni mbiingu. Syana

iyamba kuvuna ii mbemba sya tumikeve twili. Syana iitonya kuvuna mbemba sya selekali mbaitu ii mwaka umwe tumikeve twili.

Tafsiri:

Kamwanamke Kazembe

Kamwanamke kazembe mvua imenysha, Kamwanamke kazembe mvua imenysha, chukua kiondo, jembe na mbegu na kisha uelekee shambani Kamwanamke kazembe mvua imenysha. Watoto hawawezi shibishwa na mahindi ya serikali jamani mwaka mmoja mikebe miwili, Watoto hawawezi shibishwa na mahindi ya serikali jamani **mikebe** miwili kwa mwaka mzima. Kamwanamke kazembe mvua imenysha.

NA.31. Muika wia Nukunwe (Vijana Kazi Itekelezwe)

Yii muika ii wia nukunwe, kasi nukunwe waemwa utungwe na musyi. Ve ndeke ikwitwa Manyali ikukua Konza ii nake Songola Manyali akakua andu ma wia. Yii muika ii wia nukunwe, kasi nukunwe waemwa utungwe na musyi ve ndeke ikwitwa Manyali ikukua Konza ii nake Songola Manyali akakua andu ma wia. Onake Sungula Manyali akakua andu ma wia. Onake Sungula Manyali akakua andu ma wia.

Tafsiri:

Vijana Kazi Itekelezwe

Eee vijana, kazi ifanywe, kazi ifanywe na ukishindwa urudishwe nyumbani. Kuna **ndege** inaitwa Manyali, inabeba watu Konza, naye Songola Manyali atabeba watu wa kazi. Eee vijana, kazi ifanywe, kazi ifanywe na ukishindwa urudishwe nyumbani. Kuna **ndege** inaitwa Manyali, inabeba watu Konza, naye Songola Manyali atabeba watu wa kazi. Naye Songola Manyali atabeba watu wa kazi.

NA. 32. Kavuli Vula (Kavuli Twanga Mawele)

***Kavuli** vula mwee witu. Kavuli vula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. Kavuli vula mwee witu. Kavuli vula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. Nikilya nekalila kivalo ngivulavula mwee witu. **Ngima** yumaa kwi kuthie, ii vulavula mwee witu. **Isandi** yumaa kwi kukime ii vula vula mwee witu **Kinaa** kyumaa kwi kuthie ii vula vula mwee witu. Nikilya nathia kakautwa, nikilya nathia kakautwa nila imutengea ya kiveti yukilasya kwoko ta ikwaunya Kavuli vula mwee witu.*

Tafsiri:

Kavuli Twanga Mawele

Kavuli twanga mawele yetu, Kavuli twanga mawele yetu. Ninakaa hapa uwanjani nikitwangatwanga mawele yetu. Ninakaa hapa uwanjani nikitwangatwanga mawele yetu. Kavuli twanga mawele yetu, Kavuli twanga mawele yetu. **Ugali** hupatikana kwa kusiaga mawele, twanga twanga mawele yetu. **Isandi** (aina ya chakula cha

kitamaduni) hupatikana baada ya kusaga mawele, twanga twanga mawele yetu. **Kinaa** (aina ya chakula cha kitamaduni) hupatikana kwa kusiaga mawele, twanga twanga mawele yetu. Unga inapungua kadri ninaposiaga, unga inapungua kadri ninaposiaga. Yule mwanamke mzembe ndiye anapunguza).

NA. 33. Lulu Mwana (Lulu Mwana)

*Lulu mwana, koma twithukiisye ee Aa mwaitu mayuka aa Maithingithya **syaamba** aa Mailonzanya ii Mailonzanya No ta maliu ii no ta masuni lulu mwana aaa*

Tafsiri:

Lulu Mwana

Lulu mwana, lala tusikilize ee, aakina mama wakija aa, wakitingiza **syaamba** aa, wakipiga kelele ee, wakipiga kelele ee, ni kama ndege ii lulu mwana aaa.

NA. 34. Ndukilye Mwana (Mwana Nyamaza)

*Lulu mwana ndukilye mwa ndukese kulika ni mbiti. Lulu mwana ndukilye mwa ndukese kulika ni mbiti. Lulu mwana nduvindye mwa mbiti yina maeo moi. Lulu mwana ndukilye mwa ndukese kulika ni **mbiti**. Lulu mwana ndukome mwa, asyai maende muundani. Lulu mwana ndukilye mwa ndukese kulika ni mbiti.*

Tafsiri:

Mwana Nyamaza

Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na **fisi**. Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na fisi. Lulu mwana tulia we! Fisi ana meno makali. Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na fisi. Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na fisi. Lulu mwana lala we! Wazazi waende shambani. Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na fisi. Lulu mwana nyamaza we! Usije ukaliwa na fisi.

NA. 35. Natwaie Valua (Nilipeleka Barua)

*Natwaie **valua** kwa tata ii na waia nziaani ii. Natwaie valua kwa tata ii na waia nziaani ii, Natwaie valua kwa tata ii na waia nziaani ii. Natwaie valua kwa tata ii nawaia nziaani ii. Indi tiwe, indi tiwe, indi tiwe, indi niwe.*

Tafsiri:

Nilipeleka Barua

Nilipeleka **barua** kwa baba na ikapotelea njiani. Nilipeleka barua kwa baba na ikapotelea njiani. Nilipeleka barua kwa baba na ikapotelea njiani. Lakini si wewe, si wewe, si wewe na ni wewe.

NA. 36. Na Muyo Ndwalasya (Furaha Haiumi)

*Na muyo ndwalasya, na muyo ndwalasya kethia niwalasya ndikoma ni **kyalya**. Na muyo ndwalasya, na muyo ndwalasya kethia niwalasya ndikoma ni kyalya. Na muyo ndwalasya, na muyo ndwalasya kethia niwalasya ndikoma ni kyalya. Na syana mwiiw'a ata ii? Ii twiiw'a muyo tuyosa **kikombe**. Alimu mwiiw'a ata ii? Ii twiiw'a muyo tuyosa kikombe. Asyai mwiiw'a ata ii? Ii twiiw'a muyo tuyosa kikombe.*

Tafsiri:**Furaha Haiumi**

Utamu hauumi, utamu hauumi kama ungekuwa unauma singeweza kulala kwa sababu ya **maumivu**. Utamu hauumi, utamu hauumi kama ungekuwa unauma singeweza kulala kwa sababu ya maumivu. Utamu hauumi, utamu hauumi kama ungekuwa unauma singeweza kulala kwa sababu ya maumivu. Watoto mnahisi vipi? Tunafurahia tukichukua tuzo. Walimu mnahisi vipi? Tunafurahia tukichukua **tuzo**. Wazazi mnahisi vipi? Tunafurahia tukichukua tuzo.

NA. 37. Osa Kindu Wikye Kingi (Chukua Kitu Urushe Kingine)

*Nuu ula twimutuma, nuu ula twimutuma, nuu ula twimutuma?
Na nduku twimutuma, na Nduku twimutuma, na Nduku twimutuma.
Ukakethye andu Nduku, Ukakethye andu Nduku, Ukakethye andu Nduku.*

*Osa **kindu** wikye kingi, Osa kindu wikye kingi, Osa kindu wikye kingi.
Ai ai isokote, isokote isokote, isokote isokote.
Ai ai isokote, isokote isokote, isokote isokote.*

Tafsiri:**Chukua Kitu Urushe Kingine**

Ni nani tutamtuma, ni nani tutamtuma, ni nani tutamtuma?
Na Nduku tunamtuma, na Nduku tunamtuma, na Nduku tunamtuma?
Ukawasalimu watu Nduku, Ukawasalimu watu Nduku, Ukawasalimu watu Nduku.

Chukua **kitu**, urushe kingine, Chukua kitu, urushe kingine, Chukua kitu, urushe kingine.
Ee Ee, cheza, cheza cheza, cheza cheza
Ee Ee, cheza, cheza cheza, cheza cheza.

NA. 38. Tingilingili

*Tingilingili, tingilingili, **ng'ombe** sya utuku syuyawa utuku tingilingili.
Tingilingili, tingilingili, ng'ombe sya nau syuyawa utuku nula **mukavi** akanywe iia tingilingili.
Tingilingili, tingilingili, ng'ombe sya utuku syuyawa utuku tingilingili.
Tingilingili, tingilingili, ng'ombe sya nau syuyawa utuku nula mukavi akanywe iia tingilingili.
Tingilingili, tingilingili, ng'ombe sya nau syuyawa utuku tingilingili.*

Tafsiri:***Tingilingili***

Tingilingili, tingilingili, ng'ombe wa usiku wanaoibwa usiku tingilingili, tingilingili.

Tingilingili, tingilingili, **ng'ombe** wa baba wanaoibwa usiku na yule **Mmasai**, akanywe maziwa, tingilingili, tingilingili.

Tingilingili, tingilingili, ng'ombe wa baba wanaoibwa usiku tingilingili, tingilingili.

Tingilingili, tingilingili, ng'ombe wa baba wanaoibwa usiku na yule Mmasai, akanywe maziwa, tingilingili, tingilingili.

Tingilingili, tingilingili, ng'ombe wa baba wanaoibwa usiku tingilingili, tingilingili.

NA.39. Ngulu wa Ngao

Nguluuu iii Ngulu Mwelela Nguluuuu Ngulu Mwaiwaa. Nguluuu iii Ngulu Mwelela Nguluuuu Ngulu wa Kasimbili. Iwe Ngulu, wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. Malenge meene mwatemangie, no mukaiva, Ngulu wa Ngao, iwe Ngulu wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. Malenge meene mwatemangie, no mukaiva, Ngulu wa Ngao, iwe Ngulu wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. Ngulu, wa Ngao, Ngulu, wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili.

Tafsiri:**Ngulu wa Ngao**

Nguluuu iii Ngulu Mwelela Nguluuuu Ngulu Mwaiwaa. Nguluuu iii Ngulu Mwelela Nguluuuu Ngulu wa Kasimbili. Iwe Ngulu, wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. **Maboga** ya wenyewe mliyatakata, mtalipa tu. Maboga ya wenyewe mliyatakata, mtalipa tu Ngulu wa Ngao, wewe Ngulu wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. Ngulu wa Ngao, wewe Ngulu wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili. Ngulu, wa Ngao, Ngulu, wa Ngao, Ngulu wa Kasimbili.

NA.40. Ngune Kithuki (Nipige Mbiu)

Ngune kithuki mutambo ukaye, Ngune kithuki mutambo ukaye. Musumali niwaleile na ng'ombe. Ekwatya ii Mbiki ni ngulu mbiingi. Ekwatya ii Mbiki ni ngulu mbiingi. Teka Misi waleile Veveloni mwa umiloni wa syua mwa Elisavethi tavya munene nake atume watho ngwaithangye mukau wilingile ii iya u mututu uu ng'ombe ii sya ndia sya kwinukya kioko vayi undu ekai tuthi utwa nzuke Musumali niwaleile na ila ingi.

Niwanengie ndata yayu, nengi naendie kithekani ta mbusya, ngithi ukwama Kalisa nde ngua. Kitheka ki munyambu ii na mbusya ii o ili tunamanzaa inaa. Syangomisye Kalisa ii nde ngua, kitheka ki minyambu na mbusya o ili tunamanzaa inaa.

Tafsiri:**Nipige Mbiu**

Nipige mbiu mtambo utoe sauti, Nipige mbiu mtambo utoe sauti. Msomali amekatalia na ng'ombe. Anadhani mimi Mbiki nina maringo mengi. Anadhani mimi Mbiki nina maringo mengi. Kama Misi hangelinda Veveloni, upande wa Mashariki jamani Elisavathi, mwambie mkubwa naye atoe amri nipige mbiu isikike ii iya! Hivi vita, hawa ng'ombe wa wajinga wanaoibiwa asubuhi, hamna neno wacheni twende tukaonane nao, tujue bivu na bichi Msomali amekatalia na wale wengine.

Alinipa **fimbo** jamani, kisha nilienda kichakani kama **kifaru**. Nilikwama Garisa bila mavazi. Kichaka kilicho na **simba** na vifaru, ng'ombe wawili tuliokuwa tukiwatafuta wakapotea. Walinifanya nilale Garisa bila mavazi. Kichaka kilicho na simba na kifaru, wawili tuliokuwa tukiwatafuta wakapotea.

NA. 41. Nzoka ya Mukelele (Nyoka Maridadi)

***Kakiti** ukathua ta mukala ii. **Kakiti** ukathua ta mukala ii. Taambukya kwoko ngutwile **mata** ii pu! Ndyi kyeni syoka syoka **Kakiti** ii ukathua ta Mukala. Taambukya ingi, pu! Ndyi kyeni syoka syoka **Kakiti** ii ukathua ta Mukala*

***Nzoka** ni ya uthwii ii nzoka, ya mukelele. **Nzoka** ni ya uthwii ii nzoka, ya mukelele. Aume mwisila va ni nzoka? Ya mukelele. Iveti mwisila va ni nzoka, ya mukelele. **Nzoka** ni ya mumo nzoka, ya mumo. **Nzoka** ni ya mumo nzoka, ya mumo. Aume mwisila va ni nzoka? Ya mumo, iveti mwisila va ni nzoka, ya mumo.*

*Katiia kutava we umaala utave indo. Aaaa! umaala utave indo. Katiia kutava we umaala utave indo. Aaaa! umaala utave indo. **Nzoka** ni ya kutava we umaala utave **ng'ombe**, Aaaa! umaala utave ng'ombe. **Nzoka** ni ya kutava we umaala utave indo, Aaaa! umaala utave **indo**.*

Tafsiri:**NYOKA MARIDADI**

***Kakiti** utatajirika kama Mgalla ee. **Kakiti** utatajirika kama Mgalla ee. Nyoosha mkono nikutemee **mate** pu! Sina mkosi geuka **Kakiti** ee utatajirika kama Mgalla. Nyoosha tena pu! Sina mkosi geuka **Kakiti** ee utatajirika kama Mgalla.*

***Nyoka** ni wa utajiri huyu nyoka, maridadi. **Nyoka** ni wa utajiri huyu nyoka, maridadi. Wanaume mtapitia wapi juu ya huyu nyoka? Maridadi. Wamama mtapitia wapi juu ya nyoka? Maridadi. **Nyoka** ni wa nehema huyu nyoka, wa nehema. **Nyoka** ni wa nehema huyu nyoka, wa nehema. Wanaume mtapitia wapi juu ya huyu nyoka? Wa nehema. Wamama mtapitia wapi juu ya nyoka? wa nehema.*

Harakisha kuchota wewe toka uchote mifugo. Aaaa! toka uchote mifugo. Harakisha kuchota wewe toka uchote mifugo. **Nyoka** ni wa kuchota wewe toka uchote **ng'ombe**, Aaaa! toka uchote ng'ombe. **Nyoka** ni wa kuchota wewe toka uchote ng'ombe, Aaaa! toka uchote **mifugo**.

Kiambatisho 2: Idhini ya Utafiti – PPMC**REPUBLIC OF KENYA****MINISTRY OF GENDER, CULTURE, THE ARTS AND HERITAGE
PERMANENT PRESIDENTIAL MUSIC COMMISSION**

Telephone: 2721052/2717645
Tel/Fax: 2716869
Email: infoppmc@go.ke
directorppmc@gmail.co

State House Road
P. O. Box 48534-00100
NAIROBI

Ref No: PPMC/8/18/Vol. VIII (6)**22nd April 2024****To whoever it may concern,****RE: PERMISSION TO USE PPMC AUDIO AND VIDEO MATERIALS FOR
EDUCATIONAL RESEARCH WORK**

The Permanent Presidential Music Commission (PPMC) hereby confirms that Ms Elizabeth Kasau Mue of ID NO. 22257301 undertook part of her educational research work at our Audio Visual department from which she sourced a number of audio and video recordings for further reference.

Ms. Mue has the authority of PPMC to use these materials as part of her research work.


Danson Siminyu
Assistant Director

Kiambatisho 3: Cheti cha Kutozingatia Wizi (Anti-plagiarism)

SR478

ISO 9001:2019 Certified Institution

THESIS WRITING COURSE***PLAGIARISM AWARENESS CERTIFICATE***

This certificate is awarded to

MUE ELIZABETH KASAU

SASS/DPIL/KIS/06/2017

In recognition for passing the University's plagiarism

Awareness test for Thesis entitled: **UFUMBAJI WA ITIKADI KUJAZANDA KWENYE NYIMBO ZA KIASILI ZA KIKAMBA** with similarity index of 3% and striving to maintain academic integrity.

Word count: 57650

Awarded by

Prof. Anne Syomwene Kisiu

CERM-ESA Project Leader Date: 04/04/2024